# TANZANIA OSAKA ALUMNI

# Kitabu cha

# Mbinu Bora 5

**Ofisi ya Rais**
**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
**P.O. Box 1923,**
**Dodoma.**

**AGOSTI, 2018**

# KITABU CHA MBINU BORA 5

# (2018)

**Kimeandaliwa kwa ajili ya Tanzania Osaka Alumni (TOA) na:**

| | | |
|---|---|---|
| **Paulo Faty,** | - | **Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe** |
| **Ahmed Nassoro** | - | **Mhadhiri Msaidizi, LGTI** |
| **Michiyuki Shimoda** | - | **Mshauri Mwanadamizi, OR-TAMISEMI** |

**Na kuharimiwa na:**

| | |
|---|---|
| **Liana Hassan** | **– Makamu Mwenyekiti, TOA** |
| **Stella Paschal** | **– Afisa Serikali za Mitaa Mkuu, OR-TAMISEMI** |
| **Honorina Ng'omba** | **– Mtaalamu wa Kitaifa, OR-TAMISEMI** |

## YALIYOMO


| Mada | Kurasa |
|---|---|
| Vifupisho | i |
| Dibaji | iii |
| Utangulizi (TOA) | iv |
| Utangulizi (JICA) | v |
| **SURA YA KWANZA: UTANGULIZI; MASUALA YALIYOIGWA KUTOKANA NA UZOEFU WA JAPANI** | 1 |
| **SURA YA PILI: JITIHADA ZA JAMII KWA AJILI YA HUDUMA BORA** | 20 |
| Jiji la Mwanza : Udhibiti Shirikishi wa Magugu Maji Katika Ziwa Viktoria | 22 |
| H/W Geita : Jitihada za Kijiji Katika Kuboresha Utoaji wa Huduma | 30 |
| H/W Chato : Jitihada za Jamii Katika Kuanzishaji Shule Shikizi | 39 |
| **SURA YA TATU: UGATUAJI WA MASUALA YA FEDHA UBORESHAJI WA MAPATO** | 46 |
| H/ W Bariadi : Uboreshaji wa Mapato kwa Utoaji Bora wa Huduma | 47 |
| **SURA YA NNE: USHIRIKISHWAJI WA JAMII KATIKA UTOAJI WA HUDUMA** | 54 |
| H/W Itilima : Uboreshaji wa Mazingira na Uongezaji wa Kipato Katika Jamii | 57 |
| H/W Misungwi : Uboreshaji wa Mazingira ya Kuishi na Elimu kwa Watoto Wenye Ulemavu wa Ngozi | 65 |
| H/W Musoma : Kukuza Mfuko wa Afya ya Jamii kwa Huduma Bora za Afya | 72 |
| H/W Bukombe : Usimamizi Shirikishi wa Skimu ya Maji | 79 |
| H/W Ngara:Ushiriki wa Jamii Katika Kufungua na Kuboresha Barabara | 86 |
| H/W Ukerewe : Uhifadhi Jumuishi wa Misitu ya Asili | 93 |
| **SURA YA TANO: MAENDELEO YA JAMII KIUCHUMI** | 99 |
| H/W Misenyi : Uwezeshaji, Utaftaji Masoko na Mitaji kwa Wazalishaji wa Vijjini | 101 |
| H/W Ukerewe : Kuboresha Uzalishaji na Kuongeza Thamani ya Zao la Muhogo | 109 |
| H/W Itilima: Ukuzaji wa Kilimo Hifadhi kwa Uhakika wa Chakula | 119 |
| H/W Tarime : Kukuza Uzalishaji wa Kahawa ya Vikonyo na Kuongeza Kipato | 126 |
| H/W Rorya : Umwagiliaji wa mpunga Kuboresha Kipato na Uhakika wa Chakula | 135 |
| H/W Bunda : Ufugaji wa Samaki katika Vizimba na Urejeshaji wa Mazalia ya Samaki | 141 |
| **REJEA** | 154 |

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ADF | Agency Delegated Functions |
| ALAT | Association of Local Authorities In Tanzania |
| AMCOs | Agricultural Marketing Cooperatives |
| AMSDP | Agriculture Market Support Development Programme |
| BMU | Beach Management Unit |
| BRELA | Business Registration and Licensing Agency |
| CAVA | Cassava Adding Value for Africa |
| CBHF | Community Based Health Financing |
| CDCF | Constituency Development Catalyst Fund |
| CDD | Community Driven Development Projects |
| CHMT | Council Health Management Team |
| CMT | Council Management Team |
| COWSO | Community Owned Water Supply Organization |
| CPU | Coffee Processing Unit |
| DASIP | District Agriculture Support Programme |
| DbyD | Decentralization by Devolution |
| DFT | District Facilitation Team |
| ECOVIC | East African Community Organization for Management of Lake Victoria Resources |
| ESRF | Economic and Social Research Foundation |
| FBO | Faith Based Organization |
| FETA | Fisheries Education and Training Agency |
| FRMP | Forest Resource Management Project |
| HFGC | Health Facility Governing Committee |
| IFAD | International Fund for Agricultural Development |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| KCMC | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| KMK | Kamati ya Maendeleo ya Kata |
| LAT | Local Allocation Tax Grant |
| LED | Local Economic Development |
| LGRCIS | Local Government Revenue Collection Information System |
| LGRP | Local Government Reform Programme |
| LGTI | Local Government Training Institute |
| LVEMP | Lake Victoria Environmental Management Programme |
| LVFO | Lake Victoria Fisheries Organization |
| LVRLACC | Lake Victoria Region Local Authorities and Counties Cooperation |
| MIVARF | Market Infrastructure Value Addition and Rural Financing |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania |
| MMEM | Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi |
| MSM | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| MUVI | Muunganisho Ujasiriamali Vijijini |
| NGOs | Non - Governmental Organizations |
| NSSF | National Social Security Fund |
| O&OD | Opportunities and Obstacles to Development |
| OJT | On the Job Training |
| OR - TAMISEMI | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| OVOP | One Village One Product Movement |
| PICS | Purdue Improved Crop Storage |
| POS | Point of Sales |

| | |
|---|---|
| POT | Post Osaka Trainings |
| PPP | Public –Private- Partnership |
| PRF | Poverty Relief Fund |
| RAS | Regional Administrative Secretary |
| RC | Regional Commissioner |
| RCH | Reproductive and Child Health |
| RFSP | Rural Financing Support Programme |
| RHMT | Regional Health Management Team |
| RS | Regional Secretariat |
| SACCOs | Savings and Credit Cooperative Societies |
| SAP | Structural Adjustment Programme |
| SATF | Social Action Trust Fund |
| SFNE | Standard Four National Examination |
| SHIB | Social Health Insurance Benefit |
| TACRI | Tanzania Coffee Research Institute |
| TANESCO | Tanzania Electric Supply Company |
| TBS | Tanzania Bureau of Standards |
| TFDA | Tanzania Food and Drugs regulatory Agency |
| TOA | Tanzania Osaka Local Government Reform Alumni |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNESCO | United Nations Education, Science and Culture Organization |

# Dibaji

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yamelenga katika utoaji bora wa huduma wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sera za kitaifa za Tanzania. Maboresho yamekaribisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine tangu awamu ya kwanza hadi sasa. Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) iliwekwa dhahiri mwaka 1998 na utekelezaji wake ukaanza mwaka 2000. Kupitia ushirikiano huu maboresho ya Serikali za Mitaa hapa Tanzania yamefanikiwa kuleta Serikali za Mitaa za kidemokrasia, matumizi bora ya raslimali watu, kuongozeka kwa ruzuku toka hazina, kuimarika kwa utawala bora katika Serikali za Mitaa, kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi; na kwa ujumla kuongezeka kwa uhuru wa Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma.

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yametekelezwa kwa mkakati wa jumla ambao umejumuisha kujifunza jitihada za maboresho na utekelezaji wake katika nchi nyingine, Afrika na kwingineko na kuunda mkakati sahihi wa utekelezaji wake na mbinu mbadala kwa Tanzania. Tangu mwaka 2002, Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI – Wakati huo) na Serikali ya Japani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) kwa pamoja wameendesha mafunzo kuhusu ugatuaji nchini Japani kupitia mafunzo ya Osaka. Mafunzo haya yamehudhuriwa na Wakurugenzi na Watumishi wengine toka OR – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) na wadau wengine wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Mafunzo haya pia yalitolewa kwa Makatibu Tawala Wasaidizi, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na wakuu wa idara kupita mafunzo ya mikoa baada ya mafunzo ya Osaka (Reginal Post Osaka Training).

Mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa yametoa fursa kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kujifunza uzoefu wa ugatuaji madaraka wa Kijapani, kuchagua mbinu bora za ugatuaji wa Kijapani na kutekeleza mbinu hizo katika Sekretarieti za Mikoa na MSM. Hili limeibua umuhimu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa mbinu hizi bora kupitia kitabu, ili kuzifanya Sekretarieti za Mikoa na MSM kuona na kujifunza utekelezaji na siri zake humuhumu nchini.

Kitabu hiki cha Tano ni mwendelezo wa juhudi za pamoja kati ya OR – TAMISEMI na JICA kuimarisha sera ya ugatuaji wa madaraka Tanzania. Kitabu hiki kinaanza kwa kuonesha historia ya mafunzo ya Osaka na mbinu bora kama ifuatavyo; Sura ya Kwanza inaonyesha kwa ufupi Masuala mazuri yaliyoigwa toka Japani; Sura ya pili inahusu Jitihada za Jamii katika kuboresha utoaji wa huduma ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Halmashauri za Wilaya za Geita na Chato. Sura ya Tatu inahusu Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi. Sura ya Nne inahusu Ushiriki wa Jamii Katika Utoaji Huduma ambayo inawasilisha Mbinu bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Itilima, Misungwi, Musoma, Bukombe, Ngara na Ukerewe. Sura ya Mwisho inahusu Maendeleo ya Jamii Kiuchumi na inawasilisha Mbinu Bora toka Halmashauri za Wilaya za Missenyi, Ukerewe, Itilima, Tarime, Rorya na Bunda.

OR – TAMISEMI inashauri watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, MSM na wadau wote wa maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania kusoma kitabu hiki, kufahamu jitihada za ndani, kujifunza siri za mafanikio na kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao kuonesha utendaji mzuri katika mazingira ya ugatuaji wa madaraka.

**Mhandisi Mussa Iyombe**
**KATIBU MKUU**
**OR-TAMISEMI**

# Utangulizi (TOA)

Kitabu cha mbinu bora cha Tano ni matokeo ya jitihada za pamoja za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia OR – TAMISEMI na Serikali ya Japani kupitia JICA tangu mwaka 2002 kwa kuendesha mafunzo huko Osaka na mafunzo baada ya Osaka katika kila Mkoa juu ya uzoefu wa Ugatuaji Madaraka huko Japani. Mafunzo haya yalitoa fursa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, MSM na wadau mbalimbali wa maboresho hapa Tanzania kujifunza uzoefu wa Kijapani kuhusu Ugatuaji katika maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa na Usimamizi wa Raslimali Watu, Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato, Upangaji na Utoaji Huduma Shirikishi na Maendeleo ya Kiuchumi katika MSM hususan kupitia wimbi la OVOP. Masuala mazuri yaliyoigwa yametekelezwa katika Sekretariati za Mikoa na MSM nyingi kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa jamii ndani ya sera ya ugatuaji, yaani "D by D". Mbinu Bora nyingi za utekelezaji zimeonyesha mafanikio na matokeo chanya kwa jamii. Kamati ya Utendaji ya TOA imeamua kutoa Mbinu Bora ambazo zimewasilishwa kwenye toleo hili la tano. TOA itaendelea kutoa matoleo mengine ya kitabu hiki siku za mbele sambamba na utekelezaji unaondelea wa Masuala mazuri yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa.

Kukamilika kwa kitabu hiki cha Tano cha Mbinu Bora kumetokana na misaada kutoka taasisi na watu binafsi mbalimbali. TOA inapenda kutambua na kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufikia makubaliano na Serikali ya Japani, kufadhili na kuruhusu watumishi wa Tanzania kuhudhuria mafunzo ya Ugatuaji nchini Japani toka mwaka 2002 hadi sasa. Pili, TOA inaelekeza shukrani za dhati kwa Serikali ya Japani na JICA kwa kuandaa, kusaidia na kufadhili mafunzo ya Osaka na Mafunzo ya Mikoa na uzalishaji wa kitabu hiki. Aidha, TOA inapenda kutambua na kushukuru juhudi za utekelezaji wa yale yaliyojifunzwa za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa MSM na utayari wao wa kuandika Mbinu Bora kamilifu kama zinavyoonekana kwenye kitabu hiki.

Uchambuzi na uunganishi wa Mbinu Bora zilizopo kwenye kitabu hiki ulifanywa na Bwana Paulo F. Faty (Mhadhiri - Chuo Kikuu Mzumbe) na Bwana Ahmed Nassoro (Mhadhiri Msaidizi - Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo). Masuala yaliyoigwa Japani yamechambuliwa na Bwana Michiyuki Shimoda (Mshauri Mwandamizi, OR – TAMISEMI). TOA inapongeza kwa dhati mchango wao na inawashukuru sana.

TOA inapenda kuwashukuru watumishi wote wa OR – TAMISEMI, JICA na TOA kwa kushiriki katika mikutano mbalimbali iliyoboresha na kuunda kitabu hiki. Siyo rahisi kutaja wote waliochangia katika kazi hii, hata hivyo TOA inaheshimu michango yote iliyotolewa na Taasisi na Watu mbalimabali.

Mwisho, ingawa watu na Taasisi nyingi zimechangia katika kitabu hiki, TOA na timu ya uchambuaji wanawajibika kwa makosa na mapungufu yanayoweza kuhisiwa na wasomaji wa kitabu hiki.

-----------------------------------------------------

**MUSSA NATTY**
**MWENYEKITI WA TOA**

# Utangulizi (JICA)

Wasomaji Wapendwa!

Utekelezaji wa sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) umechukua zaidi ya miaka 10 sasa ukiwa na lengo la kuboresha huduma kwa kugatua shughuli, majukumu na raslimali toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Kutokana na ukweli huu hapo juu Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) limejikita katika kusaidia utekelezaji wa sera hii hasa katika kuimarisha utoaji huduma katika ngazi za msingi kwa kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na maendeleo ya sekta za afya, kilimo, maji na barabara.

Toka mwaka 2002, JICA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) imekuwa ikiendesha mafunzo kuhusu maboresho katika Serikali za Mitaa yanayoitwa "Mafunzo ya Osaka". Mafunzo haya yalilenga Maofisa wa juu wa Menejimenti katika maboresho ya Serikali za Mitaa, yaani Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa MSM, Maofisa wa OR – TAMISEMI na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa malengo ya kujifunza uzoefu wa Kijapani katika maboresho ya Serikali za Mitaa. Katika kurudi kwao, waliwasilisha na kujadiliana uelewa na uzoefu walioupata kwenye warsha za mafunzo za mikoa (2003 – 2007). Matokeo yake Umoja wa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa MSM (TOA) ulianzishwa ili kuwa na jukwaa ambalo wajumbe wa TOA wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu, mbinu bora na changamoto zilizopo. JICA imekuwa ikisaidia uimarishaji wa taasisi ya TOA.

Kutokana na utekelezaji wa Masuala yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka, mbinu bora nyingi ziliwasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika warsha za Mikoa zilizofanyika katika kanda sita mwaka 2011/12 na 2013 - 2017. Baada ya uhakiki na uchambuzi wa mbinu hizi bora, toleo la kwanza, la pili, la tatu, la nne na hili la tano la "kitabu cha mbinu bora" hatimaye limetoka. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa ***"tunatakiwa kujifunza siyo tu kutoka nchi nyingine bali katika jitihada nyingi zilizopo ndani ya nchi".***

Nitafurahi kama mtajifunza vipengele muhimu kutoka kitabu hiki na kuchukua hatua ndogo lakini za uhakika ili kuboresha utendaji katika eneo husika.

JICA ina mpango wa kuisaidia TOA kuendesha mafunzo ya watumishi waandamizi wa Sekretarieti za Mikoa na MSM katika Mikoa yote kwa kutumia vitabu hivi. Tungependa kufuatilia na kujua mbinu bora zitakazofuata zilizotokana na kitabu hiki na mafunzo yake. Tunatarajia kuanzisha jukwaa la kujifunza wenyewe kwa wenyewe (Horizontal Learning) katika ngazi za Msingi.

**Toshio Nagase**
***Mwakilishi Mkuu – Ofisi ya JICA Tanzania***

# Sura ya Kwanza: Utangulizi; Masuala Yaliyoigwa Kutokana na Uzoefu wa Japani

## 1.0 MAFUNZO YA OSAKA

Kitabu hiki kimeandaliwa na Umoja wa Washiriki wa Mafunzo ya Osaka kuhusu Serikali za Mitaa wanatoka Tanzania (TOA). TOA ni Umoja wa washiriki wa kozi inayotolewa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Mafunzo yenyewe yanaitwa "Mafunzo yenye Mrengo wa Nchi – Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania", lakini yajulikanayo sana kama "Mafunzo ya Osaka". Umoja una wanachama ambao ni Makatibu Tawala wote wa Sekretarieti za Mikoa na Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini.

Mafunzo ya Osaka yalianza mwaka 2002. Kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, Makatibu Tawala wote kutoka Mikoa 21 (kipindi hicho) pamoja na Wakurugenzi wa Halmahauri wawili kutoka kila Mkoa walihudhuria. Pia maofisa wa juu toka OWM – TAMISEMI (wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi)[1], Katibu Mkuu wa ALAT na baadhi ya wanataaluma mashuhuri walihudhuria kozi hii.

Kutokana na mafanikio na matokeo dhahiri, JICA iliamua kuendelea na mpango huu, kwa kupanua wigo wake kwa kuongeza nchi nyingine tatu za kiafrika ambazo zilikuwa zikipanga maboresho ya ugatuaji, yaani Kenya, Uganda na Zambia, pamoja na Tanzania. Mpaka leo zaidi ya viongozi 100 wa maboresho wanaojumuisha Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wamefaidika moja kwa moja na mafunzo ya Osaka. Pia washiriki hawa waliporudi katika mikoa yao waliendesha warsha za ndani zijulikanazo kama "mafunzo ya Post Osaka" ili kubadilishana uzoefu na uelewa walioupata Osaka kwa kuwaalika Wakurugenzi waliobaki pamoja na wakuu wa idara. Hivyo wafaidika wa mafunzo haya waliongezeka mpaka kufikia zaidi ya 1,500, ingawa uanachama wa TOA ulibakia kuwa wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Kutoka katika Masuala mbalimbali yaliyoigwa Osaka na mafunzo ya Post Osaka, Halmashauri zilizohudhuria ziliandaa mipango kazi ya kuboresha utendaji wao. Kukiwa na zaidi ya miaka 10 ya utendaji, imethibitishwa kuwa kuna idadi kubwa ya mbinu bora zinajitokeza katika Halmashauri nyingi kwa kutekeleza ile mipango kazi ambayo ni vyema kuwashirikisha wengine. Kwa hiyo TOA iliamua kuhakiki na kuchambua kesi hizo za mbinu bora na kutengeneza kitabu hiki, ili viongozi wa Halmashauri waweze kuzirejea kesi hizi na kuzitumia pale wanapoona zinafaa na zina tija, katika kuboresha kazi zao.

[1] Pamoja na Makatibu wakuu wawili wa Zamani wa OWM-TAMISEMI, yaani, MS. Tarishi M.K. na Bwana H.A. Katanga

Kabla ya kuingia kwenye kesi zenyewe za mbinu bora, ni vyema katika sura hii tukaangalia kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya kwa viongozi wa maboresho wa kitanzania, nini ilikuwa maana ya mafunzo ya Osaka kwa Tanzania na Masuala gani yalijadiliwa kwenye mafunzo haya.

## 2.0 HISTORIA YA MAFUNZO YA OSAKA

Kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya? Na yalikuwa na maana gani kwa Tanzania?

### 2.1 Maoni ya JICA Kuhusu Msaada kwenye Ugatuaji

JICA ina maoni ya kipekee kuhusu misaada kwenye utawala ambayo yanaweza kutofautiana na maoni ya washirika wengine wa maendeleo. JICA imeshuhudia programu kubwa kubwa za maboresho zikifanywa katika nchi zinazoendelea na washirika wa maendeleo kama Programu wa kurekibisha Miundo ya Uchumi (SAPs) na maboresho ya utawala ikiwa ni pamoja na Ugatuaji wa madaraka. Inaweza kusemwa kuwa programu hizi na maboresho haya yaliyofanywa katika nchi zinazoendelea ni sawa kabisa na yale yanayojaribiwa sasa katika nchi zilizoendelea bila kujali tofauti iliyopo ya kihistoria na mazingira kati ya nchi hizi. Pia mara kwa mara inajidhihirisha kuwa maboresho haya yanatekelezwa kwa msukumo mkubwa toka kwa wafadhili, bila kuzingatia asili ya mchakato wa maendeleo na umiliki wa nchi husika.

Kutokana na machungu ya kushindwa kufikia malengo katika ushirikiano wa kimataifa wa aina hii, JICA imekuwa na msimamo ufuatazo katika kusaidia ugatuaji.

(i) Hakuna mfumo wowote unaoweza kutumika katika nchi zote.

(ii) Ugatuaji wenyewe siyo lengo bali ni njia ya kufikia lengo fulani.

(iii) Kuasilisha na kukuza mfumo ndani ya nchi kupitia majadiliano ya kitaifa ni muhimu.

(iv) Jinsi gani ya kuhakikisha viwango vya chini vya kitaifa vya huduma[2] vinafikiwa ni muhimu katika kuandaa maboresho ya Ugatuaji.

(v) Maboresho ya Ugatuaji ni mchakato mrefu, ambao hautakiwi kuchukuliwa kama Mradi au Programu tu.

(vi) Maboresho ya Ugatuaji ya haraka haraka yanaweza kuleta fujo. Katika kila maboresho ya Ugatuaji (d by d), ni lazima kuhakikisha kuna mazingira sahihi kwa upande wa Halmashauri na wanajamii kupokea majukumu makubwa yanayogatuliwa.

### 2.0 Changamoto Kubwa Iliyogunduliwa katika Programu ya Tanzania ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na Ujumbe wa Maandalizi ya Mafunzo wa Mwaka 2002

Baada ya maombi ya Serikali ya Tanzania kuhusu kuwepo kwa Mpango wa mafunzo wa maboresho katika serikali za mitaa mwaka 2001, JICA iliamua kutuma ujumbe kwenda kuchambua hali ilivyo ili kuunda kozi ya mafunzo yenye maudhui ya kumaliza Masuala muhimu. Ujumbe ule ulipofika Tanzania, Novemba mwaka 2002, uligundua kuwa Programu ya maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania ilikuwa na changamoto zifuatazo;

[2] Viwango vya chini vya kitaifa vya huduma ni nadharia kuwa kiwango fulani cha huduma lazima kifikiwe hata kama ni katika jamii maskini vijijini sawa na kwenye miji mikubwa.

(i) Jedwali kubwa na lenye hatua nyingi za utekelezaji (Zaidi ya kurasa 80)

(ii) Programu ya maboresho ilikuwa ukitekelezwa kwa jedwali zuri sana lakini halikuruhusu maboresho/mabadiliko zaidi. Ujumbe uliona kulikuwa na nafasi ndogo sana iliyoachwa ya kuweza kubadili lolote ili kuruhusu majaribio ya suala ambalo ni muhimu. Ujumbe uliona kuwa kila kitu kimeshadhamiriwa, na Serikali ya Tanzania ililazimika kufuata reli hiyo bila kwenda pembeni au kurudi vyuma.

(iii) Programu iliandaliwa kwa msaada mkubwa kutoka kundi la wafadhili.

(iv) Wafadhili wa kawaida waliopo kwenye mfuko "Basket funding" waliunda kamati ya msukumo pamoja na serikali. Kuandikwa kwa Programu yenyewe kulifanywa na wataalamu washauri wa nje na hata utekelezaji wenyewe. Ujumbe ulihofia kuwa Programu ya maboresho iliandaliwa bila kupitia mchakato stahiki wa kujenga uelewa ndani ya nchi na kupata makubaliano yanayohusu mahitaji ya mabadiliko.

(v) Hatari ya kukimbilia kwa haraka Ugatuaji wa Madaraka (D by D).

Sera ya ugatuaji (D by D) iliyokuwa ikihamasishwa na Serikali ilidhihirika kwenye ujumbe huo kuwa ni kama vile Tanzania ilikuwa inatekeleza ugatuaji wa madaraka sawa na ule wa nchi zilizoendelea. Swali likawa; Je ni kweli uwezo na mtazamo wa Halmashauri na Wizara zote ulikuwa tayari kwa mabadiliko haya ya haraka? Ujumbe huu uliaona changamoto zifuatazo katika hili;

- Upinzani kutoka Wizara za kisekta
- Ukosefu wa majadiliano ya kina kuhusu ugatuaji katika jamii
- Hakukuwa na uwezo kamilifu kwa upande wa Halmashauri kuchukua majukumu yote yaliyogatuliwa

**2.3 Uwezekano wa Umuhimu wa Uzoefu toka Japani katika Ujenzi wa Taifa na Maboresho ya Ugatuaji - Ujumbe kutoka Japan kwenda Tanzania kupitia Mafunzo ya Osaka.**

Baada ya kuona hali halisi ya Tanzania iliyoelezewa hapo juu, JICA iliamua kuwa uzoefu wa Japani kwenye ujenzi wa Taifa na Maboresho yaliyokuwa na mchakato wa muda mrefu ya Ugatuaji ungeweza kuwa unastahili na muhimu kwa viongozi wa maboresho wa Tanzania kujifunza na kupitia upya maboresho yao.

Japani ni nchi ndogo huko Bara la Asia isiyo na ustaarabu wa Magharibi, ambayo ilianza ujenzi wa taifa kama nchi iliyo nyuma kabisa lakini ikafikia maendeleo ya ajabu. Japani ina uzoefu mwingi wa aina yake wa kutumia mifano (models) ya nje (mfano wa Magharibi) ambayo wafadhili wengine hawana. (Mataifa ya Ulaya yamekuwa mara zote mstari wa mbele na katikati ya dunia na hujiona hayana sababu ya kujifunza toka nje). Kwa kweli, Japani ilianza Ujenzi wa taifa na maendeleo, kwa kujaribu kuiga mifano ya Magharibi lakini ikashindikana mwanzoni kabisa. Tokea hapo ikawa ni mchakato mrefu wa kujaribu na kushindwa mpaka hatimaye ilipofikia Japani ikaunda mfumo wake wa kipekee unaoitwa "Nusu kijapani nusu Magharibi". Japani inaamini kuwa aina hii ya uanzishaji wa mfumo, pamoja na umiliki wake

thabiti kupitia kujaribu na kushindwa mara nyingi ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya nchi.

Mchakato huu ambao Japan ilitumia ili kuanzisha mfumo wake wa serikali za mitaa na maboresho ya Ugatuaji ni tofauti kabisa na mifano ya Ulaya ambayo nchi zinazoendelea zinajaribu kuanzisha kwa sasa. JICA ilifikiri kuwa kuwasilisha "mfumo huu tofauti" unaweza kuwa muhimu, kwani kuwa na mfano mmoja tu, inaonekana kama vile "ndio njia pekee" hakuna nyingine. Lakini kukiwa na mifano zaidi ya miwili, wanaweza wakaanza kulinganisha na kuona ni mfano upi unafaa zaidi katika mazingira yao, na ni hatua ipi iwe ya kwanza katika kuandaa mfumo wao wenyewe.

Ifuatayo ni mifano tu ya kuvutia ya vigezo vinavyoweza kuigwa toka mfumo wa kijapani kati ya mengi yaliyopo;

**(1) Mchakato wa Maboresho wa Polepole Sana Lakini wa Uhakika**

Japani ilitumia miaka 110 toka ilipoanza kuunda mfumo wa Serikali za Mitaa na Ugatuaji; ingawa tunahesabu miaka 55 ya Maboresho Makuu baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia hadi kufika ugatuaji halisi (D by D) mwaka 2000. Serikali ilijaribu kuhakikisha kuwa Halmashauri zimeshajengewa uwezo wa kutosha kabla ya kugatua majukumu, na siyo kukimbilia kurekebisha taasisi za Ugatuaji (D by D). Uzoefu huu wa Japani unaipa Tanzania fursa ya kufikiria mara mbili kama mwendo wa maboresho siyo kasi sana, na kama nchi inataka kuendelea na mwendo kasi uliopo, basi haina budi kuhakikisha kuna ujenzi wa uwezo stahiki kwa upande wa Serikali za Mitaa.

**(2) Ukasimishaji wa Shughuli/Majukumu kwa Wakala (Agency Delegated Functions)**

Katika kipindi tajwa cha miaka 55, serikali ilichagua mfumo wa "kukasimu" unaoitwa ADF kama hatua ya mpito, badala ya kurukia Ugatuaji moja kwa moja. Kwa sababu ya mfumo huu Japani ilipingwa sana na nchi za Magharibi kwa kipindi kirefu kuwa haijafanya Ugatuaji sahihi, na mwishoni kabisa Serikali ikaamua kuingia katika Ugatuaji halisi mwaka 2000 na kuondokana na mfumo wa kukasimu (ADF). Hata hivyo sasa hivi imethibitika kuwa ADF ilichangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mfumo mzuri wa Serikali za Mitaa na kupelekea kufikiwa kwa ugatuaji halisi (D by D) nchini Japani; hasa katika vipengele vifuatavyo;

- Shukrani kwa ADF, Halmashauri zilifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara husika, na zikaweza kujenga uwezo wao kupitia mafunzo kazini (on the job training) kukiwa na usaidizi wa kitaalamu wa karibu toka wizarani. Kila walipopata changamoto, maofisa wa Serikali za Mitaa waliweza kuwasiliana na maofisa wa wizara husika kwa simu na maofisa wa wizara waliweza kusaidia kwa wema na kumaliza changamoto hizo pamoja. Haya yote yaliwezekana kwa sababu kimsingi shughuli zote zilikuwa ni wajibu wa Wizara na zilikasimishwa tu kwa Halmashauri. Hivyo hakukuwa na upinzani wowote toka wizarani, zaidi ya ushirikiano ilipofikia Ugatuaji wa shughuli; kinyume kabisa na yanayotokea katika nchi zinzoendelea zinapotekeleza ugatuaji.

- Hoja ya msingi ilikuwa ni kuhakikisha kuwa raslimali ambazo ni chache zilizopo ndani ya nchi zinaweza kutumika vizuri zaidi kuelekea upande mmoja yaani maendeleo ya nchi, badala ya kuzigawa na kutengeneza tofauti kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.
- Ilikuwa ni muhimu sana katika hatua za mwanzo ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na uwezo dhaifu. Bila mfumo wa kukasimu (ADF) kipindi hicho Halmashauri zisingeweza kufanya vizuri shughuli zao za kuhudumia watu wala uwezo wao usingejengeka.
- Sababu nyingine muhimu ilikuwa mafunzo kazini (OJT). Shukrani kwa mchakato wa mafunzo kazini (OJT), kwa miaka 55, watumishi wote wa Serikali za Mitaa pamoja na muundo wao kwa ujumla walijenga uwezo thabiti, kwa kupokea ufahamu na utaalamu kutoka wizarani, na kuwa tayari Serikali Kuu ilipoamua kugatua madaraka (D by D).

Uzoefu huu wa Japan unaleta swali moja la msingi kwa Tanzania juu ya namna gani nchi inaweza kujithibitishia uhakika na ubora wa mchakato wa kuzijengea uwezo Halmashauri ilihali Ugatuaji (D by D) ukiendelea; kuhakikisha matumizi mazuri ya raslimali chache zilizopo nchini na kukwepa kabisa upinzani toka Wizara za kisekta.

**(3) Mfumo wa Kubadilishana Watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa**

Nchini Japani, kipindi cha hatua za mwanzo za maboresho, mtindo wa kubadilishana watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ulitumika sana kama mbinu bora kabisa ya (a) kujaza upungufu wa watumishi hasa wenye sifa katika Halmashauri za pembezoni na (b) kuhakikisha uhamishaji wa ujuzi na utaalamu kutoka kwa wasomi wa Wizara kwenda kwa watumishi wa Halmashauri waliokuwa na ujuzi na uzoefu mdogo ili kujenga uwezo wa Halmshauri hizo.

Serikali iliunda jopo kubwa la maofisa wataalamu katika wizara ya Serikali za Mitaa na kuwapeleka kwenda kwenye Halmashauri zilizokuwa na uwezo mdogo huko pembezoni ili kuzisaidia. Hatua hii ya uhamisho wa muda ilidumu kwa muda wa miaka 4 - 5 na baadaya watumishi hawa walirudishwa kwenye nafasi zao za kawaida kwenye wizara zao. Kadri walivyokuwa na uwezo wa kitaalamu kuwezesha wengine ndivyo walivyopelekwa kwenye Halmashauri za mbali na zenye udhaifu mkubwa. Pale walipofaulu na kutenda vizuri katika vituo hivi vipya, waliahidiwa kupanda vyeo zaidi wanaporudi, ambayo iliwapa motisha wataalamu hawa waliobobea kwenda kwenye sehemu zisizovutia kwa hamasa ya juu kabisa. Pia Halmashauri nyingi zilipeleka watumishi wao kwenye wizara mbalimbali kufanya kazi, katika misingi ya mafunzo kazini kwenye maeneo ambayo Halmashauri husika ilihitaji.

Baada ya kurudia mizunguko kadhaa ya kubadilishana watumishi, ujuzi na utaalamu wa kutosha ulihamishwa kikamilifu toka Wizara kwenda Halmashauri, kitu ambacho kilisaidia sana kujenga uwezo wa Halmshauri nchini Japanni. Sasa Halmashauri zinajitegemea katika raslimali watu bila kuitegemea Serikali Kuu tena.

Nidhahiri kuwa ugatuaji wa raslimali watu ukifanyika kwa ukamilifu wake bila kuwa na mbinu za kutatua matatizo, hupelekea upungufu mkubwa wa watumishi kwenye

Halmashauri ambazo zipo katika maeneo maskini na pembezoni. Ni kwa sababu hii Tanzania iliamua kurudisha Masuala ya raslimali watu kwa sehemu kubwa Serikali Kuu. Hata hivyo haina mantiki kuendeleza Ugatuaji wa madaraka (D by D) bila Ugatuaji halisi wa raslimali watu. Badala ya "0 au 100", serikali inatakiwa kutafuta mkakati wa namna ya kugatua raslimali watu na wakati huohuo kukwepa kutengeneza upungufu katika maeneo ya vijijini, na kujiridhisha kuwa kuna mchakato wa kujenga uwezo wa baadaye wa Halmashauri.

## 3.0 MASUALA YALIYOJITOKEZA NA KUJADILIWA WAKATI WA MAFUNZO YA OSAKA

Kutokana na upungufu wa nafasi Masuala machache tu ya msingi yameweza kuwasilishwa kwenye sehemu hiyo hapo juu, kati ya mambo mengi yanayotokana na uzoefu wa Japani ambayo Tanzania imepewa. Hapa vipengele vingine vitatajwa na kuelezewa kwa kifupi.

### 3.1 Masuala ya Jumla

Masuala na Maswali yafuatayo yalijitokeza na kujadiliwa wakati wa mafunzo ya Osaka:

**(1) Umuhimu wa kukuza uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama kigezo cha mafanikio ya Ugatuaji wenyewe**

- Je hakuna hatari ya kudidimiza utoaji huduma, kugatua wajibu mkubwa kiasi hiki ndani ya muda mfupi?
- Ni namna gani ya kukabiliana na hali halisi kuwa Halmashauri zinahitaji uwezo zaidi ili kutekeleza shughuli zilizogatuliwa?
  - Vipi kuhusu ajira? Namna gani itawezekana kupata watumishi wenye sifa katika Halmashauri zilizopo kwenye maeneo maskini na pembezoni?
  - Ni jinsi gani ya kuziba pengo kati ya ujuzi na utaalamu katika Serikali za Mitaa na kuziendeleza? Je siyo muhimu kwanza kuweka mbinu za kuhamisha ujuzi na utaalamu, pamoja na usaidizi wa kitaalamu kutoka serikali kuu kwenda Halmshauri? Siyo muhimu kwanza kuimarisha mahusiano ya ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Halmashauri badala ya kutegemea misaada toka nje?

**(2) Ugatuaji na Maendeleo**

- Ili kuweza kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi na kwa raslimali chache zilizopo, ni muhimu kutafuta mbinu mkakati ya kuzitumia raslimali hizi (hivi ndivyo ambavyo Japani imekuwa ikifanya kujiletea maendeleo yake)
- Namna gani unaweza kusimamia maendeleo ya nchi na ugatuaji kwa pamoja wakati mara kadhaa hupingana? Unawezaje kujiridhisha kuwa hakutakuwa na utengano wa raslimali na tofauti (kutokuelewana) kati ya Serikali Kuu na Halmashauri au kati ya Halmashauri zenyewe?

**(3) Ugatuaji na Viwango vya chini vya kitaifa**

- Jinsi gani ya kusimamia ugatuaji na kuzingatia viwango vya chini vya kitaifa? Ni jinsi gani itahakikishwa kuwa Halmshauri zilizopo vijijini zitakuwa na uwezo wa kutosha kama zilivyo zile tajiri katika kigezo cha utoaji huduma kwa watu? (uwezo wa watumishi na fedha).

**(4) Ukweli Kuhusu Uwezo wa Halmashauri kuweza Kutoa Huduma**

- Swali liliulizwa; Ni Maofisa Ugani wangapi waliopo katika Halmashauri ukijumuisha na wale ambao wanatumikia katika kata na vijiji? Swali hili liliulizwa kwa washiriki ili kuwafanya waelewe hali ilivyo mbaya ambayo Halmashauri za Tanzania zinatakiwa kukabiliana nayo. Ukichukua Mkoa mmoja kama mfano, Mkoa wa Nagano nchini Japani, ni mkoa mdogo kabisa ulioko maeneo ya vijijini lakini una maofisa ugani wa kilimo wapatao 1500. Pia kuna Halmshauri 77 za ngazi za chini katika Mkoa huu ambazo kila moja inaajiri maofisa ugani kati ya 20 – 30. Maana yake kuwa wakulima katika Mkoa (prefecture)[3] wa Nagano wanafurahia huduma zinazotolewa na zaidi ya maofisa ugani 3,000 wa Halmshauri ikilinganishwa na wakulima wa Tanzania ambao wana maofisa ugani wasiozidi 100[4]. Pia nchini Japani kuna mashirika mengi ya binafsi yanayouza mashine za kilimo, mbolea, madawa, mbegu n.k pamoja na taasisi za ushirika zilizo imara; zote hizi hutoa huduma mbalimbali za ugani na ushauri wa kitaalamu.
- Ni vyema kutambua hali ngumu iliyoelezewa hapo juu na kuanzisha mkakati mpya. Hatutakiwi kuota ndoto kwamba Tanzania inaweza kufikia kutoa huduma nzuri kama za nchi zilizoendelea kwa idadi ndogo hivi ya watumishi kwenye eneo lote hata kama Serikali Kuu itaamuwa kufanya kila kitu peke yake.

**(5) Umuhimu wa Juhudi za Wananchi na Ushirikiano kati ya Halmashauri na Jamii**

- Kutokana na Ukweli ulioongelewa hapo juu, haikwepeki kutumia kwa kiasi kikubwa Uwezo wa watu na Juhudi za kujitegemea ili kutoa huduma zilizo bora.
- Ni imani ya JICA kuwa kama watu wataongozwa na kuwezeshwa vizuri, wana uwezo wa kufanya mambo mengi wenyewe, kama kujenga shule za msingi, zahanati, barabara zao na kuzitunza.
- Kwa Japani pia, kipindi cha hatua za mwanzo za Maendeleo, Serikali haikuwa na uwezo wa kujenga shule za msingi. Kwa mfano, ilikuwa ni watu katika jamii zao waliochangia kutoka mifukoni mwao na wakafanya kazi pamoja kujenga na zaidi wakatafuta watu

---

[3] Mkoa (prefecture) huko Japani ni karibu sawa na wilaya za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. (Ingawa Wilaya nyingine za Tanzania ni kubwa sana kuliko Mikoa ya Kijapani).

[4] Pia si kwamba Japani ina hali nzuri katika maana hii. Kinyume chake, Japani ni nchi ambayo ina idadi ndogo kabisa ya watumishi kwa idadi ya watu waliopo ikilinganishwa na nchi zilizoendelea. Maana yake ni kuwa Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia n.k wana watumishi wengi zaidi wa serikali.

wanaoweza kufundisha na wakawalipa mishahara yao. Ndiyo maana shule nyingi za kipindi hicho hazikuwa za "umma" bali "binafsi", kwa maana ya "shule zinazomilikiwa na jamii; ilikuwa ni baada ya miongo kadhaa, serikali ilipotajirika na ikaanza kuzimiliki na hatimaye kuwa shule za umma.

- Inahitaji mabadiliko ya mtazamo wa Serikali na Watu, kutoka fikra kuwa ni jukumu la Serikali kutoa huduma zote kwa watu kuelekea mtazamo kuwa watu wanaweza kufanya mengi sana kwa juhudi zao wenyewe na serikali ikawezesha tu mchakato huo badala ya Serikali kutekeleza peke yake.

**(6) Umuhimu wa Kuainisha Ukubwa Sahihi wa Sehemu za Serikali za Mitaa; na Kuunda Mbinu Mpya za Kuzifikia Jamii kutoka makao makuu ya Halmashauri**

- Kutokana na vigezo hivyo hapo juu ni lazima kuunda mbinu imara sana za Halmashauri kuzifikia jamii. Hapa Tanzania, Halmashauri za Wilaya ni kubwa mno, hivyo ni muhimu kufikiria jinsi ya kujenga daraja kati ya Halmashauri na jamii.
- Kutoka kwenye wazo la kukuza mtazamo wa watu kuwa na uhuru wao, eneo la Halmashauri linatakiwa kuwa dogo sana ili watu waweze kuona kuwa sehemu hiyo kweli ni yao. Kwa upande mwingine sehemu hii ndogo ya Serikali za Mitaa inatakiwa iwe na uimara wa kutosha kutoa huduma za kutosha ambayo inahitaji kiasi cha raslimali fedha na watu. Haya ni mahitaji muhimu mawili yanayopingana.
- Kuweza kutoa majibu kwa swali hili hapa juu linalojipanga lenyewe, sahihisho lililopo ni kuwa na mfumo wenye ngazi nyingi kutoka Halmashauri hadi jamii. Kwa Japani mfumo huu wa ngazi nyingi unafanya kazi vizuri. Lakini Tanzania pia ina mfumo mzuri wenye wilaya – kata – kijiji – kitongoji. Hii inasaidia sana kukuza uhuru wa jamii na jitihada shirikishi za maendeleo kati ya Halmashauri na jamii. Zaidi ya hayo, Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii (O&OD) unaweza kuwa jukwaa zuri zaidi la kuboresha mfumo huu na kuuwezesha kufanya kazi vizuri zaidi.

### 3.2 Usimamizi na Ugatuaji wa Raslimali Watu

Kama ilivyo kwenye sehemu iliyotangulia, mafunzo ya Osaka yalitoa tahadhari kwa Viongozi wa Tanzania katika miaka michache ya mwanzo kuwa waangalifu kuhusu kutoharakisha kugatua na kupeleka madaraka maarufu kama *D-by-D*. Hata hivyo, kuhusu ugatuaji wa masuala ya rasilimali watu, ujumbe ulikuwa tofauti kidogo kwa vile ilionekana kwamba madaraka haya yalikwisha anza kurudishwa Serikal Kuu; kwani uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmasahuri na Wakuu wa Idara unafanywa na Wizara pamoja na kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira ili kuendesha mchakato wa ajira kwa kada nyingine za watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Nchi ya Japani haikugatua madaraka na kuyapeleka Halamashauri kwa haraka, bali Serikali Kuu ilendelea kuhodhi baadhi ya shughuli. Kwa mantiki hii, ugatuaji nchini Japani haukuwa umekamilika kwa miaka mingi mpaka ilipofika mwaka 2000. Hata hivyo, kuhusiana na kugatua

masuala ya usimamizi wa rasilimali watu, Japan ilihakikisha kwamba madaraka haya yamegatuliwa na kupelekwa Halmashauri kikamilifu tangu mwanzo kabisa wa maboresho.

Hii ni kwa sababu kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu ndiyo jambo la muhimu sana na msingi wa ugatuaji. Kulingana na mfumo wa Serikali za Mitaa Japani, masuala yote huamuliwa na kutekelezwa ndani ya Mamlaka za Serikali Mitaa husika bila kuingiliwa na Serikali Kuu, yaani kuajiri na kufukuza, kuendesha mafunzo, kupanga ngazi za mishahara, kufanya uhamisho, kupandisha vyeo , mpaka kustaafu. Mamlaka za Serikali za Mitaa Japani huajiri wahitimu wapya kutoka vyuo vikuu kila inapofika mwezi Aprili kulingana na mahitaji yao. Wahitimu walioajiriwa na Mamlaka fulani ya Serikali za Mitaa, wataitumikia Mamlaka husika kwa maisha yao yote mpaka watakapostaafu. Hakuna kanuni ya uhamisho kutoka Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa kwenda mamlaka nyingine.

Zaidi ya hayo, Wenyeviti au Mameya ni wanasiasa na huchaguliwa na wananchi kwa njia ya kura, na ndio wakuu wa Tawi la Utawala/Utendaji sambamba na Tawi la Baraza la Madiwani la Halmashauri husika. Watendaji wanawajibika kwa Meya/Mwenyekiti na siyo kwa Madiwani, kwa hiyo masuala ya watendaji hulindwa na huwakilishwa na Meya/Mwenyekiti katika Baraza la Madiwani.

Kwenye mafunzo ya Osaka, mambo matatu yafuatayo yalitiliwa mkazo kwamba ndivyo vitu muhimu katika kufikia uwezo wa juu wa rasilimali watu katika Halmashauri:

1) <u>Kuajiri</u>
   Kuajiri watumishi <u>wenye sifa kuliko wote na wanaofaa katika kufikia dhima/malengo</u> ya mamlaka husika; na
2) <u>Mafunzo</u>
   Baada ya kuajiri, <u>kuwapa mafunzo</u> yanayolenga na kuwezesha kufikiwa kwa <u>dhima/malengo</u> ya mamlaka husika (siyo malengo ya mtu binafsi); na
3) <u>Kujipanga</u>
   Kuhakikisha kuwa <u>uwezo wote wa Raslimali watu katika Halmashauri unatumika kikamilifu</u> ili kutimiza malengo ya mamlaka husika

Kwa minajili hiyo, Japani iliona kuwa ni jambo lisilokwepeka kutangulia kugatua madaraka yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu ili kila Halmashauri iweze kuchambua hali halisi, kupanga mipango, kuajiri, kutoa mafunzo, kupanga majukumu na kudhibiti watumishi. Mtumishi wa Halmashauri lazima awe mtu anayelipenda eneo husika na watu waliopo, anayefanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watu, anayeelewa vizuri kuhusu hali ya eneo husika, anayewafahamu watu vizuri na kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa karibu na wakazi wa eneo husika; hii ndiyo mantiki ya ugatuaji. Ni uzoefu wa nchi ya Japani kwamba, kwenye Halmashauri zenye mafanikio ya kuridhisha, kuna maofisa na watendaji wanaofanya kazi kwa kujituma hasa katika kuwahudumia watu, na kushirikiana na wakazi; na walio wengi wao ni wale watendaji waliozaliwa na kukulia katika maeneo hayo na wanayapenda makazi hayo, pamoja na uongozi thabiti wa Meya/Mwenyekiti ambaye naye ni mzawa.

Jambo jingine muhimu linalozifanya Halmashauri za Japani ziwe na nguvu ni juhudi waliyonayo katika kuwapa watumishi wao mafunzo. Halmashauri za Japani zinawekeza sana kwa watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo pamoja na mpango wa mafunzo kazini ambao uko kimkakati kulingana na mahitaji ya kitaasisi (siyo mahitaji binafsi) na kwa mtazamo wa mbali.

Hili linawezekana kule Japani kwa sababu hakuna uhamisho wa watumishi toka Halmashauri moja kwenda nyingine ya na kiwango cha kubakiza/kushikilia watumishi kazini ni kikubwa sana, hivyo Halmashauri huwekeza bila hofu kwamba baada ya kuwasomesha watakimbia.

Kinyume chake, Tanzania kuna uhamisho wa mara kwa mara wa watumishi muhimu kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine na hivyo ni vigumu sana kuwabakiza/kuwashikilia watumishi kwenye Halmashauri moja. Katika hali kama hii, changamoto kubwa ni jinsi ya kuhakikisha kwamba matokeo yatokanayo na mafunzo ya watumishi yanabaki ili yalete maboresho katika utendaji kazi wa mamlaka husika, na kuzifanya Halmashauri ziwe na bidii katika kujenga uwezo wa watumishi licha ya uwezekano mkubwa wa kuwapoteza baada ya kuwasomesha. Swali moja liliulizwa kwenye mafunzo ya Osaka kama Tanzania inaweza kuandaa na kutekeleza mpango mkakati na thabiti wa muda mrefu wa mafunzo ya kuwajengea watumishi wake uwezo katika hali hii.

Kwa upande mwingine, mafunzo ya Osaka yaliibua suala la "kufanya kazi kama timu" ili kuweza kutumia asilimia 120 ya uwezo wa nguvu kazi iliyopo na kuyafikia malengo ya kitaasisi. Kule Japani, kuna mambo kadhaa kuhusu mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu ambayo yamefafanuliwa kwa uangalifu mkubwa kwa ajili hiyo, kama vile:

1) Ngazi za mishahara zimewekwa makusudi kwa lengo la kuondokana na rushwa na kuchochea watumishi wafanye kazi kwa bidii hadi watakapostaafu;
2) Mfumo wa kipekee wa Japani "kuchelewesha upandishaji vyeo" ili kumfanya kila mtu afanye kazi kwa bidii kwa miaka mingi kabla ya kupandishwa cheo (kukamua asilimia 120 ya uwezo wa kila mmoja);
3) Watumishi kufanya kazi kwa kuzunguka kila idara ya Halmashauri husika na mtindo wa kuweka kumbukumbu za kila mwaka za utendaji wa kila mtumishi ili kufanya za tathimini kwa haki na kwa malengo na kuchagua wale wenye uwezo mkubwa na wanaostahili kupandishwa vyeo kuwa Wakurugenzi;
4) Shughuli zote zinazohusu rasilimali watu ziko chini ya Idara ya Uendelezaji Rasilimali Watu ili iwezeshe namba 3) hapo juu;
5) Mazingira ya kipekee ya Japani yanawezesha "utendaji kazi kama timu", usimamizi unaofanywa na wakuu/viongozi, na mafunzo kazini yanayoendeshwa na wasimamizi, mtindo unaojulikana kama mtindo wa "chumba kikubwa" yaani ofisi ya wazi mithili ya ofisi za benki.


Yote yaliyoelezwa kwenye sehemu hiyo hapo juu yamewekwa na kanuni zinazotawala Mamlaka za SM za Japani ili kuhakikisha mambo matatu yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu yanazingatiwa mfano 1) Kuajiri; 2) Mafunzo; na 3) Kushughulika kwa bidii. Swali liliulizwa, katika mazingira ya sasa ya Halmashauri za Tanzania, ni kwa jinsi gani zinaweza kutekeleza mambo haya matatu.

### 3.3 Fedha za Serikali za Mitaa na Ugatuaji wa Masuala ya Fedha

**a) <u>Misingi ya kifedha katika Halmashauri</u>**

Michoro (1) na (2) inaonyesha japo kwa ufupi hali ya Halmashauri za Japani kuhusu masuala ya fedha.

Mchoro (1) unaonyesha ukubwa wa majukumu ya Halmashauri katika matumizi ya kutoa huduma ndani ya kila sekta. Ukiangalia sekta ya afya, Halmashauri hutumia 94% ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya afya ya taifa na Serikali Kuu hutumia 6% tu. Kwenye elimu uwiano kati ya Halmashauri na Serikali Kuu ni 85% kwa 15%. Ukizingatia uhusiano wa karibu uliopo kati ya uzito wa majukumu na matumizi,




**Mchoro (1) Uwiano wa Matumizi ya SK na SM kwa kila sekta**
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010
(Ministry of Home affairs of Government of Japan)

Halmashauri za Japani zinafanya sehemu kubwa zaidi ya majukumu ya Serikali ya kutoa Huduma. Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kwamba kiasi kikubwa cha bajeti <u>hutengwa</u> kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu mazito yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao.


Je hali ikoje Tanzania? Ukweli ni huu, ukiangalia majukumu yote yaliyogatuliwa na kupelekwa kwenye ngazi za msingi katika Halmashauri Tanzania, ukubwa wa majukumu ni sawa tu yale ya Halmashauri za Japani. Lakini, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri Tanzania, ilikuwa pungufu ya TZS trilioni 3 ya bajeti ya taifa ya zaidi ya TZS trilioni 11 ya mwaka 2011/12.

Ulinganisho unaofanywa, ni ule unaohusu bajeti za Halmashauri zenye kuwa na masharti au uhuru wa matumizi. Mchoro (2) unaonyesha viwango na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri za Japani. Kama ilivyothibitishwa na takwimu hizi, 51% ya mapato hutokana na vyanzo vya ndani ( kodi ushuru na malipo mbalimbali). Pia kuna <u>ruzuku ambazo hazina masharti yoyote ya matumizi</u> zinazoitwa "ruzuku toka SK kwenda SM " (ruzuku za LAT). Ruzuku ya LAT ni <u>fedha nyingi inayotoka SK kwa mara moja</u> kwenda SM na serikali za mikoa. Fedha hii inahamishwa toka Wizara ya Fedha kwenda kwenye akaunti kuu ya kila Halmashauri <u>siku ya kwanza ya kila robo mwaka</u>. Ukijumlisha mapato ya ndani na ruzuku za LAT toka SK, Halmashauri za Japani zina aslimia 75% ya bajeti yao isiyo na masharti na wanaweza kutumia kama wanavyoamua wenyewe.

Mchanganuo huu ni wa muhimu sana kwa Halmashauri SM za Japani katika kufikia malengo ya mipango yao ya maendeleo, kwani wana bajeti ya kutosha na ya uhakika kila mwaka. Washiriki toka Tanzania walipochunguza hali za Halmashauri za kwao, walithibitisha kwamba zina hali mbaya ya kifedha pia fedha nyingi wanayopokea ina masharti ya matumizi kama ilivyo kwenye Mchoro, (3).




**Mchoro(2): Vyanzo na viwango vya mapato ya SM za Japani**
**Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010 (Ministry of Home Affairs of Government of Japan)**





**Mchoro (3): Muundo wa vyanzo mapato ya SM za Tanzania**
**Chanzo: Ni hesabu zilizofanywa na mwandishi toka tovuti ya serikali ya Tanzania**

Ama kwa hakika, hata kwa hali hii ingelikuwa jambo la maana kama 94% ya ruzuku wanayopokea isingelikuwa na masharti ili Halmashauri ziwe na uhuru wa kuzitumia. Bahati mbaya, kuna ruzuku mbalimbali zinazokuja zikiambatana na masharti katika matumizi. Hivyo basi, hata kama Halmashauri itaanda mipango mizuri ya maendeleo, ni vigumu sana kutekeleza miradi yao ya vipaumbele kwa sababu ya ruzuku zenye masharti, ambazo husababisha mipango ya maendeleo isitekelezeke kirahisi.

Ikumbukwe kwamba kiasi cha fedha inayotengwa kwenye bajeti za Halmashauri ni kidogo mno cha Shilingi trilioni 3 kati ya trilioni 11 za bajeti ya taifa (2011/12). Hizi Shilingi trillioni 3 ni sawa na 94% ya bajeti nzima ya Halmashauri, na hii inathibitisha jinsi ambavyo hawana vyanzo vya ndani vya kutosha.

Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Serikali ya Tanzania kutenga kiasi cha kutosha cha bajeti kutekeleza wingi wa majukumu ya Halmashauri yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao kama kweli wameazimia kufikia ugatuaji wa madaraka. Fedha hii inaweza kuwa zile kutoka vyanzo vya

ndani au katika ruzuku isiyo na masharti[5]. Kama hakuna bajeti ya kutosha inayotengwa, basi hakuna sababu ya kugatua majukumu kwenda ngazi za Halmashauri. Vinginevyo, shughuli hizo hazitatekelezwa na mwishowe jamii itateseka kwa kukosa huduma. Kama tulivyoona kwa Halmashauri za Japani, ikitokea kwamba 85% ya majukumu ya kutoa huduma za elimu yamegatuliwa na kupelekwa ngazi za Halmashauri, basi kiasi cha kutosha cha bajeti ya kutekeleza majukumu hayo hugatuliwa na kupelekwa Halmashauri ili kufikia malengo. Vinginevyo si haki hata kidogo kwa Halmashauri na hasa kwa watu wanaotegemea huduma.




**Mchoro (4): Aina za Kodi kwenye Majiji/Miji**
**Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010**
**(Ministry of Home Affairs of Government of Japan)**

## b) <u>Kodi za Ndani kwa ajili ya Uendelevu na ushamiri wa Serikali za Mitaa</u>

Kule Japani, kuna sababu zilizo wazi kabisa kuhusu aina zote za kodi zinazotengwa kwenye ngazi zote mbili za SM. Prefectures(SM za Wilaya ndiyo ngazi ya juu za SM) na Municipalities (Miji na Majiji) ndiyo ngazi za chini za SM[6]). Japokuwa Wilaya (Prefecture) ndiyo ngazi ya juu ya SM ya Japani, zinaweza kulinganishwa na Halmashauri za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. Kuhusu majukumu, ngazi za chini za SM Japani (Municipalities) ndizo zinalinganishwa na ngazi za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji kwa Tanzania. Hata hivyo kule Japani, huduma zote za muhimu kwa jamii hutolewa na Majiji/Miji (Municipalities) kwa sababu ndizo ngazi za msingi zilizo karibu na watu, huku Prefecture/Wilaya wanahusika hasahasa na maendeleo ya kiuchumi kwa vile majukumu haya yanahitaji eneo kubwa kwa ajili ya mipango na kuyatekeleza kimkakati.

Kulingana na majukumu yalivyo na wajibu wa Majiji/Miji, zifuatazo ni kodi ambazo zinaweza kutozwa na Majiji :

Kama inavyoonekana katika mchoro (4), kodi za nyumba na mali zisizo hamishika ni sawa na 45.3% ya mapato yatokayo na kodi, ambayo ni karibu na nusu ya mapato yote yatokanayo na kodi. Ukijumlisha na "Kodi ya mkazi"(kodi ya Kichwa) pamoja na "kodi ya mipango miji", inakuwa ni zaidi ya 80% ya mapato yatokanayo na kodi. Kodi za nyumba na kodi ya mipango miji hutozwa kwenye ardhi na majengo na hizi ni kodi ambazo hakuna awezaye kuzikwepa. Kama ardhi yote na majengo yote yamesajiliwa na kuthaminiwa vizuri, basi hivi ni vyanzo vya uhakika kwa serikali za Mitaa.

[5] Kwa hatua zilipofikia kwa sasa, bado haishauriwi kugatua madaraka ya kifedha na kuwapa SM mamlaka makubwa ya kutoza kodi. Hii ni kwa sababu hali hii itaziumiza zile SM zilizo kwenye maeneo yenye ufukara ya vijijini, kwa vile hazina vyanzo vya uhakika vya kodi, huku zile SM tajiri za mijini zitakuwa na mapato mengi kutoka vyanzo vyao vya ndani . Kwa hiyo ni busara zaidi kuendelea kutoa ruzuku kutoka chanzo kimoja, lakini SM ziwe na uhuru na maamuzi wa kuzitumia kulingana na vipaumbele vyao kwa sasa.

[6] Kuna Prefecture/Wilaya 47 na (Munispaa) 1,742 hadi kufikia Octoba 2012. Manispaa za Japani zinajumuisha Majiji**<u>, Miji na Vijiji</u>**, na tofauti na mgawanyiko wa ngazi za SM za Tanzania.

"Kodi ya kila mkazi wa Halmashauri za Japani" ni "kodi ya kichwa" iliyofutwa hapa Tanzania ambayo ni "kodi ya maendeleo"[7]. Chanzo hiki cha kodi pia huwa ni chanzo cha kuaminika kwa sababu wakazi wote wameandikishwa na Halmashauri inajua wanapoishi. Tukiangalia hali ya Tanzania, vyanzo vingi vya mapato ni vile vinavyohusiana na shughuli za kiuchumi, mfano ushuru wa mazao (23%), ushuru wa huduma (18%), ushuru wa nyumba za kulala wageni(3%), leseni (10%), karo na malipo mbalimbali (17%), ambazo hubadilika kulingana na mabadiliko ya hali ya uchumi wa eneo husika, na cha kushangaza ni kwamba kodi ya majengo ni 8% tu ya mapato yatokanayo na kodi.

Mafunzo ya Osaka yaliwapa viongozi wa Tanzania changamoto kwamba ili Halmashauri ziweze kutoa huduma endelevu zinazohitajika kwa wakati na viwango vinavyotegemewa, ni lazima kujenga wigo mpana na mfumo wa uhakika wa kukusanya kodi ndani ya Halmasahuri zenyewe. Uzoefu wa Japani unaonyesha kwamba bila kuweka msisitizo kwenye vyanzo vyenye uhakika vya kodi/ushuru kama vile kodi za majengo, kodi ya kichwa/kodi ya maendeleo, siyo rahisi hata kidogo kwa Halmashauri kutekeleza majukumu yake. Kwa mazingira haya, ni muhimu kuwa na mfumo wa daftari la kuandikisha ardhi na mali zisizo hamishika pamoja na daftari la wakazi wote kwa kila Halmashauri, hii itasaidia nchi nzima siyo tu kwenye masuala ya kukusanya mapato, bali kwa matumizi mengine mengi.

Kuhusu utaratibu huu, inafaa kusema kwamba tayari Tanzania kuna mifano ya kufurahisha na inayotia moyo ya Halmashauri zinazotekeleza kile kinachopendekezwa hapa, rejea kisa mkasa cha Manispaa ya Mtwara Mikindani kwenye Sura ya Tatu.

### 3.4 Maendeleo ya Kiuchumi ya Serikali za Mitaa – Uzoefu wa kufurahisha wa dhana ya ki-Japani ya "Kijiji kimoja zao moja" au (OVOP)"

Hitaji la maendeleo ya kiuchumi ya Halmashauri limekuwa likisumbua vichwa vya Wakurugenzi wengi wa Tanzania. Kuhusiana na hili, kuna uzoefu maarufu nchini Japani wa dhana ijulikanayo kama "zao moja kwa kijiji kimoja" maarufu kama OVOP, iliyoanzia kwenye wilaya/ Prefecture ya Oita ambayo hapo awali ilikuwa moja ya wilaya fukara kuliko zote nchini humo. Uzoefu unaotokana na dhana hii unaweza kuwa muafaka kwa Tanzania kama utatafsiriwa na kutumika inavyostahili kulingana na mazingira ya Tanzania.

#### (a) Zao moja kwa kijiji kimoja (OVOP) ni nini?

Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ni mkusanyiko wa ubunifu wa shughuli za maendeleo ya jamii zilizobuniwa na kupata msukumo wa viongozi kutoka jamii husika katika Wilaya (Prefecture) ya Oita, ambao waliipenda jamii yao na wakahuzunishwa kutokana na hali ya ufukara uliokuwa umekithiri huko miaka ya nyuma. Japokuwa juhudi kama hizo za mtu mmoja mmoja zilikuwepo hapa na pale kwenye Wilaya (Prefecture)ya Oita tangu miaka ya

[7] Tofauti pekee ni kwamba kodi ya kichwaTanzania hutozwa kwa kiwango sawa kwa kila mtu, kwa Japani kodi ya mkazi hutozwa kulingana na viwango vya kipato cha kaya. Kama hakuna kipato cha kiasi fulani kinachokubalika, basi wanakaya wa kaya hiyo hawana sababu ya kulipa kodi ya mkazi.

1960, dhana yenyewe ya "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilianzishwa rasmi mwaka 1979 na Dr. Morihiko HIRAMATSU, akiwa Gavana[8] wa Wilaya hiyo kwa kuanza kuzitambua baadhi ya juhudi za jamii zilizokwisha anza na kuziendeleza.

Dr. HIRAMATSU, alikuwa ni msomi mwenye mafanikio makubwa akiwa mtumishi wa cheo cha juu kwenye Wizara ya Biashara za kimataifa na Viwanda yaani "Ministry of International Trade and Industry (MITI)". Hii ilikuwa Wizara yenye nguvu sana, lakini aliamua kuacha kazi hiyo na kurudi kwenye Wilaya ya Oita yaani nyumbani kwao. Kilichomsukuma ni kwa sababu alihofia sana kuwa Wilaya ya nyumbani kwake iliendelea kubaki nyuma kimaendeleo na kuwa miongoni mwa Wilaya fukara kuliko zote nchini Japani kwa wakati huo.

Baada ya kurudi kwao, aligombea na kushinda cheo cha Ugavana wa Wilaya ya Oita. Alipoanza kazi hii jambo la kwanza alilolifanya ni kutembelea vijiji vyote kwenye Wilaya hiyo. Wakati akifanya matembezi haya, alikuta kuna miradi ya maendeleo na jitihada mbalimbali za watu wenyewe kujaribu kujinasua huko vijijini. Aliguswa sana na jitihada hizo za wananchi wakiongozwa na viongozi wao wenye mapenzi mema na juhudi hizi zilikuwa hazijulikani kwa serikali. Alithamini sana juhudi za jamii, na akawatia moyo waendelee na jitihada za kujikwamua. Kwa wanavijiji, wengi wao walikuwa hawajawahi kutoka nje ya vijiji vyao, kwa hiyo kwao ilikuwa ni faraja kubwa kutembelewa na mtu mkubwa kama Gavana na kusifiwa kwa kile walichokuwa wanakifanya!. Hawakuwahi kuwaza kwamba kile walichokuwa wanakifanya kilikuwa ni kitu cha kipekee na cha thamani machoni pa wengine. Tangu Gavana wao Dr. HIRAMATSU alipofanya matembezi haya, juhudi hizo za jamii zilipewa msukumo mkubwa na watu wakahamasika zaidi na kujisikia fahari wenyewe.

Kwa upande wake, Dr. HIRAMATSU alifikiri ni jukumu muhimu kwa Serikali ngazi ya Wilaya kuunga mkono na kuendeleza juhudi za thamani kubwa zilizoanzishwa na wananchi kutaka kuboresha maisha yao wenyewe, kuzieneza zaidi na kubadilisha uzoefu huu mzuri na viongozi wa vijiji vingine ndani ya Wilaya yao.

Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP ina mambo muhimu yanayolitofautisha na dhana nyingine kwani Vuguvugu hili hupelekea kuzalisha bidhaa za kipekee (ikijumuisha utalii), ili kupata maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii husika. Hata hivyo, jambo jingine la tofauti kwenye vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" ni kwamba: kuna uzoefu dhabiti wa jamii unaopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi midogo ya maendeleo ya shughuli za kiuchumi ngazi za msingi. Wananchi husika huunganisha uwezo wao wa kujipanga na kutekeleza mustakabali wa maisha yao; jamii zimejijengea uwezo, zimeamka na zina ujasiri; Jamii zimeimarika na zimefikia uwezo wa kujitawala na kujiendesha wenyewe kama kijiji. Ukweli uliopo hapa ni kwamba wananchi wana uzoefu wa kufanikiwa na wakati mwingine kushindwa (lakini wamejijengea uwezo na tabia ya kujikwamua katika kushindwa huko), siyo tu kwamba jamii inategemea kupata mafanikio ya kiuchumi pekee, bali pia jamii inatarajia kujijengea uwezo, uzoefu na ujasiri na kupata nguvu zaidi katika mchakato huo. Ukweli huu ni muhimu ufahamike ili kulielewa vizuri vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja". Ikumbukwe

[8] Cheo cha Gavana wa Prefecture ni cheo cha juu zaidi kwenye SM za juu Japani ikilinganishwa na Meya wa kwenye SM za Tanzania (Ona "3.2. Usimamizi wa Rasilimali Watu na Ugatuzi wa madaraka" kwa Meya.)

kwamba ni rahisi sana kupata mafanikio au faida ya mara moja katika biashara au mradi fulani kutokana na msaada wa mara moja kutoka nje ya jamii, lakini kama jamii hiyo itakumbana na vikwazo fulani fulani baadaye, hawataweza kuvishinda kama watakuwa hawajajijengea uwezo kupitia michakato iliyotangulia ya kutatua matatizo yao kwa nguvu na jitihada zao wenyewe.

Kwa mantiki hii, ni vyema kutambua kwamba nyingi kati ya juhudi zilizojitokeza kwenye Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" kule Oita, zilipitia mchakato ufuatao:

- Kabla ya vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja"au OVOP, wanavijiji wa Oita walikuwa fukara sana, walikuwa wamekata tamaa kuhusu mabadiliko, wenye kijicho na kuoneana wivu wao kwa wao, kutokana na hali hii haikuwezekana kushirikiana baina yao ili kuboresha maisha kwa pamoja. Hata hivyo, kupitia Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" walianza kujitambua kwamba "Ndiyo, tunaweza kama tunataka!" Haya ni mafanikio makubwa katika mchakato wa kubadili fikra.
- Katika badiliko la fikra hapo juu, wanavijiji walianza kujijengea uzoefu wa kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali ndani ya jamii, wakizikabili changamoto wanazokutana nazo na kuzishinda kwa pamoja. Mchakato huu uliwafanya waweze kujipanga vizuri na vizuri zaidi.
- Kupitia mchakato huo huo, waliimarisha mahusiano na taasisi za nje zenye usaidizi ikijumuisha Halmashauri na Asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Pamoja na ujenzi wa uwezo wa jamii ulioelezwa hapo juu, jamii husika zilifanikiwa kupata matokeo dhahiri ya maendeleo ya kiuchumi.

**(b) Dr. HIRAMATSU alifanya nini akiwa Gavana wa Wilaya?**

Kwanza kabisa, ieleweke vizuri kwamba vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" halikuwa ni programu ya lazima("maamrisho ya kutoka juu kwenda ngazi za msingi") iliyoandaliwa na Dr. HIRAMATSU na kwamba watu hawakuambiwa cha kufanya. Kwa bahati mbaya, baadhi ya nchi zinazoendelea ambazo zilivutiwa na Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja", waliuelewa vibaya ukweli huu. Walizingatia tuu zile faida za kiuchumi zinazotokana na OVOP na kujaribu kuendeleza vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" kama sera ya taifa na kutoa maamrisho kutoka juu kwamba kila kijiji kizalishe kitu ambacho kinaweza kuuzwa hapa nchini au nje ya nchi. Kinyume chake sasa, alichokifanya Dr. HIRAMATSU kwenye Wilaya ya Oita ilikuwa ni, kwanza, kutembelea vijiji vyote, kuzitambua juhudi za wananchi za thamani ambazo zilikwishaanza, akawasifia na kuwatia moyo.

Pili, alivishirikisha vijiji vingine na viongozi wao kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa ili habari hii iwe kichocheo, waanze na wao kufikiri kuhusu maendeleo yao wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye maeneo husika, badala ya kulalamika eti hawana chochote kwenye vijiji vyao na kukata tamaa.

Tatu, alipotambua bidhaa fulani za kipekee kwenye baadhi ya vijiji, alisaidia kutafuta soko la ndani na nje ya Wilaya ya Oita. Alitumia maarifa yake, uzoefu na mitandao ambayo alikwisha jijengea alipokuwa afisa wa ngazi za juu Wizara ya Biashara ya Kimataifa na Viwanda. Alizitangaza bidhaa hizi nchi nzima.

Nne, aliwezesha suala zima la kubadilishana uzoefu baina ya viongozi wa vijiji mbalimbali ili wajifunze na kuhamasika kutokana na kujifunza kwa watu walio kwenye ngazi moja na siyo kujifunza kwa ngazi tofauti ya maendeleo. Alianzisha shule ya kuendeleza rasilimali watu[9]" iliyoitwa "*Toyonokuni*[10]. Juhudi hizi za Gavana, zilisaidia kuchochea ari ya viongozi na hii ikapelekea kuibuka kwa miradi mingi yenye sura ya "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP.

Kama inavyoonekana hapo juu, dhamira ya vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilikuwa ni Halmashauri kuzitambua, kuzisifia, kutia moyo juhudi za kimaendeleo zinazojitokeza kwa jamii. Jukumu la Halmashauri ni "uwezeshaji" na siyo "utekelezaji" au "uelekezaji". Dr. HIRAMATSU hakuwaambia wanavijiji jambo la kufanya katika kuendeleza vuguvugu hili, bali aliheshimu juhudi zao na umiliki wao, pamoja na nguvu zao. Mafunzo ya Osaka yanasisitiza vuguvugu la"zao moja kwa kijiji kimoja", kwani ni dhana muafaka kwa mazingira ya Tanzania, na inaaminika kwamba tayari zipo juhudi za namna hiyo kwenye Vijiji na wapo viongozi wazuri wanaojali maendelo ya nyumbani kwao. Ingelikuwa ni jambo la manufaa makubwa kwa Tanzania kuunga mkono vuguvugu hili na kutoa fursa ya wazalishaji kujifunza kwa wenzao walio ngazi moja. Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Tanzania kudhani kwamba eti hakuna chochote kwenye vijiji vyao. Kuna mambo mengi mazuri yanayostahili kuigwa lakini pengine wao ndio hawajayatambua. Ni wajibu wa viongozi wa Halmashauri kuanza kuzitambua juhudi za jamii zilizopo, kuzitia moyo, na kubadilishana uzoefu na wengine. Ingekuwa ni njia yenye tija zaidi ya wazalishaji kujifunza kutoka kwa wenzao walio kwenye ngazi moja kuliko kujifunza watu wa ngazi tofauti au kutoka kwenye vitabu. Ni kutokana na mtizamo huu ndipo kitabu hiki kikaandaliwa.

### 3.5 Masuala Mengine

Kuna mengi ambayo hatukugusia hapo juu kutokana na kukosa nafasi. Lakini, yapo ambayo ni ya muhimu kugusia ambayo yanafaa kwa Tanzania kama vile kisamkasa cha Minamata na uzoefu unaotokana na "Ugonjwa wa Minamata"(Minamata Disease) na jinsi walivyoweza kuhuisha jamii kutokana na mkasa huo; Upangaji mipango shirikishi jamii; mipango miji; mipango ya matumizi bora ya ardhi na marekebisho ya ardhi, uzoefu wa Japani kuhusu maendeleo ya kiuchumi na mchango wa Halmashauri katika mkasa huo, n.k.

Kuhusu kisamkasa cha Minamata, mafunzo ya Osaka yanaweka msistizo kwenye umuhimu wake, na inaaminika kwamba nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zina mengi ya kujifunza kutokana na kisa mkasa hiki. Masuala ya kisa hiki yatagusiwa kwa undani kwenye kitabu kinachofuata.

## 4.0 MAENDELEO BAADA YA MAFUNZO YA OSAKA YALIYOSABABISHA KUCHAPWA KWA KITABU HIKI

[9] Inaitwa "shule" lakini hakuna majengo. Huwa ni aina fulani ya mafunzo kwanjia ya warsha kwa ajili ya viongozi ili kuwakutanisha pamoja.

[10] "Toyonokuni" jina la kienyeji la eneo hili la Wilaya ya Oita

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 1 hapo juu, mafunzo ya Osaka yalikuwa yameandaliwa mahsusi kwa nchi ya Tanzania kwenye miaka mitano ya mwanzo(2002 – 2007), yaliendelea kwa miaka mingine sita lakini wigo wake ukapanuliwa na kuingiza nchi nyingine tatu (2008 – 2012). Mafanikio makubwa katika miaka hii 11 hapa Tanzania ni kule kuanzishwa kwa Umoja wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi waliosoma Osaka, kwa kifupi TOA. Huu ni mfano wa pekee Duniani kuwa na Umoja wa Wahitimu wa kozi ya aina moja ukijumuisha Wadau Maarufu ambao ni viongozi wa maboresho kama vile Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) na Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na wakuu wengine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI). Japokuwa haikutegemewa, lakini ni jambo la kupendeza hata kwa JICA ambao wanaendesha maelfu ya kozi za mafunzo duniani kote.

Kwa nyongeza, TOA wameshaanza kuendesha semina mbalimbali na warsha za mafunzo kama vile Mafunzo baada ya Osaka na Warsha za Mafunzo za Kanda kwa ajili ya kubadilishana uzoefu baina ya Halmaushauri wanachama. Fursa hizi, siyo tu kwamba zina saidia kubadilishana maoni baina ya Halmashauri wanachama, bali yametoa uwanja ambao ni nadra kuupata wa majadiliano na kuhusu uhalisia wa Ugatuaji wa Madaraka, hususan changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza maboresho ya Serikali za Mitaa.

Mpaka sasa, hakuna asasi ya namna hii hapa Tanzania, inayowahusisha Watendaji wa Serikali za Mitaa na wale wa Sekretarieti za Mkoa. Jumuia ya Serikali za Mitaa (ALAT) ipo, lakini wahusika wake wakuu ni Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya na Wabunge. Vikao vya Jumuiya hii haviwapi fursa Wakurugenzi wa Halmashauri kushiriki kikamilifu na kutoa ushauri wa kitaalamu ingawa wao pia ni wajumbe. Kwa mantiki hii, TOA ina uwezekano mkubwa wa kukua hadi kuwa Umoja wa Watendaji Wakuu wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa yaani Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa ambao ni wataalamu na watekelezaji wa ugatuaji wa madaraka na maboresho nchini. Hawa ndio wanaoshughulika kila siku kwenye mstari wa mbele wa maboresho. Maoni na mapendekezo yao ya pamoja yanaweza kuwa ni ya maana sana na ya kuongeza ufanisi kwenye kutekeleza maboresho.

Kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa, tayari Tanzania imekwishajijengea uzoefu kwa zaidi ya muongo mmoja wa utekelezaji Ugatuaji wa Madaraka kwenda ngazi za msingi katika kila Mamlaka ya Serikali za Mtaa. Lazima kutakuwepo na idadi kubwa ya mambo ya kufurahisha na uzoefu mzuri kwenye Halmashauri nyingi kote nchini ambao unafaa kushirikisha Halmashauri nyingine. Japani inaamini kwamba aina hii ya kujifunza kwa taasisi zilizo kwenye ngazi zinazofanana inaweza kuwa muafaka zaidi kuliko kujifunza kutoka nje ya nchi yaani kutoka kwenye ngazi tofauti au ya juu sana. Tanzania inaweza kujifunza vizuri kutokana na uzoefu ulioko ndani mfano shughuli za OVOP kama zilivyoelezwa kwenye 3.4. hapo juu. Kitabu hiki cha rejea kiliandaliwa kwa kuzingatia maelezo na msingi huo ulioelezwa hapo juu. Ni matumaini ya TOA na mafunzo ya Osaka kwamba yatachangia kuboresha utendaji ndani ya Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa, kila moja ikimchochea mwenzie, na kuendeleza mambo mema yanayojitokeza, ambayo yatapelekea kwenye ufanisi na mafanikio ya ugatuaji wa madaraka katika nchi hii.

Mwishowe, inastahili kusema kwamba kutokana na matokeo ya kufurahisha yaliyotokana na mafunzo ya Osaka kwa nchi ya Tanzania, ambayo yameelezwa kwenye sura hii, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani (JICA) limeaamua kuendelea kutoa mafunzo ya Osaka kwa miaka mingine mitano, yakilenga Tanzania kwa mara nyingine tena na litatoa msisitizo maalumu katika kuwezesha shughuli za wanaumoja wa TOA na juhudi zake za ujenzi wa kitaasisi. Hii ina maana kwamba, viongozi wengine wengi wa maboresho Tanzania watafaidika kutokana na mafunzo ya Osaka ili waweze kuchangia utekelezaji mzuri zaidi wa maboresho ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi za msingi nchini.

# Sura ya Pili: Jitihada za Jamii Katika Kuboresha Utoaji wa Huduma

Mtazamo wa Jitihada za Jamii ni mfumo mpya katika eneo la maendeleo vijijini, ambao lengo kuu ni maendeleo vijijini. Malengo Mahsusi ya mfumo huu ni kuongeza ubora wa maisha ya watu maskini, na kuboresha miuondombinu. Ni mfumo wa hiari wa kundi la watu wanojiendesha wenyewe wakiwa na tabia zinazofanana za kijamii na kiuchumi, ambao wanaungana ili kuanzisha fikra zitakazochochea maendeleo endelevu. Mtazamo wa Jitihada za Jamii kwa ajili ya Maendeleo Vijijini katika hali ya kendesha mipango ya kiuchumi huleta ajira, miondombinu ambayo jamii inaweza kujitengenezea, stadi za kazi pamoja na shughuli mchanganyiko. Pia mtazamo huu huleta mipango ya ustawi wa jamii ili kuboresha afya, lishe na maslahi ya jamii kwa ujumla.

Jitihada za jamii huwa na maana ya majaribio ya jamii kupambana na changamoto zinazoikabili kijamii na kiuchumi bila kusubiri miradi mikubwa kutoka serikalini. Jitihada za jamii hujumuisha maazimio ya kutatua matatizo ya jamii kupitia jamii kujipanga, kushiriki na kutekeleza. Katika haya yote jamii yenyewe huona hitaji, hupanga namna ya kufikia hitaji, hutafuta raslimali zilizopo zinazohitajika kufikia hitaji, hujipanga katika makundi ya utekelezaji na kutekeleza mradi.

Mara nyingi jitihada za jamii huwa na maana ya uundaji wa vyama vya hiari katika jamii, ambapo wanchama huwa na malengo yanayofanana, hujipanga na kuratibu mipango wakiwa na lengo mahsusi la kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi katika jamii yote. Tafiti zinaonesha kuwa vikundi katika jamii kwa miaka mingi vimefanikiwa kujiendesha katika kujenga barabara, vituo vya afya, madaraja na nyumba, kulima mashamba, kufadhili masomo, na kuanzisha taasisi za viwanda;  kutaja machache. Ushahidi wa haya umeleta ongezeko na kupanuka kwa uanachama na jitihada za jamii katika vijiji.

Hapa Tanzania, Jitihahada za Jamii na Ushiriki wa Jamii vimekuwa dhahiri kutokana na historia ya itikadi ya kijamii na kiuchumi ya kujitegemea. Tangu Uhuru, jamii katika vijiji vyao zilishauriwa kuishi katika jamii na kutumia mbinu za ushirika katika kutatua matatizo yao. Kileleni kabisa mwa itikadi hii, kati ya miaka ya 1960 na 1970 na hasa baada ya Azimio la Arusha, jamii zilianzisha miradi mbalimbali na kuitekeleza ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule na zahanati, kuchimba visima na mabwawa madogo, kulima barabara na kuendesha kilimo cha ushirika.

Pamoja na kuwa mbinu hizi zilipungua katika miaka ya 1990 kuelekea milenia mpya kutokana na madai ya serikali kuwa inaweza kutoa huduma zote, kuna jamii ambazo siku za karibuni zimetumia jitihada za jamii kwa kina katika ujenzi wa shule, zahanati, madarasa na majengo ya serikali; vyote vikilenga kuboresha utoaji wa huduma.

Katika Sura hii Mbinu Bora zimewasilishwa kutoka Jiji la Mwanza na Halmashauri za Wilaya za Geita na Chato.

Mbinu Bora ya Jiji la Mwanza inahusu Udhibiti Shirikishi wa Magugu Maji katika Ziwa Viktoria. Halmashauri na Jamii kwa ujumla iliamua kujikita katika jitihada hii kwa kuwa tegemeo kuu la kipato lilikuwa hatarini kupotea kutokana na ongezeko kasi la magugu maji katika Bonde lote la Ziwa Viktoria. Kuongezeka kwa magugu maji kulisababisha kupungua kwa aina mbalimbali za samaki na kuibuka kwa

wanyama hatari kama mamba, viboko na nyoka. Gugumaji hili pia lilisababisha kero katika usafirishaji na utiaji nanga wa meli. Ili kuboresha uvuvi na ufugaji wa samaki ziwani, Halmashauri ilianzisha jitihada mbalimbali kama kuziandaa jamii na wadau kushiriki katika kuondoa magugu maji, kuunda vikundi mbalimbali vya uangalizi wa fukwe (Beach Management Units - BMU) ili kudhibiti magugu maji, kujenga uelewa wa wanavikundi kupitia mafunzo, uundaji wa katiba za vikundi na uzalishaji wa mbawa kavu (wadudu wanaotumika kudhibiti magugu maji kibaolojia). Jitihada zilizochukuliwa na vikundi vya uangalizi wa fukwe (BMUs), Halmashauri na Jamii zote zimefanikisha kupunguza usambaaji wa magugu maji ziwani na kwenye fukwe zake na hivyo kuwepo kwa mazingira bora ya shughuli za uvuvi na kupungua kwa mazalio ya wanyama hatari.

Mbinu Bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita inahusu Jitihada za Kijiji cha Nyakagwe za Kuboresha Utoaji wa Huduma. Kijiji hiki ambacho ni kituo cha shughuli za uchimbaji wa madini kilikumbwa na ukuaji wa kasi wa idadi ya watu swala lililoleta hitaji kuu la utoaji huduma muhimu kama utawala, afya, elimu na usalama. Kijiji hakikuwa na shule ya msingi wala zahanati; wanafunzi walilazimika kutembea takriban 4km kwenda shule katika shule ya msingi ya Butobela, hii ilichangia kuongezeka kwa utoro na ufaulu duni. Wanakijiji, hasa wanawake wajawazito na watoto walilazimika kusafiri 14km hadi Zahanati ya Bukoli iliyopo katika Kata ya Bukoli ili kupata huduma za afya. Baada ya kutambua mapungufu haya yote, Kijiji cha Nyakagwe na kwa msaada wa Halmashauri na wadau wa maendeleo kiliamua kuboresha huduma za utawala kwa kujenga jengo la kisasa la Serikali ya Kijiji, kituo cha kudumu cha polisi ili kudhibiti matukio ya wizi na ujambazi wa kutumia silaha na zahanati ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya ya msingi. Aidha, Kijiji kilijenga shule ya msingi ili kuongeza uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule. Kijiji cha Nyakagwe kiliamua kupambana na changamoto hizi kwa kutumua mfumo wa usikivu kwa hitaji unaozingatia maamuzi sahihi ya mahitaji ya jamii, na jamii ipo tayari na ina hiari ya kuchangia kuondoa changamoto iliyopo.

Mbinu Bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Chato inahusu Jitihada za Jamii katika Kuanzisha Shule Shikizi. Kati ya mwaka 2007 na 2012, Halmashauri ilikumbwa na upungufu wa shule za msingi kutokana na ongezeko la idadi ya watu. Idadi ya wanafunzi iliongezeka kutoka 12,814 mwaka 2007 hadi 22,421 mwaka 2016, ilihali idadi ya shule za msingi ikibaki ileile. Bajeti ya Halmashauri haikutosha kujenga shule katika vijiji vipya; ililazimu wanafunzi kutembea umbali mrefu (6km – 10km) kutoka nyumbani kwenda shule katika vijiji vingine. Hali hii ilisababisha mahudhurio dhaifu, utoro, mimba za utotoni, ajali na ufaulu duni wa mitihani. Wazazi hawakufurahia hali hii hivyo kuamua kujikita katika uanzishaji wa shule shikizi. Mwaka 2012/2013, pendekezo la jamii kuanzisha shule shikizi lilipitishwa na Baraza la Halmashauri ya Wilaya. Halmashauri iliunda kikosi kazi cha elimu chenye wataalamu mbalimbali ili kuhamasisha jamii na kusimamia utekelezaji wa jitihada hii. Jamii ziliunganishwa katika ngazi zote kupitia mikutano na majadiliano na kusaidia ukusanyaji wa raslimali ili kujenga miundombinu mipya ya shule. Kukamilika kwa jitihada hii kulileta ongezeko katika uandikishaji, kuliondoa utoro, kulipunguza umbali wa kwenda shule, kulitokomeza ajali za barabarani na hatimaye kuboresha ufaulu wa wanafunzi katika Halmashauri kwa ujumla.

# JIJI LA MWANZA

**UDHIBITI SHIRIKISHI WA MAGUGU MAJI KATIKA ZIWA VIKTORIA**




***Uzoefu wa Jiji la Mwanza***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Jiji la Mwanza inapatikana katika fukwe za kusini za Ziwa Viktoria, Kaskazini Magharibi mwa Tanzania. Jiji lina eneo la 1,325km$^2$ ambapo 425km$^2$ ni ardhi na 900km$^2$ zimefunikwa na maji, hasa Ziwa Viktoria ambalo huwa ni takribani 67% ya eneo lote. Kati ya 425km$^2$ za ardhi, takriban 86.8km$^2$ ni eneo la makazi ya mjini. Jiji linapatikana katika mwinuko wa 1,140m juu ya usawa wa bahari likiwa na wastani wa joto kuanzia 25.7$^O$C na 30.2$^O$C msimu wa Joto na 15.4°C na 18.6$^O$C msimu wa baridi. Jiji la Mwanza hupata mvua za mwaka kati ya 700mm miezi ya Oktoba hadi Desemba na 1000mm miezi ya Februari hadi Mei.

Kiutawala, Jiji lina Tarafa 1, Kata 18 na Mitaa 175. Kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012, Jiji la Mwanza lina watu 363,452, kati yao 177,812 ni wanaume na 185,640 ni wanawake. Ongezeko la idadi ya watu kwa mwaka ni 3.0% kukiwa na wastani wa watu katika kaya ni 4.7, ambao unakaribia wastani wa kitaifa wa 4.8. Wakazi wa Jiji la Mwanza hutegemea shughuli za viwandani, kazi za maofisini, kilimo kisicho cha kibiashara na shughuli za uvuvi ambazo ndizo chanzo kikuu cha kipato.

Maliasili katika Jiji hili ni ni pamoja na maeneo mazuri ya uvuvi, mabonde yafaayo kwa kilimo cha mpunga na ardhi yenye rutuba kwa ajili ya mazao mengine. Mazao makuu ni pamoja na mazao ya nafaka, matunda na mbogamboga. Shughuli za uvuvi ziwani hutumia mitumbwi ya kisasa na ngalawa. Samaki wapatikanao kwa wingi ni sangara, sato na dagaa. Licha ya kilimo na uvuvi, baadhi ya wakazi wa Jiji hujihusisha na ufugaji. Shughuli nyingine za kiuchumi ni pamoja na kazi za viwandani, maduka, huduma za starehe, karakana za ufundi na huduma za hoteli.

Ziwa Viktoria likiwa na eneo la 68,800km$^2$ ni ziwa la pili kwa ukubwa duniani baada ya ziwa Superior lililopo Marekani. Ziwa hili linachangiwa umiliki na Tanzania (51%), Uganda (43%) na Kenya (6%). Pato la mwaka kwa bonde lote la ziwa ni Dola za Kimarekani bilioni 3-4. Ziwa hili huhudumia takriban watu milioni 25 wenye kipato cha Dola za Kimarekani kati ya 70-270. Bonde la ziwa hili ni chanzo cha kipato kwa 1/3 nzima ya wakazi wa Tanzania, Uganda na Kenya. Hivyo, kuwepo kwa ubora wa mazingira ya ziwa na kuboresha viwango vya maisha vya wakazi wa ziwani ni shabaha tarajiwa ya maendeleo Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi. Ziwa Viktoria huzalisha samaki, umeme (maporomoko ya Owen), maji ya matumizi ya nyumbani, maji ya umwagiliaji na hutumika kama sehemu ya kuelekeza na kutakatisha uchafu utokanao na binadamu, kilimo na viwanda.

Pamoja na kuwa Ziwa hili ni chanzo cha kipato kwa wakazi wengi kupitia uvuvi, kumekuwa na changamoto za kimazingira zinazotokana na uvuvi haramu, uchafuzi unaotokana na taka za makazi ya watu, mbolea za chumvichumvi na kukua kwa kasi kwa magugu maji. Tatizo la magugu maji limeshughulikiwa sana kwa miongo miwili na nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki. Kama matokeo; kuna miradi katika kila nchi inayoshughulika na uangalizi wa Mto Kagera, Mto Nile na Ziwa Viktoria kwa ujumla.

Gugumaji *(Eichhornia crassipes)* katika Ziwa Viktoria ni mmea wenye asili ya Amerika Kusini na sasa ni maarufu katika mabara ya Amerika Kaskazini, Afrika, Asia na Australia. Gugu hili kwa mara ya kwanza lilijitokeza Afrika Mashariki, hasa Tanzania katika mto Sigi mwaka 1956 na baadaye mto Pangani katika Mkoa wa Tanga. Inawezekana lililetwa kama mmea wa mapambo. Nchini Kenya, gugu hili lilijitokeza katika Ziwa Naivasha na Uganda lilipatikana Ziwa Kyoga miaka ya mwishoni mwa 1980. Madhara ya gugu hili yalijidhihirisha katika Ziwa Viktoria mwanzoni mwa miaka 1990. Inasemekana Chanzo cha maambukizo ya gugumaji ni Mto Kagera upande wa Rwanda ambapo gugu hili lilitumia kama mapambo. Inasemekana pia mbegu za gugu hili huishi kwa kipindi kinachozidi miaka 20. Kilele cha usambaaji wake kilikuwa mwaka 1997, ambapo gugu maji linasemkana lilifunika maji yenye eneo la 120km$^2$. Usambaaji

huu ulileta madhara kwa kipato cha wakazi wa nchi za Afrika Mashariki za Kenya, Uganda na Tanzania kwa ujumla. Madhara haya yalilazimu uhitaji wa kudhibiti usambaaji wa gugu maji kwa nchi zote tatu.

**2.0 TATIZO**

Katika miaka ya 1990, kipato cha wakazi wa Bonde la Ziwa Viktoria hasa wale wanaotegemea shughuli za uvuvi na mazao ya samaki kiliathirika kufuatia uvamizi wa gugu geni kwenye Ziwa. Gugu, ambalo baadaye lilifahamika kama gugumaji lilileta tishio kubwa kwa viumbe waishio majini katika Ziwa na hata usafirishaji ulianza kukwama kutokana na kusambaa katika eneo kubwa pamoja na uzito wa aina ya gugu hili geni ambalo lilizaliana kwa kasi kuliko ilivyotarajiwa. Inasemekana gugu hili lilisafiri kuja Afrika kutoka Amerika ya Latino, hasa Bonde la Amazon kwa makosa ya kudhani ni ua la mapambo na liliwavutia watu kuliotesha pembezoni mwa mabwawa na mito.

Kadiri gugumaji lilivyoenea kwa kasi ziwani, mavuno ya uvuvi wa baadhi ya aina ya samaki yalianza kupungua na wanyama tishio kama mamba, viboko, nyoka na wa aina hizi walianza kujitokeza katika fukwe zilizokuwa salama; ambapo huko nyuma wanyama hawa hawakuwepo. Zaidi ya haya, ubora wa maji ya ziwa kwa matumizi ya nyumbani uliporomoka kwa kasi. Aidha, kulitokea uzibaji wa njia za vyombo vya majini zilizotumika kwa usafirishaji na kupungua kwa kina cha maji. Kutokana na hali hii, wataalamu wa sayansi za maji ndani na nje ya Tanzania na watafiti wengine walifanya tafiti kuhusu gugu hili jipya na matokeo ya tafiti hizi yalionesha kuwa kama hatua za haraka hazitachukuliwa, ziwa litatangazwa kuwa mfu kwa sababu gugumaji linawanyima viumbe wa majini hewa ya oksijeni na mwanga wa jua muhimu kwa kuzaliana. Pamoja na hilo, usafirishaji ziwani uligundulika kukabiliwa na changamoto ya gugumaji kuziba maeneo ya kutia nanga na njia za vyombo vya usafiri majini na mitumbwi. Jedwali No.1 hapa chini linaonesha kusambaa kwa gugumaji katika Wilaya za Nyamagana na Ilemela kati ya Desemba 2010 na Novemba 2016 nchini Tanzania.

**Jedwali 1: Usambaaji wa Gugu Maji Wilayani Nyamagana na Ilemela**

| Wilaya | Msimu wa Utafiti | Usaambaaji wa gugu maji (Ha) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| **NYAMAGANA** | OKTOBA -NOV. 2016 | 21.8025 | Kusambaa kwa gugu maji hubadilika kutegemea na hali ya hewa (mvua, na mwelekeo wa upepo). Katika ngazi ya udhibiti, gugumaji lilipungua, hata hivyo kiwango cha udhibiti hubadilika kulingana na muda.<br><br>Udhibiti wa gugu maji kibaolojia kwa kutumia mbawakavu haukufanikiwa sana katika mkondo wa Mwanza, uanzishaji wa mbawakavu na wadudu wengine kibaolojia (mchwa, kuvu) ulikadiriwa kuwa chini kipindi chote cha utafiti. |
| | APRILI-MEI, 2016 | 14.1445 | |
| | NOVEMBA, 2015 | 10.22 | |
| | MACHI, 2015 | 6.3915 | |
| | NOVEMBA, 2014 | 7.5235 | |
| | MEI, 2014 | 18.1465 | |
| | JANUARI, 2014 | 13.725 | |
| | SEPTEMBA, 2013 | 22.6 | |
| | DESEMBA, 2012 | 17 | |
| | JULAI, 2012 | 20.35 | |
| | DESEMBA, 2010 | 11.95 | |
| **ILEMELA** | OKTOBA-NOV, 2016 | 5.285 | |
| | APRILI-MEI, 2016 | 2.56 | |
| | NOVEMBA, 2015 | 1.835 | |
| | MACHI, 2015 | 3.55 | |
| | OKTOBA, 2014 | 3.575 | |
| | MEI, 2014 | 4.54 | |
| | JANUARI, 2014 | 3.5 | |
| | SEPTEMBA, 2013 | 9 | |
| | DESEMBA, 2012 | 7.3 | |
| | JULAI, 2012 | 15.32 | |
| | DESEMBA, 2010 | 8.2 | |

Hali hii ililazimu jamii ya kitaifa na kimataifa kuanzisha jitihada mbalimbali za kupambana na kudhibiti usambaaji wa gugumaji na ilihusisha mashirika kama ECOVIC, LVRLAC and LVEMP I & II na mengineyo. Hata hivyo ilijitokeza kuwa kila kukiwa na ukosefu wa fedha, gugumaji lilizaliana sana na hali kuwa mbaya kama zamani. Hii ilitokana na ukweli kuwa jitihada za awali hazikushirikisha jamii kumiliki mchakato mzima; kwani zilitumia zaidi utatuzi wa kitaalamu. Kudumu kwa tatizo hili ziwani kulileta maswali mengi kama; je jamii za wakulima na wavuvi zipo mstari wa mbele kukabiliana na tatizo hili? Pamoja na Jitihada zote za awalii, ni shughuli zipi za kijamii na kiuchumi ambazo zinaweza kumaliza tatizo hili katika jamii za wakulima na wavuvi? Kutatua mapungufu haya yote, Halmashauri ilianzisha Vikundi shirikishi (BMUs) ili kudhibiti magugu maji katika fukwe za Ziwa.




***Magugu maji Katika Ziwa Viktoria***

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuwezesha uondoaji sahihi wa magugu maji ziwani kama mbinu ya kuongeza shughuli za ustawi wa viumbemaji ziwani. Jitihada hii inatumia uzoefu wa Vikundi Shirikishi vya Ufukweni (BMUs) vya Sweya na Mkuyuni. Ili kufikia lengo hili, malengo mahsusi yafuatayo yalielekeza utekelezaji;

(i) Kuboresha kina cha maji ziwani, usafirishaji na utiaji nanga katika fukwe za ziwa Viktoria.

(ii) Kuboresha ubora wa maji ya ziwa kwa matumizi ya nyumbani na viwandani.

(iii) Kuboresha uvuvi na shughuli za ustawi wa viumbe maji ziwani ili kuwepo kwa uendelevu wa kipato wa jamii za wakulima wavuvi katika bonde la ziwa.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Ili kufikia malengo yaliyotarajiwa ya kudhibiti magugu maji katika Ziwa Viktoria, Halmashauri ilitekeleza mikakati mbalimbali. Kwanza, Halmashauri ilichukua jukumu la kuendesha mikutano katika ngazi mbalimbali za jamii ili kujenga uwezo na kuhamasisha ushiriki wa wadau. Halmashauri iliendesha mikutano ya Mitaa kujenga uelewa kati ya wanajamii na kwa namna hii kuimarisha umiliki wa jitihada. Baadaye maamuzi yaliyofanyika katika mikutano ya Mitaa yalifikishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata (KMK) kwa maamuzi zaidi na hatimaye kupitishwa na Baraza kwa ajili ya utekelezaji. Uamuzi ulipitishwa wa kuvishirikisha vikundi vya uangalizi wa fukwe (BMUs) kushiriki katika shughuli za udhibiti wa magugu maji kwa kuvipatia mafunzo kuhusu uondoaji wa magugu maji kibaolojia na kifizikia. Mikutano hii ilisababisha kuundwa kwa vikundi vingi vya uangalizi wa fukwe (BMUs). Vikundi hivi vilitarajiwa kudhibiti uvuvi haramu, kuhakikisha usalama ziwani na kutunza mazingira kwa kuyaondoa na kuyateketeza magugu maji. Halmashauri iliendelea kutoa mafunzo wa wanavikundi wa uangalizi wa fukwe. Mafunzo mbalimbali yaliendeshwa kuhusu utunzaji wa mazingira, uchakataji wa dagaa, usimamizi wa fedha, upangaji na usimamizi wa mipango na uendeshaji wa mikutano chini ya usaidizi wa mradi wa LVEMP II.

Mkakati mwingine muhimu ulikuwa uundaji wa katiba za vikundi; vikundi vyote vya uangalizi wa fukwe (BMUs) viliunda katiba ili kutoa miongozo kuhusu uongozi na shughuli za kila siku, wajibu na uwajibikaji wa viongozi na wanachama. Baada ya hapo, vikundi vilisajiliwa rasmi katika idara ya Maendeleo ya Jamii ya Jiji. Hii ilifuatiwa na kutambuliwa kwa maeneo (ardhi) ya vikundi na uanzishaji wa miradi ambapo kila kikundi kilipanga miradi yake na kuanisha ardhi itakayotumika. Ardhi iliyoainishwa ilitakiwa kuwa kwenye fukwe za ziwa ambapo makazi ya watu hayaruhusiwi.

Uondoaji wa magugu maji kibaiolojia kutumia mbawakavu (*Neochetina eichhorniae* na *N. bruchi*) ulitekelezwa kwa kutumia mtumbwi ulilonunuliwa kupitia mradi wa LVEMP II. Hili lilipata msukumo kutoka kwa viongozi wa vikundi kwa kushirikiana na wanafunzi wa FETA ambao hutumia zoezi hili kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo, baada ya masomo ya darasani. Mbawakavu hula magugu na ndicho chakula pekee wanachotumia. Mwanzoni, mbawakavu hufugwa kwenye mapipa ya plastiki ya lita 200 ambapo huzaliana na baada ya kipindi cha mwaka mmoja hupelekwa ziwani na mto Kagera. Kwa kutumia mbawakavu, kuzaliana (kusambaa) kwa magugu maji ziwani kumepungua kwa 80%. Idadi ya mbawakavu haiwezi kuongezeka siku zote. Chakula cha mbawakavu (magugumaji) kikipungua, mbawakavu huanza kufa. Kwa mfano mwaka 2012 Kikundi cha Sweya (BMU) kilijenga ofisi ya kikundi na eneo la kuzalisha mbawakavu, ofisi ya kazi na viwanja vya kukuzia mbawakavu, pamoja na ununuzi ya mtumbwi wenye injini wa kikundi kurahisisha usafiri wa ziwani wakati wa kutawanya mbawakavu.

Shughuli moja ya kuvutia ni uondoaji wa magugu maji wa moja kwa moja kwa kukusanya na kuzoa; Licha ya kudhibiti magugu maji kwa mbinu za kibaiolojia, kuna uondoaji wa moja kwa moja kwa kutumia mitumbwi; na katika hili, viongozi wa vikundi huandaa taratibu ili waendesha mitumbwi waingie ziwani kuvuna magugu maji, kuyabeba kwenye mitumbwi na kuyatupa nje ya fukwe. Wavunaji hawa hutumia sepeto kuvuna magugu maji na kuyatupa katika ardhi kavu mbali na ziwa ili yaoze. Kusaidia uondoaji huu wa magugu maji, kikundi (BMU) kilinunua mtumbwi, injini, matoroli, reki na vifaa vingine muhimu vya kuvunia magugu maji. Kikundi pia kilitoa mafunzo kuhusu namna ya kuyashughulikia magugu maji baada ya kuyatoa ziwani ili kuzuia kusambaa kwenye maeneo mengine. Pale inapowezekana, wanajamii wamekuwa wakishiriki katika uvunaji wa magugu maji. Katika kikundi cha Mbuyuni (BMU), vijana hupewa mikataba ya kuondoa magugu maji kutoka ziwani na kuyaozesha kwenye ardhi kavu, mbali na ziwa.

Ilikuwa muhimu kuanzisha ratiba za zamu za kufanya ukaguzi ziwani kugundua mapema kuwasili kwa magugu maji mapya, kiasi kilichoteketezwa na mbawakavu na udhibiti wa uvuvi haramu. Kila miezi mitatu, wanavikundi hutembelea maeneo ambayo mbawakavu wamewekwa na kukagua maendeleo ya uteketezaji wa magugu maji. Kuhusu magugu maji mapya yanayoingia ziwani, wanavikundi hutembelea maeneo hayo, hutathmini athari na kuandika taarifa ya tatizo. Taarifa hii hutumika kuamua mbinu inayofaa zaidi kuteketeza magugu maji. Aidha, wanavikundi huwa na ziara za mara kwa mara ziwani kudhibiti uvuvi haramu kwa kukagua nyavu na vifaa vya uvuvi.



***Wanakikundi (BMU) wakizoa magugu maji***

**5.0 RASLIMALI**

Udhibiti wa magugu maji katika Jiji la Mwanza ni jitihada ambayo iliunganisha wadau wengi tangu miaka ya 2000 chini ya mradi wa LVEMP I. Jitihada hii ilirithiwa na mradi wa LVEMP II ambao ulianza mwaka 2013 na kuimarisha vita dhidi ya magugu maji kupitia Kikundi cha Uangalizi wa Fukwe cha Sweya (BMU). Raslimali kwa ajili ya shughuli hii zilitoka Serikali Kuu, Jamii na Wahisani. Serikali ilitoa utaalam tangu awali na hatua mbalimbali zilichukuliwa kushirikiana na FETA ambayo ni taasisi ya utafiti wa viumbemaji. Taasisi hii ilikuwa mhuhimu kwenye ufugaji wa mbawakavu.

Maofisa wa Serikali walishiriki katika kuziandaa jamii kwa mikutano ya kujenga uelewa na iliyopelekea kuundwa kwa vikundi vya uangalizi wa fukwe (BMUs) pamoja na chaguzi za viongozi wa kusimamia shughuli za kila siku za vikundi. Maofisa wa Serikali walifanya kazi kwa karibu na viongozi wa jamii kuhakikisha kuwa ardhi inapatikana na kumilikishwa kwa vikundi ili kujenga ofisi na kuanzisha maeneo ya kufugia mbawakavu. Mikutano ya uhamasishaji iliyoendeshwa kabla ya jitihada hii iliimarisha hali ya umiliki wa jamii.

Wahisani kupitia mradi wa LVEMP II walitoa usaidizi fedha uliowezesha jamii kujenga ofisi ya kikundi (BMUs), yenye ubora, maji, umeme na samani. Aidha, fedha hizi zilitumika kununua mtumbwi, injini yake na vifaa vingine muhimu vya kuondolea magugu maji ziwani. Ili kukifanya kikundi kuwa endelevu, banda la kukaushia dagaa lilijengwa katika eneo la kikundi. Shughuli zote hizi ziligharimu TZS 53,000,000/=, ukiondoa raslimali nyingine zilizokuwepo kwenye eneo. Usimamizi wa mradi unafanywa kwa pamoja kati ya jamii kupitia kikundi (BMU) na maofisa wa Halmashauri; FETA hutoa utaalamu kuhusu udhibiti wa kibaolojia.

Mchakato mzima wa kudhibiti magugu maji ziwani hutegemea nguvukazi ambayo hutolewa na Kikundi cha Sweya (BMU). Pamoja na changamoto mbalimbali kama vile ukosefu wa uhakika wa posho za mwezi, mafanikio haya yanatokana na umiliki, umoja na kujitoa kwa viongozi wa kikundi katika ngazi mbalimbali.

**Jedwali 2: Raslimali Fedha**

| Shughuli | Fedha (TZS) | Chanzo | Kikundi (BMU) |
|---|---|---|---|
| Utunzaji wa mazingira (ununuzi ya mtumbwi, vifaa vya afya, ujenzi wa ofisi, ujenzi mabanda ya kukaushia dagaa,mapipa ya kufugia mbawakavu na mafunzo) | 47,800,000 | LVEMP II | SWEYA |
| | 5,200,000 | SWEYA BMU | SWEYA |
| Mafunzo na kujenga uwezo | 5,000,000 | LVEMP | MKUYUNI |
| Ununuzi wa Mtumbwina vifaa vyake, reki na matoroli | 9,000,000 | LVEMP | MKUYUNI |
| Ujenzi wa ofisi na vyoo | 17,000,000 | LVEMP | MKUYUNI |
| Ujenzi wa ofisi na vyoo | 1,000,000 | MKUYUNI BMU | MKUYUNI |
| Utaalamu wa usimamizi na ufuatiliaji | | Halmashauri ya Jiji la Mwanza | SWEYA & MKUYUNI |
| Ardhi na vifaa vya ujenzi | | Jamii | SWEYA & MKUYUNI |
| Nguvu kazi na utaalam | | FETA | SWEYA & MKUYUNI |
| Nguvu kazi | | Wanachama BMU | SWEYA & MKUYUNI |

**6.0 MATOKEO**

Shughuli za vikundi vya uangalizi wa fukwe (BMUs) katika udhibiti wa magugu maji zimeleta matokeo mbalimbali katika ziwa lenyewe na mazingira yake. Jitihada iliyofanywa na vikundi hivi imewezesha udhibiti endelevu wa kuenea kwa magugu maji ziwani na katika fukwe, hivyo kuwepo kwa mazingira safi kwa shughuli za uvuvi na kupungua kwa maeneo ya mazalio ya wanyama hatari. Pale ambapo mitumbwi haitumiki kupeleka mbawakavu ziwani au uondoaji wa magugu maji, hukodishwa kwa wavuvi ili kuongeza pato kwa ajili ya shughuli nyingine.

Halmashauri na Jamii ya Mwanza imeshuhudia kuimarika kwa shughuli za uvuvi ziwani kutokana na kuongezeka kwa maeneo safi ya kuzaliana samaki yanayoruhusu samaki wachanga kukua kwa uhakika. Aidha, pamekuwepo na urahisi wa kutembea kwa vyombo vya usafiri wa maji na utiaji nanga kwa mitumbwi, vivuko na meli katika ziwa. Uwepo wa Vikundi vya uangalizi wa fukwe (BMUs) umeimarisha ushirikiano na mamlaka nyingine kama TAFIRI na kitengo cha udhibiti wa uvuvi Jijini Mwanza katika kukamata wavuvi ambao hutumia nyavu haramu na sumu.

Jitihada hii imesaidia kukuza ajira kupitia biashara ndogondogo kama za chakula (mama lishe) na shughuli nyingine za kijasiriamali zinazohitajiwa na wavuvi, uvuvi wa dagaa kwa niaba ya vikundi (BMUs), utoaji wa magugu maji na ukusanyaji wa ada za huduma katika vyoo na vitega uchumi vya vikundi. Pamoja na hayo, wanavikundi hutoa misaada ya fedha kwa ajili ya shughuli za mitaa na miradi ya maendeleo, hivyo kuimarisha ushirika na jamii. Kutokana na uimara wa vikundi hivi, wanavikundi wanafaidika kwa kupata mikopo yenye masharti nafuu kwa kutumia akiba zao.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuwepo kwa uendelevu wa mafaniko yaliyopatikana, ni muhimu hatua zifuatazo za kijamii, kiuchumi, kimazingira na kitaalamu zichukuliwe;

(i) Ushiriki kamilifu wa wanafunzi wa FETA katika miradi kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo utasaidia uhakika wa uzalishaji wa mbawakavu ambao watakuwa wanapelekwa ziwani kila miezi mitatu ili kuharibu magugu maji yaliyoota upya.

(ii) Ruhusa iliyotolewa kwa viongozi wa vikundi wa kutumia mtumbwi kuongeza kipato hutia hamasa viongozi na hivyo kuongeza juhudi katika jitihada hii.

(iii) Ofisi ya Kikundi (BMU) hutumika kama eneo la kuchakata dagaa na ofisi ya Mtendaji wa Mtaa ambavyo huimarisha umiliki na kuimarisha usalama katika eneo hili.

(iv) Kuendelea kudhibiti shughuli za kilimo cha mbogamboga karibu na fukwe kutokana na ukweli kuwa mbolea za viwandani zitumikazo mashambani huchochea kasi ya ukuaji wa magugu maji kipindi cha mvua.
(v) Uchafu kutoka kwenye makazi unaoingia ziwani kupitia mito kama Mirongo, Mkuyuni, na vijito vingine kutoka Igogo/Pamba unadhibitiwa.
(vi) Kuendelea kuhamasisha ushiriki wa wavuvi katika kuzalisha na kutumia mbawakavu ili kupunguza nakisi iliyopo kwenye uzalishaji wa mbawakavu unaofanywa na FETA na Vikundi; hii itaongeza eneo linawekewa mbawakavu.
(vii) Kuendelea kusimamia sheria ndogo zinazozuia matumizi ya magugu maji kama maua ya kupendezesha mazingira.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Sababu za mafanikio ya udhibiti wa magugu maji katika fukwe za Ziwa Viktoria ndani ya Jiji la Mwanza zimechangiwa na mambo yafuatayo;

(i) Ushiriki hai wa jamii, elimu na umiliki wa mchakato wote.
(ii) Uwepo wa ushiriki wa karibu wa taasisi za utafiti na hali ya kushirikishana utaalam kati ya FETA na taasisi nyingine za utafiti katika eneo hili.
(iii) Ushirika wa kutegemeana. Mtumbwi hutia nanga katika eneo la TAFIRI ambapo kuna usalama wa kutosha ili hali jengo la Kikundi (BMU) hutumiwa pia na Afisa mtendaji wa Mtaa. Ushirikiano huu huwezesha shughuli kufanyika kikamilifu.
(iv) Kujituma kikamilifu kwa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kumechochea mafanikio ya jitihada hii.
(v) Uwepo wa uhuru wa maamuzi katika kutumia fedha zilizotokana na misaada ya mradi wa LVEMP II uliwafanya viongozi wa vikundi kuwa watekelezaji na wawajibikaji.
(vi) Usimamizi thabiti wa sheria ndogo inayozuia watu kutumia magugu maji kama maua na matumizi mengine.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA


**JITIHADA ZA KIJIJI KATIKA KUBORESHA UTOAJI WA HUDUMA**




*Uzoefu wa Kijiji cha Nyakagwe*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Geita ni mojawapo ya Halmashauri 6 mkoani Geita na ipo katika mwinuko wa kati ya 1,100m hadi 1,300m juu ya usawa wa bahari, katika Latitudo $2^{o}8$ hadi $3^{o}28$ Kusini na Longitudo $32^{o}45$ to $37^{o}$ Mashariki. Halmashauri hii inapakana na Halmashauri za Wilaya za Muleba (Kaskazini), Sengerema na Misungwi (Mashariki), Kahama, Mbogwe na Bukombe (Kusini) na Biharamulo na Chato (Magharibi). Halmashauri ina eneo la $7{,}825km^2$ ambapo $6{,}775km^2$ ni ardhi $1{,}050km^2$ maji ya Ziwa Viktoria. Hali ya hewa ni wastani wa $17^{o}C$ na $30^{o}C$, na wastani wa mvua wa 1200mm kwa mwaka. Halmashauri hii ina Tarafa 4, Kata 37, Vijiji 145 na Vitongoji 626.




**Ramani ya H/W ya Geita (Kabla ya kugawanywa)**

Kijiji cha Nyakagwe kilichopo katika Kata ya Butobela ni mojawapo ya vijiji 145 vya H/W ya Geita. Kijiji kilianzishwa mwaka 1995 baada ya kupandishwa hadhi kutoka kuwa Kitongoji cha Kijiji cha Butobela. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Kijiji cha Nyakagwe kina jumla ya wakazi 4,331. Kijiji kimejaliwa kuwa na hifadhi ya dhahabu, hivyo shughuli kuu za kiuchumi ni uchimbaji wa dhahabu (70%), kilimo (20%) na Biashara (10%).

**2.0 TATIZO**

Kijiji cha Nyakagwe kilishuhudia hitaji kuu la huduma za utawala, afya, elimu na usalama kijijini lakini fedha zilizopatikana toka Halmashauri na Serikali kuu hazikutosha kutimiza mahitaji ya Jamii ambayo yalikuwa yakiongezeka. Kama kitovu cha uchimbaji wa madini, Kijiji cha Nyakagwe kimekabiliwa sana na ukuaji kasi wa idadi ya watu. Kijiji kilipoanzishwa mwaka 1995, idadi ya watu ilikuwa kati ya 600-1,000 ikilinganishwa na idadi ya watu ya siku za karibuni ya 4,331. Sababu kubwa ya ongezeko hili kasi la idadi ya watu ni uhamiaji wa watu kutoka maeneo mbalimbali wanaotafuta fursa ya uchimbaji wa dhahabu. Kama ilivyoelezwa na Afisa Mtendaji wa zamani wa Kata ya Butobela, ambaye pia aliishi Kijijini Nyakagwe tangu mwaka 1991; uhamiaji wa aina mbalimbali za watu kuingia kijijini uliambatana na changamoto nyingi kama uhalifu wa wizi na ujambazi wa kutumia silaha. Taarifa zinaonesha kuwa ujambazi wa kutumia silaha ulikuwa ukitokea kila baada ya wiki mbili.

Kwa mujibu wa mhudumu wa zahanati ya Nyakagwe, uhamiaji kasi wa watu uliambatana na kuenea na kuongezeka kwa magonjwa hasa UKIMWI, malaria, maambukizi ya kifua, maambukizi ya njia ya mkojo, upungufu wa damu na magonjwa ya zinaa; magonjwa haya yaliongoza. Ongezeko la watu na ushiriki katika uchimbaji madini ulioshirikisha pia watoto vilichangia uandikishaji duni katika shule za msingi. Kwa mfano, mwaka 2011 ni watoto 119 tu wenye umri wa kwenda shule waliandikishwa kuanza darasa la kwanza ikilinganishwa na watoto 283 mwaka 2016 baada ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu. Changamoto hizi ziliathiri maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya kijiji.

Watoto wa shule katika Kijiji cha Nyakagwe walikuwa wakitembea kwa miguu 4km kuhudhuria masomo katika Shule ya Msingi Butobela. Mara kwa mara wanafunzi walikabiliwa na jua, mvua, mafuriko na wanyama wakali. Hii ilichangia kuongezeka kwa utoro na ufaulu duni wa wanafunzi. Kijiji pia kilikuwa na changamoto nyingi za kiafya; wakazi wa Nyakagwe hasa wanawake wajawazito na watoto walilazimika kutembea takribani 14km kwenda zahanati ya Bukoli katika Kata ya Bukoli kupata huduma za afya. Wakati mwingine walilazimika kufuata huduma za afya 5km katika H/W ya Nyang'hwale; Halmashauri jirani.

Kijiji kikiendeshwa na uongozi shupavu na usiotetereka kiligundua kuwa kwa kuitegemea tu Halmashauri, ikizingatiwa uhaba na kukosekana uhakika wa ruzuku ya maendeleo, kama ilivyo kwa vijiji vingine, kijiji hiki kingesubiri kwa miaka mingi kuboresha huduma.

**3.0 LENGO**

H/W ya Geita inatambua kuwa kama watu wataongozwa kikamilifu na kutiwa moyo, wanao uwezo wa kufanya mambo mengi katika ujenzi wa shule za msingi, zahanati na barabara; na kuzikarabati. Kijiji cha Nyakagwe kimethibitisha hili kama moja ya vijiji vichache ambavyo vimeweza kuboresha huduma za jamii kwa kujenga miundombinu bora ya shule, zahanati na kituo cha polisi kwa kutumia jitihada za jamii. Miundombinu hii imekuwa na matokeo dhahiri katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya kijiji hiki. Mwaka 2000 Kijiji cha Nyakagwe kwa kusaidiwa na Halmashauri na wadau wengine wa maendeleo kiliamua kujenga uwezo wa wanajamii ili kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutekeleza malengo yafuatayo;

(i) Kuboresha huduma za utawala kwa kujenga jengo la kisasa la ofisi ya Serikali ya Kijiji.
(ii) Kupunguza matukio ya wizi na ujambazi wa silaha kwa kujenga kituo cha kudumu cha polisi.
(iii) Kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa kujenga zahanati ya kijiji.
(iv) Kuongeza uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule kwa kujenga shule ya msingi ya kijiji.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Baada ya kuziainisha changamoto, Kijiji kiliamua kutumia jitihada za jamii kutatua changamoto hizo. Baadaye, Jitihada hizi ziliungwa mkono na Halmashauri na wadau wengine wa maendeleo. Upekee wa mbinu hii umejikita katika asili ya mikakati iliyotumika kutekeleza miradi. Kijiji cha Nyakagwe kiliazimia kukabiliana na changamoto hizi kwa kutumia mfumo wa kuitikia mahitaji ya jamii yenye uelewa wa mahitaji na ipo tayari kuchangia. Jitihada hizi zimeelezwa kwa kina hapa chini.

Ujenzi wa madarasa matatu; wazo la kujenga shule ya msingi Nyakagwe lilianza mwaka 2000 baada ya kijiji kusajiliwa. Afisa Mtendaji wa Kijiji wa kujitolea (mwaka 2000), Mbunge na baadhi ya wachuuzi wadogo wa madini walianza kujenga madarasa matatu na ofisi mbili za walimu. Katika utekelezaji wanakijiji wote walichangia kwa hiari kiasi cha chini kikiwa TZS 3,500 kwa kila mtu mzima. Wakati wa ujenzi kila Kitongoji kilishiriki kwa makundi kukusanya mawe na kuchimba mashimo kwa ajili ya vyoo vya shule. Kupitia mpango wa MEM, Halmashauri ilichangia mabati, mbao na saruji kukamilisha ujenzi.

Baada ya kukamilisha ujenzi, Halmashauri ilipeleka mwalimu mmoja na kumhamisha mmoja kutoka shule ya msingi Butobela kwenda shule mpya ya msingi ya Nyakagwe. Shule ilizinduliwa mwaka 2000 ikiwa na walimu wawili.

Ujenzi wa madarasa mengine; mwaka 2009 Serikali ya kijiji ilipata eneo kwa ajili shughuli za uchimbaji mdogo wa madini. Eneo hili lilikodishwa kwa wachimbaji wadogo na kuwezesha kijiji kukusanya mapato. Baadhi ya mapato yalitengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu. Viongozi wa Kijiji waliamua kukopa mabati katika duka moja la mfanya biashara maarufu ndani ya kijiji. Halmashauri ilichangia TZS 7.2 milioni ambazo zilitumika kununua madawati kwa ajili ya madarasa matatu yaliyokamilika.

Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa soko la kijiji; mwezi Machi, mwaka 2010 kijiji kilinunua kipande cha ardhi kwa ajili ya kujenga soko, eneo ambalo baadae liligundulika kuwa na hifadhi kubwa ya dhahabu. Badala ya kujenga soko kwenye eneo hili lenye hifadhi ya dhahabu, viongozi wa kijiji waliamua kuikodisha kwa wachimbaji. Uamuzi huu ulisaidia kijiji kukusanya kiasi kikubwa cha mapato na kuyatumia kukamilisha ujenzi wa madarasa; na kufanya shule ya msingi Nyakagwe kuwa na madarasa tisa, ofisi mbili za walimu, vyoo vya kisasa na nyumba mbili za walimu.

Kuimarisha ukusanyaji wa mapato; kwa kukodisha ardhi kwa wachimba madini, kijiji kiliimarisha ukusanyaji wa mapato na kupata mapato ya juu kuzidi vijiji vingi nchini Tanzania. Kwa mfano, mwaka 2010 akaunti za kijiji kwenye benki za NMB na CRDB zilikuwa na jumla ya TZS 120 milioni.

Ujenzi wa majengo ya kutolea huduma; mwaka 2010 viongozi wa kijiji walipitisha uamuzi wa kununua ardhi katikati ya kijiji na kujenga jengo kubwa lenye nafasi ya kutosha la ofisi ya kijiji. Viongozi na wanakijiji walikubaliana kujenga zahanati ili kukabiliana na kuporomoka kwa huduma za afya kijijini. Mwaka 2011, ujenzi wa zahanati ya kijiji na nyumba ya watumishi wa zahanati ulikamilika. Mwaka 2012 Halmashauri ya Kijiji ilianza ujenzi wa kituo cha polisi cha kijiji kwa lengo la kuimarisha usalama na ulinzi. Ikumbukwe kuwa kijiji kilishuhudia uvamizi wa mara kwa mara uliofanywa na vibaka na majambazi waliojaribu kuwaibia wachuuzi wa dhahabu. Ofisi ya Polisi Wilaya ilitoa ramani ya jengo na baada ya kukamilika kwa ujenzi polisi watatu walipangiwa kituo hicho mara moja. Kabla ya hapo jamii na walanguzi wa dhahabu walichangia kodi za nyumba na posho ya chakula kwa ajili ya polisi. Kwa sasa kijiji cha Nyakagwe kimekamilisha ujenzi wa kituo cha polisi kikiwa na nyumba mbili za watumishi.

Utekelezaji huu ndio huitwa jitihada dhahiri za jamii kwani sehemu kubwa ya fedha kwa ajili ya miradi ni michango ya jamii. Pamoja na michango ya kifedha, jamii ilishiriki kikamilifu katika kukusanya vifaa vya ujenzi na kutoa nguvukazi kipindi cha ujenzi wa madarasa, ofisi ya kijiji, zahanati na kituo cha polisi.

Mbinu hii bora ya kijiji cha Nyakagwe inaonesha namna ambavyo vijiji vinaweza kutumia kwa ufanisi jitihada za jamii na misaada kutoka kwa wadau wengine wa maendeleo, kuboresha huduma ili kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hii ni kwa sababu vijiji vyote vya H/W ya Geita vina raslimali mbalimbali ambazo huvipa fursa kubwa kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kijiji cha Nyakagwe kimeweza kujitokeza kati ya vijiji vyote kwa kufanikiwa kutumia raslimali zake kuboresha huduma na fursa ya maendelo.

**5.0 RASLIMALI**

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kijiji ilihitaji raslimali fedha na watu. Hata hivyo jamii ilitambua kuwa fedha zisingepatikana mapema kutoka Halmashauri au Serikali Kuu. Iliamuliwa kuwa fedha zinazohitajika zipatikane kupitia michango ya jamii. Fedha kutoka Halmashauri na wadau wengine wa maendeleo zitumike kujazia jitihada ya jamii.

**Jedwali 1: Michango ya Wadau**

| Mradi | Chanzo cha Fedha | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Jamii | Wadau | Halmashauri | SK | Jumla |
| **Ofisi ya Kijiji** | 36,105,000 | - | - | - | 36,105,000 |
| **Zahanati na nyumba 2** | 97,800,000 | - | 26,000,000 | - | 123,800,000 |
| **Kituo cha Polisi na Nyumba 1** | 65,723,800 | 7,600,000 | | | 73,323,800 |
| **Madarasa na vyoo** | 105,666,000 | - | - | - | 105,666,000 |
| **Nyumba 2 pacha** | 46,766,000 | | | | 46,766,000 |
| **Jumla** | 352,060,800 | 7,600,000 | 26,000,000 | - | 385,660,800 |

## 6.0 MATOKEO

Jitihada ya Kijiji cha Nyakagwe imeboresha utoaji wa huduma za utawala kwa jamii. Jitihada hii ya kuboresha huduma za utawala ilifanikiwa kupitia ujenzi wa ofisi ya kijiji iliyopelekea kuimarika kwa ubora na ufanisi wa huduma za utawala zitolewazo kijijini. Wengi wa wananchi waliohojiwa walikuwa na maoni kuwa ujenzi wa ofisi ya kisasa ya kijiji umeomgeza nafasi ya mikutano ya Serikali ya kijiji, umepunguza mwingiliano kati ya Mwenyekiti na Afisa Mtendaji wa Kijiji, umeongeza demokrasia, umeboresha utoaji wa huduma na umeimarisha ulinzi na usalama wa nyaraka.




***Ofisi ya Kisasa ya Kijiji cha Nyakagwe***

Akiongelea ofisi ya kijiji, Mwenyekiti alisema, *"kabla ya ujenzi wa ofisi hii tulikuwa na chumba kimoja tu cha kukodi tulichotumia kama ofisi ya mwenyekiti na afisa mtendaji wa kijiji. Lakini kama unayoona katika jengo hili Mwenyekiti ana ofisi tofauti na ya Afisa Mtendaji. Tuna ukumbi huu mzuri wa mikutano ambapo tunakaa kuendesha mikutano kufanya maamuzi muhimu. Nyaraka sasa zinatunzwa kwa usalama. Kama mtu anataka kuongea na Mwenyekiti au Afisa Mtendaji, sasa inafanyika kwa faragha"*

Maoni ya Mwenyekiti yaliungwa mkono na mjumbe mmoja wa serikali ya kijiji ambaye alisema *"ujenzi wa ofisi hii umekuwa na faida kubwa. Umetuondolea adha ya kupanga chumba kwa matumizi ya ofisi. Pia shughuli za usalama "Sungusungu" wetu zimeboreshwa kwa sababu wamepata nafasi ya ofisi kwenye vyumba vya pembeni vya jengo hili.*

Tokeo jingine kuu la jitihada hii ya jamii katika kuboresha huduma za afya ni kijiji kumiliki zahanati ya kisasa. Kwa mujibu wa wananchi waliohojiwa, ujenzi wa zahanati umeleta mabadiliko makuu kwani huduma za msingi za afya zinapatikana masaa 24 kwa wakazi wa Nayakagwe ndani ya mzingo wa 1km.

Zahanati pia inahudumia vijiji vya jirani na imepunguza kwa kiasi kikubwa vifo hasa vya akina mama na watoto.



***Zahanati ya Kijiji cha Nyakagwe***

Zahanati pia imerahisisha utoaji wa chanjo; zahanati imeongeza utoaji wa chanjo kwa 99% kwa watoto wanaotakiwa kupata chanjo kwenye muda unaotakiwa. Zahanati pia inatoa huduma za kifua kikuu na UKIMWI ambazo zilipatikana Hospitali ya Mji wa Geita tu.

Ongezeko la uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule; jitihada ya jamii ya Nyakagwe kujenga shule ya msingi ya kijiji imefanikiwa kuongeza uandikishaji kutokana na maboresho katika urahisi wa kufika shuleni, mazingira ya kujifunzia na ushiriki wa wazazi. Kwa mujibu wa wanakijiji waliohojiwa, shule imeleta mabadiliko katika maisha ya kiuchumi kwa sababu imepunguza mzigo wa kusindikiza watoto kwenda Butobela kwa hofu ya vibaka, wanyama, mvua na mafuriko. Akichangia kwenye hili, afisa mtendaji wa zamani, wa Kata ya Butobela, pia mkazi wa Kijiji cha Nyakagwe alisema, *"kabla ya kuwepo kwa shule hii hali ilikuwa mbaya sana, kwamba siku hizo tulilazimika kuwakusanya waoto wetu kanisani na kujitolea kuwafundisha".* Kwa ujumla uwepo wa shule umepunguza sana utoro, umeboresha ufaulu, umeongeza uandikishaji wa watoto wa shule ya awali na msingi na umeimarisha afya za watoto.



***Shule ya Msingi ya Kijiji cha Nyakagwe***

Mazingira bora ya kufanyia kazi; ujenzi wa shule, zahanati na kituo cha polisi vilienda sambamba na ujenzi wa nyumba za watumishi. Makazi haya yameboresha mazingira ya kufanyia kazi kwani watumishi wanao uhakika wa kuishi karibu na vituo vya kazi.



***Nyumba pacha za watumishi wa zahanati ya Kijiji cha Nyakagwe***

Akitoa maoni kuhusu jitihada hizi, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyakagwe alikuwa na haya ya kusema,*"moja ya mambo ambayo hufanya mazingira ya kazi kuwa magumu hasa kwa walimu ni kukosekana kwa makazi. Nyakagwe ni kituo changu cha pili cha kazi tangu kuhamishiwa H/W ya Geita. Nafahamu jinsi walimu wanavyoteseka kutokana na ukosefu wa nyumba. Hapa, hali ni tofauti kabisa. Jamii inatambua umuhimu wa makazi ya watumishi na waliazimia kujenga nyumba za watumishi kupitia michango ya jamii. Hii inafanya mazingira ya kazi kuwa na motisha zaidi na hivyo kuvutia watumishi kupenda kuishi na kufanya kazi kwenye kijiji hiki".*

Kuimarika kwa Usalama; usimamizi wa sheria, usalama na amani katika kijiji umeimarika kutokana na ujenzi wa kituo cha polisi cha kijiji. Hii ni zaidi ya mazoea kuwa vituo vya polisi kawaida vinakuwepo kwenye makao makuu ya Tarafa tu. Mkuu wa kituo cha polisi alisema, *"ujenzi wa kituo hiki ulikuwa wa lazima ili kukanbiliana na ujambazi wa silaha wa mara kwa mara uliotishia amani na usalama kijijini. Hali ya uhalifu imedhibitiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuwepo kwa polisi wachapakazi kijijini".*



***Kituo cha Polisi na Nyumba ya Watumishi kijijini Nyakagwe***

Kituo cha polisi kimeleta mabadiliko makubwa katika masuala ya amani na usalama kijijini. Kwa mujibu wa wanajamii, matukio ya wizi na ujambazi wa kutumia silaha vimepungua sana. Akitoa maoni kuhusu hili, mfanya biashara mmoja alisema ,*"tangu tukio la mwaka 2011 lililosababisha kifo cha mfanya biashara mmoja, hapajatokea ujambazi wa kutisha tena".*

Kuimarika kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi; matokeo ya jumla yanayoambatana na maboresho katika huduma za utawala, jamii na usalama yanaonekana dhahiri katika kuimarika kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Haya yanadhihirika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kwa mfano, kijiji kimeshuhudia kupanuka kwa maduka ya jumla, maduka ya rejareja na stoo za vifaa vya ujenzi. Nyumba za kisasa ambazo zinatarajiwa kuonekana katika miji mikuu sasa zipo kijijini. Huduma kama umeme, simu za mikononi na huduma za fedha kimtandao zimesheheni kijijini, vyote vikidhihirisha ustawi wa jamii, ulinzi na usalama na uchumi changamfu. Kijiji pia kimefaidika na kuongozeka kwa uwekezaji; kwa mujibu wa viongozi wa kijiji, kumekuwa na ongezeko la uwekezaji katika sekta za ujenzi, biashara za rejareja na uchimbaji wa madini. Hii ina maana kuwa watu wameridhika na huduma bora, na wanaamini ni salama kuwekeza Nyakagwe.

Mwisho, kijiji hiki kimekuwa kijiji cha mfano katika vijiji vya jirani vya H/W ya Geita, Nyang'whale na Kahama. Mwaka 2014 Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyakagwe alialikwa kufanya majadiliano na Mwenyekiti wa H/W ya Kahama kuhusu siri za mafanikio ya Kijiji chake.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Kujihakikishia uendelevu, kijiji kimebuni mikakati mbalimbali. Mkakati mmoja ni kupima ardhi yote ya kijiji. Upimaji huu utasaidia kijiji kuwa na mapato endelevu kutoka kwenye ardhi ya machimbo inayomilikiwa na Kijiji. Kijiji kipo tayari kwa maboresho zaidi katika ukweli na uwazi. Hili linatarajiwa kufikiwa kwa kuhakikisha kuwa mikutano yote ya umma inafanyika mara kwa mara na inahudhuriwa na watu wazima wote kijijini. Aidha, licha ya kubandika taarifa za fedha kwenye mbao za matangazo, wajumbe wote hupatiwa taarifa hizo ili kuendeleza uaminifu na usaidizi.

Mkakati mwingine muhimu ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato; hili litafanikishwa kwa kuwashirikisha wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji katika kukusanya mapato kwenye vyanzo vilivyopo kwa zamu. Motisha itatolewa kwa wakusanyaji kwa asilimia ya kiasi kilichokusanywa. Utekelezaji utafanyika ndani ya mipango ya kuhakikisha kuwa miamala yote ya fedha inafanyika na kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo za fedha na manunuzi. Kijiji pia kina mpango wa kuhakikisha viongozi wote wanapata mafunzo ya misingi ya usimamizi wa fedha na uandishi wa taarifa za fedha. Mpango wa mafunzo utatekelezwa kwa kushirikiana na idara ya fedha na biashara ya H/W ya Geita.

Kijiji kimeweka mkakati wa kuanzisha kituo cha kuwapatia vijana fursa ya kujifunza stadi mbalimbali za ufundi ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya jamii. Shughuli hii itaimarisha hali ya uchumi ya kijiji na kuzalisha ajira.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kama ilivyoelezwa na Serikali ya Kijiji siri ya mafanikio ya jitihada hii inajumuisha:

(i) Uwepo wa migodi ya dhahabu; kijiji kina hazina kubwa ya dhahabu.
(ii) Uamuzi wa kukodisha ardhi yenye hazina ya dhahabu na ukusanyaji bora wa mapato.
(iii) Utayari wa wanajamii kuchangia maendeleo yao. Wanajamii wamekuwa mstari wa mbele kuanzisha mipango ya maendeleo na kuchangia raslimali fedha na vitu kukamilisha utekelezaji.
(iv) Uongozi wa kijiji ulio imara na wenye kujituma; wakazi wengi waliohojiwa walihusisha mafanikio haya na kujituma kwa mwenyekiti na afisa mtendaji wa kijiji.

(v) Ukusanyaji fanisi wa mapato na udhibiti madhubuti wa matumizi; hii ilisaidia kuhakikisha malipo yote yanafanyika kwa wakati na miradi kukamilika kwa muda.

(vi) Kutumia mafundi wa Kijijini badala ya wakandarasi katika miradi ya ujenzi; suala hili lilichangia sana mafanikio, kwa kuwa na gharama za chini za utekelezaji.

(vii) Ufuatiliaji wa karibu; ufuatiliaji shirikishi na wa karibu (Halmashauri na Jamii) ulitumika muda wote kuhakikisha thamani ya fedha inafikiwa kwenye utekelezaji wa miradi.

(viii) Mikutano ya kijiji ya mara kwa mara; kwa kuendesha mikutano yote ya kisheria; masuala yote yaliyojitokeza yalifanyiwa maamuzi katika mikutano na kuwezesha utekelezaji kuendelea. Mbinu hii iliimarisha imani ya jamii kwa uongozi wao.

(ix) Nafasi ya Kamati za Kudumu; kamati huwa na nafasi muhimu sana katika kuwezesha utekelezaji wa miradi iliyopangwa. Zoezi hili hufanyika kwa kuitisha mikutano ya mwezi ambapo mapendekezo hutolewa kuhusu maendeleo ya miradi.

(x) Motisha kwa wakusanyaji wa mapato; 10% ya mapato yaliyokusanywa hutolewa kama motisha kwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wanaokusanya mapato kwenye vyanzo vilivyopo.

(xi) Ushiriki wa jamii katika kila mpango wa maendeleo utakaotekelezwa kijijini na uwasilishaji wa maendeleo ya miradi na taarifa za fedha kwenye vikao vya kijiji.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO

**JITIHADA ZA JAMII KATIKA KUANZISHA SHULE SHIKIZI**



*Uzoefu wa H/W ya Chato*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Chato ni mojawapo ya Halmashauri 6 za Mkoa wa Geita. Halmashauri nyingine ni Geita, Bukombe, Nyang'wale, Mbogwe na Mji wa Geita. H/W ya Chato ilianzishwa baada ya kuigawa H/W ya Biharamulo iliyopo Mkoa wa Kagera, mwaka 2007. Halmashauri inapatikana Latitudo $2^0$ 15' – $3^0$ 15' Kusini na Longitudo $31^o$ – $32^o$ Mashariki, ikiwa kwenye mwinuko kati ya 1135m – 1410m juu ya usawa wa bahari. Halmashauri ina eneo la 3,572$km^2$ ambalo ni nchi kavu na 100$km^2$ ni Ziwa Viktoria. Kiutawala, H/W ya Chato ina Tarafa 5 za Buzirayombo, Buseresere, Kachwamba, Bwanga and Nyamirembe, Kata 23, Vijiji 115 na Vitongoji 548. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina wakazi 365,127 (181,368 wanaume na 183,759 wanawake). Zaidi ya 80% ya wakazi hufanya shughuli za kilimo, uvuvi na uchimbaji wa madini. Mazao ya chakula ni pamoja na mpunga, mahindi, muhogo, kunde, viazi vitamu na karanga. Mazao ya bishara ni pamba na alizeti. Shughuli nyingine za kiuchumi ni ufugaji, ufugaji nyuki, biashara ndogondogo na utunzaji wa misitu.

Halmashauri ina shule za msingi 128 ambazo 3 ni za binafsi. Jumla ya wanafunzi katika Kata zote 24 ni 104,384. Idadi ya walimu ni 1,862 ambapo 1,230 ni wanaume na 632 ni wanawake. Takwimu zinaonesha kuwa uandikishaji wa wanafunzi umeongezeka kutoka 12,814 mwaka 2007 hadi 22,421(57%) mwaka 2016 kama ilivyo kwenye jedwali 1 hapa chini.

**Jedwali 1: Mtiririko wa Uandikishaji Shule za Msingi**

| Mwaka | Uandikishaji | | Jumla | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| | wavulana | wasichana | | |
| 2007 | 6,673 | 6,141 | 12,814 | 105 |
| 2008 | 6,793 | 6,519 | 13,312 | 111 |
| 2009 | 6,593 | 6,370 | 12,963 | 100 |
| 2010 | 6,340 | 6,298 | 12,638 | 109 |
| 2011 | 7,174 | 6,606 | 13,780 | 108 |
| 2012 | 6,941 | 6,652 | 13,593 | 100 |
| 2013 | 7,650 | 7,264 | 14,914 | 110 |
| 2014 | 7,473 | 7,148 | 14,621 | 98 |
| 2015 | 8,387 | 8,269 | 16,656 | 113 |
| 2016 | 11,411 | 10,954 | 22,421 | 133 |

Halmashauri ina vituo vya mafunzo ya maarifa ya nyumbani na ufundi. Vituo vya mafunzo ya ufundi vipo kwenye maeneo ya shule za msingi. Vituo hivi ni vya Chato, Kibehe na Bwanga. Vituo vya mafunzo ya maarifa ya nyumbani vipo shule za msingi za Chato na Kibehe. Vituo hivi ni muhimu katika kuimarisha kujiajiri.

**2.0 TATIZO**

Shule shikizi ni mwendelezo wa shule mbali na shule ya msingi mama katika vijiji na vitongoji vipya. Shule hizi husaidia kutoa elimu kwa watoto katika jamii mpya zenye ongezeko kubwa la watu. Jamii zenyewe hujenga shule na huanza kutafuta usajili wakati wanafunzi wakiendelea kupata elimu karibu na jamii; mara nyingi kwa kutumia walimu wa kujitolea. Shule hizi zinakuwa hazijasajiliwa hivyo si vituo vya mitihani; zimeunganishwa kwenye shule za msingi "mama". Kimsingi, uandikishaji katika shule hizi hutokana na ongezeko la watu, umbali kutoka shule mama, shughuli za kiuchumi za wazazi na ugumu wa mazingira. Miundombinu ya shule shikizi hujengwa na jamii na huwa si ya kutosha kwani wanafunzi hubanana katika madarasa madogo na mara nyingi hayana madawati.

Kati ya mwaka 2007 na 2012, idadi wa watu katika H/W ya Chato iliongezeka sana. Mwaka 2007 idadi ya watu ilikuwa 251,264 wakati mwaka 2012 iliongezeka na kufikia 365,127. Hii ina maana kuwa kulikuwa na ongezeko la watu la juu la 43.3% kati ya sensa za kitaifa za mwaka 2002 na 2012. Katika ongezeko hili

kulikuwa na ongezeko la idadi ya wanafunzi kutoka 12,814 mwaka 2007 hadi 22,421 mwaka 2016. Ilihali uhitaji wa shule za msingi ulikuwa ukiongezeka katika vijiji kwa 75% mwaka 2016, idadi ya shule za msingi ilibaki hiyohiyo. Pia, bajeti iliendelea kuwa hiyohiyo, na mapato ya ndani hayakutosha kuwepo kwa miundombinu ya kuhifadhi wanafunzi wote katika Halmashauri. Hali hii ilipelekea upungufu mkubwa wa raslimali mashuleni. Aidha, ilichangia matatizo mengine kama mahudhurio duni, utoro (2013-58.4%; 2014-68.4%; 2015-70.2%), umbali kutoka nyumbani hadi shule (zaidi ya 6km-10km), mimba za ututoni, ajali na ufaulu wa chini katika mitihani. Pamoja na Wizara ya Elimu kuelekeza kuwa wastani wa uwiano wa mwalimu na wanafunzi uwe 1:45, uwiano halisi ulikuwa 1:69. Matatizo haya yalisababisha wanafunzi katika vijiji na vitongoji vipya kukosa elimu ya msingi. Wazazi hawakufurahia hali hii, hivyo waliamua kujenga shule shikizi.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuanzisha shule shikizi ili kupunguza changamoto walizopata wazazi, wanafunzi na walimu kuhusu utoaji wa elimu ya msingi. Halmashauri ililenga:

(i) Kufikia uandikishaji na mahudhurio ya juu na kuondoa utoro kwa kaunzisha shule shikizi.
(ii) Kupunguza utoro (kutoka 70.2% hadi 5%).
(iii) Kusajili shule shikizi zote ambazo zimetimiza vigezo.
(iv) Kupunguza umbali wa kuzifikia shule za msingi mpaka 2km.

Kimsingi, Halmashauri ililenga kuongeza idadi ya shule kwa kutoa usaidizi katika shule shikizi zilizoanzishwa na Vijiji vipya. Vijiji hivi ni Dodoma, Mhororo, Songambele, Imalamawazo, Ilangala, Rusungwa, Mkolani, Nyabilele, Nyarwerwe, Mkuyuni, Butobela, Izumangabo na Bwanga 'B'.

**4.0 UTEKELEZAJI**

H/W ya Chato ilitumia nafasi, haki na sheria mbalimbali kuhusu elimu na kuzitumia kukabili changamoto kwa kutekeleza uanzishaji wa shule shikizi. Mwaka 2012/2013 Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi katika Halmashauri aliwasilisha suala la shule shikizi ili lijadiliwe. Idara ilipitisha hoja ya jamii kuanzisha shule shikizi. Pendekezo hili liliwasilishwa kwenye Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na baadaye kuridhiwa na Baraza. Septemba mwaka 2013, mikutano mbalimbali ya ushauri iliyolenga utekelezaji wa mapendekezo ya Baraza iliendeshwa ikiwashirikisha viongozi wa vijiji.

Afisa Elimu wa Wilaya anayeshughulika na elimu ya msingi aliwasilisha kwenye Halmashauri nia ya kujenga shule shikizi kwa kutumia ushiriki wa jamii na wadau wengine wa elimu katika shule zilizoainishwa. Kamati za shule na walimu waliridhia pendekezo hili Desemba mwaka 2013 na kuandaa maeneo na mahitaji ya ujenzi.



***Vifaa vya ujenzi vilivyoletwa na jamii katika shule shikizi ya Dodoma Kata ya Kigongo***




***Uandaaji wa Matofali katika shule shikizi ya Imalamawazo – Butobela***

Desemba mwaka 2013, Halmashauri iliandaa na kuendesha mikutano ya uhamasishaji katika ngazi zote (Kitongoji, Vijiji na Kata). Uhamasishaji huu uliendeshwa na kikosi kazi cha elimu chenye mchanganyiko wa fani kilichokuwa na wajumbe 5; afisa elimu wa wilaya, afisa taaluma wa wilaya, afisa ardhi wa wilaya, mratibu wa elimu Kata na Diwani. Timu ya Mejenimenti ya Halmashauri ilishiriki kikamilifu kuweka mikakati na kupokea taarifa za uhamasishaji wa jamii kuhusu uanzishaji wa shule shikizi H/W ya Chato. Hili lilifanyika kwa miezi mitano (Julai – Novemba 2013). Halmashauri pia iliendesha mikutano ya umma kwa watu wazima na wazazi kuwashawishi kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wao. Mpango huu pia ulizingatia mahitaji mengine ya elimu hasa ununuaji wa sare za shule na kuzingatia afya ya jamii. Katika shughuli hizi za uhamasishaji, jamii ziliunganishwa ili kujenga miundombinu ya shule.

Uchangiaji wa rasmali; jamii kupitia kamati za shule na walimu zilihamasishwa kuchangia nguvu au fedha taslimu (TZS 5,000/=) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na miundombinu mingine ya shule. Jamii, pia ziliombwa na kukubali kuchangia fedha taslimu za kununua vifaa vya viwandani kama saruji, mabati, misumari, mbao na chokaa. Viwango vya uchangiaji viliainishwa kulingana na uwezo wa kaya katika eneo husika. Kwa mafano katika kijiji cha Nywarwerwe kila kitongoji kilikuwa na kiwango chake kuanzia TZS 500/= hadi TZS 1,000/= kwa mwezi kwa kila mwanafunzi. Jamii pia ilichangia kuni na mahindi kwa ajili ya uji wa wanafunzi.

## 5.0 RASLIMALI

H/W ya Chato ilitumia aina mbalimbali za raslimali. Raslimali watu zilijumuisha madiwani, watumishi wa elimu, watumishi wa Halmashauri, walezi wa Kata, Waratibu wa Elimu Kata, Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji, na walimu. Halmashauri pia ilitumia kiasi kikubwa cha raslimali fedha. Jedwali 2 linaonesha raslimali fedha zilizochangiwa na H/W ya Chato, wadau, mfuko wa kuchochea maendeleo wa jimbo (CDF) na jamii.

**Jedwali 2: Raslimali Fedha**

| S/N | SHULE SHIKIZI | JAMII | HALMASHAURI | WADAU | MFUKO (CDCF) | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MKUYUNI (ujenzi ulianza 2006, 3km kutoka Shule ya Msingi Chato) | 8,552,000 (ujenzi wa madarasa 4 na ofisi 1) | 12,000,000 | - | 8,000,000 | 28,552,000 |
| 2 | NYARWERWE (ujenzi ulianza 1994, 15km kutoka shule za Msingi za Nyantimba and Kanyindo) | 7,210,550 (ujenzi wa madarasa 3, vyoo na ofisi 2) | 7,000,000 | 22,000,000 | 1,000,000 | 37,210,550 |
| 3 | MKOLANI (ujenzi ulianza 2010, km 6 kutoka shule ya Msingi Katete A). | 12,043,000 (ujenzi wa madarasa 5, vyoo na ofisi 2) | 21,000,000 | - | - | 33,043,000 |
| 4 | IZUMANGABO (ujenzi ulianza 2008, 3km kutoka shule ya msingi Bwanga A | 5,554,600 (ujenzi wa madarasa 2, vyoo na ofisi 2) | - | - | - | 5,554,600 |
| 5 | BWANGA 'B' (ujenzi ulianza 2007, 3km kutoka shule ya msingi Bwanga A) | 16,200,500 (ujenzi wa madarasa 7, vyoo na ofisi 2) | 17,000,000 | - | - | 33,200,500 |
| 6 | BUTOBELA (ujenzi ulianza 2012, 8km kutoka shule ya msingi Mwendakulima | 12,226,000 (ujenzi wa madarasa 2, vyoo na msingi wa madara 2 na ofisi 1) | 7,000,000 | - | 1,000,000 | 20,226,000 |
| 7 | SONGAMBELE (ujenzi ulianza 2012, 6km kutoka shule ya Msingi | 5,027,600 (ujenzi wa madarasa 3, vyoo na ofisi 1) | 7,000,000 | | | 12,027,600 |

| S/N | SHULE SHIKIZI | JAMII | HALMASHAURI | WADAU | MFUKO (CDCF) | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mnekezi) | | | | | |
| 8 | DODOMA (ujenzi ulianza 2004, 6km kutoka shule ya msingi Nyisanzi) | 8,000,000 (ujenzi wa madarasa 3, vyoo na ofisi 1) | 12,000,000 | | | 20,000,000 |
| 9 | ILANGALA (ujenzi ulianza 2012, 4km kutoka shule ya msingi Kibumba 'A') | 17,783,000 (ujenzi wa madarasa 2, vyoo na ofisi 1) | - | - | 1,000,000 | 18,783,000 |
| 10 | IMALAMAWAZO (ujenzi ulianza 2003, 5km kutoka shule ya msingi Kibumba 'B' | 15,737,000 (ujenzi wa madarasa 2, vyoo na ofisi 1) | - | - | 1,500,000 | 17,237,000 |
| 11 | MHORORO (ujenzi ulianza 2009, 5-10km kutoka shule ya msingi Makurugusi) | 12,225,500 (ujenzi wa madarasa 6, vyoo, nyumba pacha 2 za walimu, na ofisi 1) | 7,000,000 | 28,000,000 | 2,000,000 | 49,225,500 |
| 12 | RUSUNGWA (ujenzi ulianza 2002, 5-7km kutoka shule ya msing Kalebezo | 5,830,000 (ujenzi wa madarasa 4, vyoo na ofisi 1) | 7,000,000 | - | 900,000 | 13,730,000 |
| 13 | NYABILELE (ujenzi ulianza 2007, 4.5km kutoka shule ya msingi Rutunguru 'A' | 3,605,000(darasa 1, vyoo na ofisi 1) | 5,000,000 | - | - | 8,605,000 |
| JUMLA | | 129,994,750 | 102,000,000 | 50,000,000 | 15,400,000 | 297,394,750 |

## 6.0 MATOKEO

Matokeo ya ujenzi wa shule shikizi katika H/W ya Chato ni mengi. Shule shikizi zimeisaidia Halmashauri kufikia haraka lengo la kuongeza uandikishaji wa wanafunzi kwa 113% kutoka 2007 hadi 2016 na kupunguza utoro kutoa 4% (2012/13) hadi 1% (2014/15). Mafanikio haya yalitokana na kupunguza umbali wa kwenda shule kutoka 7-8km mpaka 2km hali inayowavutia wanafunzi kuhudhuria shule. Mkakati huu umefanikiwa kupata matokeo mbalimbali kama alivyoeleza Mwl. Angasirini O. Kweka, Mkuu wa Idara ya Elimu (Msingi). *"… nilikuta jitihada hizi zikiwepo, nilichofanya ni kukihimiza kikosi kazi kufanya kazi kwa bidii katika kufuatilia shule shikizi na kufanya kazi na wadau mbalimbali wa elimu katika utekelezajii. Halmashauri imepunguza sana kiwango cha utoro na imeongeza uandikishaji…….watu wametambua umuhimu wa elimu kwa watoto wao…..na sasa wanachangia sana……matokeo ya jitihada hii yapo dhahiri….ndio…..tunafikia lengo letu kuu…"*



***Maafisa Elimu walipotembelea Shule Shikizi ya Dodoma***

Jitihada hii imepunguza ajali za mara kwa mara katika shule za msingi za Katete 'A', Rutunguru, Makurugusi, Nyisanzi, Bwanga, na Chato. Ajali zilitokea sana kwani wanafunzi walilazimika kwenda shule nje na mbali ya vitongoji vyao. Uwekaji wa matuta ya barabarani kwa usalama wa wanafunzi wavukao na kutembea pembezoni mwa barabara pia ulichangia kupunguza ajali.



***Ujenzi wa matuta barabarani kupunguza ajali***





***Shule shikizi ya Kitongoji cha Rusungwa, 18km kutoka shule ya msingi Kalebezo***

Kuongezeka kwa ufaulu; uwepo wa shule shikizi umeongeza ufaulu kuanzia mwaka 2014/2015 na kufanya H/W ya Chato kuwa nafasi ya kwanza katika matokeo ya mitihani kati ya Halmashauri nyingine za Mkoa wa Geita, kwa darasa la nne. Matokeo ya mtihani wa mwaka 2015 yameoneshwa kwenye jedwali 3 hapa chini.

**Jedwali 3: Ufaulu darasa la Nne (2015)**

| N | Wilaya | Ufaulu (%) | Nafasi Kimkoa | Nafasi Kitaifa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Chato | 97.45 | 1 | 17 |
| 2 | Mbogwe | 94.18 | 2 | 43 |
| 3 | Geita (TC) | 94.04 | 3 | 45 |
| 4 | Geita (DC) | 94.00 | 4 | 46 |
| 5 | Nyang'hwale | 93.13 | 5 | 53 |
| 6 | Bukombe | 92.90 | 6 | 57 |

Jitihada imesababisha kuongezeka kwa ari ya ushiriki wa wadau. Halmashauri, washirika wa elimu, na jamii wamejipatia stadi za kufanya kazi pamoja kama timu katika kutekeleza mipango. Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji cha Kibumba, Bwana Shija Matoto alisema; *"watu sasa wanaelewa umuhimu wa kushiriki katika shughuli za maendeleo…..hivyo kushiriki kikamilifu katika kuanzisha shule shikizi. Tuna shule shikizi mbili katika kijiji chetu, Ilangara na Imalamawazo……..zote zimejengwa na wanakijiji, kwa msaada kidogo kutoka mfuko wa kuchochea maendeleo ya jimbo (CDCF)".*

Uanzishaji wa shule shikizi umewezesha kuimarika kwa ubora wa kitaaluma mwaka hadi mwaka. Jitihada hii imewezesha kuongezeka kwa idadi ya walimu walioajiriwa, kujituma kwa walimu, usimamizi mzuri unaofanywa na maafisa elimu, maafisa wa ubora wa elimu, waratibu wa elimu kata na walimu wakuu. Madiwani wamejipanga vyema na huwatia moyo walimu kushiriki kikamilifu na kufanya kazi kwa bidii katika kufundisha na kusaidia wanafunzi na wazazi. Matokeo yanaonesha kuwa H/W ya Chato ni moja ya Halmashauri inayofanya vizuri katika elimu ya msingi, ikishika nafasi kwanza katika Halmashauri sita za Mkoa wa Geita.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kutunza na kuendeleza matokeo yaliyopatikana H/W iliweka mikakati mbalimbali. Baraza limejipanga kuwaomba madiwani kuendelea kuwachochea watu kufanya kazi kwa bidii kukamilisha majengo ya shule shikizi ambayo yalianzishwa na jamii. Halmashauri imejipanga kuwatia moyo wadau mbalimbali kushiriki katika masuala ya elimu ili kuondoa upungufu. H/W ya Chato inaendelea kuhamasisha vitongoji kujenga shule shikizi ambazo zinaanzishwa na kuendeshwa na jamii kwa kutumia rasilimali zake ili kuleta maendeleo endelevu. Hii itasaidia kufuta ugonjwa wa utegemezi kwa Halmashauri na Serikali Kuu.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio yaliyoainishwa yametokana na kufanya kazi kama timu, uongozi bora, utashi wa kisiasa, ushiriki wa jamii na michango ya wadau katika kuanzisha shule shikizi. Mengine ni ushirikiano thabiti kati ya Baraza, Kamati ya Elimu, Afya na Maji, Maafisa watendaji wa Kata na Vijiji na wadau wa taasisi za dini. Uongozi bora uliooneshwa na Mkurugenzi Mtendaji Bwana Clemence Berege na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Maisha Marando umechangia sana kuanzishwa kwa shule shikizi katika H/W ya Chato. Utashi wa kisiasa ulikuwa kigezo mojawapo muhimu cha mafanikio kwani utayari wa wanasiasa hasa madiwani kukubaliana na jitihada ya uanzishaji wa shule shikizi ulitoa msaada mkubwa. Sababu nyingine za mafanikio ni ushiriki thabiti wa jamii, uwazi katika taarifa za fedha na ushirikishaji wa wadau kama Padri Honoratus, Poverty Relief Fund (PRF) na H & C Whitehead LTD ya Uingereza ambao walichangia sana katika kufanikisha jitihada hii.

# Sura ya Tatu:
# Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato

Ugatuaji wa Masuala ya Fedha nchini Tanzania huzingatia MSM kuwa na vyanzo vya mapato vya uhakika, kuwepo kwa mfumo bora wa kutoa na kupokea fedha toka Serikali Kuu, utoaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya huduma zilizogatuliwa, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuhakikisha uwazi na usawa katika kutenga fedha na kuhakikisha usawa katika utoaji wa huduma (rejea sera ya maboresho ya Serikali za Mitaa ya 1998). Kimsingi, Ugatuaji wa masuala ya fedha kwa Tanzania hujumuisha yafuatayo;

(i) Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitakiwi kupewa majukumu ambayo hayatengewi fedha.
(ii) Mfumo wa ruzuku lazima uzingatie utekelezaji wa sera (vipau mbele) za kitaifa kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, na ambazo zitapatiwa fedha kwa ruzuku zenye masharti na kuongozwa na viwango vya chini vya kitaifa.
(iii) Mfumo wa ruzuku lazima uzihamasishe Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka vipaumbele vyao kupitia uanzishaji wa ruzuku ambazo hazina masharti na ruzuku za shughuli za maendeleo.
(iv) Ruzuku zisizo na masharti zitatolewa kwa utaratibu wa usawa na kwa kufidia Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye uwezo mdogo wa rasilimali.
(v) Ukokotoaji wa ruzuku lazima ufanyike kwa kutumia kanuni yenye vigezo vya uhakika, haki na visivyo na upendeleo.
(vi) Ruzuku kutoka Wizara za kisekta lazima zipunguzwe kadri iwezekanavyo.

Uboreshaji wa Mapato ni ile hali ya MSM kutumia madaraka waliyopewa na Serikali Kuu kukusanya mapato na kutumia kulingana na vipaumbele vyao. Uboreshaji wa mapato hujumuisha shughuli kama utafutaji wa vyanzo vya mapato, upanuaji wa wigo wa mapato, uhamasishaji wa shughuli za kiuchumi zinazoongeza vyanzo vya mapato na utungaji wa sheria ndogo zinazoongoza ukusanyaji na utumiaji wa mapato. Katika sura hii, mbinu bora ya H/W ya Bariadi imewasilishwa.

Mbinu bora ya H/W ya Bariadi inahusu Uboreshaji wa Mapato kwa ajili ya Utoaji Bora wa Huduma. Jitihada hii ilitekelezwa kufuatia uamuzi wa Serikali kuigawa Halmashauri Maarufu ya Wilaya ya Bariadi kuwa Halmashauri tatu (Mji wa Bariadi, na Halmashauri za Wilaya za Bariadi na Itilima). Mgawanyiko huu ulipunguza uwezo wa kimapato wa Halmashauri. Licha ya wigo wa kodi kuwa mwembamba kulikuwa na kikosi kazi dhaifu cha ukusanyaji wa mapato, viwango vya kodi vilivyopitwa na wakati, motisha kwa wakusanya mapato usiokidhi, usafiri usiokuwa wa uhakika, matumizi ya mbinu na vifaa vya kizamani na sheria ndogo za ukusanyaji mapato zilizopitwa na wakati. Hali hii ilikuwa na madhara katika uwezo wa Halmashauri wa kutoa huduma za kijamii na kiuchumi kwa wananchi. Halmashauri ililazimika kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia mpango kabambe wa uhamasishaji, ziara za mara kwa mara kwenye vyanzo vikubwa vya mapato, mapitio ya sheria ndogo na viwango vya kodi, uanzishaji wa motisha stahiki kwa wakusanya mapato, uimarishaji wa wigo wa kodi na uanzishaji wa mfumo wa malipo wa ki-eletroniki. Jitihada hii ilileta mabadiliko chanya katika tabia za walipa kodi na kuongeza mapato ambayo yaliwezesha Halmashauri kufadhili miradi mbalimbali kama ujenzi wa mabwawa, madarasa na maabara.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI

## UBORESHAJI WA MAPATO KWA UTOAJI BORA WA HUDUMA



*Uzoefu wa H/W ya Bariadi*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ni moja kati ya Halmashauri 6 katika Mkoa wa Simiyu. Halmashauri inapatikana kati ya Latitudo $2^0 15'$ and $3^0 10'$ Kusini na Longitudo $33^0$ 40′ to $35^0 10'$ Mashariki. Halmashauri inapakana na H/W ya Busega upande wa Magharibi, H/W ya Bunda na Serengeti (Mkoa wa Mara) upande wa Kaskazini, Pori tengefu la Maswa upande wa Mashariki, na H/W za Maswa na Itilima upande wa Kusini. Kiutawala, H/W ya Bariadi ina Tarafa 3 za Mhango, Dutwa and Nkololo, Kata 21, Vijiji 84 na Vitongoji 515. Halmashauri ina eneo la 5,091.21 $km^2$ ambazo 1,096.21 $km^2$ zinafaa kwa kilimo na ufugaji, na 790 $km^2$ ni Pori Tengefu la Maswa na 3,160$km^2$ ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Eneo lililobaki la 45 $km^2$ ni maji, misitu na milima midogo.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 267,296 ambao 139,426 ni wanawake na 127,870 ni wanaume, kukiwa na ongezeko la wastani wa 3.0%. Idadi ya watu imeongezeka hadi 300,843 mwaka 2016. Wastani wa wakazi katika kaya ni 7.5 ambao upo juu kidogo ya wastani wa Mkoa wa 6.9.

Kwa ujumla hali ya hewa ya Halmashauri ni ya kitropiki yenye mvua za mwaka kati ya 700mm - 950mm. Msimu wa mvua za vuli ni kati ya Oktoba – Desemba ukiambatana na msimu wa ukame miezi ya Januari na Februari. Mvua za masika hunyesha katika miezi ya Machi hadi Mei. Msimu wa ukame ni kati ya Juni na Septemba ukiwa na wastani wa joto kati ya $19^0$C na $29^0$C .

Uchumi wa Halmashauri hutegemea kilimo ambacho ndio chanzo cha 3/4 ya kipato na huajiri takribani 80% ya wakazi. Kaya nyingi ni wakulima wafugaji ambazo ni 70% ya wakazi wote. Hii inaonesha kuwa ufugaji ni sehemu muhimu ya uchumi. Mazao makuu ya biashara ni pamoja na pamba, karanga na alizeti. Mazao ya chakula yanayolimwa ni pamoja na mahindi, uwele, mpunga, viazi vitamu na mihogo (tazama jedwali 2 hapa chini). Mwaka 2015 idadi ya wanyama ilikuwa 803,914 ambayo ilijumuisha ng'ombe (262,835), kondoo (54,328), mbuzi (113,013) na kuku (373,738). Zaidi ya hayo, utalii wa kuwinda hufanyika kipindi cha uwindaji katika Pori tengefu la Maswa sehemu za Kaskazini za Halmashauri.

**Jedwali 2: Eneo linalolimwa na Mazao mwaka 2014/2015**

| | *eneo lililolimwa (Ha)* | *Uzalishaji halisi (kwa tani)* |
|---|---|---|
| ***Mazao** ya Chakula* | | |
| ***Uwele*** | 12,702.0 | 25,755.0 |
| ***Mahindi*** | 39,051.0 | 68,339.3 |
| ***Mpunga*** | 8,638.0 | 32,392.0 |
| ***Viazi** Vitamu* | 2,209.0 | 17,328.7 |
| ***Mihogo*** | 7,775.0 | 38,875.0 |
| ***jumla** ndogo* | 70,375.0 | 182,690.0 |
| ***Jamii** ya Kunde* | | |
| ***Maharage*** | 5,778.0 | 3,622.8 |
| ***Maharage** ya Kijani* | 12,510.7 | 12,510.7 |
| ***Mbaazi*** | 6,068.9 | 4,468.2 |
| ***Choroko*** | 6,684.9 | 9,301.6 |
| *Njegere* | 3,216.5 | 3,216.6 |
| ***Jumla** ndogo* | 34,259.5 | 33,119.8 |
| ***Mazao** ya biashara* | | |
| ***Pamba*** | 31,027.4 | 34,905.0 |
| *Alizeti* | 2,872.2 | 4,397.3 |
| ***Karanga*** | 101.0 | 40.2 |
| ***Jumla** ndogo* | 34,000.7 | 39,342.6 |
| ***Jumla** Kuu* | 138,635.0 | 255,152.5 |

## 2.0 TATIZO

Julai mwaka 2012 Serikali iliamua kuigawa H/W ya Bariadi ya zamani na kuwa sehemu mbili za H/W ya Bariadi na Halmashauri ya Mji wa Bariadi. Mwaka 2013, H/W ya Bariadi iligawanywa tena kuanzisha H/W ya Itilima na H/W ya Bariadi ya sasa. Kabla ya mgawanyo huu wa kiutawala, H/W ya Bariadi ya zamani ilikuwa na wigo mpana wa kodi uliopelekea makusanyo makubwa ya mapato ya ndani. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2011/12, jumla ya TZS 2.7 zilikusanywa (tazama jedwali 6). Kutokana na uamuzi wa Serikali wa kuigawa Halmashauri kuwa Halmashauri tatu, maeneo mengi yaliuyokuwa vyanzo vya uhakika na vikubwa vya mapato ya ndani vilihamia kwenye Halmashauri mpya. Vyanzo hivi vilijumuisha mnada wa mifugo wa Bariadi, eneo la biashara la Bariadi na masoko ya Mwamapalala, Bariadi, Laini, Lagangabilili na Migato. Hivyo, makusanyo kwa mwaka 2012/13 na 2013/14 yalipungua sana. Kwa mfano, mwaka 2012/13 na 2013/14, Halmashauri ilikusanya mapato ya ndani ya kiasi cha 1.52 bilioni na 1.08 bilioni. Hali hii ilikuwa na madhara katika uwezo wa Halmashauri kutoa huduma za kijamii na kiuchumi.

Licha ya wigo mwembamba wa kodi, kupungua kwa makusanyo ya mapato ya ndani kulitokana na kuwepo kwa kikosi kazi dhaifu, viwango vya kodi vilivyopitwa na wakati, motisha ndogo kwa wakusanyaji wa mapato, usafiri usio wa uhakika, matumizi ya mifumo na vifaa vya kizamani na sheria ndogo zilizopitwa na wakati. Aidha, ushiriki duni na uelewa mdogo wa jamii, walipakodi na wadau wengine kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ulichangia mapato duni. Baada ya kugawanywa kwa Halmashauri, ujazo wote wa wigo wa kodi haukuvunwa kikamilifu. Ukusanyaji wa mapato uliendelea kupungua kwa 29% kati ya mwaka 2012/13 na 2013/14. Hali hii ililazimu Halmashauri kujipanga ili kuboresha ukusanyaji wa mapato ndani.

## 3.0 LENGO

Lengo kuu lilikuwa kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuongeza uwezo wa kulipia shughuli za kawaida na za maendeleo. Halmashauri ililenga kupitia na kubadili sheria ndogo za ukusanyaji wa mapato zilizopitwa na wakati, kuboresha mazingira ya ukusanyaji wa kodi na kujikita katika ujenzi wa uelewa wa walipa kodi.

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Ili kuongeza mapato ya ndani, Halmashauri iliamua kuongeza shughuli zake katika mipango ya uhamasishaji, majadiliano ya jamii, mikutano na ziara za mara kwa mara katika maeneo yenye uwezekano wa kuwepo vyanzo vya mapato. Halmashauri ilifanya ziara za mafunzo katika maeneo husika, ikaboresha vifaa/miundo/mifumo, ikapitia na kufuta sheria na viwango vilivyopitwa na wakati na kuunda utaratibu wa kuwapa motisha wakusanyaji wa mapato. Mikakati hii ilitekelezwa kwa kutenga rasilimali watu, vifaa na fedha za kutosha.

Usimamizi na ufuatiliaji; mwaka wa fedha 2013/14, madiwani waliishauri Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kufanya ziara kuhusu usimamizi na ufuatiliaji stahiki wa ukusanyaji wa mapato. Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ililikubali pendekezo na kufanya ziara ya kina H/W ya Moshi ambayo ilikuwa moja ya Halmashauri zenye mafanikio katika ukusanyaji wa mapato ya ndani. Kamati ya fedha, utawala na mipango iliitembelea H/W ya Moshi kwa ajili ya kujifunza zaidi kuhusu mifumo na mbinu zinazotumika kukusanya mapato kwa mafanikio.

Kujenga uelewa; kwa miaka miwili mfululizo (2014 na 2015), Halmashauri ilijenga uelewa kwa walipa kodi kupitia matangazo kwa umma, warsha na mikutano ya majadiliano ya mara kwa mara katika maeneo ya masoko, minada, sehemu za biashara na katika mikutano ya Kamati za Maendeleo za Kata. Uelimishaji ulijikita katika tozo mpya za kodi, sheria ndogo mpya na maridhiano ya utekelezaji.

Kuimarisha Kikosi kazi na kuanzisha kanzidata ya mapato; katika mwaka wa fedha 2014/15, Halmashauri iliimarisha kikosi kazi cha ukusanyaji mapato kwa kuteua watumishi 11 kutoka sekta za teknolojia ya mawasiliano, kilimo, mifugo, maliasili, ushirika, uvuvi, afya na utawala kujiunga na watumishi wa idara za

fedha na biashara. Jukumu la kikosi kazi lilikuwa kuishauri Timu ya Menejimenti kuhusu masuala ya mapato na kufanya ukaguzi katika maeneo yote yenye uwezekano wa kuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato. Maeneo yaliyokaguliwa yalijumuisha masoko, minada, vituo vya kuuzia pamba na sehemu za biashara. Kikosi kazi kilianisha, kuandika taarifa na kuweka vigezo vya kanzidata ya mapato kwa vyanzo vyote kwa lengo la kuzuia udanganyifu wa wakusanyaji.

Kuanzishwa kwa mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji mapato; mwaka 2015/16 Halmashauri iliingia makubaliano na Kampuni ya Lwachu (Ltd) ili kuanzisha mfumo wa kieletroniki wa ukusanyaji mapato. Makubaliano haya yalifuatiwa na uendeshaji wa mafunzo ya kina kwa wakusanyaji na wahasibu juu ya matumizi ya mfumo. Halmashauri ilinunua vifaa 8 vya kieletroniki (printa na simu janja) ili vitumike kukusanyia mapato katika maeneo mkakati na vifaa vingine 10 kwa ajili ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Kata. Mfumo huu ulimsaidia Mweka Hazina wa Halmashauri na Mkurugenzi kuona moja kwa moja mtiririko na miamala ya ukusanyaji. Kwenye makubaliano, kampuni kwa kutumia mitambo yake kuhifadhia taarifa (seva) ilikuwa na jukumu la kufuatilia na kulinda taarifa zote zinazoingia kwenye mfumo, kuwabaini wote waliotumia mfumo vibaya na kutoa taarifa kwa Halmashauri. Kikosi kazi kiliwasaidia wakusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha malipo yote yanaingizwa kwenye mfumo. Hata hivyo, tangu Agosti 15, 2016 Halmashauri ilikusanya mapato kupitia mfumo wa taarifa wa ukusanyaji mapato wa Serikali za Mitaa (LGRIS) unaoendeshwa na OR-TAMISEMI ambao hauna gharama isipokuwa gharama za mtandao zinazokadiriwa kuwa TZS 5,000 kwa mwezi kwa kila kifaa.

Mapitio ya Sheria Ndogo; mwaka 2015/16, Halmashauri ilirekebisha na kufuta sheria ndogo ya mapato ili kuboresha viwango vya tozo. Mchakato wa kurekebisha, kutunga na kubadili sheria ndogo ulianzishwa na kitengo cha sheria kwa kuandaa rasimu. Rasimu ilijadiliwa katika idara mbalimbali, timu ya menejimenti, kamati ya utawala na fedha na baadaye katika Baraza. Mapendekezo haya ya sheria ndogo yaliwasilishwa kwenye Kamati za Maendeleo za Kata ili kukusanya maoni. Halmashauri iliwasilisha mapendekezo haya kwenye Sekretarieti ya Mkoa kwa ajili ya uchambuzi na kuwasilisha kwa Waziri anayeshughulikia masuala ya Serikali za Mitaa ili kupitishwa. Sheria ndogo zilizoidhinishwa zilipelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwenye gazeti la Serikali. Halmashauri ilisimamia sheria hii kikamilifu kwa kuhakikisha kuwa wote wanaotakiwa kulipa wanalipa ushuru, kodi na ada mbalimbali ndani ya muda. Kufuatia mabadiliko ya sheria ushuru wa mazao uliongezwa kutoka TZS 1,000 - TZS 3,000 kwa gunia moja. Vyanzo vipya vya mapato vilivyoongezwa ni ada za mabango na vibao. Sheria ilianzisha adhabu kali kwenye ukwepaji na udanganyifu wa kodi.

Kuanzishwa kwa vituo vya ukaguzi; kuhakikisha sheria inatekelezwa, Halmashauri ilianzisha vituo vya ukaguzi 7 katika vijiji vya Mwamoto, Igegu, Dutwa, Ngasamo, Isuyu Sapiwi, Ngulyati na Kasoli kwa ajili ya ukaguzi, ufuatiliaji na kuhakikisha ushuru wa mazao unalipwa na kukusanywa. Halmashauri iliingia mkataba na kampuni ya ulinzi ya DAWAPA ambayo huhakikisha kila kituo kinapatiwa walinzi kwa masaa 24. Kikosi kazi hufanya ukaguzi wa kushtukiza ili kubaini udanganyifu.

Uanzishaji wa vyanzo vipya vya mapato na utoaji wa motisha; Halmashauri ilijenga miundombinu ya masoko na vyoo vya umma (kwa mfano Dutwa Sokoni) kama vyanzo vipya vya mapato na kuboresha mazingira ya wakusanyaji wa kodi kwa kuwapatia usafiri wa uhakika (gari na pikipiki). Halmashauri inatoa posho ya chakula (TZS 10,000) kwa kila mkusanyaji wa mapato ili kuwapa motisha.

## 5.0 RASILIMALI

H/W ya ilitumia aina mbalimbali za rasilimali kufanikisha jitihada ya uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato. Kuhusu rasilimali fedha Halmashauri ilitumia jumla ya TZS 131,938,529 katika jitihada hii. Jedwali 3 hapa chini linaonesha shughuli na gharama zilizotumika.

**Jedwali 3: Gharama, Shughuli na Chanzo cha Fedha**

| MWAKA | SHUGHULI | GHARAMA (TZS) | CHANZO |
|---|---|---|---|
| **2013/14** | Safari ya Mafunzo H/W ya Moshi | 13,270,000 | Mapato ya ndani |
| **2014/2015** | Uanzishaji wa mabani 7 barabarani | 4,200,000 | Mapato ya ndani |
| **2014-2016** | Ufuatiliaji wa Kikosi kazi | 26,500,000 | Mapato ya ndani |
| **2014-2016** | Ufuatiliji wa kamati ya fedha | 5,400,000 | Mapato ya ndani |
| **2014-2015** | Mikutano ya Kikosi Kazi na walipa kodi | 9,500,000 | Mapato ya ndani |
| **2015-2016** | Mikutano ya Kikosi Kazi kwenye Masoko | 11,500,000 | Mapato ya ndani |
| **2015-2016** | Ujenzi wa ofisi na vyoo | 10,000,000 | Mapato ya ndani |
| **2015/16** | Ununuzi ya mfumo wa kieletroniki | 24,150,000 | Mapato ya ndani |
| **2015/16** | Ujenzi wa ofisi ya malipo na vyoo | 10,000,000 | Mapato ya ndani |
| **2015/16** | Posho za chakula za wakusanyaji | 11,707,000 | Mapato ya ndani |
| **2015/16** | Gharama za mafunzo ya wakusanyaji | 5,711,529 | Mapato ya ndani |
| | **Jumla** | **131,938,529** | |

Halmashauri ilitumia raslimali watu kwa namna mbalimbali. Watumishi wengi walitumia muda na stadi zao kama wakusanyaji au kikosi kazi kukusanya takwimu, kusimamia na kufuatilia mchakato wa ukusanyaji mapato. Baraza likishirikiana na Timu ya Menejimenti lilisimamia na kufuatilia mchakato wa ukusanyaji mapato katika mipaka yake.

**6.0 MATOKEO**

H/W ya Bariadi ilitekeleza jitihada ya uboreshaji wa mapato na kuweza kushuhudia mabadiliko makubwa katika ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma. Matokeo muhimu ni pamoja na mabadiliko ya tabia yaliyotokana na mpango wa elimu kwa umma, matumizi ya tozo na faini yaliyoleta kujituma kwa jamii, uwajibikaji na ushirikiano katika kuwasaidia wakusanya mapato, madiwani na walipa kodi. Tabia njema ya kulipa kodi imesambaa kwa jamii zote katika H/W ya Bariadi. Mafaniko haya yametokana na uwepo wa kikosi kazi chenye taaluma mbalimbali na kanzidata ya ukusanyaji pamoja na mfumo wa kieletroniki wa kukusanya mapato.



***Printa, risiti ya kieletroniki na Simujanja***

Matokeo ya jitihada hii yapo dhahiri katika kuwepo kwa mazingira mazuri kwa wakusanyaji na walipa kodi na uwepo wa vituo vya ukaguzi vinavyodhibiti ukusanyaji wa ushuru wa mazao. Mapato ya ndani yameongezeka kutoka TZS 1,08 billioni mwaka 2013/14 hadi TZS 1.18 billioni na TZS 1.2 billioni mwaka 2014/15 na 2015/16. Maboresho katika mapato ya ndani yameongeza uwezo wa Halmashauri katika matumizi ya kawaida na

maendeleo. Jedwali 4 hapa chini linaonesha mtiririko wa matumizi baada ya maboresho na ongezeko la mapato.

**Jedwali 4: Mtiririko wa Matumizi**

| N | Kipengele | Gharama TZS |
|---|---|---|
| 1. | Mishahara | 173,136,600 |
| 2. | Vibarua | 71,358,000 |
| 3. | Uwezeshi kwa madiwani kufuatilia miradi | 41,324,520 |
| 4. | Kukamilisha miradi iliyoanzishwa na jamii | 35,762,319 |
| 5. | Kupima viwanja 90 eneo la kibiashara la Dutwa | 7,500,000 |
| 6. | Fidia kwa wamiliki wa ardhi kwenye ujenzi wa Bwawa Mwasubuya na Kasoli | 150,000,000 |
| 7. | Kusaidia Ushirika wa Wanawake na Vijana (SACCOS) (TZS 5.0 Mil) | 30,324,529 |
| | **JUMLA** | **264,911,368** |

Maboresho katika ukusanyaji wa mapato yamewezesha Halmashauri kujikita katika kuboresha huduma katika sekta za maji na elimu. Kwa mfano, ujenzi wa mabwawa; baada ya kulipa fidia kwa wamiliki wa ardhi katika maeneo ya Mwasubuya and Kasoli, Halmashauri ilijenga bwawa la Mwasubuya. Bwawa hili linatumika kwa uvuvi na umwagiliaji wa mashamba madogo. Halmashauri imeboresha mazingira ya kujifunzia; kwa mfano katika shule ya sekondari ya Nkololo ujenzi wa maabara ulikamilika kwa kutumia fedha za ndani TZS 10,000,000.00.



*Ukuta wa Bwawa*



*Bwawa*



*Matoleo ya Maji*





*Maabara mpya katika Sekondari ya Nkololo*

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuendeleza matokeo yaliyopatikana,Halmashauri imeweka mbinu nyingi za uendelevu. Mkakati mmojawapo ni kuimarisha kikosikazi cha mapato kuendelea kufanya ziara katika maeneo yote yenye vyanzo vya uhakika vya mapato. Hii itasaidia ukusanyaji wa taarifa, uainishaji wa vyanzo vipya vya mapato na ugunduzi wa changamoto zinazokabili mchakato wa ukusanyaji wa mapato. Halmashauri imejipanga kuendeleza shughuli za kujenga uelewa kuhusu ulipaji kodi kwa walipa kodi, madiwani na wadau wote kupitia uhamasishaji wa mara kwa mara na mikutano. Kazi hii itaenda sambamba na usimamizi endelevu utakaofanywa na kikosikazi, maafisa watendaji wa vijiji na kata, ambao husimamia, hufuatilia na hukagua mchakato mzima wa ukusanyaji mapato. Aidha, Halmashauri imejipanga kukasimu ukusanyaji wa mapato kwa ngazi za Vijiji na Kata kwa kuwapatia maafisa watendaji vifaa vya kieletroniki.

Mkakati mwingine muhimu wa uendelevu ni usimamiaji thabiti wa sheria ndogo; Halmashauri imejipanga kufanya mapitio ya sheria mara kwa mara na kurekebisha sheria zinazohusu ukusanyaji wa mapato ya ndani kuwa na viwango vya tozo vyenye sababu za msingi na ushindani; kodi, faini, ada na adhabu zinaendana na uhalisia. Mchakato huu ni endelevu kwani hali za kiuchumi za walipa kodi na wigo wa kodi hubadilika. Halmashauri itaendelea kuboresha mazingira ya kazi ya wakusanyaji wa mapato na walipaji kwa kuhakikisha uwepo wa usafiri wa uhakika na posho. Suala hili litatia hamasa kwa wakusanyaji na kuzuia kujiingiza katika vitendo vya rushwa kati yao na walipaji.

Kukamilisha ujenzi wa mabwawa ya Mwasubuya and Kasoli ni mkakati mwingine wa uendelevu. Mabwawa haya yanatarajiwa kutia hamasa ukuaji wa shughuli za kiuchumi kama uzalishaji wa mpunga kwa umwagiliaji na kuongeza vyanzo vya mapato kupitia ada za kutumia maji na ushuru wa mazao.

## 8.0 SIRI ZA MAFANIKIO

H/W ya Bariadi ilipata mafanikio makubwa kutokana na siri mbalimbali. Kikosikazi imara na chenye mchanganyiko wa wataalamu; kikosikazi hiki hufanya kazi kama timu na hushirikiana kuainisha vyanzo, kuhamasisha, kufuatilia na kuhakikisha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kamilifu. Kutokana na ukweli kuwa kikosikazi hiki kina wajumbe wenye elimu, stadi na uzoefu mbalimbali pamoja na mtazamo chanya kuhusu uboreshaji wa mapato, ilikuwa rahisi kubuni na kupata malengo makubwa lakini yanayofikiwa. Siri ya pili inahusu uongozi imara wa Halmashauri ulioweza kuratibu wadau wote wa maboresho ya kodi. Kupitia uongozi huu Halmashauri iliwaunganisha madiwani na timu ya menejimenti kufanya kazi kwa maelewano katika kuongeza mapato ya ndani. Mbinu hii ilileta fikra ya uwajibikaji wa pamoja kwa wafanya maamuzi na watekelezaji katika kusimamia, kufuatilia, na kuongoza mchakato wote wa ukusanyaji mapato.

Kupitia na kurekebisha sheria ndogo ambazo zaikuwa na tija kwa muda unaotakiwa ni siri nyingine muhimu kwani ilisaidia Halmashauri kupunguza ukwepaji na udanganyifu wa kodi. Halmashauri ilianzisha na kusimamia vizuri faini/tozo za adhabu ambazo huwalazimisha walipa kodi kukamilisha malipo yao mapema. Hii imeleta tabia mpya kati ya walipa kodi; kukubaliana na kulipa ada na tozo kulingana na sheria za Halmashauri. Siri nyingine ni uwepo wa wakusanyaji wenye motisha ambao wameleta mazingira stahiki kwa pande zote kutekeleza majukumu yao bila Halmashauri kutumia faini na adhabu. Hili liliwezekana kupitia ushirikishwaji wa wadau.

Uanzishaji wa mfumo wa kieletroniki wa kukusanya mapato ulileta uwazi. Tofauti na awali, mfumo umeongeza sana uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato. Kila muamala wa ukusanyaji mapato una nakiliwa vyema na mara moja unaweza kutazamwa na watumishi wa Halmashauri walioidhinishwa. Pia, mfumo umezuia udanganyifu na rushwa.

Jitihada za jamii zilianzisha masoko na minada ambayo ilitumiwa na Halmashauri kama vituo vya ukusanyaji mapato. Hii ilitoa fursa kwa walipa kodi na wakusanya mapato kufanya shughuli zao katika mazingira rafiki.

# Sura ya nne: Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma

Utoaji huduma ni jukumu muhimu katika mahusiano ya taasisi za Serikali na wananchi. Huduma ni mfumo au mpangilio unaokidhi mahitaji ya jamii. Helmsing (1995) anaeleza kuwa utoaji wa huduma ni uamuzi wa lazima unaofanywa na maafisa wa kuchaguliwa au kuajiriwa kutumikia au kutoa bidhaa na huduma kwa wapokeaji. Utoaji wa huduma ni wa namna ya mtazamo na mwelekeo, ukihusisha sifa na desturi za kimataifa..

Utoaji huduma ni mchakato endelevu na unaojirudia wa kupanga na kutoa huduma zinazozingatia mpokea huduma. Huhusu ushiriki wa mpokea huduma katika kuainisha wapokea huduma na kutambua mahitaji yao. Utoaji wa huduma pia unahitaji mchakato wa kubuni na kupanga huduma kati watumiaji, watoaji, wasambazaji na washirika katika kuanzisha, kubuni na kupanga huduma na kuhakikisha mahitaji ya watumiaji wa huduma yanafikiwa. Hatimaye utoaji wa huduma unahusu uzalishaji, usambazaji na uwasilishaji wa huduma ambazo zinakidhi lengo na zinafaa kwa mahitaji ya watumiaji. Katika utoaji wa huduma muda wote panahitajika mfumo wa ufuatiliaji na uboreshaji wa kukusanya maoni ya watumiaji na vipimo vya utendaji ili kuwezesha ufuatiliaji na uboreshaji wa bidhaa na huduma wa mara kwa mara.

Utoaji wa huduma ni shughuli ya msingi ya Serikali. Serikali huwepo, pamoja na sababu nyingine, kwa sababu ndio chombo pekee kinachoweza kutoa kwa usahihi maelekezo kuhusu huduma muhimu kama usalama wa raia, ulinzi, miundombinu, usimamizi na ukarabati wa barabara na kadhalika. Ulazima na umuhimu wa masuala haya huleta uhalali katika shughuli za Serikali. Imewekwa katika katiba na mikataba ya kimataifa kwamba Serikali inawajibika na huduma za msingi katika maeneo mengi ya kijamii ambayo ni pamoja na elimu, hifadhi ya jamii, mahitaji ya msingi, ulinzi wa kisheria na makazi. Serikali lazima iwapatie wananchi uhakika wa kuendeleza utoaji huduma; kupatikana huduma kwa wote bila kujali tofauti za kijamii na kiutamaduni na kwa bei zinazofaa. Hili lina matokeo kwa taasisi za Serikali. Uwazi, ufanisi, upatikanaji na mambo mengine, huleta ubora katika bidhaa zitolewazo na Serikali kama huduma kwa wananchi wake.

Kwa wananchi wengi, Serikali yao ya Mtaa ndio Serikali yenye mashiko zaidi, pia ndiyo ngazi ya Serikali ambayo huwasiliana nayo zaidi katika maisha yao ya kila siku. Mfumo wa Tanzania wa Serikali za Mitaa unaonesha kuwa MSM hutoa huduma ambazo zina asili ya kijamii, yaani, afya, maji, elimu, ustawi, usimamizi wa taka, na zile zenye asili ya kiuchumi, yaani, ardhi na makazi, muindombinu, kilimo, mazingira na maendeleo ya jamii.

Nadharia ya utoaji huduma shirikishi iliyotumika katika sura hii, ina maana ya utoaji huduma ambao huhusisha wadau wote. Kiini cha ushiriki ni jamii ambayo hufaidika na huduma zitolewazo na jamii yenyewe, MSM, Serikali Kuu, mashirika yasiyo ya kiserikali na hata mashirika ya kimataifa. Utoaji huduma shirikishi huweka jamii faidika kama msingi wakati wa kupanga, utoaji wa huduma na upimaji wa ubora wa huduma. Utoaji huduma shirikishi huleta uendelevu wa huduma inayotolewa.

Katika sura hii, mbinu bora sita kuhusu utoaji huduma shirikishi zimewasilishwa kutoka Halmashauri za Wilaya za Itilima, Misungwi, Musoma, Bukombe, Ngara na Ukerewe.

Jitihada ya H/W ya Itilima inahusu Utunzaji wa Mazingira na Uongezaji wa Kipato Katika Jamii. Jitihada hii ilitekelezwa na Kikundi cha Malela cha Kijiji cha Isengwa kandokando ya Mto Simiyu. Mto Simiyu ambao huingiza maji katika Ziwa Viktoria uliathirika sana kutokana na matumizi mabaya ya pembejeo za kilimo na

mmonyoko wa udongo uliosababishwa na shughuli za binadamu, usimamizi mbovu wa sheria na kanuni za mazingira na utupaji holela wa taka. Lengo kuu la Halmashauri na kikundi cha Malela lilikuwa kupunguza uharibifu wa mazingira katika maeneo ya mto yaliyokuwa yameathirika na kuboresha vipato vya jamii zinazotegemea maliasili za Mto Simiyu na Ziwa Viktoria. Kwa kushirikiana na wataalam wa LVEMP II, Halmashauri ilijenga uelewa kwa jamii za karibu na mto kuhusu madhara ya kuendesha shughuli za kiuchumi ndani ya 60m kutoka kingo za mto, ilihamasisha watu binafsi na kaya kushiriki katika uhifadhi wa mazingira, ilianzisha shughuli za uzalishaji kipato rafiki kwa mazingira, iliunda vikundi mbalimbali vya kijamii vya kutekeleza jitihada hii na iliwezesha utungaji wa katiba na sheria ndogo za vijiji za uhifadhi wa mto, kingo za mto na mazingira kwa ujumla. Jitihada hii imedhihirisha mafanikio yake katika kupungua kwa uchafu katika mto na ziwani, maboresho katika mbinu za kilimo na jamii kuwa rafiki na watetezi wa uhifadhi wa mazingira.

Mbinu bora ya H/W ya Misungwi inahusu Uboreshaji wa Mazingira ya Kuishi na Elimu kwa Watoto Wenye Ulemavu wa Ngozi. Tangu mwaka 2007 watu wenye ualbino walinyanyaswa kutokana na imani potofu zilizoenezwa na baadhi ya waganga wa kienyeji kuwa viuongo vya miili ya watu wenye ualbino huleta bahati na utajiri. Dhana hii ilisababisha mashambulizi na mauaji ya watu wenye ualbino hasa watoto. Ili kukabili tatizo hili Halmashauri ilianzisha kituo katika Shule ya Msingi Mitindo cha kulea watoto wenye ualbino waliotelekezwa na kuwapatia elimu bora. Utekelezaji wa jitihada hii ulihusu uundaji wa kamati ya uhamasishaji, ujenzi wa miundombinu ya shule, ununuaji wa vifaa vya kujifunzia na utafutaji wa wadau wa kuchangia maboresho ya kituo. Utekelezaji wa jitihada hii umefanya H/W ya Misungwi kuwa mojawapo ya Halmashauri nchini zenye vituo vya watoto wenye ualbino waishio sehemu salama na kupata elimu ya msingi kwa uhakika. Kituo kina miundombinu ya kutosha watoto 92 wenye ualbino kama mabweni, madarasa, bwalo, jiko, na matundu 8 ya vyoo ambavyo vinawezesha kutoa huduma bora za elimu, afya na usalama.

Mbinu Bora ya H/W ya Musoma inahusu Kukuza Mfuko wa Afya ya Jamii kwa Huduma Bora za Afya. Kabla ya jitihada hii Halmashauri ilitoa huduma duni za afya kutokana na upungufu wa fedha au fedha kuchelewa kutoka Serikali Kuu, uelewa duni wa jamii kuchangia gharama za afya, vipato duni na uratibu mbovu wa vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, mfumo wa kulipia huduma za afya kwa fedha taslimu ulikuwa na changamoto, tabia za rushwa na matumizi ya risiti zisizo rasmi. Hali hii ililazimu Halmashauri kukuza uelewa wa jamii ili kuchangia huduma za afya, kuongeza uandikishaji na uratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na kuboresha uwezo wa vituo vya kutolea huduma kununua madawa na vifaa tiba na kuwapa motisha watumishi. Kutatua changamoto hizi Halmashauri ilitunga sheria ndogo ya CHF, kuunda Bodi ya Halmashauri ya huduma za afya, kuanzisha kikosi kazi, kuunda kamati za uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma, kujenga uelewa wa jamii na kuandikisha kaya katika mfuko. Uandikishaji wa kaya katika mfuko uliongezeka na fedha za mfuko zilitumika kuboresha miundombinu ya afya na kutoa huduma bora za afya.

Jitihada ya H/W ya Bukombe inahusu Usimamizi Shirikishi wa Skimu ya Maji iliyotekelezwa katika Kata ya Uyovu. Kata hii ilikuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji safi na salama. Wanawake walitumia muda mrefu kutafuta maji kutokana na umbali. Wanawake na wasichana walinyanyaswa kijinsia wakiwa njiani kutafuta maji. Watoto wa shule iliwabidi kusaidia wazazi kutafuta maji kabla ya kwenda shule suala lililoongeza utoro. Kulikuwa na kiwango cha juu cha magonjwa yatokanayo na maji machafu kama homa ya matumbo, kuhara, kichocho na kipindupindu. Halmashauri iliamua kutafuta chanzo cha uhakika cha maji, kujenga miundombinu ya maji na kuunda Jumuia ya Watumia Maji (COWSO). Jitihada hii imepunguza umbali wa kupata maji toka 3km hadi 200m, imewezesha kuwepo kwa jumuia ya watumia maji iliyo imara, imezalisha ajira na kupunguza magonjwa yatokanayo na maji yasiyo salama. Jumuia ya Uyovu imekuwa kituo cha kujifunzia usimamizi wa miundombinu ya maji.

Jitihada ya H/W ya Ngara inahusu Ushiriki wa Jamii Katika Kufungua na Kuboresha Barabara katika Miji Midogo ya Ngara, Rulenge, Kabanga na Benaco. Ufunguaji wa Barabara ulikuwa na changamoto kwani jamii zilihitaji kulipwa fidia za maeneo ambapo barabara zingepita. Upangaji na ufunguaji wa barabara katika miji

hii ulikuwa mgumu kutokana na uhitaji wa mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Usafirishaji na ujenzi wa miundombinu ya huduma za jamii ulikuwa mgumu kutokana na ukosefu wa barabara. Changamoto zote hizi zililazimu Halmashauri kushirikisha jamii kwenye shughuli za ufunguaji barabara kwa kufanya uhamasishaji kuhusu faida za barabara na kuimarisha makubaliano ya ushiriki wa jamii. Jamii zilikubali na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa jitihada. Matokeo ya ufunguaji wa barabara yanajumuisha ongezeko la thamani ya ardhi, uwepo wa miundombinu ya huduma za jamii, kuongezeka kwa shughuli za biashara pembezoni mwa barabara na kuimarika kwa usafirishaji ndani ya miji.

Mbinu Bora ya H/W ya Ukerewe inahusu Uhifadhi Jumuishi wa Misitu ya Asili. Kabla ya jitihada hii Halmashauri ilishuhudia kuongezeka kwa uharibifu wa misitu kutokana shughuli za binadamu kama kilimo, malisho na makazi. Kukua kwa soko la samaki ambapo watu walitumia kuni kukausha samaki kulichochea uharibifu wa mazingira. Halmashauri iliamua kuhifadhi maliasili na kuruhusu kurejea kwa uoto wa asili kwa kuanzisha vitalu vya miche, kujenga uelewa katika jamii ili zilihifadhi misitu na kuhamasisha uanzishaji wa vitalu vya miche katika kaya. Jitihada hii imewezesha jamii kuelewa umuhimu wa uhifadhi, kuongezeka kwa maeneo yanayohifadhiwa, kurejea kwa uoto wa asili na kuongezeka kwa shughuli za ufugaji wa nyuki katika maeneo yanayohifadhiwa.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA

ITILIMA
DISTRICT COUNCIL

## UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA UONGEZAJI WA KIPATO KATIKA JAMII





*Uzoefu wa Kikundi cha Malela katika Kijiji cha Isengwa*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ni moja ya Halmashauri 6 za Mkoa wa Simiyu iliyoanzishwa mwaka 2012 ikitokana na mgawanyo wa Halmashauri za Wilaya za Bariadi na Maswa. Halmashauri inapakana na H/W za Busega upande wa magharibi, Bariadi upande wa Kaskazini, Meatu na Maswa upande wa Kusini na Ngorongoro (Mkoani Arusha) upande wa Mashariki. Kijiografia, Halmashauri inapatikana katika Latitudo $3^0$44′ Kusini na Longitudo $33^0$29′ Mashariki. Halmashauri ina eneo la 2,647.7km$^2$ ambalo 1,938.70km$^2$ ni ardhi inayofaa kwa kilimo na ufugaji, 640km$^2$ ni pori tengefu la Maswa na sehemu iliyobaki, 69km$^2$ ni mito midogo, vichaka na vilima.

Kiutawala, H/W ya Itilima imegawanyika katika Tarafa 4 yaani Kanadi, Bumera, Itilima and Kinang'weli, Kata 22, Vijiji 102, Vitongoji 581 na kaya 43,597. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ilikuwa na wakazi 313,900; 165,398 wakiwa wanawake na 148,502 wanaume. Wastani wa wakazi katika kaya ni 7.2 na ongezeko la watu la 1.8%.




***Ramani ya H/W ya Itilima na Mkoa wa Simiyu***

Shughuli kuu za kiuchumi za H/W ya Itilima ni uzalishaji wa mazao na ufugaji unaohusisha zaidi ya 80% ya wakazi. Kilimo cha kujikimu ndio mfumo mkuu ambapo mahindi ndio zao kuu la chakula na mazao mengine ni uwele, mpunga, viazi vitamu, mhogo, maharage, maharage ya kijani na njegere. Mazao ya biashara ni pamba, alizeti na dengu. Ufugaji ni shughuli kuu ya pili ya kiuchumi inayochangia kwa kiasi kikubwa kwenye uchumi wa Halmashauri.

Kikundi cha Malela kilichopo katika Kijiji cha Isengwa, Kata ya Lagangabilili kilianzishwa Juni, 5 2012 kikiwa na wanachama 60 kwa lengo la kutunza kingo za mto Simiyu na kujihusisha na shughuli rafiki kwa mazingiza kama uhamasishaji wa mbinu za kilimo endelevu kwa ardhi na kwa kutumia matuta, upandaji miti na urejeshaji wa mazingira ya asili (ngitili). Kikundi pia kinajihusisha na uboreshaji wa uwepo wa maji kwa ajili ya mifugo kwa kupunguza uwepo wa mifugo kwenye kingo za mto, kuhamasisha utunzaji endelevu wa kingo za mto Simiyu na kuendesha shughuli rafiki kwa mazingira za uongezaji wa kipato karibu na mto. Pia, kikundi kinajihusisha na uanishaji wa maeneo mbadala ya kuchimba mchanga na kokoto kwa ajili ya ujenzi na shughuli za kiuchumi kama ufugaji wa nyuki. Shughuli kuu za kiuchumi za jamii ya kijiji cha Isengwa ambapo kikundi cha Malela kipo ni ufugaji na kilimo kisicho cha kibiashara karibu na mto Simiyu. Wanachama wa kikundi cha Malela waliamua kutokomeza shughuli zote haribifu katika kingo za mto.

## 2.0 TATIZO

Mto Simiyu hutiririka kuelekea Ziwa Viktoria katika eneo la Maziwa Makuu la Afrika. Kama mojawapo ya mito sita iingizayo maji Ziwa Viktoria, Mto Simiyu ni moja ya vyanzo vya juu vya Mto Nile. Mto Simiyu huanzia mlima Loolmalasin na miinuko ya Ngorongoro. Hutiririka kupitia Serengeti kuelekea ghuba ya Magu katika Ziwa Viktoria. Mto Simiyu una matawi mawili yanayoingia, kutokea kulia, Mto Duma na Komahola na kutokea

kushoto, Mto Maloho. Kabla ya kuingia ziwani, Mto Simiyu huunda chanzo muhimu cha kipato kwa jamii za H/W za Maswa na Itilima. Ukweli huu ulileta mgandamizo katika mto na kingo zake kama inavyoelezwa hapa chini.

Utafiti uliofanywa kuhusu uchafu katika mito yote inayoingiza maji Ziwa Viktoria ulionesha kuwa Mto Simiyu ulichangia 42.3% ya uchafu wote kwa mwaka ikiwa ni pamoja viuatilifu, viuamagugu na mbole za viwandani. Jamii zinazoishi karibu na mto huu zilisababisha mmonyoko mkuu wa udongo kama matokeo ya mbinu zisizo endelevu za kilimo, ukataji miti hovyo, kuzidi kwa mifugo kuliko uwezo wa ardhi iliyopo, kuingia kwenye ardhi oevu, usimamizi duni wa sheria na kanuni za mazingira na utupaji taka usiodhibitiwa. Haya yote yalileta uharibifu wa mazingira, uchakavu wa kingo za mito na uchafuzi wa maji.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la Halmashauri na Kikundi cha Malela chini ya uangalizi na ufadhili wa Mradi wa Menejimenti ya Mazingira ya Ziwa Viktoria (LVEMP II) lilikuwa kupunguza mgandamizo wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya mto yaliyokuwa yameharibika sana na kuboresha vipato vya jamii zilizotegemea mali asili za Mto Simiyu na Ziwa Viktoria kwa Ujumla. Mradi huu ulikuwa suluhisho kwa changamoto zilizokabili eneo la mto Simiyu katika H/W ya Maswa/Itilima kama ilivyoainishwa na wataalamu wa Halmashauri kwa kushauriana na jamii zinazoishi karibu na mto  kwa kutumia mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD). Changamoto hizo zilijumuisha mmonyoko wa udongo, kupanuka kwa kingo za mto, kupungua kwa ubora wa maji, kupotea kwa misitu na ukosefu wa taasisi za kusimamia mazingira na raslimali ya maji katika jamii.

Mradi huu ulilenga katika kupunguza madhara haya kwa kuhamasisha jamii na kujenga uwezo wa jamii kutunza mazingira. Mradi ulilenga kuanzisha jumuia za watumia maji, kupima na kuweka alama na mipaka ya mto, kuboresha uoto katika bonde la mto kwa kupanda miti na majani mapya na kuweka mifumo ya ufuatiliaji na upimaji thabiti wa utekelezaji.

Katika kusaidia na kuwezesha kikundi cha Malela, Halmashauri ililenga kutunza maliasili hasa Mto Simiyu, na kuboresha vipato vya jamii. Jitihada hii ililenga kuanzisha mpango wa upandaji miti karibu na mto, kushirikisha jamii katika kulinda na kutunza mazingira na kuongeza kipato kupitia ufugaji wa nyuki.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Utekelezaji wa mradi huu ulihakikisha ushiriki kamilifu wa jamii, wataalamu wa Halmashauri na watumishi wa wa mradi (LVEMP II). Mkakati mojawapo muhimu ulikuwa uhamasishaji wa jamii na kujenga uelewa. Mkakati huu ulihusu utoaji wa elimu kwa jamii zote za karibu na kingo za mito kuhusu madhara ya kuendelea kuendesha shughuli za uzalishaji ndani 60m kutoka Mto Simiyu. Vijiji vyote vilielimishwa kuhusu uharibifu wa mazingira utokanao na mbinu duni za kilimo. Mbinu za kilimo zilizotumika kabla ya mradi huu zilijumuisha ukataji miti yote, kuchoma moto ili kuandaa mashamba, kulima kwenye kingo za mito, utumiaji wa mbolea za kemikali kwenye mashamba yaliyopo kwenye kingo za mito na kuchunga mifugo kwenye mashamba baada ya kuvuna. Utoaji wa elimu ulijikita katika masomo ya kuwapa taarifa wakulima kuhusu kuharibika kwa mto, kupungua kwa uzalishaji wa ardhi pamoja na madhara ya muda mrefu endapo mto utakauka.

Mafunzo ya mwanzo na uandaaji wa jamii vilifanyika kwa pamoja. Wataalmu wa Mradi wakishirikiana na Halmashauri waliendesha mafunzo kwa wawezeshaji wa wilaya (DFTs). Wawezeshaji hawa walipatiwa stadi za namna ya kuingia katika jamii, kuwaunganisha wanajamii na kaya, usimamizi wa mabadiliko, usimamizi wa msingi wa mazingira, miradi ya kuongeza kipato na namna ya kuunda vikundi vya kijamii rafiki kwa mazingira. Wawezeshaji waliainisha kaya zote katika vijiji zilizoendesha shughuli za uzalishaji karibu na mto na kuendesha mikutano ili kuwaandaa kwa ajili ya mabadiliko kuelekea matumizi sahihi na endelevu ya ardhi. Kwa kutumia mfumo wa O&OD, wanajamii waliamua na kuridhia uanzishaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo ya jamii.

Halmashauri iliwezesha vijiji vilivyopo karibu na kingo za mto kuendesha mikutano ya vijiji kwa kutumia wawezeshaji. Mikutano hii ilikuwa muhimu katika kuainisha na kuridhia kaya halisi ambazo zilimiliki ardhi kisheria na kiasili karibu na kingo za mto. Ilikuwa muhimu kwa kijiji kwa ujumla wake kukubaliana kuhusu umiliki; ambayo ingesaidia kuunda vikundi vya kaya ambazo zingeathirika ili kutoa usaidizi toka mradi (LVEMP II) na Halmashauri. Mikutano ya vijiji ilikuwa muhimu pia kwa ajili ya kufikia makubaliano chanya na endelevu kuhusu utunzaji wa mazingira wa jumla wa kingo za mto na jamii yote. Ni muhimu kufahamu kuwa kaya nyingi katika jamii hizi hazilimi tu ili kujipatia kipato bali huchunga mifugo bila mipaka hivyo kuongeza mgandamizo kwenye matumizi ya ardhi, mto pamoja na kingo zake. Makubaliano toka makundi mbalimbali ya vijiji yalikuwa muhimu kwa utekelezaji usiokuwa na vikwazo na uendelvu wa jitihada hii.

Uandaaji wa jamii; mikutano ya vijiji na uwezeshi fanisi wa wawezeshaji (DFTs) ulipelekea kuundwa kwa vikundi mbalimbali vya kijamii. Mojawapo ya vikundi hivi ni Kikundi cha malela. Kwa ridhaa yao, baada ya uhamasishaji na kujengewa uelewa kwa wanavijiji waliolima na kuchunga mifugo karibu na kingo za mto, wanachama 60 waliunda kundi lao liitwalo Malela TAMTAM. Kikundi hiki kilianzishwa kikiwa na lengo dhahiri la kulinda ardhi na mto ndani ya mpaka wa 60m za kisheria. Kikundi kuliandika katiba na kujisajili Halmashauri ili kuendesha shughuli zake kisheria. Shughuli za kikundi zinahusu uandikishaji wa wanachama na utunzaji wa mazingira, utunzaji wa kingo za mto kwa gharama zozote, utoaji wa mafunzo kwa wasio wanachama kuhusu umuhimu wa mto na mazingira, ufugaji nyuki wa kisasa kwa ajili ya kuzalisha kipato, upandaji miti na ulinzi wa hifadhi ya mto ndani ya 60m. Licha ya katiba, kikundi na kijiji wametunga sheria ndogo za udhibiti wa mto, kingo zake na mazingira kwa ujumla. Kikundi kimeweka taratibu na ratiba ya doria kwenye maeneo yanayotunzwa na kuhifadhiwa.



***Viongozi wa Kikundi cha Malela***

Halmashauri, kwa kutumia wawezeshaji, iliendesha mafunzo ya kina kuhusu ufugaji wa nyuki. Mafunzo yalijikita katika taarifa muhimu kuhusu ufugaji nyuki wenye tija, uzalishaji na vigezo vya ubora wa mazao ya

asali, mbinu unganishi za mazao ya nyuki na utafutaji wa masoko ndani ya nchi na kimataifa. Wanavijiji na wanachama wa vikundi walihudhuria mafunzo kwa vitendo kuhusu utengenezaji wa mizinga na uchaguaji wa maeneo ya kutundika mizinga, utundikaji wa mizinga, kalenda ya ufugaji nyuki, msimu na mbinu za uvunaji, utunzaji wa kumbukumbu za uzalishaji na michango ya wanachama, manunuzi na taratibu za kifedha, ufungashaji bora wa mazao ya nyuki na masoko.



***Wavunaji asali tayari kuvuna***



***bidhaa za Kikundi cha Malela***

**5.0 RASILIMALI**

Mradi wa LIVEMP II, H/W ya Itilima, Afisa Mtendaji wa Kata na wanakijiji walichangia, kusaidia na kutekeleza jitihada hii ya kijiji. Mradi wa LIVEMP II kama mwanzilishi wa jitihada ya utunzaji na uhifadhi wa bonde lote la Ziwa Viktoria ulitoa fedha za awamu ya kwanza TZS 33,700,068.00 kwa ajili ya shughuli za uhifadhi. H/W ya Itilima ilichangia TZS 1,685,003.00 kusaidia jamii kujikita katika uhifadhi na shughuli ambazo ni rafiki kwa mazingira.  Katika jitihada hizi, jamii zilichangia TZS 7,190,000.00 kama inavyooneshwa kwenye jedwali 1. Rasilimali hizi zilitumika kununua vifaa vya ofisi, vifaa vya ufugaji wa nyuki, kuweka mipaka na mabango ya onyo na maadalizi ya maeneo ya uhifadhi. Halmashauri ilitumia fedha kwa ajili ya usafiri, shughuli za mafunzo na uwezeshi wa watumishi. Jumla ya TZS 42,575,071.00 zilitumika kufikia malengo.

**Jedwali 1: Rasilimali Zilizotumia**

| N | Chanzo | Kiasi TZS | Asilimia | Aina ya Mchango |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Jamii | 7,190,000.00 | 17% | Nguvukazi |
| 2 | LIVEMP II | 33,700,068.00 | 79% | fedha |
| 3 | H/W yaItilima | 1,685,003.00 | 4% | Utaalamu |
| Jumla | | 42,575,071.00 | 100% | |

**Jedwali 2: Muhtasari wa Matumizi (Malela)**

| N | Shughuli | Fedha zilizotumika |
|---|---|---|
| 1 | Ununuzi wa Mizinga | 10,712,000/= |
| 2 | Ununuzi wa vifaa vya uvunaji asali, vifungashio na mashine za kuchakata asali | 11,901,000/= |
| 3 | Mafunzo na uhamasisjaji kwa jamii | 7,948,000/= |
| 4 | Uandishi wa katiba | 95,000/= |
| 5 | Mbao za matangazo na vipeperushi | 72,000/= |
| 6 | Tathmini na Taarifa | 530,000/= |
| 7 | Vifaa vya ofisi | 158,000/= |
| 8 | Maandalizi ya eneo la mradi | 135,000/= |
| 9 | Mabango | 1,930,000/= |
| 10 | **Jumla** | **33,481,000** |

**6.0 MATOKEO**

Jitihada hii ya pamoja ya uhifadhi wa mazingira ya Mto Simiyu umeleta matokeo mbalimbali yenye faida kwa Halmashauri, jamii na bonde lote la Ziwa Viktoria. Jitihada hii kwa uhakika imeonesha faida katika kupungua kwa uchafuzi wa mazingira. Maboresho katika mbinu za kilimo na kujizuia kwa jamii kuingia katika kingo za mto kumewezesha kupungua kwa kiasi cha udongo, takataka na mabaki ya viwatilifu vinayoingia Mto Simiyu na Ziwa Viktoria. Kupungua huku ni matokeo ya uelewa wa kutosha wa jamii kuhusu uhifadhi na utunzaji wa eneo la 60m na kingo za mto. Jamii zimekuwa rafiki na mawakili wa utunzaji mazingira kupitia maamuzi ya vijiji na shughuli za vikundi. Urafiki kwa mazingira unajionesha dhahiri katika udhibiti wa uchungaji wa mifugo na kilimo cha mazao ndani ya 60m za kingo za mto ambapo tatizo hili limedhibitiwa kwa 90%. Wakulima na wafugaji wamekubali kutumia ardhi iliyo mbali na maeneo ya hifadhi za mto na kufanya doria ya pamoja, ambapo kila mwanakijiji na mwanachama wa kikundi anawajibika kwa hiari kutoa taarifa za ukiukaji wa sheria za mazingira kwa Serikali za vijiji au uongozi wa vikundi.

Mchangiaji mkuu wa pili kwenye maboresho ya mazingira ya Mto Simiyu ni programu endelevu za upandaji miti katika kingo za maji. Upandaji miti na kujizalisha kwa uoto wa asili unaotokana na kutokuwepo kwa shughuli haribifu za binadamu vimeondoa uwezekano wa uchafu kuingia kwenye mto. Miti iliyopandwa na uoto wa asili uliojizalisha vimeboresha ardhi, kurejesha miti dari na kuponya kingo za mto. Hali hii kwa ujumla huitwa urejeshaji wa vigezo vya ikolojia ya asili vya kingo za Mto Simiyu ambapo jamii zinaendelea kwa hamasa kutunza na kuhifadhi mazingira. Mto unaendelea kuwa na sifa yake ya zamani katika miaka ya 1970.



***Mikuyu na Migunga ikishamiri kando ya Mto Simiyu***

Jitihada za uhifadhi na utunzaji wa mazingira zimeleta kwa mara nyingine mazingira yanayofaa kwa wanyama wa porini kuishi. Kwa mfano, Fisi ambao walikimbia kingo za mto, wamerudi; hii inaonesha kurejea kwa sifa za makazi asilia ya wanyama. Fisi hula wanyama wengine na huua wanyama wa jamii ya paka; ishara kuwa kuzaliana kwa misitu kumerejesha wanyama mbalimbali wa porini kutokana na ukweli kwamba misitu na majani huwapatia wanyama chakula na sehemu za kujificha na hivyo kuleta uwiano wa kiikolojia. Miti na majani vimedhibiti majanga mbalimbali yaliyokuwa yakitokea. Mafuriko na mmonyoko wa udongo ambayo yalitokea kila msimu wa mvua yamedhibitiwa. Udhibiti wa mafuriko na mmonyoko wa udongo vimeondoa kabisa hasara za mazao yaliyokuwa yakisombwa na maji ya mvua. Hali hii imeboresha uzalishaji na uhakika wa chakula.

Ubora wa mazingira ya hifadhi za kingo za mto umeboresha uzalishaji wa ardhi iliyo karibu na kingo hizo. Uzalishaji wa mazao ya kilimo na ufugaji wa nyuki umeongezeka. Haya yote yamechamgia kwenye vipato vya wanakijiji; hasa kwa wanachama wa Kikundi cha Malela. Vipato vya wanachma wa Malela vimeongezeka na kuleta viwango bora vya kuishi na motisha kuongezeka kushiriki katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Aidha, ongezeko la kipato limetokana na mbinu za kisasa za ufugaji wa nyuki. Kikundi cha Malela kina

mizinga 140 katika eneo la hifadhi ambapo mwaka 2014/13 jumla ya TZS 6,200,000.00 zilipatikana kutokana na uuzaji wa asali iliyovunwa. Kama matokeo ya kuongezeka kwa kipato na hadhi ya wanachama wa Malela; kiongozi mmoja wa kikundi amekuwa Diwani wa Kata ya Lagangabilili. Umaarufu wa kiongozi wa kikundi hiki kugombea na kushinda uchaguzi ulitokana na shughuli za utunzaji mazingira na ufugaji nyuki. Vijiji vyote katika Kata hii vilitambua huduma na jitihada zake katika kuunganisha jamii na kuongoza kikundi, hivyo kumpatia zawadi kwa kumchagua kuwa mwakilishi wao katika Halmashauri.





***Mizinga ya Kisasa pembeni mwa Kingo za Mto Simiyu***

Kikundi cha Malela kinatambua thamani ya asali kwa afya, hivyo hupatia kila kaya ya mwanachama lita moja ya asali kwa matumizi ya chakula au dawa. Pamoja na kuongezeka kwa fedha taslimu, asali inayotolewa kwa familia imeongeza ari na hiari ya jamii kuthamini uhifadhi wa mazingira na kushiriki kwa furaha katika shughuli za uhifadhi. Hili linajidhihirisha kwa wanavijiji kuonesha uzalendo kwa kushiriki katika uondoaji wa magugu maji yanayotishia uhai wa mto na ziwa.

Kikundi cha Malela kinatambulika kitaifa na kimataifa kwani shughuli zake zinasambaa kupitia maonesho na makongamano mbalimbali. Kikundi cha Malela kinashiriki katika kumbukumbu za mazingira kidunia. Katika kongamano moja la Arusha kikundi kilishinda nafasi ya pili katika upimaji wa mbinu bora za usimamizi wa maeneo chepechepe katika Jumuia ya Afrika Mashariki na Sekretatieti ya Tume ya Bonde la Ziwa Viktoria. Kikundi cha Malela pia hushiriki maonesho ya nanenane katika kanda zote. Katika maonesho na makongamano kikundi huuza asali iliyochakatwa na kufungashwa vema. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha vyeti vya kutambuliwa kwa utendaji bora katika ngazi mbalimbali.


EAST AFRICAN COMMUNITY
LAKE VICTORIA BASIN COMMISSION SECRETARIAT
Lake Victoria Environmental Management Project Phase Two
(LVEMP II)
CERTIFICATE OF PARTICIPATION
Awarded to
Isengwa Lagangabilili Bee Keeping
Sub-project
For Emerging the 1st Runner-up in the Evaluation of Good Practices in
Watershed Management
5th June, 2014
MR TELLY-EUGENE MURAMIRA
Deputy Executive Secretary, Projects and Programmes


BARIADI DISTRICT COUNCIL
The societies (Application for Registration), Sections, 1991
(Sections 29)
CERTIFICATE OF RECOGNITION CD/BRD/CBO'S
NO 289
I here by certify that MALELA GROUP- ISENGWA
Has this day been recognized under the societies ordinance
1991
Ag: Recogniser of CSO
Community Development Department
BARIADI

***Vyeti vya ushirki na kutambuliwa***

H/W ya Itilima sasa inajivunia kuwa kituo cha kujifunzia ufugaji nyuki. Vikundi vingi vya ufugaji nyuki na watu binafsi wamekuwa wakitembelea Kikundi cha Malela kupata ushauri wa kitaamu katika ufugaji nyuki pamoja na masuala ya utawala na uendeshaji wa vikundi. Kikundi cha Malela pia ni kituo cha kujifunza uongezaji wa thamani wa mazao ya nyuki.

Kuhitimisha kuhusu matokeo ya jitihada ya H/W ya Itilima, ni muhimu kutambua kuwa wanakijiji, jamii na vikundi vimeshuhudia kuongezeka kwa vipato kutoka mazao yasiyo ya miti, kuimarika kwa elimu ya jamii kuhusu uhifadhi na matumizi ya maji, kuongezeka kwa usawa katika ugawaji wa maji na uhifadhi thabiti wa vyanzo vya rasilimali maji. Ingawa jitihada hii imetekelezwa katika H/W ya Itilima, matokeo yake yamesambaa kufuata mto, mbali kabisa na mipaka ya Halmashauri, moja kwa moja hadi Ziwa Viktoria.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Halmashauri imeweka mikakati ya uendelevu ifuatayo;

(i) Kikundi kina akaunti ya benki ili kujiridhisha kuhusu usimamizi stahiki wa fedha na kuwezesha uwekezaji siku za mbele.

(ii) Kikundi kimesajiliwa na huendesha shughuli zake kwa kutumia katiba iliyo hai. Katiba inasisitiza kuwa kila mwanachama lazima awe na walau mizinga miwili anayomiliki mwenyewe.

(iii) Kuendelea kujenga uelewa wa jamii kuhusu utunzaji wa mazingira, uhifadhi na upandaji miti pamoja na mbinu stahiki za ufugaji nyuki, ufungaji bora wa mazao ya nyuki na utafutaji wa masoko.

(iv) Mipango ya kuanzisha kituo cha kukusanyia asali kukidhi mahitaji ya Vijiji na Jamii za H/W ya Itilima.

(v) Kuboresha na kusimamia kikamilifu sheria ndogo zinazolinda maeneo ya mradi. Uvamizi katika eneo la uhifadhi hutozwa adhabu kali ya faini ya TZS 50,000/= .

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya mradi huu yamejikita katika utayari wa jamii kushiriki katika uhifadhi wa mazingira, kukubali utaalamu ulitolewa na wawezeshaji (DFTs), uongozi bora wa Mwenyekiti wa Kikundi cha Malela, uwajibikaji wa wanachama wote na matumizi mazuri ya rasilimali. Siri kubwa katika jitihada hii ni kutambua madhara ya uharibifu wa mazingiza na faida za uhifadhi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI

**UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA KUISHI NA ELIMU KWA WATOTO WENYE ULEMAVU WA NGOZI**




*Uzoefu wa H/W ya Misungwi*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ni moja ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Mwanza iliyopo Kusini mwa Mkoa. Halmashauri hii inapakana na Jiji la Mwanza kwa upande wa Kaskazini, H/W za Shinyanga upande wa Kusini, Sengerema, Buchosa na Nyang'hwale upande wa Magharibi na Kwimba na Magu upande wa Kaskazini Mashariki. Halmashauri ina eneo la 2,553km$^2$ ambapo kati yake 2378km$^2$ ni eneo la nchi kavu na 175km$^2$ ni Ziwa Viktoria. Halmashauri ina Tarafa 4 ambazo ni Misungwi, Mbarika, Inonewa na Usagara, Kata 27, Vijiji 113 na Vitingoji 721.

Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina jumla ya watu 326,503 kati yao wanawake ni 166,230 na wanaume ni 160,273. Idadi ya watu kwa kilometa ya mraba ni 118 na wastani wa ongezeko ni 2.8% kwa mwaka. H/W ya Misungwi inapatikana katika ukanda wenye hali ya ukame wa wastani ambapo kuna mvua zisizo za uhukakika kati ya 700mm - 1000mm kwa mwaka. Kiwango cha joto ni kati ya 18$^0$C - 30$^0$C na mwinuko wa 1000m - 1500m kutoka usawa wa bahari.

Asilimia 92 ya wananchi wanaishi vijijini na wanaendesha maisha yao kutokana na kilimo kidogo cha kujiimu, ufugaji na wachache wanajihusisha na biashara ndogondogo na uvuvi kwa wale wanaonshi pembezoni mwa fukwe za Ziwa Vitoria. Eneo linalofaa kwa kilimo 1358 km$^2$ (53%), eneo la ufugaji ni 960 km$^2$ (37.6%) na misitu ni 60 km$^2$ (2.4%). Mazao makuu yanayozalishwa ni uwele, mtama, mpunga, mhogo, viazi vitamu na pamba. Watu wanaoishi karibu na fukwe za Ziwa Viktoria wanajihusisha na uvuvi kama chanzo kikuu cha mapato; uvuvi huchangia 5% ya mapato ya Halmashauri na kutoa ajira kwa 1% ya wakazi wa Halmashauri. Shughuli za uvuvi zinafanywa kwa kutumia mitumbwi ambapo kuna jumla ya mitumbwi 837 na nyavu zipatazo 4,162. Samaki wanaovuliwa hukusanywa katika maeneo tofauti ya fukwe ambayo yamebuniwa na wananchi wenyewe.

Halmashauri ina utajiri wa rasilimali za madini zinazojumuisha dhahabu na almasi. Shughuli za uchimbaji wa madini zinafanywa na wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo tofauti. Wachimbaji hawa wanatumia nguvu kubwa na tekinolojia duni. Hata hivyo, kuna baadhi ya makampuni kutoka nje ambayo yanajihusisha na uchimbaji wa madini katika maeneo ya Halmashauri.

Kuhusu elimu, Halmashauri ina shule za msingi 145 kati yake 138 ni za Serikali; 3 (Misungwi, Busagara na Kikgongo) ni shule kwa watoto wenye mahitaji maalumu ambapo ( 1 kwa ajili ya watoto wenye utindio wa ubongo, 1 watoto wenye upofu, uoni hafifu na wenye ulemavu wa ngozi na nyingine ya viziwi). Shule 7 zilizosalia ni binafsi na za mchepuo wa kingereza (Misungwi, Exodus, Lwasa, Rishor, Butibubage na Usagara). Hadi kufikia mwezi Januari 2016, idadi ya wanafunzi wa shule za msingi ilikuwa 86,166, kati yao 43,871 ni wavulana na 42,295 wasichana. Idadi ya walimu mwaka 2016/2017 ilikuwa ni 1,492 kati yao 795 ni wanaume na 697 ni wanawake. Kiwango cha undikishaji kiliongezeka kutoka 62% mwaka 2010 hadi 98 % mwaka 2015. Uandikishaji mwaka 2016 ulikuwa 93%. Sababu za kuongezeka kwa uandikishaji ni kufutwa kwa ada za shule na kampeni za uandikishaji wa lazima. Kwa upande wa elimu ya sekondari, Halmashauri ina shule za sekondari 27. Mwaka 2015/2016 kulikuwa na jumla ya wanafunzi 10,643 katika shule za sekondari kati yao wanafunzi 5,173 ni wavulana na 5,470 ni wasichana. Mahitaji ya walimu katika shule za sekondari mwaka 2015/2016 yalikuwa 723, hata hivyo, idadi ya walimu waliokuwepo ilikuwa 602 ambapo 400 ni wanaume na 202 ni wanawake.

Shule ya Msingi Mitindo ipo katika mji wa Msingwi, umbali wa 4km kutoka makao makuu ya Halmashauri. Shule hii ilianziswa mwaka 1956 kama shule ya kati. Mwaka 1961 ilibadilishwa na kuwa shule ya msingi kamili na mwaka 1975 ilihuishwa na kuwa na masomo ya ufundi na sayansi ya jamii. Mwaka 1978 elimu maalumu ilianzishwa kwa watoto wenye tatizo la uoni. Mwaka 1989 shule ilianza kuandikisha watoto wenye uoni hafifu na hadi kufikia mwaka 2011 wanafuzi viziwi walianza kuandikishwa. Kufikia mwaka 2016, shule iliuwa na jumla ya wanafunzi 1,317 ambapo wanafunzi 92 walikuwa na ulemavu wa ngozi, wanafunzi 130 walikuwa na ulemavu wa aina nyingine. Shule ina waalimu 51, daktari 1, walezi wa wanafunzi (2 wakiume na 2 wakike),

wapishi 4 na mlinzi 1 ambaye analinda wakati wa mchana; usiku ulinzi unafanywa na jeshi la polisi ambapo polisi 2 hulinda eneo lote la shule.

**2.0 TATIZO**

Binadamu wote wana haki ya kuishi bila kubaguliwa, hata hivyo, kuanzia mwaka 2007, ilibainika kuwepo kwa mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi hususani katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Geita kutokana na imani potofu. Baadhi ya waganga wa jadi waliaminisha watu kwamba viungo vya wenye ulemavu wa ngozi vinasaidia kuleta bahati na utajiri. Hali hii ilisababisha mauaji na utekaji wa watu wenye ualibino hasa watoto. Uhitaji wa watoto wenye ualibino kujiunga na shule ya msingi Mitindo uliongezeka kuanzia mwaka 2008 wakati mauaji yalipokithiri. Juhudi zilifanywa na Halmsahauri na Serikali kuu kulinda watu wenye ualibino na janga hili na kuamua kuwahifadhi katika shule ya Msingi Mitindo. Awali kabla ya kuanza kwa mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi shule ilikuwa na wanafunzi wa aina hii 10 tu, lakini kuanzia kipindi ambacho mauaji hayo yamekithiri wanafunzi 16 kutoka shule mbalimbali walihamishiwa shule ya Mitindo na kuongeza idadi kufikia wanafunzi 26 mwaka 2008 na kufikia mwaka 2016 wanafunzi wenye ualibino waliongezeka kufikia 92.

TAKWIMU YA WANAFUNZI WA BWENI – 2016
SHULE YA MSINGI MITINDO

| DARASA | VIZIWI WAV | VIZIWI WAS | VIZIWI JML | ALBINISM WAV | ALBINISM WAS | ALBINISM JML | WASIOONA WAV | WASIOONA WAS | WASIOONA JML | UONI HAFIFU WAV | UONI HAFIFU WAS | UONI HAFIFU JML |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| AWALI | | | | 14 | 9 | 23 | 4 | 2 | 6 | | | |
| I | 14 | 11 | 25 | 4 | 12 | 16 | 4 | 2 | 6 | | 1 | 1 |
| II | 6 | 5 | 11 | 4 | 6 | 10 | 2 | | 2 | | 3 | 3 |
| III | 7 | 8 | 15 | 10 | 10 | 20 | 4 | 1 | 5 | 3 | 4 | 7 |
| IV | 2 | 4 | 6 | 2 | 5 | 7 | 4 | 1 | 5 | 2 | 1 | 3 |
| V | 7 | 7 | 14 | 2 | 3 | 5 | 2 | 1 | 3 | 1 | 3 | 4 |
| VI | 2 | 1 | 3 | 2 | 1 | 3 | 3 | | 3 | 2 | 1 | 3 |
| VII | 2 | | 2 | 2 | | 2 | 1 | | 1 | 1 | 1 | 2 |
| JML | 40 | 36 | 76 | 40 | 46 | 86 | 24 | 7 | 31 | 9 | 14 | 23 |

| AINA YA ULEMAVU | WAV | WAS | JML |
|---|---|---|---|
| VIZIWI | 40 | 36 | 76 |
| ALBINISM | 40 | 46 | 86 |
| WASIOONA | 26 | 8 | 34 |
| UONI HAFIFU | 9 | 11 | 20 |
| JUMLA KUU | 115 | 101 | 216 |

***Takwimu za Wanafunzi wenye ulemavu katika shule ya msingi Mitindo***

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la kuanzishwa kwa kituo katika Shule ya Msingi Mitindo ni kuwaokoa watoto walioko katika mazingira hatarishi na kuimarisha upatikanaji wa ubora wa elimu kwa watu wenye ulemavu. Malengo mahususi ni pamoja na;

(i) Kujenga miundombinu ya kutosha (madarasa, mabweni, vyoo, uzio na kisima kirefu cha maji) kwa ajili ya watoto wenye ulemavu wa ngozi na kuwafanya waishi maisha ya furaha na kujifunza katika mazingira rafiki.

(ii) Kupatikana kwa vifaa vya kutosha vya kujifunzia ili kujenga uwezo wa watoto wenye ulemavu wa ngozi kupata elimu, upendo na matunzo ili kuwaandaa kwa shughuli za uzalishaji katika jamii.

(iii) Kuwapa huduma za chakula, ulinzi, usafiri na kulipia gharama za makazi ya kudumu katika kituo cha Mitindo

(iv) Kujenga uelewa kwa jamii ili kuachana na imani potofu kuhusu watu wenye ulemavu wa ngozi.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kituo cha watoto wenye ulemavu wa ngozi kilanzishwa katika Shule ya Msingi Mitindo mwaka 2008. Watu kutoka jamii mbalimbali walio kuwa na watoto wenye ulemavu wa ngozi na ambao walikuwa na umri wa kwenda shule waliruhusiwa kuwaleta na kuanza ama kuendelea na masomo katika kituo chini ya uangalizi na ulinzi imara. Uanzishaji wa kituo hiki ulihusisha kuzungusha uzio katika eneo lote la shule ili kuhakikisha

usalama. Wageni kutoka maeneo mbalimbali wakitaka kuitembelea shule inawalazimu kupata kibali kutoka kwa Mkuu wa Wilaya.

Shule ya Msingi Mitindo, kwa kushirikiana na Halmashauri, Serikali Kuu, Mashirika yasio ya kiserikali (NGOs), Washirika wa Maendeleo ya Elimu, taasisi binafsi na jamii kwa ujumla walitoa michango iliyowezesha ujenzi wa madarasa, bwalo, jiko, mabweni na vyoo. Halmashauri ilinunua vifaa vya kujifunzia kama kompyuta, mashine ya *thermoform,* mashine ya *Braille*, *CCTV magnifier*, na vifaa vingine vya kujifunzia ambavyo vilileta ufanisi katika kujifunza.

Halmashauri iliunda kamati tendaji iliyojumuisha makundi mbalimbali ya jamii. kamati ilikuwa na jukumu la kuelimisha jamii kuhusiana na mila na imani potofu kuhusu watoto wenye ualibino. Kamati iliwatia moyo wazazi na kuwahusia, kuwapenda, kuwalinda na kuwapeleka shule watoto wenye ualibino ili wapate elimu ya msingi katika shule ya msingi Mitindo. Kamati pia iliendesha kampeni za uhamasishaji kwa jamii katika kuelimisha jamii kuhusiana na ualibino. Ualibino na mauaji yanayombatana, vilifanywa agenda mtambuka ya kujadiliwa katika ngazi zote kuanzia Vitingoji, Vijiji hadi Wilaya. Uhamasishaji wa jamii kuhusu kuachana na imani potofu juu ya watu wenye ulemavu wa ngozi ulilenga kubadilisha mitizamo ya jamii. Progamu za uelimishaji ziliendeshwa kwa pamoja kati ya NGOs, Halmashauri na Jamii. Njia shirikishi zilitumika wakati wa utekelezaji. Elimu ya kutosha ilitolewa kwa jamii mbalimbali kuhusu ualbino na kusisitiza kuachana na waganga wa jadi ambao wanahamasisha mauaji ambayo ni kinyume na haki za binadamu. Kwa kiasi kikubwa jamii imepokea elimu hii na kukubali kushiriki katika progamu hii kwa kutoa ulinzi na taarifa kuhusu watu wenye mipango na majaribio ya kuua watu wenye ualibino. Mikutano mbalimbali ya kuelezea ukubwa wa tatizo iliendeshwa kwenye shule, jamii, Vijiji, Kata Tarafa na Halmshauri.

Halmashauri iliunganisha wadau mbalimbali kama jamii, NGOs, sekta binafsi, washirika wa maendeleo ya elimu na wadau wengine kufadhili ujenzi wa kituo. Ushawishi ulilenga kupata fedha za ujenzi wa miundombinu na utoaji wa huduma nyingine. Shughuli zilizotekelezwa zilijumuisha kuandaa michoro ya majengo, kuweka bajeti ya makisio ya ujenzi, kukusanya malighafi za ujenzi kama mawe, matofali, mchanga na rasilimali nyingine zinazotumika katika ujenzi, utangazaji wa zabuni, kuchagua mkandarasi na kusaini mikataba. Jamii ilishirikiana na Halimashauri katika hatua za awali za ujenzi wa msingi, kuta, kuezeka, kupiga ripu, rangi, kuweka umeme na kununua samani kama vitanda, magodoro, shuka, vyandarua vya mbu na mito ya kulalia. Kituo kinatoa huduma za malazi pamoja na chakula, maji safi na salama, na waalimu wanajihusisha na ufundishaji na kubuni mbinu za kuwawezesha watoto wenye ulemavu wa ngozi kujifunza.

Halmashauri iliendesha zoezi ufuatiliaji na tathmini ya kina katika ngazi zote kuhakikisha usalama wa watoto wenye ulemavu wa ngozi unasimamiwa kupitia watendaji wa Vijiji na Kata ambao ndio huunganisha jamii katika maswala ya ulinzi na usalama. Juhudi hizi zimesababisha kupungua kwa kwa imani potofu na vitendo hatarishi kwa watu wenye ualbino; na kuwafanya watoto wenye ualbino kutambua haki zao za kuishi kama ilivyo kwa watoto wengine.

Halmsahauri ilianzisha progamu ya uchunguzi wa afya kwa watoto wenye ulemavu wa ngozi shuleni; uchunguzi wa madaktari ulibainisha matatizo mabalimbali ya kiafya yanayoathiri watoto wenye ualbino. Daktari kutoka KCMC alishauri namna ya kutunza ngozi kwa kutumia aina ya mafuta ya kuifanya ngozi kuwa nyororo muda wote na kuvaa kofia na miwani za kuzuia mwanga wa jua kupenyeza na kuwaletea madhara.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulitumia rasilimali mbalimbali. Uongozi wa kituo ulihitaji kuwa na watumishi wenye sifa (Waalimu, Walezi, Askari, walinzi, wapishi, madaktari, na washauri). Jamii ilishiriki kikamilifu katika kuchangia kupitia nguvu kazi kwa kukusanya mawe ya ujenzi, mchanga na kutengeneza madawati. Rasilimali fedha zilitumika katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa madarasa, mabweni, bwalo la chakula, matundu ya

vyoo, ununuzi wa vitanda, magodoro, vyandarua, mito ya kulalia na shuka za kujifunika. Jedwali lifuatalo linaonesha matumizi ya rasilimali fedha.

**Jedwali Na 3: Rasilimali Fedha**

| No | Shughuli | Idadi | Gharama (TZS) | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa bwalo na jiko | 1 | 97,800,400 | H/W ya Misungwi |
| 2 | Ujenzi wa madarasa | 3 | 105,000,000 | Ubalozi wa Japani, Halmashauri na Jamii |
| 3 | Ununuzi wa kompyuta | 28 | 42,000,000 | Lions' Clubs |
| 4 | Ujenzi wa Vyoo | 8 | 4,500,000 | Lions' Clubs, Halmashauri na Jamii |
| 5 | Ujenzi wa uzio | 1 | 200,000,000 | Serikali Kuu |
| 6 | ununuzi wa shuka | 200 | | Social Action Trust Fund (SATF) |
| 7 | Ujenzi wa bweni na ununuzi wa vitanda | 1 | 150,000,000 | Lions Clubs |
| 8 | Ujenzi wa kisima kirefu | 1 | 5,000,000 | Lions Clubs |
| 9 | Utengenezaji wa madawati | 11 | 825000 | Jamii |
| 10 | Utengenezaji wa madawati | 120 | 72,000,000 | Social Action Trust Fund (SATF) |
| 11 | Utengenezaji wa madawati | 18 | 720,000 | Social Action Trust Fund (SATF) |
| 12 | Utengenezaji wa mabenchi | 50 | 750,000 | Living Children Centre Fund |
| 13 | Ununuzi wa magodoro | 100 | 7,000,000 | Living Water Children Centre Fund |
| 14 | Utengenezaji wa mabenchi | 45 | 1,935,000 | Good Neighbors |
| 15 | Ujenzi wa kisima | 1 | 5,000,000 | Lions Clubs |
| | **Jumla** | | **692,530,400** | |

**6.0 MATOKEO**

Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imekuwa moja wapo ya Halmashauri Tanzania zilizoanzisha vituo vya watoto wenye ulemavu wa ngozi ambapo wanaishi katika mazingira salama na kupata elimu kwa urahisi. Kituo cha Mitindo kinatoa huduma ya elimu na ulinzi kwa watoto hao ambapo miundombinu mbalimbali ya kuhifadhi watoto zaidi ya 92 wenye ualbino imejengwa. Miundombinu hiyo ni pamoja na mabweni 5, madarasa 3, bwalo 1, jiko 1, na matundu ya choo 8. Bweni 1 na darasa 1 bado vipo kwenye hatua za ujenzi.





***Darasa, uzio na Kompyuta***





***Kisima, Bwalo na Jiko***






***Vyoo na bweni***

Watoto wenye ualbino wamepata kituo sahihi cha hifadhi; Watoto wanaletwa kutoka Halmashauri mbalimbali za kanda ya ziwa na kutoka Wilaya nyingine za Tanzania kuja kusoma katia kituo cha Mitindo ambapo usalama umeimarishwa na elimu bora inapatikana. Jedwali lifuatalo linaonesha uandikishaji.

**Jedwali Na 4: Watoto wenye ualibino waliopokelewa**

| Mwaka | Wavulana | Wasichana | Jumla |
|---|---|---|---|
| 2012 | 20 | 20 | 40 |
| 2013 | 21 | 24 | 45 |
| 2014 | 20 | 22 | 42 |
| 2015 | 37 | 41 | 78 |
| 2016 | 42 | 50 | 92 |

**Jedwali Na 5: Uandikishaji mwaka 2016**

| Darasa | Wavulana | Wasichana | Jumla |
|---|---|---|---|
| Chekechea | 14 | 10 | 24 |
| I | 6 | 16 | 22 |
| II | 4 | 6 | 10 |
| III | 10 | 10 | 20 |
| IV | 2 | 5 | 7 |
| V | 2 | 2 | 4 |
| VI | 2 | 1 | 3 |
| VII | 2 | | 2 |
| **Jumla** | **42** | **50** | **92** |

Watoto wenye ualibino wanapata mahitaji maalumu; kituo kinawapatia watoto hao makazi bora, chakula malazi, nguo, viatu, kofia, miwani ya jua, maji safi na salama na mafuta maalumu ya ngozi. Elimu ya msingi wanayoipata inatolewa kwa njia rahisi ikihusisha vifaa kama *CCTV magnifier*, mashine za *braille* , darubini kuwawezesha kuona kwa urahisi. Watumishi mbalimbali wameajiriwa kutoa huduma kwa watoto hawa. Watumishi hao ni pamoja na walimu wenye uzoefu, walezi, mpishi na mlinzi. Huduma hizi zimewekwa kuhakikisha watoto wenye ulemavu wa ngozi wanajisikia kujaliwa kama binadamu wengine na wana haki sawa ya kuishi na kupata elimu kama wananchi wengine wa Tanzania.



*Wanafunzi na mavazi yao ya kuzuia jua*



*Mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi Mitindo, Walezi na Muuguzi*

Mbali na kuishi maisha mazuri kutokana na makazi mazuri na huduma ya ulinzi, watoto hawa wanapatiwa huduma ya uchunguzi wa kiafya mara kwa mara na wadau wa afya. Wadau hawa ni pamoja na Hospitali za Bugando, KCMC na Hospitali ya Wilaya ya Misungwi. Uhakika wa huduma za afya ni moja ya hitaji muhimu kwa watu wenye ualibino.

Mabadiliko katika jamii; jamii imefahamu namana ya kutunza na kuwalinda watu wenye ulemavu wa ngozi kutokana na elimu Iiliyotolewa na Serikali na AZAKI mbalimbali kama *Under the Same Sun* na *UNESCO*. Mitazamo ya jamii na imani potofu kuhusu watu wenye ualibino imebadilika. Jamii ipo tayari kutoa taarifa kwa jeshi la polisi kuhusu watu wanaohisiwa kuwa na tabia ambazo siyo rafiki kwa watu wenye ulemavu wa ngozi.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**


Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imekusudia kufanya kituo hiki kuwa endelevu; uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule wenye ulemavu wa ngozi kutoka maeneo mbalimbali Tanzania unaendelea. Miundombinu ya huduma katika kituo inaendelezwa na kuboreshwa. Uelimishaji wa jamii kuachana na mila na dhana potofu kuhusu watu wenye ualibino unaendelea. Timu ya Menejimenti ya Halmashauri inafanya ufuatiliaji kuhakikisha huduma za kituo zinatolewa ipasavyo. Halmashauri ina mpango wa kuajiri waalimu wa kutosha wenye taaluma ya kufundisha watoto wenye ualbino. Halmashauri ina mpango wa kutafuta wadau ili kufanya tathmini ya ufanisi wa kituo na kutoa ushauri katika maeneo yanayohitaji maboresho.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

Mafanikio ya jitihada hii yanatokana na kufanya kazi kama timu katika ngazi zote. Timu mbalimbali katika shule, jamii, Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya na Mkoa zilifanya kazi kubwa kufanikisha uandikishaji wa watoto wenye ulemavu wa ngozi na kuhakiksha ulinzi wao. Utayari wa Serikali na wadau mbalimbali kutoa rasilimali za kuanzisha kituo hiki ni siri nyingine ya mafanikio. Kuheshimu haki za binadamu kama inavyotambulika katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tamko la ulimwengu kuhusu haki za binadamu la mwaka 1948, haki ya kusikilizwa, haki ya utu, haki ya kuishi, uhuru wa kwenda sehemu yeyote, na haki ya kuwa huru na usalama kwa wote ni kichocheo kilichochangia kufanikiwa kwa jitihada hii.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA

## KUKUZA MFUKO WA AFYA YA JAMII KWA HUDUMA BORA ZA AFYA


HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA
STAKABADHI YA MCHANGO WA
MFUKO WA AFYA WA JAMII – (CHF)

29319

Tarehe 20/10 20 16

Nimepokea kwa EDA JIRANI DAUDI

ya (anwani)

Hesabu ya shilingi

senti

Kwa ajili ya CHF

Taslimu/Hundi No. TASLIMU




*Uzoefu wa H/W ya Musoma*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ni mojawapo ya Halmashauri 9 za Mkoa wa Mara. Halmashauri ina eneo la 2,653km$^2$ ambalo 2,456km$^2$ ni nchi kavu na 197km$^2$ ni maji. Halmashauri inapakana na H/W ya Butiama upande wa Mashariki, H/W ya Bunda upande wa Kusini na Kusini Mashariki na Ziwa Viktoria kwa upande wa Magharibi. Halmashauri ina Kata 21, Vijiji 68 na Vitongoji 375. Kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012 Halmashauri ina wakazi 216,409 ambao 106,163 ni wanume na 110,246 ni wanawake.

H/W ya Musoma ina kanda mbili za kijiografia zilizopo kati ya mwinuko wa 1000m na 1500m juu ya usawa wa bahari. Ukanda wa chini ambao huanza katika fukwe za Ziwa Viktoria una mwinuko wa 1200m juu ya usawa wa bahari ukichukua umbali wa kati 0 – 15km kutoka ziwani ambayo ni makazi ya jamii za wavuvi. Ukanda wa juu ni 1100m - 1500m juu ya usawa wa bahari na una milima, rasi, ghuba, miamba, tambarare na mito midogo iendayo ziwani. Hali ya hewa huwa na mvua kati ya 800mm - 1000mm kwa mwaka zikiwa na misimu miwili. Mvua za vuli hunyesha kipindi cha Oktoba hadi Desemba na masika huanza Machi hadi Juni; hali ya joto ni wastani kati ya 24$^0$C - 32$^0$C. Hali ya hewa huunda mazingira bora kwa uzalishaji wa mhogo, viazi vitamu, mtama, mahindi, maharage, mpunga, pamba na alizeti na inaruhusu kilimo cha mbogamboga kama nyanya, kabichi, biringanya, pilipili, pilipili hoho, mchicha, vitunguu na matango. Wakazi wa H/W ya Musoma hushughulika na uvuvi, kilimo na ufugaji.




***Ramani ya Mkoa wa Mara ikionesha H/W Musoma***

Halmashauri haina Hospitali ya Wilaya. Hata hivyo ina kituo cha afya 1, na Zahanati 27 ambazo 4 ni za mashirika ya dini. Kuna magari ya wagonjwa 5 yaliyopo Kituo cha Afya cha Murangi, na katika zahanati za Mugango, Nyakatende, Masinono and Kurugee. Kuna watumishi 206 wa afya. Vituo vyote vya kutolea huduma za afya vina akaunti za benki na vina kamati za uendeshaji zinazofanya kazi. Huduma za afya hutolewa kwa ushirikiano na Michango ya Serikali Kuu, Mapato ya Ndani ya Halmashauri na michango ya Jamii kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii.

Kugharamia huduma za afya katika jamii kulianza kujitokeza katika nchi zinazoendelea kukabiliana na changamoto zilizokuwepo kwenye mfumo wa kugharamia afya zilizojumuisha ukuaji duni wa uchumi, vikwazo katika sekta ya umma na uwezo mdogo kitaasisi. Kulipia gharama za afya katika jamii (Community Based Health Financing - CBHF) ni mbinu ambayo wanajamii (kaya) hulipia au kushiriki kulipia gharama za huduma za afya, ikiwapatia wanajamii nafasi kubwa ya kushiriki katika uendeshaji wa skimu ya ulipiaji na muundo wa huduma za afya.

Kutoka kwenye mfumo wa CBHF, skimu ya Mfuko wa Afya ya Jamii (Community Health Fund) nchini Tanzania ilitokana na utafiti uliofanywa kitaifa kuanzia mwaka 1990 hadi 1992 ulioonesha kuwa watu wengi vijijini na

mijini walikuwa tayari kuchangia ili kukabibiliana na tatizo la upungufu wa madawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya. Mfuko wa Afya ya Jamii uliundwa mwaka 1995 na wataalamu washauri wa kitanzania na kufanyiwa majaribio katika H/W ya Igunga mwaka 1996. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 1996, watu 21,046 kati ya 26,308 walikubali kuchangia mfuko wa afya ya jamii. Kabla ya utekelezaji wa mfuko huu kila kituo cha kutolea huduma ya afya kilipata dawa muhimu kupitia mfumo maalumu uliolenga kutoa dawa zenye thamani ya TZS150,000 kwa kisanduku, ikiwa ni 45% tu ya mahitaji ya kituo. Fedha zilizopatikana kutokana na mfuko zilijaza pengo kati ya mahitaji ya huduma za afya na raslimali chache za kutolea huduma. Mchakato uliotumika kuanzisha mfuko wa afya ya jamii ilikuwa mbinu ya kupata raslimali katika jamii za kujazia ulipiaji wa huduma za afya.

Kwa mujibu wa sheria ya mfuko wa afya ya jamii ya mwaka 2001 (Community Health Fund Act No.1 of 2001) malengo ya mfuko ni (i) kukusanya fedha kutoka kwa jamii ili kutoa huduma za afya kwa wanachama (ii) kutoa huduma bora na rahisi kwa mbinu endelevu kifedha (iii) kuboresha usimamizi wa huduma za afya katika jamii kwa kugatua na kujenga uwezo wa jamii kufanya maamuzi na kuchangia katika masuala ya afya.

Mfuko wa afya ya jamii ni utaratibu wa hiari unaoruhusu ukusanyaji wa rasilimali fedha katika jamii ili kutoa huduma za afya kwa wanachama wake. Mfuko huu huhitaji malipo ya awali kwa ajili ya huduma za afya na wanachama huchangia dharura kwa kupata huduma za bure. Kuna misamaha kwa ajili ya maskini na makundi maalumu. Misamaha pia hutolewa kwa wagonjwa ambao hawana sifa kisheria kusamehewa moja kwa moja lakini wanahitaji msamaha na huitwa "wasio na uwezo wa kulipa". Utaratibu huu unafanya kazi kwa ushirikiano kati ya jamii na Serikali; Serikali hutoa fedha 'tele kwa tele' katika ngazi ya Halmashauri na jamii hulipa michango yao pale wanapokuwa na fedha taslimu na kupata huduma kwa mwaka mzima. Kamati za afya za jamii huchangisha na kusimamia fedha zinazopatikana. Mfuko wa Afya ya Jamii hauchukui nafasi ya Serikali kulipia gharama za afya.

Mfuko wa Afya ya Jamii unatarajiwa kutoa huduma bora na rahisi kwa mbinu ambazo ni endelevu kifedha. Hurahisisha usimamizi wa huduma za afya katika jamii kupitia ugatuaji. Huhakikisha uwepo wa dawa na vifaa tiba vya kutosha katika vituo vya kutolea huduma za afya. Mfuko huu huboresha huduma za afya kwa kuhahikisha uwepo wa watoa huduma za afya wenye stadi na motisha na zaidi huboresha ushiriki wa jamii.

**2.0 TATIZO**

Tanzania, kama nchi nyingine za Afrika chini ya Jangwa la Sahara, hukabiliwa na changamoto mbili za bajeti finyu ya afya na hitaji la kuboresha huduma za afya, hasa kwa maskini na wale waishio maeneo ya vijijini au katika sekta isiyo rasmi. Licha ya maboresho mapana katika ulipiaji wa huduma za afya, Tanzania ilianzisha ada za huduma tangu mwaka 1993. Hii ilitokana na kushindwa kwa Serikali kutoa huduma za afya bure kwa wananchi wote kwa kutumia fedha za kodi kutokana na kuongezeka kwa gharama tiba, kujitokeza kwa magonjwa makuu kama UKIMWI, na ukuaji duni wa uchumi. Baada ya muda mbinu nyingine za kulipia huduma za afya ziliongezwa zikijumuisha uanzishaji wa mifumo ya kulipia bima kabla kama Mfuko wa Bima ya Afya wa Taifa, Mfuko wa Afya ya Jamii na mijini (TIKA) na skimu ndogondogo za bima za afya kama Umasida na Vibindo. Siku za karibuni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umeanzisha fao la afya lijulikanalo kama fao la bima-jamii ya afya.

Kabla ya mwaka 2007 H/W ya Musoma ilitoa huduma duni za afya kutokana na bajeti ndogo na ucheleweshaji wa fedha toka Serikali Kuu. Kadhalika, kulikuwa na changamoto katika mapato ya ndani, uelewa mdogo wa jamii katika kuchangia huduma za afya, vipato duni vya kaya na uratibu mbovu katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kulikuwa na upungufu wa watumishi wa afya, mfumo mbovu wa utunzaji wa taarifa na mfumo dhaifu wa rufaa ambavyo vilifanya huduma za afya kuwa mbaya zaidi. Utoaji wa huduma za afya katika ngazi za chini ulifanyika kwa kutumia fedha taslimu zilizolipwa na wagonjwa ambazo zilikuwa na matatizo mengi katika ukusanyaji na mara nyingi kulikuwa na tabia za rushwa ikiwa ni pamoja na matumizi ya

vitabu bandia vya risiti. Zaidi ya hayo, kulikuwa na upungufu mkubwa wa madawa, vifaa tiba na motisha kwa watumishi na kusababisha ongezeko la maradhi na vifo.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la Halmshauri katika jitihada hii lilikuwa kuboresha utoaji wa huduma za afya; Halmashauri ililenga:

(i) Kuongeza uelewa wa jamii ili kuchangia utoaji wa huduma za afya.
(ii) Kuboresha uandikishaji na uratibu wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).
(iii) Kuongeza uwezo wa Halmashauri na vituo vya kutolea huduma za afya kununua madawa na vifaa tiba, kutoa motisha kwa watumishi na kuboresha uendeshaji.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Ili kutekeleza mchakato wa Mfuko wa Afya ya Jamii, H/W ya Musoma iliandaa sheria ndogo, ikafanyiwa maamuzi na kuanza kutumika mwaka 2002, na ilianzisha Bodi ya Halmashauri ya Huduma za Afya chini ya kifungu cha 86A cha sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 ya 1982.

Kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Halmashauri ilitekeleza mradi wa *Tibu Homa* tangu Machi 2011 hadi Septemba 2015. Mradi ulisaidia Halmashauri za Ukanda wa Ziwa Viktoria kupunguza maradhi na vifo kwa watoto chini ya miaka mitano kwa kuboresha upimaji na tiba ya homa kali. H/W ya Musoma ilitumia fursa hii ya Mradi wa *Tibu Homa* kuongeza upatikanaji wa huduma ya afya ya mtoto, na kuunganika zaidi na jamii katika kuimarisha tabia ziletazo afya njema. Utekelezaji ulihusu hatua zifuatazo;

(i) Kuunda Kikosi Kazi (wajumbe 4) katika Timu ya Halmashauri ya Menejimenti ya Afya (CHMT) kwa ajili ya uhamasishaji wa CHF. Kikosi kazi hiki kiliwajibika katika kusimamia mikutano ya kujenga uelewa katika jamii.
(ii) Kujenga uelewa kuhusu Mfuko wa CHF; mradi wa *Tibu Homa* uliwezesha kujenga uelewa kwa viongozi wa Vijiji na Kata kwa kuendesha mikutano ya uhamasishaji kupitia mikutano ya Vijiji, mikutano ya Halmashauri za Vijiji na mikutano ya Vitongoji. Kikosi kazi hiki kikishikiana na watumishi wa vituo vya kutolea huduma za afya na wawezeshaji wa jamii walikuwa na jukumu la mikutano ya uhamasishaji na ziara za nyumba kwa nyumba. Halmashauri ilielekeza kuwa uandikishaji wa CHF uwe ni ajenda ya kudumu katika vikao vyote vya kisheria kama vikao vya Baraza, Menejimenti ya Halmashauri, Kamati za Maendeleo za Kata, mikutano ya Vijiji, na mikutano ya Vitongoji. Wakati wa mikutano ya uhamasishaji wa jamii, wajumbe wa CHMT walitoa maelezo kuhusu uandikishaji na uendeshaji wa Mfuko.
(iii) Kuanzisha na kuimarisha kamati za uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya; kupitia mikutano ya vijiji, wawakilishi wa jamii walichaguliwa kuunda kamati kwa kila zahanati na kituo cha afya. Majukumu ya kamati hizi ni kuhamasisha jamii, usimamizi wa fedha, manunuzi ya dawa na vifaa tiba, na usimamiaji wa shughuli za kila siku za vituo vya kutolea huduma za afya.
(iv) Kujenga uwezo wa wajumbe wa kamati za vituo vya kutolea huduma za afya; mafunzo yalifanyika kwa wenyeviti na makatibu wa kamati kuhusu wajibu wao. Kuboresha utendaji wa kamati hizi, Halmashauri ilielekeza kamati kuwa zinakutana walau mara mbili kwa wiki na kwa robo mwaka kufuatilia uandikishaji wa wanachama wa CHF na utendaji wake. Halmashauri ilielekeza CHMT na kamati za vituo vya kutolea huduma za afya kukutana mara kwa mara kufanya maamuzi kuhusu utendaji wa CHF.
(v) Uandikishaji wa wanachama kwenye rejesta ya CHF; kila kaya ilihamasishwa kujiandikisha na CHF (watu 6/Kaya) kwa kulipa TZS 10,000 tu kwa mwaka. Risiti zilizotolewa hutumika kama kadi ya wanachama kupata huduma za afya.







***Rejesta ya CHF na Risiti***

(vi) Kuunda mfumo wa usimamizi na uendeshaji (ufuatiliaji wa wiki na mwezi); kamati zinafanya ufuatiliaji wa shughuli za mfuko mara mbili kwa wiki.

(vii) Kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na huduma nyingine; eneo hili linahusu manunuzi kwa kutumia fedha za CHF. Kamati za vituo vya kutolea huduma za afya inawajibika kuhakikisha michango inapelekwa kwenye akaunti mama ya Halmashauri na maombi ya matumizi yanafanywa mapema. Halmashauri huhamisha fedha kwenda akaunti za vituo vya kutolea huduma za afya, baada ya mchakato huu dawa na vifaa tiba hununuliwa mapema iwezekanavyo.

(viii) Kuboresha huduma kwa mteja; katika kila vituo vya kutolea huduma za afya, dawati limetengwa kwa ajili ya wanachama wa CHF ili kuwapatia huduma za haraka. Baadaye, lilianzishwa dawati la wazee (miaka 60+) kuwezesha huduma za haraka kwa wazee. Zaidi ya hayo malipo ya fedha taslimu yaliongezwa kutoka TZS 1,000 hadi TZS 2,000. Mipango yote hii iliandaliwa ili kuwavutia wanajamii wengi kujiunga na mfuko wa CHF na kuwakatisha tamaa kutumia fedha taslimu.

(ix) Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mfuko wa CHF; vituo vya kutolea huduma za afya vinalazimika kutumia risiti rasmi na kuhifadhi kumbukumbu, kuweka makusanyo yote kwenye akaunti hodhi ya Halmashauri, kuomba fedha kwa ajili ya matumizi rasmi ya fedha za CHF, kuwa na fomu za CHF zilizojazwa vema, kuziwasilisha fomu hizo kwa mratibu wa mfuko wa CHF kwa wakati na kufanya manununzi ya haraka ya madawa na vifaa tiba.

**5.0 RASILIMALI**

Halmashauri ilitumia rasilimali zifuatazo;

(i) Uhamasishaji wa jamii na shughuli zake; TZS 5.6m kwa usaidizi wa mradi wa *Tibu Homa*.

(ii) Fedha kadhaa kutoka mfuko wa bima ya afya wa (NHIF) kusaidia mafuta ya gari, vitini na gharama za kujikimu kipindi cha uhamasishaji.

(iii) Rasilimali watu; madiwani, wajumbe wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri, wajumbe 4 wa kikosi kazi, watumishi wa afya, viongozi wa jamii, na wajumbe wa kamati za vituo vya kutolea huduma za afya.

**6.0 MATOKEO**

Halmashauri imefanikiwa kupata matokeo yaliyoandikwa kwa muhtasari hapa chini;

(i) Uandikishaji wa wanachama wa CHF umeongezeka toka 28% (wanachama 9,554) mwaka 2014 hadi 44% (wanachama 15,013) mwaka 2015.

(ii) Kufaulu kupata fedha za tele kwa tele; kutokana na kujiandikisha kwa wingi na michango stahiki ya jamii katika mfuko wa CHF, Halmashauri imeshuhudia kuongezeka kwa makusanyo na kuongezeka kwa fedha za tele kwa tele kutoka Serikali Kuu. Mwaka 2015 Halmashauri iliomba TZS 22.9m kutoka Serikali Kuu na kupewa TZS 18.9m. Mwaka 2016 Halmashauri iliomba TZS 65.7m za tele kwa tele.

(iii) Uhakika na ugatuaji wa Manunuzi ya dawa na vifaa tiba.

(iv) Fedha za mfuko wa CHF zinatumika kukarabati na kujenga majengo ya vituo vya kutolea huduma za afya kama wadi ya wazazi, jengo la afya ya mama na mtoto, kituo cha kuteketeza taka, vyoo, ofisi na nyumba za watumishi.



*Zahanti ya Tegeruka*



*Wadi ya wazazi, kituo cha afya Muranga*





*Nyumba ya watumishi na ujenzi wa zahanati ya Mugango*

(v) Uwepo wa dawa muhimu na vifaa tiba umeongezeka toka 47% mwaka 2014 hadi 80% mwaka 2015.

(vi) Wanawake wanaojifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya wameongezeka kutoka 33% mwaka 2014 hadi 74% mwaka 2015.

(vii) Vifo vya akina mama na watoto chini ya miaka mitano na rufaa kwenda Hospitali ya Mkoa vimepungua sana.

(viii) Kamati za afya za vituo vya kutolea huduma za afya zina uwezo wa kulipa posho za kuanza kazi za kati ya TZS100,000 na 200,000 kwa watumishi wapya.

(ix) Kumekuwepo na watumishi wenye motisha wakiwa na tabia za kujitoa kwa moyo kufanya kazi kutokana na kuimarika kwa mazingira na vifaa vya kazi.



*Mkunga, zahanati ya Mugango*



*Daktari, kituo cha Afya Murangi*

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kutekeleza jitihada hii, Halmashauri ilipata changamoto kama upungufu wa mara kwa mara wa madawa na vifaa tiba katika bohari ya taifa ya madawa, uchache wa vituo vya kutolea huduma za afya, mfumo mbovu wa rufaa na ucheleweshaji wa fedha za tele kwa tele. Kupambana na changamoto hizi na kuhakikisha jitihada ya mfumo wa CHF in endelevu, Halmashauri imejiwekea mikakati ifuatayo:

(i) Uhamasishaji wa Jamii na undikishaji wa wanachama katika mfuko wa CHF usiokoma.
(ii) Kuendelea kutoa dawa na vifaa tiba kwa kutumia vyanzo vingine kama HBF, NHIF na wadau wengine.
(iii) Kuendelea kuboresha majengo na uwepo wa huduma za maji, umeme, samani, ukarabati mdogo na ujenzi wa majengo mapya.
(iv) Kuboresha mfumo wa rufaa (kutoa rufaa kutoka zahanati kwenda kituo cha afya cha Murangi na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa).
(v) Kupanua wigo kijiografia wa undikishaji wa wanachama wa CHF na kuvifikia vijiji vyote.
(vi) Kuongeza fungu la mapato ya ndani linalotengwa kwa ajili ya huduma za afya.
(vii) Kuwepo na taratibu za ndani za kuazimana madawa na vifaa tiba panapotokea upungufu na dharura kati ya vituo vya kutolea huduma za afya.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

(i) Jitihada za Halmashauri kuratibu wadau mbalimbali (NHIF, TIBU HOMA, MCSP) ili kufanikisha uhamasishaji na matumizi ya mfuko wa CHF.
(ii) Uhamasishaji wa Kaya kwa Kaya uliofanywa na kikosi kazi cha Halmashauri, watumishi na Kamati za vituo vya kutolea huduma za afya kujitoa kwa moyo na umoja.
(iii) Kuzuia matumizi ya fedha taslimu kwa kuongeza viwango vya kulipia ili kuhamasisha kujiunga na mfuko wa CHF.
(iv) Kufanya majaribio ya matumizi ya mfuko wa CHF katika jamii chache kabla ya kueneza mfumo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.
(v) Uwazi; taarifa za mara kwa mara katika mikutano ya Vijiji na Vitongoji kuhusu makusanyo na matumizi ya fedha za mfuko wa CHF.
(vi) Jitihada za Mkuu wa Wilaya kwa kuchukua Kampeni ya CHF kama kipaumbele chake; viongozi wote wa Wilaya na timu yote ya wanasiasa ilitoa ushirikiano katika kampeni hii.
(vii) Wanachama wa CHF kupata huduma za afya katika kituo chochote cha kutolea huduma za afya ndani ya H/W ya Musoma.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

**USIMAMIZI SHIRIKISHI WA SKIMU YA MAJI**



*Uzoefu wa Kata ya Uyovu*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe ni moja kati ya Halmashauri 6 za Mkoa wa Geita. Halimashauri hii inapatikana katika mwinuko wa 1,100m - 1,300m juu ya usawa wa bahari na kati ya Latitudo $2^{o}8'$ na $3^{o}28'$ Kusini na Longitudo $32^{o}$ 45' na $37^{o}$ Mashariki. Halmashauri inapakana na Halmashauri za Geita na Chato kwa upande wa Kaskazini, Biharamulo (Mkoa wa Kagera) kwa upande wa Kaskazini Magharibi, Mbogwe kwa upande wa Mashariki, Urambo (Mkoa wa Tabora) kwa upande wa Kusini na Kibondo (Mkoa wa Kigoma) upande wa Magharibi. Halmashauri ina eneo la 8,482km$^2$. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 3 (Ushirombo, Siloka na Bukombe), Kata 17, Vijiji 52, Mitaa 97 na Vitongoji 372.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ilikuwa na idadi ya watu 224,542 kati yao 110,857 (49.3%) ni wanaume na 113,685 (50.7%) ni wanawake. Wastani wa idadi ya watu kwa eneo ni 27 kwa kilomita moja ya mraba, ongezeko la watu kwa mwaka ni 5.9%. Ongezeko hili linatokana na watu kuzaana (55%) na wahamiaji (45%).

Kilimo na mifugo ndio sekta inayoongoza kiuchumi katika Halmashauri. Mazao makuu ya chakula ni mahindi, muhogo, maharage na mazao ya biashara ni pamba, karanga na alizeti. Wakulima wanafuga ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, punda, kuku na mbwa. Shughuli nyingine za kiuchumi ni pamoja na biashara na uchimbaji wa madini ambazo zimekuwa zikiwavutia watu kutoka maeneo mbalimbali. Shughuli za biashara zinaweza kugawanywa katika biashara ndogondogo ambazo zinafanywa na sekta isiyo rasmi na biashara za makampuni kama TANESCO, Nsagali Gold Mine, Benki ya Posta na Kahama Cotton Mill.

Rasilimali asili katika Halmashauri ni misitu na wanyamapori. Misitu ni muhimu katika kutunza tabia nchi, kulinda vyanzo vya maji, kutunza rutuba ya udongo na kuzuia mmommonyoko wa udongo. Maji ni moja ya rasilimali kubwa inayotegemewa katika maisha ya mwanadamu. Hata hivyo, ikiwa maji hayana ubora yanaweza kuwa chanzo kikubwa cha magonjwa kwa binadamu. Jamii katika Halmashauri ya Bukombe zinategemea maji kutoka kwenye mito mabayo kwa kiasi kikubwa hayana ubora kwa matumizi ya binadamu. Halmashauri ilitambua hali hii na kuamua kusaidiana na jamii katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama.

## 2.0 TATIZO

Mwaka 2016, Kata ya Uyovu na vijiji vinavyoizunguka vilikabiliwa na tatizo kubwa la maji safi na salama. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Kata ilikuwa na idadi ya watu 29,909 ambao walitegemea maji kutoka chanzo kilichokuwepo katika umbali wa kati ya 3km – 4km kutoka eneo la makazi. Wananchi wengine walilazimika kutumia maji kutoka kwenye visima vya asili ambavyo maji yake hayakuwa safi na salama kwa matumizi ya binadamu. Wanawake ndio kundi lililoathirika kwa kiasi kikubwa katika kutafuta maji. Mara nyingi walitumia muda mwingi kati ya saa 3 hadi 5 kutafuta maji na iliwalazimu kuamka alfajiri kati ya saa 10:00 na 11:00 kila siku. Kutokana na hali hii, uchumi uliathirika kwa kutumia muda mchache katika shughuli za uzalishaji na muda mwingi kutafuta maji. Baadhi ya watoto wa kike walihujumiwa kingono kwa kubakwa, kuambukizwa magonjwa na kupata ujauzito wakati wa kutafuta maji. Kadhalika, watoto walilazimiaka kuwasiaidia wazazi wao katika kuchota maji kabla ya kwenda shule, jambo hili lilioongeza utoro shuleni.

Gharama za maji safi zilikuwa kubwa ambapo lita 20 ziliuzwa kati ya TZS 500 na TZS 1000. Takwimu za kituo cha afya cha Uyovu zilibainisha kwamba 40% ya wagonjwa wanaotembelea kituo hicho ni wagonjwa ambao wameathiriwa na maji machafu wakisumbuliwa na homa ya matumbo, kipindupindu na kuhara.

## 3.0 LENGO

Lengo kuu la jitihada hii ni kuwezesha jamii kupata maji safi na salama. Malengo mahususi ya Halmashauri ni pamoja na kuanzisha chanzo cha maji na kuunda jumuiya ya watumia maji (COWSO) ambayo itasimamia utoaji wa maji na kufanya tathmini ya utendaji kazi wa mradi, kuunganisha maji kwa watumiaji wapya, kufanya marekebisho na matengenezo ya mabomba na usimamizi wa shughuli za kila siku za mradi.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Halmashauri kwa kushirikiana na jamii waliweka mikakati mbalimbali na mbinu za utekelezaji kama ifuatavyo; Kufanya upembuzi yakinifu ili kutambua eneo lenye maji ya kutosha; mwaka 2009, Halmashauri kwa kushirikana na wataalamu ilifanya upembuzi yakinifu kubaini eneo la kuchimba visima virefu. Baada ya upembuzi huu eneo la Lwoboka lilibainika kuwa na maji ya kutosha. Mwaka 2011, Halmashauri ilichimba visima vya majaribio. Kwa miezi 3 kazi zote zilizohusu uchimbaji na usambazaji wa maji zilikuwa chini ya Afisa Mtendaji wa Kata. Hata hivyo mradi haukufanikiwa.

Kuunda kamati ya usimamizi wa maji; ili kuhakikisha matumizi sahihi ya maji, Halmashauri iliamua kuishirikisha jamii kuanzisha kamati ya usimamizi wa maji. Kamati ilijumuisha wajumbe 12 kutoka katika Vitongoji 4 ambapo kila kitongoji kilitoa wawakilishi wa 3. Majukumbu ya kamati yalikuwa ni pamoja na kusimamia shughuli zote za mradi kama kutunza na kukarabati miundombinu ya maji, kugawanya maji na kuendelea kujenga vituo vya kutolea maji. Kamati ilitakiwa kufungua akaunti benki kutunza fedha zitokanazo na mauzo ya maji na kuendesha vikao vya mwaka kujadili namna ya kuimarisha huduma.

Kuundwa kwa Umoja wa Watumia Maji (COWSO); ili kuendeleza ufanisi wa mradi wa maji, jamii ilipaswa kuunda umoja wa watumia maji ili kuumiliki mradi na kuufanya kuwa endelevu. COWSO ilianzishwa kuchukua majukumu ya usimamizi wa mradi baada ya kukabidhiwa na mkandarasi. Kukabidhiwa mradi kwa jamii kulilenga kuimarisha ushiriki wa jamii na umiliki wa mradi.

Ujenzi wa matangi ya maji na upanuzi wa vituo vya kutolea maji; mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri ilitenga TZS486,463,960 kwa ajili ya upanuzi wa mradi kufikia maeneo yote ya Kata na kusababisha mradi kuitwa " Mradi wa Maji wa Kata ya Uyovu". Katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji, Halmashauri ilijenga matangi mawili , moja lenye uwezo wa kuhifadhi lita 90,000 za maji na jingine lita 45,00 za maji. Baada ya mradi kukamilika, Halmashauri ilipitia tena sera ya maji na kuongeza mikakati mipya ya kuhakikisha mradi unakuwa endelevu.

Utoaji wa elimu kuhusu matumizi sahihi ya maji na utunzaji wa maji kwa wanachama wa jumuiya ya watumia maji na wananchi kwa ujumla; elimu hii ilitolewa na Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kutoka Halmashauri, Watendaji wa Kata na Vijiji kwa kushirikiana na Mh. Diwani wa Kata ya Uyovu. Jumuiya ya watumia maji ilihusishwa katika uelimishaji wa jamii kupitia matangazo, mikutano na mafunzo kwa viongozi. Halmashauri na jumuiya ya watumia maji ilifanya uhamasishaji wa jamii kuunda viundi vya upandaji miti na kuhamasisha kupanda miti rafiki katika maeneo karibu na chanzo cha maji kwa lengo la kuhifadhi mazingira na chanzo cha maji. Uhamasishaji ulifanywa na Afisa Mazingira wa Halmashauri, Mhandisi wa Maji, Afisa Maendeleo ya Jamii, Mtendaji wa Kata na Diwani. Mikutano yote ya kisheria ilitumika kama fursa ya kuhamasisha jamii.

Ukarabati wa mradi wa maji wa Musasa katika Kata ya Uyovu; Mwaka 2007 kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia, Halmashauri ilikarabati mradi wa maji wa Musasa Uyovu ambapo tangi la ujazo wa lita 10,000 na vituo vya kusambazia maji 8 vilijengwa ; vituo 4 kati ya hivyo vilitumika kutoa huduma katika kijiji cha Musasa na vituo vingine 4 kwa kijiji cha Uyovu.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa shughuli za mradi huu, ulihusisha rasilimali za Halmashauri na Jamii; Rasilimali Fedha, Rasilimali watu na vitendea kazi vilitumika katika kutekeleza shughuli za mradi huu. Jumla ya TZS51,886,000 zilitumika kwa shughuli za ujenzi. Uendeshaji wa mradi ulitegemea makusanyo ya jumuiya ya watumia maji ambapo kila robo mwaka zilikusanywa TZS 25,000,000. Fedha zinazokusanywa zinatumika kulipa watumishi 27. Jumuiya ya watumia maji ina kamati yenye wajumbe 12 na watumishi 27 ambao wanasimamia mradi

pamoja Jumuiya na kamati ndogo ndogo zinazojumuisha wataalamu wa mipango na fedha. Jamii inashiriki kutoa taarifa pale ambapo kuna tatizo kwenye mradi na kushauri kuhusu utekelezaji wa shughuli za mradi.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa Mradi wa maji wa Uyovu uemeleta matokeo yafuatayo;

Upatikanaji wa maji safi na salama katika kata ya Uyovu; Jamii inapata maji safi na salama kwa urahisi ndani ya wigo wa 200m. Magonjwa yatokanayo na maji machafu ambayo yaliathiri watu yamepungua. Wanawake wanaweza kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi kutokana na kupata muda wa kutosha na mahudhurio ya wanafunzi shuleni yameongezeka.

Uwepo wa jumuiya ya watumia maji na kamati za uendeshaji; vyombo hivi vimeweza kusimamia mradi na kufanya uwe endelevu. Mbali na kukusanya fedha za watumia maji, jumuiya ina jukumu la kushawishi wateja wengine kujiunga na huduma ya maji. Aidha, jumuiya inajihusisha na ununuzi wa vifaa vya bomba na kujenga vituo vipya vya kusambaza maji. Jumuiya imeimarika kiasi cha kujiendesha na kugharamia shughuli zote za mradi. Jumuiya imetumia TZS 7,460,000 kupanua mradi na kununua pampu ya maji iliyogharimu TZS 8,000,000.

Ajira zimepatiana kutokana na kuanzishwa kwa mradi huu. Jumuiya imeajiri watumishi wengi wa kuendesha shughuli za mradi kama mafundi kwa ajili ya matengenezo ya bomba na wauzaji wa maji. Ajira zinaendelea kuongezeka kadri vituo vya usambazaji vinavyoongezeka. Watumishi wanatakiwa kukusanya mapato, kulinda miundombinu na kuendesha shughuli za kuuuza maji. Mahusiano baina ya kamati tendaji, jumuiya na Halmashauri yameimarika kwa kiasi kikubwa.



***Vituo vya Usambazaji wa Maji***

Vituo vya afya na shule vimefaidika na huduma ya maji; jumuiya imefanikiwa kusambaza maji pembezeoni mwa barabara ya Uyovu hadi Bwanga kwa ajili kufikia na kutoa huduma ya maji kwa kituo cha afya na shule ya sekondari ya Runzewe. Kaya binafsi 24, taasisi za umma 2 na taasisi binafsi 1 zimefaidika na huduma hii. Jumuiya imepokea maombi mapya 20 ya wananchi wanaohitaji kuunganishiwa maji.



*Mantangi ya maji (kushoto lita 45,000 na kulia lita 90,000)*

Jumuiya ya watumia maji ya Uyovu imekuwa kituo cha kijifunzia ambapo wajumbe wa jumuiya za watumia maji kutoka Meatu, Ikunzi, Nampalahala, Kabagoe na Musasa walitembelea mradi wa maji wa Uyovu kwa lengo la kujifunza. Vilevile mradi umeweza kuimarisha usambazaji wa maji kutoka tangi la lita 10,000 na kujenga matangi mawili ambayo yanahifadhi na kusambaza lita 135,000 hivyo kupunguza upungufu wa maji kwa kiasi kikubwa. Idadi ya watu wanaotumia maji safi na salama imeongezeka kutoka 2,201 mwaka 2014 hadi 5,012 mwaka 2017. Vituo vya usambazaji wa maji 27 vimejengwa ambapo kila mtaa una vituo kati ya 1 - 3.



*Tangi la zamani (lita 10,000)*



*Matangi mapya (lita 45,000 na lita 90,000)*

**7. 0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kuhakikisha mradi unakuwa endelevu, Halmashauri imejiwekea mikakati mbalimbali. Usimamizi endelevu wa mradi unafanyika ambapo kila mtaa unasimamiwa na mjumbe mmoja wa jumuiya ambaye hutoa taarifa za maendeleo ya mradi, kubaini matatizo na kutoa taarifa mapema. Jumuiya ina katiba inayoelekeza uitishaji na uendeshaji wa vikao, usimamizi wa fedha na majukumu mengine.



*Wajumbe wa Jumuiya wakiwa kwenye Mkutano*

Jumuiya ya watumia maji imepunguza gharama za uendeshaji kutoka TZS 1,200,000 kwa mwezi zilizo tumika kununua diseli ya kuendesha pampu hadi TZS 300,000 kwa mwezi baada ya kuunganisha pampu na umeme wa gridi ya taifa. Kadhalika, jumuiya inaendelea kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya miundombinu ya mradi ili kuhakikisha uharibifu mkubwa hautokei. Picha zifuatayo zinaonesha usafishaji wa kisima.





*Mitambo ikisafisha visima katika mradi wa maji wa Uyovu*

Jumuiya ya Uyovu ipo katika mpango wa kuongeza wigo wa usambazaji wa maji katika vijiji vya jirani vya Kanembwa, Azimio na Buganzu ili kupeleka huduma wananchi wa vijiji hivyo na kukusanya mapato zaidi. Aidha, jumuiya ina mpango wa kufunga mita za maji za malipo kabla ili kudhibiti mapato na upotevu wa maji usio wa lazima.



*Kituo cha kusambaza maji*

Jumuiya ina mipango ya muda mrefu ya kuanzisha chanzo kingine cha maji ili kuongeza upatikanaji wa maji na uwezo wa kusambaza maji kufikia mahitaji. Vilevile, jumuiya imelenga kuendelea kupanda miti rafiki katika vyanzo vyote vya maji kukabiliana na uharibifu.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kufanikiwa kwa jitihada hii kumetokana na sababu mbalimbali. Sababu hizi ni pamoja na uwepo wa jumuiya imara ya watumia maji, uhusiano bora kati ya Serikali Kuu, Halmashauri na jamii, utayari wa wataalamu katika kubuni na kuanzisha mradi na mafunzo yaliyotolewa kwa jumuiya ya watumia maji ya Uyovu kuhusu usimamizi na uendeshaji wa mradi wa maji.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

## USHIRIKI WA JAMII KATIKA KUFUNGUA NA KUBORESHA BARABARA








*Uzoefu wa Mamlaka za Miji Midogo ya Ngara, Rulenge, Kabanga na Benaco*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Kagera. Halmashauri hii inapakana na Jamhuri ya Rwanda na Burundi. Barabara za lami katika Halmashauri ni zile zinazounganisha Ngara hadi Kigali (Rwanda), Bujumbura (Burundi) na Isaka (Wilaya ya Kahama). H/W ya Ngara ina eneo la 3,744 Km$^2$; ambapo kuna Tarafa 4, Kata 22, Vijiji 75 na Vitongoji 394.




**Ramani ya H/W ya Ngara**

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina Kaya 63,293 na jumla ya watu 320,056; kati ya hawa 30% ni wakimbizi. Wanawake raia wa Tanzania walikuwa 52% na ikiunganishwa wakimbizi, wanawake walikuwa 51% ya idadi ya watu. Ongezeko la watu kati ya sense mbili ( 1988-2002) lilikuwa 2.7% kwa raia na 5.3% baada ya ujio wa wakimbizi. Idadi ya wa wakazi katika 1km$^2$ ni 89 inayotarajiwa kupungua kufikia 62 baada ya kuondoka wakimbizi wote. Wastani wa watu katika kaya ni 4.6.

Halmashauri inapatikana katika mwinuko wa 1,200m - 1,850m juu ya usawa wa bahari. Sura ya Halmashauri ina milima, mabonde, ardhi tambarare na mito. Hali ya hewa inajumuisha mvua za vipindi viwili. Mvua fupi hunyesha miezi ya Septemba na Oktoba na mvua za masika miezi ya Machi hadi Mei. Wastani wa mvua kwa mwaka ni kati ya 800mm Kusini na 1,400mm Kaskazini. Wastani wa joto ni 17$^0$C Kusini na 25$^0$C Kaskazini. Uoto wa asili ni misitu, nyasi na vichaka.

## 2.0 TATIZO

H/W ya Ngara ina 849km za mtandao wa barabara. Barabara hizi zimegawanywa katika makundi 4; barabara kuu (86.8km), barabara za Mkoa (278.9km), barabara za Halmashauri (483.3km) na barabara za Vitongoji (306km). Barabara za mkoa 90% ni za kiwango cha changarawe na 10% ni za vumbi. Barabara za kiwango cha changarawe zinapitika kwa urahisi misimu yote. Barabara za vumbi ni za msimu na hupitika kwa shida wakati

wa mvua. Barabara za Halmashauri zilizotengenezwa kwa kiwango cha lami ni 0.6% tu ambazo zinaunganisha Mamlaka za Miji midogo ya Ngara na Rulenge. Halmashauri ina barabara zilizotengenezwa kwa kiwango cha changarawe 39.2% na barabara za vumbi 60.2%.

Kabla ya mwaka 2008 ujenzi wa barabara ulifanyika baada ya kutoa fidia kwa wamiliki wa maeneo ambayo yalipitiwa na barabara. Hata hivyo, fidia haikuhusu ardhi pekee bali mimea na mazao yaliyoathirika. Uthamini wa maeneo hayo ya barabara ulifanywa na wataalamu wakishirikiana na viongozi wa vitongoji. Kufikia mwaka 2010 ziliibuka kesi na malalamiko mbalimbali kuhusu viwango vya chini vya fidia vilivyo tolewa na Halmashauri. Katika kipindi hiki Halmashauri haikuwa na bajeti ya kutosha kufidia maeneo yote ya barabara hivyo ilikuwa vigumu kushawishi wananchi kuachia maeneo yao bila fidia ili kupitisha barabara.

Wakati wa ujenzi wa barabara za vitongoji kuzunguka Mamlaka za Miji midogo ya Ngara, Rulenge na Benaco, Halmashauri ilikumbana na changamoto ya ufinyu wa bajeti kwajili ya kufidia maeneo ya barabara pamoja na mimea iliyoathirika. Maeneo mengi hayakuwa yamepangwa na yalizungukwa na makazi ya asili na mimea ya kudumu. Upangaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo na ufunguaji barabara ulilazimu kubainisha maeneo ya barabara, ambapo baadhi ya nyumba zilipaswa kubomolewa na mimea kuondolewa. Ubomoaji wa nyumba pamoja na uondoaji mimea ulihitaji fidia. Kutokana na ufinyu wa bajeti mpango huu wa uboreshaji na upangaji wa mji ulichelewa na kwa baadhi ya maeneo mpango haukutekelezwa.

Pamoja na Halmashauri kushindwa kufidia maeneo kwajili ya ujenzi wa barabara, hitaji la wananchi juu ya kupatikana kwa barabara lilizidi kuongezeka. Halmashauri ilihitaji kiasi cha TZS 500,000,000 kwa ajili ya kufidia familia 150 ambazo zilipaswa kuachia maeneo yao ili kufungua barabara pamoja na ujenzi wa mifereji. Jamii ilihitaji barabara kurahisisha usafirishaji na kufikia huduma mbalimbali. Kwa ujumla ukosefu wa barabara ulisababisha jamii kukumbana na matatizo yafuatayo;

Gharama za ujenzi wa nyumba za makazi ziliongezeka kutokana na usafirishaji duni wa vifaa vya ujenzi. Hali hii ilithibitishwa na mmoja wa wananchi wa eneo hilo Hamduni Musa (2016) ambaye alisema *"Zamani tukijenga nyumba zetu, haikuwa rahisi kufikisha vifaa katika eneo la ujenzi na badala yake ilibidi kuajiri watu/vibarua kuvisogeza kwenye eneo la ujenzi".*

Kulikuwa na changamoto kuanzisha huduma za kijamii kama kupitisha miundombinu ya umeme, maji, pamoja na ujenzi wa mifumo ya maji taka na mifereji ya kupitisha maji kipindi cha mvua kutokana na ukosefu wa maeneo. Aidha, haikuwa rahisi kuzifikia huduma za muhimu kama hospitali, shule na ofisi za Serikali. Wananchi walilazimika kutumia muda mrefu kufikia huduma za kutolea huduma kipindi cha dharura kama kifo, ajali au ugonjwa.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la H/W ya Ngara lilikuwa kuimarisha utoaji wa huduma kwa kujenga na kukarabati barabara. Malengo mahususi yalikuwa kujenga barabara za mitaa zinazopitika katika kipindi chote cha mwaka katika Mamlzka za Miji midogo ya Ngara, Rulenge, Kabanga na Rwakaremela/Benaco, kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za jamii kama maji, umeme, makazi, usafi wa mazingira na usafirishaji, kujenga uelewa wa jamii juu ya umuhimu wa mipango miji na ushiriki wa jamii katika ujenzi wa barabara ikiwa ni pamoja na kuchangia gharama za ujenzi na kuwa tayari kuachia maeneo yao kwa ajili ya barabara bila kudai fidia.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inasisitiza umuhimu wa ujenzi na kupanua mtandao wa barabara. Katika kutekeleza dira hii, Sera ya Taifa ya Usafirishaji imeweka msukumo wa kuunganisha barabara za vijijini na miji kuwezesha jamii za vijijini kufikia soko la bidhaa zao katika maeneo ya miji ambapo zana na pembejeo za kilimo hupatikana. Mpango wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA II) umeweka malengo matatu; Kukuza kipato na kupunguza umasikini, kuboresha hali ya maisha na utawala bora.



Inatambulika kwamba miundombinu ya barabara inachochea ukuaji wa uchumi na masuala ya kijamii katika nchi kwa kuwa barabara hurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka shambani hadi sokoni hivyo kusaidia kukuza uchumi. Dhana hii inafanya miundombinu ya barabara kuwa mojawapo ya nguzo muhimu ya kufikia malengo ya MKUKUTA, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa 2025. Ili kufikia malengo, H/W ya Ngara ilishirikana na jamii kutekeleza mikakati ifuatayo;

Mikutano ya uhamasishaji na kujengea uelewa; H/W ya Ngara ilitisha mikutano ya wadau kwa lengo la kuhamasisha ushiriki katika ujenzi wa barabara. Mikutano hii ilifanyika katika vitongoji 44 ikiendeshwa na Wenyeviti wa Mamlaka za Miji Midogo ya Ngara, Benaco (Kijiji cha Rwakalemela), Kabanga na Rulegeandi. Mikutano hii ilijadili mbinu za kuhamasisha jamii kushiriki katika ujenzi wa barabara, kushawishi wananchi kukubali kuachia maeneo yatakayopitiwa na barabara pasipo kudai fidia. Mikutano ilileta ufanisi ambapo ilikubalika jamii kuhusika katika ujenzi wa barabara za mitaa kwa kujitolea nguvu kazi na kujitolea kuachia maeneo yatakayopitiwa na barabara. Jamii ilihamsika na kukubali kuvunja nyumba zao pamoja na kung'oa mimea katika eneo la barabara ili kuwezesha mitambo ya ujenzi wa barabara kupita na kuanza ujenzi. Jamii ilikubali kutoa ardhi, kubomoa nyumba, kuondoa mimea (migomba, kahawa, miparachichi, viazi na miti ya mbao) bila kudai fidia. Jamii ilipewa jukumu la kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa hatua za ujenzi kudhibiti migogoro ambayo ingetokea wakati ujenzi ukiendelea. Picha zifuatazo zinaonesha mahudhurio ya wananchi katika moja ya mikutano iliyofanyika.



***Mikutano ya Uhamasishaji na Kujenga Uelewa***

Mikataba juu ya ushiriki wa jamii; Timu ya Menejimenti ya Halmashauri iliagiza wadau wote (Idara za ujenzi, ardhi, mipango miji na jamii) kuitisha mikutano katika ngazi za vitongoji na vijiji, kuanda mihutasari na kuithibitisha na kuisambaza kwa jamii kuthibitisha ridhaa yao katika kuchangia ujenzi wa barabara kwa kuachia maeneo yanayoguswa na barabara. Wananchi ambao maeneo yao yalipitiwa na barabara walikubali kutia saini kukubaliana na mihutasari ya mikutano na kushiriki katika kung'oa miti, mazao na kuvunja nyumba zilizopitiwa na barabara. Zoezi hili lilifanyika katika vitongoji vya Mumasama, Nyamiaga, Kibimba, Nakatunga, Kabanga, Rulenge na Benaco. Mihutasari ya mikutano iliwasilishwa kwenye ofisi ya Mkurugenzi kupitia idara za ujenzi, ardhi na maliasili. Picha ifuatayo inaonesha mojawapo ya makubaliano yalifikiwa na jamii na kuwasilishwa ofisi za Halmashauri.

***Muhtasari uliowasilishwa ofisi ya Mkurugenzi***

Mchakato wa zabuni ya ujenzi wa barabara; baada ya kukamilisha mikutano na jamii pamoja na kuwasilisha mihutasari kwenye idara ya ujenzi, Halmashauri ilitenga bajeti kwa kila barabara na kuwasilisha Serikali Kuu ili kupatiwa fedha. Serikali Kuu ilitoa fedha za ujenzi wa barabara. Baada ya kupokea fedha Halmashauri kupitia Kitengo cha Manunuzi iliendelea na mchakato wa kutangaza zabuni ambapo wakandarasi wenye sifa walisainishwa mikataba na kazi ya ujenzi wa barabara za mitaa ilianza.

Ujenzi na usimamizi wa barabara; ujenzi wa barabara ulifanywa na Mkandarasi na usimamizi ulifanyika chini ya idara ya ujenzi yenye jukumu la kusimamia shughuli za ujenzi katika Halmashauri. Idara ilikuwa ilifanya ufuatiliaji, usimamizi na tathimini ya ujenzi mara kwa mara ili kuhakikisha mkandarasi anatekeleza ujenzi kwa kufuata viwango vya ubora vinavyohitajika. Picha zifuatazo zinaonesha mojawapo ya barabara kabla na baada ya ujenzi.



***Barabara ya Msikitini –sokoni kabla ya ujenzi***



***Barabara ya Msikitini- Sokoni baada ya ujenzi***

**5.0 RASILIMALI**

Ujenzi wa barabara kwa kawaida ni gharama kubwa; ili kufanikisha ujenzi wa barabara, Halmashauri ililazimika kushirikisha jamii ili kupunguza gharama. Mchango wa jamii ulikuwa ni pamoja na kutoa maeneo ya ardhi bila kudai fidia na kujitolea nguvu kazi kusafisha eneo la barabara kwa kung'oa visiki. Halmashauri ilitoa rasilimali fedha pamoja na wataalamu wa usimamizi wa ujenzi. Ujenzi wa barabara za mitaa za H/W ya Ngara ulikuwa shirikishi kuwa jamii na Halmashauri zilishirikiana kuchangia gharama za ujenzi. Rasilimali zilizotumika ni fedha, watu na vifaa. Kwa upande wa rasilimali watu, utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa barabara uliratibiwa na maafisa wa Halmashauri (Mkurugenzi wa Halmashauri, wakuu wa idara, maafisa watendaji wa Kata na Mamlaka za miji midogo, Maafisa wa Mitaa, Madiwani na Wenyeviti wa mitaa).

Maafisa hawa walishiriki katika kujenga uelewa na hamasa kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwa na mtandao wa barabara na kushawishi jamii iridhie kuachia maeneo bila kudai fidia.

Halmashauri ilitenga gari maalum kwa shughuli za ujenzi wa barabara na mafuta lita 500 yenye thamani ya TZS 1, 00,000,000. Wakati wa utekelezaji, nguvukazi ilihusisha vijana kutoka kwenye jamii inayotekeleza mradi. Mbali na raslimali watu, Halmashauri ilitenga bajeti kila mwaka wa fedha kama inavyofafanuliwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali 1: Gharama za ujenzi wa barabara**

| S/N | Jina la barabara | Urefu (Km) | Mchango wa jamii (TZS/%) | Mchango wa Serikali (TZS/%) | Jumla (TZS/%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Barabara ya Bilegea hadi Ngara Sekondari (Kitongoji cha Kumzenga Mji mdogo wa Ngara) | 0.25 | 5,400,000.00 (64.3%) | 3,000,000.00 (35.7%) | 8,400,000.00 (100%). |
| 2 | Barabara ya Msikitini hadi Kojifa (Kitongoji cha Mumasama Ngara ) | 0.9 | 13,120,000.00 (51%) | 12,600,000.00 (49%) | 25,720,000 (100%) |
| 3 | Barabara ya Katani hadi Msikitini (mji mdogo wa Rwakalemera Benaco) | 0.45 | 8,880,500.00 (58.5%) | 6,300,000.00(41.5%) | 15,180,000.00 (100%) |
| 4 | Barabara ya Kanisani hadi Makaburini (mji mdogo wa Kabanga) | 1 | 5,490,000.00 (28.2) | 14,000,000.00 (71.8%) | 19,490.000.00 (100%) |

## 6.0 MATOKEO

Ujenzi wa barabara una faida kubwa kijamii na kiuchumi. Barabara hurahisisha usafirishaji na kuongeza ajira kwenye sekta nyingine na kupunguza umasikini. Ujenzi wa barabara unafaida za muda mfupi na muda mrefu; matarajio ya muda mfupi wakati wa kuandaa mpango, utekelezaji wa ujenzi husaidia kuongeza ajira za muda mfupi ambazo ni kichocheo cha kukuza uchumi. Kwa upande mwingine, matarajio ya muda mrefu ni pamoja na kuchochea na kuongeza uzalishaji na usafirishaji wa malighafi na bidhaa ambazo ni chachu ya kuimarisha uchumi. Utekelezaji wa ujenzi wa barabara za Ngara umeleta matokeo chanya katika nyanja za kiuchumi na kijamii kama inavyofafanuliwa hapa chini.

Mtandao wa barabara zenye urefu wa 26km zimejengwa na zinapitika. Gharama zilizotumika ni TZS 240,000,000 bila kulipa wananchi fidia. Katika hali ya kawaida ujenzi huu ungegharimu TZS 800,000,000 endapo wananchi wangelipwa fidia. Halmashauri iliokoa TZS 560,000,000 ambazo zingetumika kufidia wananchi.

Thamani ya ardhi na viwanja imeongezeka kutokana na uwepo wa barabara. Maeneo yote ambayo barabara zimejengwa, thamani ya viwanja imepanda kutoka TZS 1,500,000 hadi TZS 3,000,000 kwa viwanja vidogo na TZS 3,000,000 hadi TZS 6,000,000 kwa viwanja vya kati na vikubwa. Kadhalika, viwanja katika vitongoji vya Kibimba na Kumzenga katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ngara vimeongezeka thamani kutokana na kukamilika kwa mtandao wa barabara uliojengwa kwa ushiriki wa jamii.

Miundombinu mbalimbali pembezoni mwa barabara imeongezeka. Hali hii inathibitishwa na ujenzi wa nyumba bora za kisasa zinazojengwa pembezoni mwa barabara kutokana na kurahisishwa kwa usafirishaji wa vifaa vya ujenzi. Vilevile upatikanaji wa huduma za kijamii kama maji na umeme umeimarishwa kutokana na kupitishwa miundombinu ya huduma hizo pembezoni mwa barabara. Barabara zilizojegwa zinapitika kipindi chote cha mwaka. Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya nyumba bora za kisasa zilizojengwa pembezoni mwa barabara



***Nyumba bora pembezoni mwa barabara***

Shughuli za biashara zimeongezeka na kuimarika kutokana na uwepo wa mitandao ya barabara; pembezoni mwa barabara wananchi wamejenga nyumba za biashara. Kuongezeka kwa shughuli za biashara kumeongeza kipato cha wananchi na mapato ya Halmashauri yanayotokana na leseni, ushuru na vibali vya biashara. Kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri kumeboresha utoaji wa huduma za jamii kama maji na taa za barabarani hususan katika maeneo ya biashara.

Uhusiano baina ya Halmashauri, viongozi katika ngazi za vitongoji na Mamlaka za Miji Midogo umeimarika; Mchakato wa utekelezaji wa ujenzi wa barabara umejenga mahusiano mazuri baina ya vingozi wa Halmashauri, Miji Midogo na vitongoji na hivyo kuchochea utayari na ushirikiano katika kutekeleza miradi mingine ya maendeleo katika ngazi za msingi. Kutokana na mafanikio haya jamii nyingine na vijiji ambavyo havikuwepo kwenye mradi wameiga nakuanza kuomba kujengewa barabara katika maeneo yao pasipo fidia.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Halmashauri inaendela kujenga uelewa kwa jamii juu ya umuhimu wa barabara na kuhamasisha wananchi kuachia maeneo yao bila kudai fidia ili kuendelea na ujenzi wa barabara za mitaa. Halmashauri inaendelea kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchangia maendeleo ikiwa ni pamoja na mipango miji. Halmashauri inaendeleza ushirikiano baina yake na wakazi wa pembezoni mwa barabara kutoa taarifa ikiwa kuna uharibifu wa barabara ili hatua stahiki zichukuliwe mapema. Kuwepo kwa ushirikiano na wakazi wa maeneo husika kunasidia mawasiliano ya mara kwa mara kuhusu kuridhishwa ama kutoridhishwa kwa huduma ya barabara kwa watumiaji hivyo kuisaidia Halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa mara kwa mara. Vilevile Halmashauri imeendelea kuandaa michoro ya mipango miji ambayo itasaidia kuhakikisha ujenzi wa makazi mapya unafuata utaratibu wa mipango miji. Halmashauri inalenga kuongeza mtandao wa barabara na kuziboresha katika kiwango cha lami.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya utekelezaji wa mpango huu yalitokana na ushirikishwaji wa wananchi kwa kuwatumia wazee na watu mashuhuri katika kuhamasisha jamii kukubali kushirikiana na Halmashauri kutekeleza mpango. Siri nyingine ni kuwatumia wenyeviti wa Vitongoji kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa barabara na kushiriki katika kufanikisha zoezi hili. Mikutano ya mara kwa mara katika mitaa na vitongoji ilifanyika kuhamsisha jamii kushiriki na kuchangia miradi ya maendeleo.

Jamii kushindwa kujenga nyumba bora na za kisasa kutokana na ukosefu wa barabara na ugumu wa kusafirisha vifaa vya ujenzi iliwafanya wananchi kuona umuhimu wa kutoa maeneo kuruhusu kujengwa kwa barabara. Vilevile kukosekana kwa huduma za jamii kama umeme, maji na usafirishaji kulichangia kuongezeka kwa hamasa ya kutaka kufunguliwa kwa barabara.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE

## UHIFADHI JUMUISHI WA MISITU YA ASILI






*Uzoefu wa H/W ya Ukerewe*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Mwanza, inapatikana kati ya Latitudo $1^o45$ na $2^o15$ Kusini na Longitudo $32^o$ 45 na $33^o45$ Mashariki. Inapakana na Halmashauri za Wilaya za Magu kwa upande wa Kusini, Musoma (Mkoa wa Mara) kwa upande wa Kaskazini na Sengerema kwa Upande wa Mashariki. Halmashauri ya Ukerewe ni kisiwa kikubwa ndani ya Ziwa Viktoria ambacho kipo umbali wa 54km kutoka Jiji la Mwanza. Halmashauri ya Ukerewe inaundwa na visiwa 38 ambapo visiwa 15 hutumika kwa makazi ya kudumu na visiwa vingine vilivyobaki hutumiwa kwa msimu hasa shughuli za uvuvi wa samaki. Halmshauri ina eneo la 6,400$km^2$ ambapo 5,760$km^2$ zimefunikwa na maji ya Ziwa Viktoria. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 4, Kata 25 na Vijiji 76.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, idadi ya watu kwa Halmashauri ya Ukerewe ni 260,831 kati yao; 128,842 ni wanaume na 131,989 wanawake. Ongezeko la watu linakadiriwa kuwa 2.9% zaidi ya wastani wa kitaifa ambao ni 2.6%. Katika sensa ya mwaka 2012 idadi ya watu imeongezeka kufikia 345,147 hivyo kusababisha kufikia ujazo wa watu zaidi ya 500 kwa 1$km^2$. Ongezeko la idadi ya watu umeleta uhitaji mkubwa wa ardhi hivyo kuongeza changamoto katika usimamizi wa ardhi, uzalishaji, uharibifu na umasikini uliosababisha kuvamiwa maeneo tengefu ya ardhi.

Kijografia, Halmashauri ina milima midogo midogo, mabonde, tambarare na mito midogo ya msimu (ni mito ya msimu kutokana na uharibifu wa mazingira; hapo awali ilikuwa mito ya kudumu). Halmashauri ina kanda mbili za kiikolojia; ukanda wa Mashariki una mvua za wastani, udongo mweusi wa mfinyanzi, milima ina mimea aina ya miombo kama vile *Cumbretum spp* na tambarare kuna iana ya migunga (*Acacia spp)*. Ukanda wa Magharibi una mvua nyingi kuliko ukanda wa Mashariki; sehemu ya milima imestawisha kwa wingi miti aina ya Mivule(*Melicia excelsa ),* miti mingine ni kama *Maesopsis Emenii, Albizia sp* na Mtalawanda *(Markhamia sp)*. Ukerewe ni eneo la milima ambalo lilikuwa na misitu minene ya kiikweta. Kutokana na ongezeko kubwa la watu na shughuli za kuchumi, Halmashauri imebakiwa na misitu michache iliyohifadhiwa ambayo inamilikiwa na Serikali Kuu na Halmashauri. Misitu hiyo ipo katika eneo la mlimani kwenye ukanda wa Magharibi.

Shughuli kuu za kiuchumi ni pamoja na kilimo, uvuvi, biashara na uvunaji wa mbao kutoka misitu ya Rubya na mashamba ya miti ya watu binafsi. 92% ya wananchi hutegemea kilimo na mazao yanayozalishwa ni muhogo, viazi na mpunga; mazao haya ni ya chakula na biashara. Aina mbalimbali za matunda huzalishwa zikiongozwa na uzalishaji wa machungwa. Miaka ya nyuma H/W ya Ukerewe ilikuwa ikisafirisha mazao ya chakula kwenda Wilaya jirani kama Bunda, Magu, Musoma na Mwanza; hata hivyo hali ilibadilika kufikia hatua ya Halmashauri kutegemea chakula kutoka nje ya Wilaya. Hali hii ilichangiwa na ongezeko la watu na usimamizi mbovu wa mazingira uliosababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao. Kwa sasa mazao pekee yanayozalishwa na kuuzwa nje ya Halmashauri ni matunda, samaki na mbao.

Jitihada za kuhifadhi misitu zilianza kabla ya ukoloni. Machifu wa Ukerewe walifanya jitihada za kuhifadhi misitu na visiwa vidogo. Misitu minene ilitumiwa kama sehemu za matambiko, kuabudu na kumuomba Mungu usaidizi pale jamii ilipokabiliwa na majanga kama magonjwa, njaa na ukame. Serikali za wakoloni wa Kijerumani na Waingrereza ziliendeleza jitihada za machifu. Serikali ya Waingereza ilifikia hatua ya kutangaza na kuitambua misitu mitano kwenye gazeti la Serikali mwaka 1957 ambapo misitu minne ya Kabingo 250ha, Mkigaki 116ha, Itira 109ha na Negoma 698ha ilikuwa ni misitu ya mamlaka za watu wa Ukerewe. Hifadhi ya msitu wa Rubya (1,920ha) ilimilikiwa na Serikali Kuu katika kipindi cha mwishoni mwa miaka ya 1950 na kubadilishwa kuwa shamba la miti hali iliosababisha kuongezeka kwa miti aina ya misindano (*Pinus caribea)*. Katika maeneo ya watu binafsi ilikuwepo misitu ya asili midogo midogo hasa katika maeneo ya milimani na kwenye visiwa ambavyo havikuwa na makazi ya watu. Misitu hii iliheshimiwa na kutunzwa, hata hivyo kufikia katikati mwa miaka ya 1970 uharibifu wa misitu ulikithiri kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, shughuli za kibinadamu na kukosekana kwa sheria madhubuti za kulinda misitu.

Mpango wa Uhifadhi Jumuishi wa Misitu ya Asili ulitekelezwa kwenye Kijiji cha Muleseni. Kijiji hiki kipo pwani ya Ziwa Viktoria ndani ya Kata ya Ngoma, Tarafa ya Mumbuga umbali wa kilomita 12 kutoka Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nansio ambapo ndipo makao makuu ya Halmashauri. Kijiji kipo upande wa Mashariki wa Kisiwa cha Ukerewe, kinapakana na Kijiji cha Hamkoko kwa upande wa Magharibi, Kijiji cha Nantare kwa upande wa Kaskazini na Wilaya ya Bunda kwa upande wa Kusini na Mashariki. Wakazi wengi wa kijiji hicho hutegemea kilimo, ufugaji, uvuvi na shughuli zinazolandana na uvuvi; baadhi ya wakazi hutegemea biashara ndogo ndogo. Mazao ya chakula ni pamoja na muhogo, viazi vitamu, mahindi na jamii ya mikunde.

**2.0 TATIZO**

Kabla ya mwaka 1990 Halmashauri ilibaini ongezeko la uharibifu wa misitu uliosababishwa na ongezeko la watu hivyo kuchochea kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu katika nyanja za kijamii na kiuchumi zilizohitaji ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji, makazi na taasisi, kuongezeka kwa mahitaji ya nishati, mbao za kujengea nyumba na mitumbwi kulisababisha ukataji wa miti. Kuongezeka kwa soko la samaki kulichochea uharibifu wa misitu. Mwishoni mwa miaka ya 1950 hadi 1970 uvuvi wa samaki aina ya sangara ulishamiri na kusababisha usafirishaji wa samaki kwenda maeneo mengine ya Tanzania na nchi jirani za Kenya (Kisumu) na Uganda (Kampala). Njia kuu ya kuhifadhi samaki ilikuwa kukausha kwa moshi. Njia hii ya ukaushaji ilihitaji kuni nyingi hivyo kusababisha ukataji wa miti uliokithiri katika misitu ya umma na kuhatarisha kutoweka kwa misitu hiyo. Wavuvi walifika hatua ya kujenga kambi za muda kwenye vijiji vya ufukweni mwa ziwa kwa ajili ya ukaushaji wa samaki. Kutokana na kuongezeka kwa soko la samaki vipato vya wananchi viliongezeka na kuwafanya watamani kujenga nyumba bora za tofali za kuchoma, hali hii iliongeza kasi ya ukataji wa miti kwa ajili ya kuchoma tofali, mbao za kuezekea nyumba na samani. Kutokuwepo usimamizi madhubuti wa sheria za misitu ni sababu nyingine iliyochangia uvunaji holela wa mazao ya misitu.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu ni kuhakikisha ustawishaji na utunzaji wa misitu ya asili kwenye maeneo ya umma ndani ya Halmashauri ya Ukerewe. Malengo mahususi ni pamoja na kudhibiti mmomonyoko wa ardhi ambao ni chanzo cha uharibifu ardhi, mazingira na kupoteza virutubisho vya udongo na kuhakikisha uwepo wa kuni kwa ajili ya nishati, kuboresha mazingira ya viumbe wa msituni na kuimarisha hali ya hewa.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Halmashauri imechukua jitihada mbalimbali kutatua tatizo la uharibifu wa misitu. Kwa kushirikana na wadau kama Benki ya Dunia, Halmashauri ilibuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha jamii inahusishwa katika kuhifadhi misitu ya asili. Mikakati hii ni pamoja na;

Kuanzisha kitalu kikuu cha miche ya miti; Miaka ya 1970 kupitia Mpango wa Maendeleo Vijijini (RIDEP)) uliofadhiliwa na Benki ya Dunia, Halmashauri ilianzisha kitalu kikuu cha miche ya miti na kuwagawa miche kwa wanakijiji bila kuchangia gharama yeyote. Kwa muda wa miaka 12 Halmashauri ilifanikiwa kugawa miche ya miti zaidi ya 120,000,000 ya aina tofauti bure kwa wananchi.

Kujenga uelewa; mwaka 1995 wananchi wa kijiji cha Muleseni na vijiji vingine vya jirani walipatiwa mafunzo ya uhifadhi wa misitu. Mafunzo yalitolewa chini ya Mradi wa Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu (FRMP) ambao ulijikita katika kujenga uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi misitu, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti na ufugaji wa nyuki. Mikutano ya wananchi ilitumika kukuza uelewa kuhusu uhifadhi wa misitu. Mbinu nyingine ni majadiliano katika vikundi na kuonyesha filamu zinazoonesha athari za uharibifu wa mazingira na hatua za kuchukua kuanzisha uhifadhi wa misitu jumuishi.

Uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti vya kijiji; baada ya kupatiwa mafunzo wananchi walihamasika kwa kiasi kikubwa na kuamua kutekeleza mafunzo kwa vitendo kwa kuanzisha vitalu vya miche ya miti na misitu. Jitihada zao zilivutia wananchi wengi zaidi na kuanza kukubalika na kutambuliwa. Mwaka 2005 msitu wa wanakijiji ulitembelewa na Mwenge wa Uhuru kama njia ya kuwatambua nakuwatia hamasa. Kutokana na

tukio la mwenge, wanakijiji walihamasika zaidi katika kuhifadhi misitu kwenye maeneo yanayomilikwa na umma. Halmashauri iliwasidia wanakijiji kuunda kamati za uhifadhi wa misitu na kutunga sheria ndogo za kusimamia uhifadhi wa misitu. Kamati iliyojumuisha wajumbe 10 iliundwa na kupatiwa mafunzo na Afisa Misitu wa Halmashauri.

Mafunzo kwa watu binafsi kuhusu kuanzisha vitalu vya miche ya miti; Miaka ya 1990 mradi wa FRMP ulifadhili mafunzo kwa mwanachi mmoja mmoja, vikundi na taasisi kuhusu uanzishaji wa vitalu binafsi vya miche ya miti, ufugaji wa nyuki, kutengeneza na kutumia majiko banifu kwenye vijiji 25. Mradi ulikamilika mwaka 2000; hata hivyo watu binafsi, vikundi na taasisi wanaendeleza kuzalisha na kusambaza miche ya miti kwa kuuza. Watu binafsi wanaojishughulisha na uzalishaji wa miche ya miti wapo 11, shule za sekondari 3, shule za msingi 13 na vikundi 13. Kati ya wadau hawa walioweza kufanya vizuri zaidi ni shule ya Sekondari Murutunguru, Kikundi cha bustani cha Bure ambacho kipo Kijiji cha Mukunu na kikundi cha HUNAU amabacho kipo Kijiji cha Maregea.

## 5.0 RASILIMALI

Utekelezaji wa mikakati katika mradi huu ulihusisha rasilimali kutoka kwa wadau mbalimbali kama Wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Serikali Kuu na Washirika wa Maendeleo. Rasilimali zimeainishwa katika makundi ya fedha, watu na vitendea kazi. Rasilimali watu ilihusisha nguvu kazi iliyotoewa na wanakijiji, wataalamu kutoka Halmashauri, Serikali Kuu na Washirika wa Maendeleo. Rasilimali fedha zilizotumika katika mradi zimeainishwa kwenye jedwali 1 hapo chini.

**Jedwali Na 1: Rasilimali Fedha**

| S/n | Shughuli za Mradi | Chanzo cha fedha | Kiasi TZS |
|---|---|---|---|
| 1 | Kujenga uelewa kuhusu mazingira<br>Mafunzo kuhusu utunzaji wa misitu ya asili<br>Mafunzo kuhusu matumizi ya majiko banifu na uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti<br>Uanzishaji na utunzaji wa vitalu vya miche ya miti<br>Uhifadhi wa misitu katika maeneo ya umma<br>Utengenezaji wa majiko banifu | Serikali Kuu /Halmashauri kupitia mfuko wa FRMP | 360,000,000 |
| 2 | Mafunzo ya ufugaji nyuki, ununuzi wa mizinga bora ya nyuki | HEIFER International | 2,300,000 |
| 3 | Kutoa mafunzo ya vitendo kuhusu utengenezaji wa mizinga ya nyuki<br>Ununuzi wa vitendea kazi | ROTARY International na ROTARY Club-Nansio Ukerewe | 4,800,000 |

## 6.0 MATOKEO

Baada ya kutekeleza mikakati ya uhifadhi wa misitu, H/W ya Ukerewe imefanikiwa kufikia matokeo yafuatayo.

Jamii imehamasishwa juu ya uhifadhi wa misitu; kutokana na hamasa ya jamii, eneo la hekta 13,700 la misitu limehifadhiwa kwenye maeneo ya umma ndani ya vijiji 34. Kutokana na hamasa hii, vijiji vingine ndani na nje ya Halmashauri vimeanza kuiga kuhifadhi misitu na kuitunza.

Sheria ndogo kuhusu uhifadhi wa misitu zimeandaliwa na zinafanya kazi; vijiji vimeanzisha sheria ndogo ambazo hutumika kuhimiza uhifadhi wa misitu. Sheria hizi zinabainisha majukumu ya kamati ya uhifadhi misitu, faini kwa wanaokiuka makubaliano, utaratibu wa kuvuna mazao ya misitu na matumizi sahihi ya misitu.

Baadhi ya mimea ya asili ambayo ilitoweka hapo awali imeanza kuota upya kwenye maeneo yaliyohifadhiwa. Vilevile kutokana uhifadhi wa misitu mmomonyoko wa udongo pembezoni mwa ziwa umepungua Picha ifuatayo inaonesha ustawi wa msitu pembezoni mwa kingo za ziwa.



***Urejesho wa uoto wa asili pembezoni mwa ziwa***

Kumekuwepo na ongezeko kubwa la nishati ya kupikia (kuni) kutokana na mpango mzuri wa uvunaji wa mazao ya misitu ulioanzishwa. Vilevile kutokana na uhifadhi wa misitu wanyama ambao walitoweka hapo awali kutokana na uharibifu wa mazingira wameanza kurejea kwenye maeneo yaliyohifadhiwa. Uhifadhi wa misitu kwa njia shirikishi jamii umesaidia kuimarisha ujuzi wa jamii na watu binafsi wa kutunza misitu. Jamii na watu binafsi wameweza kuanzisha misitu yao wenyewe ambayo wanaiendesha kibiashara. Uhifadhi wa misitu umetengeneza ajira kwa baadhi ya wanakijiji ambao wanajishughulisha na uoteshaji wa miche ya miti na kuiiuza ili kupata fedha.

Kuanzishwa kwa ufugaji wa nyuki ndani ya H/W ya Ukerewe; awali watu wa Ukerewe hawakujihusisha na ufugaji wa nyuki isipokuwa wachache ambao walifuga nyuki ili kupata asali ya kufanyia tambiko. Baada ya kutekeleza mradi huu, wananchi walihamasika na kuanza kufuga nyuki kama shughuli ya kujiongezea kipato. Idadi ya wafugaji wa nyuki imefikia 224, vikundi 53, wanatumia mizinga ya asili 1,463 na ya kisasa 23. Hadi kufikia mwaka 2016 jumla ya kg 413 za asali zilivunwa.  Ufugaji wa nyuki ulitekelezwa zaidi na wananchi kutoka vijiji vya Muleseni na Busiri.



***Ufugaji wa nyuki kwenye msitu uliohifadhiwa Kijiji cha Muluseni***

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Katika kuhakikisha uendelevu wa matokeo yaliyopatikana, Halmashauri ikishirikiana na wanakijiji na wadau wengine wa uhifadhi wa misitu imeandaa mikakati ya uendelevu. Sheria ndogo zilizoandaliwa na Vijiji

zinatumika na kusimamiwa vyema. Sheria hizi zinatoa katazo la kufanyika shughuli za kibinadamu ndani ya eneo lililohifadhiwa. Vilevile sheria inabainisha utaratibu wa uvunaji wa rasilimali za misitu na mwongozo kwa kamati ya usimamizi wa misitu. Wanakijiji hufanya mikutano kila robo mwaka kujadili namna bora ya kuendelea kuhifadhi misitu. Utaratibu huu wa mikutano umejenga dhana ya umiliki wa misitu katika jamii na kuifanya kutambua tija ya kusimamia na kudumisha matokeo ya mradi.

Vijiji vimeunda kamati madhubuti za kusimamia uhifadhi wa misitu; utayari wa wajumbe wa kamati ya uhifadhi misitu kutumia sheria ndogo katika usimamizi wa kila siku wa misitu, umewezesha kuwachukulia hatua za kisheria wananchi wachache ambao wanafanya uharibifu wa misitu. Mbali na kamati ya uhifadhi misitu, Halmashauri ya Kijiji cha Muluseni inasaidia kusimamia utii wa sheria ndogo. Kuwepo kwa kalenda ya uvunaji wa misitu kumesaidia kuwaelimisha wananchi utaratibu wa kuingia ndani ya msitu na kuvuna mazao ya misitu. Hii imesaidia kudhibiti uvunaji holela wa misitu.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kufanikiwa kwa utekelezaji wa mkakati huu kumetokana na siri mbalimbali. Dhana ya umiliki wa misitu kwa jamii yenyewe imesaidia kufanikiwa kwa mpango. Utayari wa jamii kuhusika kwenye shughuli zote za uhifadhi misitu ni siri nyingine ya mafanikio.

Kuwepo kwa usimamizi madhubuti na tathimini kuhusu uhifadhi wa misitu; jamii imekuwa ikiendesha mikutano kila robo mwaka kujadili mafanikio na changamoto pamoja na kubuni mikakati ya kutatua changamoto. Vilevile umakini na utayari wa kamati ya uhifadhi wa misitu kuratibu shughuli za uhifadhi ilikuwa ni chachu ya mafaniko. Ushirikiano na mahusiano yaliyojengeka kati ya jamii, H/W ya Ukerewe na wadau wa uhifadhi misitu ulichangia kufanikiwa kwa mradi huu.

# Sura ya Tano
# Maendeleo ya Jamii Kiuchumi

Sura ya Tano ina mbinu bora sita zinazohusu jitihada za wananchi kujiletea maendeleo ya kiuchumi zinazohusu dhana mpya ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"*. Dhana hii husisitiza maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe kwa kuibua miradi yenye upekee na vijiji vingine. *"Kijiji kimoja zao moja"* (OVOP) ni harakati zilizoanza miaka ya 1970 katika eneo la Oita nchini Japani malengo yakiwa kuinua uchumi vijijini. Lengo mahususi la dhana hii lilikuwa ni kuhamasisha kila kijiji cha Oita kuchagua mradi wa uzalishaji ambao una utofauti wa aina fulani katika mkoa na kuzalisha kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Dhana ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"* inalenga kuinua maendeleo ya jamii na uchumi katika mkoa kupitia kujitolea kuinua uwezo wa wananchi wa ngazi ya chini. Kabla ya kuanzisha harakati hizi katika eneo la Oita, waanzilishi walipata ushirikiano mkubwa wa jamii kupitia mashindano ya mpira na walikuwa na ushirikiano na miji rafiki ya nchi za nje. Mbinu hizi ziliwaweka watu pamoja, ziliwajengea uwezo wa kimaendeleo, na walishirikishana ujuzi waliopata. Mikakati mingine iliyofuata ilikuwa ni kuanzisha sera za jamii kuongeza zaidi thamani ya bidhaa, kuboresha mifumo, kuanzisha zao jipya au la pekee, ufundi wa kuchakata mazao ya kilimo, utalii, na mtazamo juu ya hali ya jamii.

Dhana ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"* inaonekana kuwa ni njia ya kuimarisha ujasiriamali wa watu wa vijijini kwa kutumia rasilimali, elimu na uzoefu, kufanya kazi zinazoongeza thamani kwa kuvipa utofauti bidhaa zao na kujenga uwezo wa rasilimali watu katika shughuli za uchumi kijijini. Kutumia ujuzi na rasilimali zilizopo bila kuathiri mazingira ni jambo linalotiliwa mkazo sana katika shughuli za dhana hii. Hii ina uhusiano na dhana ya maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe. Katika harakati za *Kijiji Kimoja Zao Moja*, kuna msemo maarufu usemao "Fikiri kimataifa lakini tenda kulingana na Mazingira" (*Think globally but act locally*").

Sura hii ya tano inaelezea mbinu bora sita kutoka Halimashauri za Wilaya za Misenyi, Ukerewe, Itilima, Tarime, Rorya na Bunda. Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi inahusu Uwezeshaji, Utafutaji wa Masoko na Mitaji kwa Wazalishaji wa Vijijini katika Kata za Kilimilile na Mushasha. Kabla ya utekelezaji wa mbinu hii, wananchi wa Kata za Kilimilile na Mushasha waliathirika kwa umasikini kutokana na ukosefu wa soko la uhakika wa mazao na bidhaa zilizozalishwa. Jitihada za Halmashauri zililenga kuwezesha wazalishaji kwa kuwaunganisha na soko na taasisi za fedha ili kupata mitaji na hatimaye kupunguza kiwango cha umasikini na kuimarisha uchumi. Halmashauri kwa kushirikiana na MIVRF na GEODAT Consultant Ltd iliunda vikundi vya wakulima, ikatoa mafunzo na kuviunganisha na taasisi za fedha. Vilevile wakulima waliwezeshwa kutengeneza mpango rahisi wa kibiashara na mbinu za kupata masoko na kuunganishwa katika vikundi ili kumudu soko la pamoja. Utekelezaji wa mbinu hii uliongeza uzalishaji, uhakika wa chakula, uhakika wa soko, kipato cha mkulima na vikundi na kuunganishwa kwa wakulima na taasisi za fedha.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe inahusu Kuboresha Uzalishaji na Kuongeza Thamani ya Zao la Muhogo. Jitihada hii ilitekelezwa baada ya kubaini kupungua kwa uzalishaji wa muhogo kulikosababishwa na kupungua kwa rutuba ya udongo, kuongezeka kwa magonjwa, mbinu duni za uchakataji na upungufu wa chakula. Halmashauri ililenga kuboresha maisha ya wakulima kwa kuongeza kipato na uhakika wa chakula katika kaya kupitia ongezeko la thamani na kutatua changamoto za uzalishaji, uchakataji na soko la zao la muhogo. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau illifanya utafiti kubaini aina bora ya mbegu ya muhogo na kuunganisha wakulima kwenye vikundi vya uzalishaji, uchakataji na uuzaji wa pamoja. Utekelezaji wa jitihada

hii uliwezesha kuongeza uzalishaji na kuimarisha uchakataji wa mazao ya muhogo na hatimaye kuongeza wigo wa soko, kipato na uhakika wa chakula.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Itilima inahusu Ukuzaji wa Kilimo - Hifadhi kwa Uhakika wa Chakula katika Kijiji cha Kabale. Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii, mavuno kwa eneo yalikuwa pungufu kutokana na mbinu duni za kilimo zilizotumika, kupungua kwa rutuba katika udongo, upotevu wa maji, mmomonyoko wa udongo pamoja na mvua zisizo za uhakika. H/W ya Itilima ilianzisha Kilimo - Hifadhi kwa lengo la kukuza uhakika wa chakula katika kaya, kuboresha maisha ya wakazi wa vijijini, kusaidia wakulima kutumia mbinu bora za kilimo, kuongeza uzalishaji kwa eneo na kuziwezesha jamii kushiriki katika kilimo rafiki kwa mazingira. Halmashauri ilihimiza na kuwasidia wakulima kujiunga katika vikundi, kuwajengea uelewa juu ya Kilimo - Hifadhi na kuanzisha shamba darasa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Jitihada hii iliongeza uzalishaji, kipato cha mkulima, uhakika wa chakula na rutuba ya udongo.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime inahusu Kukuza Uzalishaji wa Kahawa za Vikonyo na Kuongeza Kipato. Kabla ya jitihada hii, wakulima walikumbana na changamoto za uzalishaji duni, ongezeko la magonjwa na wadudu wanaoshambulia kahawa na kusababisha kipato duni. Halmashauri iliamua kuboresha maisha ya wakulima kwa kuongeza uzalishaji wa kahawa wenye tija kwa anzisha aina mpya ya kahawa ambayo inazaa kwa wingi na kuhimili magonjwa. Halmashauri iliwajengea uwezo wakulima kukubali na kutumia njia bora za uzalishaji na ukoboaji wa kahawa mara baada ya kuvunwa. Kadhalika, Halmashauri iliandaa na kusambaza miche bora ya kahawa kwa wakulima, safari ya kimafunzo na kujenga matandao na wadau wa kahawa kwa lengo la kupata usaidizi na ushauri. Utekelezaji wa jitihada hii ulisababisha kuongezeka kwa uzalishaji na kipato cha mkulima, mapato ya ndani ya Halmashauri kupitia ushuru wa kahawa na kuimarika kwa ushirikiano baina ya wakulima, Halmashauri na wadau wa Kahawa.

Halmashauri ya Wilaya ya Rorya imetekeleza mbinu bora inayohusu Umwagiliaji wa Mpunga, Kuboresha Kipato na Uhakika wa Chakula katika kijiji cha Irienyi. Kabla ya mwaka 1999, Kijiji kilikumbwa na upungufu wa chakula, kipato duni, uzalisahji duni, kilimo tegemezi cha mvua, matumizi ya mbegu zisizo bora, ukosefu wa huduma za ugani, miundombinu duni ya umwagiliaji na kukosekana kwa ummoja wa wakulima wa mpunga. Halmashauri ilitekeleza jitihada hii kwa lengo la kuboresha kipato na uhakika wa chakula cha kaya na jamii za watu wa kijiji cha Irienyi. Jitihada hii ilihusu kuainisha eneo linalofaa kwa umwagiliaji, kujenga miundombinu ya mwagiliaji kama bwawa la kuhufadhi maji na miferaji ya umwagiliaji, kuwapatia wakulima mafunzo kuhusu uzalishaji bora wa mpunga na kuongeza thamani, kuunda umoja wa wakulima (UWAIRO) na ujenzi wa ghala la kuhifadhia mpunga. Matokeo ya jitihada hii ni pamoja na uwepo wa miundombinu bora ya umwagiliaji, ongezeko la uzalishaji kwa eneo, uwepo wa umoja wa wakulima (UWAIRO), ongezeko la kipato cha wakulima na fursa za ajira.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Bunda inahusu Ufugaji wa Samaki katika Vizimba na Urejeshaji wa Mazalia ya Samaki. Kabla ya jitihada hii, kulikua na upungufu mkubwa wa idadi ya samaki ndani ya Ziwa Viktoria kilichosababishwa na uvuvi usiozingatia viwango na uvuvi haramu. Halmashauri ilitekeleza jitihada hii kwa kuvijengea uwezo vikundi vya usimamizi wa fukwe (Beach Management Units -BMUs), Kikosi cha Jeshi (822KJ) na jamii inayozunguka Ziwa Viktoria kuhusu namna ya kutumia vizimba na kuhakikisha uzalishaji bora wa samaki kwenye vizimba na mazalia ya samaki. Halmashauri iliwatambua wadau na kuwajenga uelewa kuhusu ufugaji wa samaki kwenye vizimba, uanzishaji wa vikundi vya uvuvi na kuwapa mafunzo ya kutengeneza vizimba vya samaki. Jitihada hii ilileta ushirikianao imara baina ya Halmashauri, UNDP, ESRF, Kikosi cha Jesshi cha 822KJ na jamii ya Kijiji cha Karukekere. Ushirikiano huu ulisababisha kukubalika kwa tekinolojia mpya ya ufugaji wa samaki, kupungua kwa uvuvi haramu, kuongezeka kwa samaki na kumarisha ikolojia.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI

**UWEZESHAJI, UTAFUTAJI WA MASOKO NA MITAJI KWA WAZALISHAJI WA VIJIJINI**



***Uzoefu wa Kata za Kilimilile na Mushasha.***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Kagera iliyoanzishwa mwaka 2007 baada ya kugawa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Halmashauri inapatikana Magharibi mwa Ziwa Viktoria. Inapakana na Nchi ya Uganda kwa upande wa Kaskazini, H/W ya Karagwe kwa upande wa Magharibi, H/W ya Bukoba kwa upande wa Kusini na Mashariki. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 2, Kata 20, Vijiji 77 na Vitongoji 352. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina idadi ya watu 202,632 kati yao 10,085 wanaume na 102,547 wanawake. Wastani wa ongezeko la watu ni asilimia 1.1.

Halmashauri ipo katika muinuko wa 1400m kutoka usawa wa bahari, Tarafa ya Kiziba ina milima zaidi ukilinganisha na Tarafa ya Missenyi ambayo kwa sehemu kumbwa ina eneo la wazi na tambarare. Tarafa zote zina mito midogo ambayo ndio inayounda Mto Ngono na Mto Mwisa inayomwaga maji Mto Kagera kabla ya kuingia Ziwa Viktoria. Halmashauri inapata mvua katika vipindi viwili; Mvua za muda mfupi kati ya mwezi Septemba na Desemba ilihali mvua za masika hunyesha kati ya mwezi Machi na Mei. Nyanda za juu hupata mvua kati ya 1000mm - 1300mm wakati upande Magharibi wa Halmashauri hupata wastani wa mvua kati ya 600mm – 1000mm. Wastani wa joto ni $20^0$C. ($15^0$C – $28^0$C). Takriban 96% ya wananchi wanajihusisha na kilimo, 2.8% biashara ndogo ndogo na 1.2% ni watumishi katika sekta za umma.

Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi ni moja kati ya Halmashauri mbili ndani ya mkoa wa Kagera inayotekeleza mpango wa umarishaji wa miundiminu ya soko, kuongeza thamini ya mazao na kusaidia mitaji kwa wakulima wa vijijini (MIVARF). Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kama Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo wa Kimataifa (IFAD) na Benki ya Maendeleo ya Afrika imetekeleza Mradi wa MIVARF kwa muda wa Miaka saba (2011-2017). Lengo la mradi huu ni kupunguza umasikini kijijini na kuchochea kukua kwa uchumi kama inavyoelekezwa na Mpango wa Taifa wa Maendeleo pamoja na MKUKUTA/ MKUZA, KILIMO KWANZA, Mpango wa Kusaidia na Kuendeleza Kilimo na Masoko (AMSDP 2002-2009), Mpango wa Kusaidia Mitaji Vijijini (RFSP) na Mpango wa Wilaya wa Kusaidia Kilimo (DASP). Miradi yote hii inasisitiza kuelimisha wakulima kwa kutumia mashamba darasa ambayo yamewezesha uzalishaji mkubwa wa mahindi na maharage.

H/W ya Missenyi, ilitekeleza MIVARF mwaka 2014 baada ya Serikali Kuu kuagiza Halmashauri ziandae andiko la miradi ya sekta ya kilimo ambayo wafadhili wangeweza kusaidia katika kupunguza umasikini vijijini. Mchakato wa ushindani wa andiko la miradi ya kilimo ulihusisha Halmashauri zote Tanzania. Ndani ya Mkoa wa Kagera, Halimashauri za Missenyi na Muleba zilichaguliwa. Andiko la H/W ya Misenyi lilihusu Uwezeshaji, Utafutaji wa Masoko na Mitaji kwa Wazalishaji wa Vijijini (*producers' empowerment, market linkage and rural financing project*). Halmashauri iliendesha zoezi la kutafuta mzabuni chini ya usimamizi wa wataalamu kutoka MIVARF ambapo kampuni ya GEODATA Ltd ya Mwanza ilishinda tenda. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Februari 2014 katika Kata za Kilimilile na Mushasha.

**2.0 TATIZO**

Uzalishaji utonekana kuwa muhimu ikiwa tu una thamani katika soko. Kwa mantiki hii, soko ni moja ya maeneo yanayosisimua biashara na ndio moyo wa biashara (Curry, 2000). Inafafanuliwa kuwa kama mzalishaji hana soko au kushindwa kupata soko kwa bidhaa zake atakuwa amepotea katika masoko ya kitaifa na ya kimataifa kwa kuwa hataweza kutambua faida ambayo ni muhimu katika uzalishaji. Curry (2002) anabainisha kwamba masoko ya bidhaa za kilimo nchini Tanzania yanakabiliwa na changamoto kubwa. Inakadiriwa kwamba 67% ya matunda nchini Tanzania huharibika yakiwa shambani kwa kukosa soko kwa wakati. Kwa wachache ambao wanafanikiwa kufika sokoni, 25% ya matunda huharibika kabla ya kununuliwa kutokana na mauzo yasiyo ya uhakika (DTB, 2007)

Serikali Kuu imekua ikiweka jithada kubwa na msisitizo kwenye uzalishaji bila kuweka kipaumbele kwenye utafutaji wa masoko jambo lililosababisha H/W ya Missenyi kuchukua hatua za kukabiliana na changamoto hii kuanzia mwaka 2010. Wananchi wa Missenyi kama ilivyo kwa Halmashauri nyingine Tanzania waliendelea kuathirika na umasikini na mzunguko dhaifu wa mifumo ya maendeleo kutokana na kukosa masoko rasmi na kutokuratibiwa kwa bidhaa za wazalishaji. Kadhalika hali hii ilizikabili kata za Kilimilile na Mushasha.

**3.0 LENGO**

Jitihada ya H/W ya Missenyi ililenga kuwaimarisha wazalishaji, na kuwatafutia masoko na kuwaunganisha na taasisi za fedha ili kujikomboa kutoka kwenye umasikini na kujimarisha kiuchumi. Malengo mahususi ni pamoja na; kuwaunganisha wakulima kwenye vikundi vya uzalishaji na kuwasidia mbinu bora za uzalishaji kwa vitendo, kuwaimarisha wazalishaji wa vijijini kupitia mafunzo, makongamano na mikutano katika kusimamia uzalishaji na majukumu yote ya vikundi.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika maeneo manne. Eneo la kwanza, linahusu shughuli zote za kujenga uwezo wa wajumbe na viongozi katika vikundi vilivyokusudiwa kuhusu kutekeleza majukumu yaliyoanishwa ili kuweza kufikia malengo ya uendeshaji wa biashara na soko la pamoja. Eneo la pili limejikita kwenye uendelezaji wa shughuli zote zilizoainishwa ambazo zilihusu kuwezesha vikundi, kubaini wanunuzi, kukusanya, kuhifadhi, kupunguza upotevu wa mazao wakati wa mavuno na kuamua namna ya kusafirisha mazao yao kwa kuzingatia faida.

Eneo la tatu lilihusu kuwezesha vikundi kukusanya taarifa ambazo zitawawezesha kukuza taswira ya kikundi na kuzitumia kushawishi wanunuzi wa mazao, wauzaji wa pembejeo na taasisi za kifedha ili kufanya nao biashara. Eneo la mwisho ni kuunganisha wazalishaji katika umoja wa SACCOS na kuwaunganisha na taasisi za fedha.

Mpango wa pamoja wa uwezeshaji uliundwa na wataalamu kutoka Geodata na Halmasahauri. Vilevile, mikutano ya tathimini ilifanyika ikiwahusisha kamati tendaji za MIVARF kutoka Mkoani na Wilayani. Timu za wataalamu zilifanya ziara kutathimini utekelezaji wa mpango na changamoto kwa vikundi na wajumbe wake. H/W ya Misenyi ilibaini kukosekana kwa muunganiko baina ya wakulima, wazalishaji wadogo na masoko na kuamua kutekeleza mikakati ifuatayo kutatua changamoto zilizobainishwa.

Uwezeshaji wazalishaji; Halmashauri kwa kushirikiana na MIVARF na kampuni ya GEODATA Consultant Ltd ilwezesha kuundwa kwa vikundi vya wakulima na kuwaunganisha na taasisi za fedha; kisha kuaanda mpango rahisi wa kibiashara na mikakati ya kupata masoko pamoja na kuwahimiza wakulima kuunganisha nguvu katika vikundi na kuuza mazao kwa pamoja. Mbinu za uzalishaji kama kutumia mbegu bora, upandaji wa kitaalamu na uvunaji kwa wakati zilitolewa ili kuhakikisha kupata soko la uhakika. Picha zifuatazo zinaonesha shamba la kikundi cha wakulima cha Uvuke na wajumbe wakichakugua mbegu.




***Shamba la kikundi cha Uvuke na wajumbe***

Uwekaji wa malengo ya vikundi vya wakulima; Jitihada hii ililenga kupata soko, uzalishaji, bei ya pamoja na kuweka mikakati ya maendeleo. Vikundi 18 viliundwa nakuwezesha mikakati ya uzalishaji na uuzaji. Jedwali Na.1 linaonesha vikundi vilivyoundwa na malengo waliojiwekea.

Jedwali Na. 1 Malengo ya Vikundi vya Wakulima

| SN | JINA LA KIKUNDI | KIJIJI | WAJUMBE | | | MALENGO YA UZALISHAJI – MAHINDI | | | MAHARAHE | | | MALENGO YA MAUZO | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Me** | **Ke** | **Jumla** | **Ekar** | **Gunia/Ekar** | **Jumla ya Kgs** | **Ekar** | **Gunia/Ekar** | **Jumla Kgs** | **Mahind** | **Maharage** |
| **1.** | Vijana Sasa Kazi | Kenyana | 10 | 8 | 18 | 9 | 7 | 6,500 | 11 | 3 | 4,950 | 4,350 | 3,960 |
| **2.** | Uvuke | Kenyana | 12 | 11 | 23 | 41.5 | 7 | 23,850 | 22.5 | 3 | 6,250 | 16,900 | 4,190 |
| **3.** | Fikiria | Mwemage | 5 | 12 | 17 | 31.75 | 7 | 16,565 | 23.75 | 3 | 4,940 | 12,475 | 4,025 |
| **4.** | Tweyambe | Mwemage | 6 | 12 | 18 | 33.5 | 7 | 18,200 | 34.5 | 3 | 8,400 | 13,400 | 6,920 |
| **5.** | Chapakazi | Mwemage | 6 | 14 | 20 | 48 | 7 | 23,600 | 23.5 | 3 | 4,750 | 15,700 | 3,160 |
| **7.** | Boresha | Kenyana | 12 | 18 | 30 | 41 | 7 | 26,000 | 30.5 | 3 | 9,410 | 11,120 | 5,235 |
| **7.** | Shubira | Kenyana | 13 | 9 | 22 | 37.5 | 7 | 24,990 | 28 | 3 | 5,500 | 13,230 | 3,710 |
| **8.** | Abajunangani | Mwemage | 18 | 9 | 27 | 64.5 | 7 | 22,400 | 58 | 3 | 10,900 | 16,300 | 8,750 |
| **9.** | Jikwamue | Kenyana | 14 | 16 | 30 | 16.5 | 7 | 11,550 | 12 | 3 | 3,600 | 6,950 | 2,050 |
| **10.** | Jitihada 1 | Kenyana | 16 | 19 | 35 | 21.8 | 7 | 15,225 | 16.5 | 3 | 4,875 | 9,050 | 2,980 |
| **11.** | Jitihada 2 | Mwemage | 17 | 8 | 25 | 38 | 7 | 17,750 | 32.5 | 3 | 10,130 | 11,600 | 7,720 |
| **12.** | Mwangaza | Kenyana | 7 | 17 | 24 | 26.5 | 7 | 83,50 | 21 | 3 | 4,150 | 3,750 | 2,090 |
| **13.** | Nazareti | Kenyana | 3 | 4 | 7 | 7.5 | 7 | 4,200 | 6.5 | 3 | 1,100 | 2,850 | 740 |
| **14.** | Tegemeo | Mwemage | 14 | 6 | 20 | 30 | 7 | 39,900 | 30 | 3 | 11,050 | 34,200 | 9,250 |
| **15.** | Wajane | Bulembo | 0 | 12 | 12 | | 7 | | | 3 | | | |
| **16.** | Umoja | Bulembo | 9 | 7 | 16 | 10.5 | 7 | 1,950 | 10.25 | 3 | 600 | 1,100 | 260 |
| **17.** | Hekima | Bulembo | 6 | 8 | 14 | 9 | 7 | 8,500 | 5 | 3 | 1,460 | 5,660 | 815 |
| **18.** | Shamrashamra | Kenyana | 1 | 5 | 6 | 9.5 | 7 | 1,960 | 7.5 | 3 | 1,190 | 1,280 | 570 |
| **19.** | Sisimuka | Mwemage | | | 30 | 28.5 | 7 | 14,950 | 24.5 | 3 | 5,200 | 8,650 | 3,180 |
| **20.** | Juhudi | Mwemage | 11 | 8 | 19 | 26.5 | 7 | 10,900 | 19 | 3 | 5,000 | 7,070 | 3,840 |
| **21.** | Umoja Nguvu | Kenyana | 10 | 4 | 15 | 18.5 | 7 | 10,600 | 21 | 3 | 5,350 | 7,070 | 4,000 |
| **22.** | Furahisha | Kenyana | 4 | 7 | 11 | 16.5 | 7 | 4,360 | 14.5 | 3 | 3,960 | 1,560 | 2,750 |
| **23.** | Upendo | Mwemage | | | | | 7 | | | 3 | | | |
| **24.** | Abanabashome | Mwemage | 17 | 9 | 26 | 26 | 7 | 6,280 | 23 | 3 | 3,375 | 3,840 | 1,935 |
| **25.** | Majaribio | Mushasha | 4 | 8 | 12 | 8.5 | 7 | 960 | 7.5 | 3 | 410 | 470 | 220 |
| | **Jumla** | | **214** | **226** | **471** | **600** | | **311,190** | **483** | | **116,550** | **208,575** | **82,350** |

Kuendesha kongamano la wadau; Baada ya kuunda vikundi vya wakulima mkutano wa pamoja uliandaliwa kwa lengo la kuunganisha wadau mbalimbali kujadili mikakati ya kuwasaidia wakulima kupata soko la uhakika la mahindi na maharage na hivyo kuboresha kipato kutokana na kilimo. Mnamo tarehe 05/05/2016 MIVARF ilialiandaa mkutano wa pamoja wa wadau kwa lengo la kuunganisha wanufaika, wafanya biashara, wasambazaji wa pembejeo, taasisi za fedha, wawakilishi wa serikali na wadau wengine kujadili namna nzuri kwa wakulima wa Missenyi kupata soko la kuuza mahindi na maharage. Kikao kilijadili mambo ya fuatayo;

(i) Wakulima kutumia dawa za kuua magugu ili kupunguza gharama za palizi.

(ii) Kila kikundi kuanzisha huduma ya kuweka na kukopa na kuongeza akiba ambazo zitaongeza fedha kwa ajili ya mikopo baina yao.

(iii) Vikundi kujiunga na SACCOSS za Tumaini na Kyaka ili kupata mikopo kutokana na SACCOSS hizo kukidhi matakwa na hivyo kukopeshwa mtaji na benki ya CRDB.

(iv) Vikundi kuongeza uzalishaji ili kuhamasisha wanunuzi kununua kiwango kikubwa cha mazao katika eneo moja. Ni gharama kubwa kwa wanunuzi ikiwa watazunguka kununua mazao kidogo kidogo kutoka sehemu tofauti, hii inapelekea baadhi ya wanunuzi muda mwingine kufikiria kununua mahindi kutoka Tabora na maeneo mengine ambapo uzalishaji ni mkubwa hivyo kuweza kununua mzigo mkubwa sehemu moja.

Ziara ya mafunzo; Kupitia utekelezaji wa PEML kwenye Kata za Mushasha na Kilimile, ilidhihirika kwamba walengwa wa programu walihitaji kupata ujuzi na uzoefu wa masoko kutoka maeneo mengine. Kamati ya Mkoa ya MIVARF ilisisitiza ziara ya mafunzo kwa wazalishaji nje ya maeneo yao ili kujifunza na kupata uzoefu wa maeneo mengine kwa lengo la kuwasaidia wakulima kubadilisha mitazamo na kuongeza ufanisi. Vikundi ambavyo wajumbe wake walishiriki ziara ya mafunzo ni Jitihada, Sisimuka, Tegemeo, Subira, Wajane, Boresha, Jikwamue na Vijana sasa kazi. Ziara hii ilihusisha muwakilishi kutoka kwa mzabuni (GEODATA Consultant), Mwakilishi kutoka Halmashauri na Afisa Ugani wa Kata ya Mushasha. Wakulima walitembelea mashamba darasa ya mazao mbalimbali kama mahindi, mpunga, maharage, alizeti, na mboga mboga (Vitunguu, nyanya na karoti), ndizi, kahawa na viazi vitamu.

Halmashauri kwa kushirikiana na mzabuni iliwezesha wakulima kushiriki maonesho ya Nanenane kwa lengo la kujifunza mambo mazuri kwenye kilimo na masoko kutoka kwa wakulima wengine waliofanikiwa. Ziara ya maonesho ya Nanenane ilihusisha wakulima 15 chini ya mradi wa PEML kutoka Kata za Mushasha na Kilimilile kati yao wanawake 8 na wanaume 7. Vilevile, washiriki waliwezeshwa kushiriki maonesho mengine yaliyoandaliwa na Halmashauri za Mkoa wa Kagera na wadau wengine kama TANICA, Kiwanda cha Sukari cha Kagera, Wazalishaji wa chai Kagera, SIDO Kagera, TACRI, Magereza, ARI Maruku, Wolrd Vision Tanzania, Missenyi ADP na MAYAWA.

Maonesho maalum ya mazao; Halmashauri ya Missenyi kupitia maonesho ya Nanenane Mkoa wa Kagera iliandaa banda maalum kwa ajili ya kutangaza mazao ya vikundi vilivyopo chini ya MIVARF. Washiriki wawili chini ya PEML walishiriki maonyesho hayo ya Nanenane ambapo walionesha mahindi 1,239kg na maharage 410kg. 551kg za mahindi zilisagwa unga ambao uliuzwa TZS 1,000 kwa kilo. Mahindi mengine na maharage yaliyobaki yalifungashwa kwenye vifungashio vya kilo moja na kuuzwa kwa TZS 700 kwa mahindi na 1,300 kwa maharage. Wazalishaji waliweza kupata TZS 551,600 kutokana na kuuza 788kg za mahindi na TZS 533,000 kwa kuuza 410kg za maharage hivyo kufanya jumla ya TZS 1,084,600.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulihusisha rasilimali watu na rasilimali fedha. Raslimali watu ni pamoja na wataalamu wa Halmashauri na GEODATA Consultant Ltd ambao walitoa utaalam. Rasilimali fedha in TZS 18,000,000 zilitolewa kusaidia shughuli za usafirishaji, ziara za mafunzo, mafunzo kwa wakulima na ununuzi wa pembejeo za kilimo.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada hii umeleta matokeo mengi kama inavyofafanuliwa hapo chini.

Uzalishaji na uhakika wa chakula viliongezeka; Kutokana na malengo yaliyowekwa na wakulima kutoka vikundi 18, uzalishaji uliongezeka kufikia magunia 5,106,5 sawa na tani 511. Uzalishaji huu uliwafanya wakulima kutenga magunia 1,888 sawa na tani 190 kwa ajili ya chakula na ziada ya magunia 3,221,5

sawa na tani 321 kwa ajili ya kuuza ambapo yalihifadhiwa kwenye ghala la kikundi wakati wa kutafuta taarifa za soko na kuunganishwa na wanunuzi mbalimbali. Vikundi vyote 18 viliubaliana kuuza mazao yao kwa pamoja.

Kuanzishwa kwa soko la uhakika; GEODATA Consultant Ltd iliwaunganisha wakulima na taasisi ndogo za mikopo, iliwaandalia mpango wa biashara na mikakati ya soko na kuunganisha nguvu ya wakulima ili kuuza mazao kwa pamoja. Kabla ya mkakati huu wakulima walikua wakiuza mazao yao kupitia madalali na bei ilikua ndogo kiasi kwamba wafanyabiashara walinufaika zaidi kuliko wazalishaji. Baadhi ya wakulima walizoea kuuza mazao yao shambani kabla ya kuvuna na mnunuzi ndiye aliyepanga bei. Kutokana na kuundwa kwa mtandao, mfanyabiashara mmoja (mnunuzi wa mahindi, Wilbroad) alinunua kilo 45,360 kutoka vikundi 7. Bei ilikuwa TZS 416 kwa kilo. Kwa kuzingatia kwamba wastani wa gharama za uzalishaji ni TZS 295 kwa kilo, faida ilikuwa TZS 121 sawa na 41% kwa kila kilo moja. Wakulima mmoja mmoja na wale ambao hawakuwa wamejiunga na vikundi waliuza mazao yao kwa bei ndogo ya TZS 278 kwa kilo. Wakulima ambao waliuza kwa pamoja kwa wauzaji wa jumla waliuza mazao yao kwa bei ya TZS 461 kwa kilo. Bei ya soko ilikuwa TZS 450 kwa kilo hivyo wastani wa bei ulikuwa TZS 418 kwa kilo.

Kipato cha wakulima na vikundi kimeongezeka; Jumla ya tani 104 ziliuzwa na vikundi kutoka kwenye Kata mbili na kupata jumla ya TZS 42m na tani 188 za chakula zilitengwa.Wakulima kutoka kwenye Kata hizi mbili wameimarisha vipato vyao kupitia utekelezaji wa jitihada hii. Fidon Muta kutoka Kijiji cha Kenyana na Pancras Nazali kutoka Kijiji cha Mwemage walithibitisha kwa kusema “ *Tulikuwa na miradi mingi lakini mradi huu ni wa kipekee. Tulikuwa na mradi uliojihusisha na mbinu za kilimo. Lakini mradi huu unatupeleka mbali zaidi kutoka kulima hadi hatua ya mwisho ya kuuza. Vilevile kuna ufuatiliaji wa karibu wa vikundi vyetu ndani ya Kijiji. Sasa tunathibitisha mavuno ya uhakika ya jitihada zetu. Kabla ya mradi tuliuza gunia la mahindi la kilo 120 kati ya TZS 18,000 na TZS 30,000 ( shs 125-250/kg) lakini kipindi hiki tunauza kwa TZS 45,000. Sasa tunaona faida ya kuuza kwa pamoja na wanakijiji ambao hawapo kwenye vikundi wanatutamani. Tuna uhakika ndani ya kipindi cha miaka mitatu tutakuwa mbali katika kuimarisha vipato vyetu”.* Kutokana na uthibitisho wa faida ya kuuza kwa pamoja , vikundi vimehamasika kuweka nguvu ya pamoja katika misimu yote ya kilimo.

Taarifa za kikundi zinaonesha kwamba mahindi kwa ajili ya kuuza ni 104,060 kg sawa na magunia 1040.6 na kiasi kilichotengwa kwa ajili ya chakula ni 188,500kg sawa na 32% ya mavuno. Hivyo basi, vikundi vinapata ziada ya TZS 10,000,000 kwa kuuza kwa pamoja kutokana na kutumia mbinu za soko walizopata kwa usaidizi wa PEML. Kutokana na uzoefu wa PEML, vikundi saba kutoka Kata ya Kilimilile waliuza tani 40 za maharage kwa pamoja kwa wastani wa bei ya TZS 1,250 kwa kilo, wakati wakulima wengine waliuza kwa TZS 1000 kwa kilo.



***Umiliki  wa pikipiki kama moja ya mafanikio ya kuuza kwa pamoja***



***Kikundi cha Jitihada kikiuza mahindi kwa vipimo halisi***

Kuanzishwa kwa mbinu bora ya kuhifadhi mazao;  Magunia 200 bora ya uhifadhi mahindi (PICS) yalitolewa kwa vikundi. Magunia haya yana wastani wa 100kg hivyo yanasaidia kuondoa udanganyifu wa vipimo vya mazao. Magunia haya ni bora na yanasaidia kuhifadhi mazao jamii ya nafaka na mikunde kwa muda mrefu. Kipindi cha ziara ya Nanenane wakulima walifundishwa mbinu za kuhifadhi mazao kwa kutumia mfumo wa magunia haya na hivyo waliunganishwa na muuzaji ambaye alifahamika kwa jina la MAYAWA.

Kuunganisha wakulima na taasisi za fedha; Halmashauri iliunganisha vikundi 26 na taasisi za fedha  na vikundi vitatu (Jitihada, Jikwamue na Boresha) vimejiunga na SACCOS ya Kyaka ili kuweza kupata mikopo. Benki ya CRDB iliziwezesha SACCOS mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya  kuhudumia wateja wao.

Kuimarika kwa ushirikiano; kutokana na mafanikio makubwa kwenye uzalishaji na kipato, vikundi vimeongezeka kufikia 26. Ushiriki wa wanawake umeongezeka kwa  14%. Hali hii imeimarisha uzalishaji wa pamoja, usindikaji na uuzaji wa mazao ya kilimo. Matokeo mengine ni pamoja na;

(i) Kuongezeka kwa ushiriki katika shughuli za kujifunza kwa 31%

(ii) Vikundi 16 vimekamilisha uundaji wa mfumo wa soko la pamoja kama kutunga katiba na kujisajili

(iii) Halmashauri ikishirikiana na vikundi inatumia uzoefu uliopatikana kuunda mfumo wa soko la maharage.
(iv) Vikundi vinavyojihusiha na soko la pamoja vimeongezeka kutoka 14 hadi 20.
(v) Vikundi 15 vimeandaa shabaha za uzalishaji na uuzaji.
(vi) Vikundi 23 vimeandaa wasifu ili kuunganika na masoko hivyo kuvutia wadau wa kilimo na taasisi za fedha.
(vii) Vikundi 5 vimeunganishwa na kampuni ya MAYAWA ili kupata magunia bora ya kuhifadhia mazao.
(viii) Vikundi 9 vimeweka akiba kwenye SACCOSs. Vikundi hivi ni Juhudi, Jitihada (Kenyana), Tegemeo, Upendo, Vijana Sasa Kazi, Boresha, Jitihada (Mwemange) na Jikwamue.

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Halmashauri imedhamiria kuhakikisha matokeo ya jitihada hii yanakuwa endelevu kwa kujikita katika kuimarisha matokeo, kuendelea kusaidia wakulima, kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuwezesha vikundi, mafunzo, ziara za mafunzo, na kuhudhuria maonesho mbalimbali. Vilevile, kuimarisha ushirikiano na wadau, mzabuni, taasisi za fedha, Serikali Kuu na kuendelea kufanya tafiti kuhusiana na masoko.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

Mambo yaliyochangia kufanikiwa kwa jitihada hii ni pamoja na; mikutano ya wadau ambayo ilisaidia wakulima kufahamu vitendea kazi na fursa kama taasisi za fedha na masoko. Ziara za mafunzo zilibadilisha mtazamo wa wakulima juu ya uundaji wa programu hii, matokeo chanya na mbinu za ushirikishwaji. Kuanzishwa kwa eneo maalumu la kuuzia mazao kuliunganisha vikundi, soko na wanunuzi wa uhakika hivyo kuchochea wakulima kushiriki zaidi katika uzalishaji na soko la pamoja.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE

## KUBORESHA UZALISHAJI NA KUONGEZA THAMANI YA ZAO LA MUHOGO









*Uzoefu wa H/W ya Ukerewe*

Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Mwanza, inapatikana kati ya Latitudo $1^o45$ na $2^o15$ Kusini na Longitudo $32^o$ 45 na $33^o45$ Mashariki. Inapakana na Halmashauri za Wilaya za Magu kwa upande wa Kusini, Musoma (Mkoa wa Mara) kwa upande wa Kaskazini na Sengerema kwa Upande wa Mashariki. Halmashauri ya Ukerewe ni kisiwa kikubwa ndani ya Ziwa Viktoria ambacho kipo umbali wa 54km kutoka Jiji la Mwanza. Halmashauri ya Ukerewe inaundwa na visiwa 38 ambapo visiwa 15 hutumika kwa makazi ya kudumu na visiwa vingine vilivyobaki hutumiwa kwa msimu hasa shughuli za uvuvi wa samaki. Halmshauri ina eneo la 6,400km$^2$ ambapo 5,760km$^2$ zimefunikwa na maji ya Ziwa Viktoria. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 4, Kata 25 na Vijiji 76.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, idadi ya watu kwa Halmashauri ya Ukerewe ni 260,831 kati yao; 128,842 ni wanaume na 131,989 wanawake. Ongezeko la watu linakadiriwa kuwa 2.9% zaidi ya wastani wa kitaifa ambao ni 2.6%. Katika sensa ya mwaka 2012 idadi ya watu imeongezeka kufikia 345,147 hivyo kusababisha kufikia ujazo wa watu zaidi ya 500 kwa 1km$^2$. Ongezeko la idadi ya watu umeleta uhitaji mkubwa wa ardhi hivyo kuongeza changamoto katika usimamizi wa ardhi, uzalishaji, uharibifu na umasikini uliosababisha kuvamiwa maeneo tengefu ya ardhi.

Kijografia, Halmashauri ina milima midogo midogo, mabonde, tambarare na mito midogo ya msimu (ni mito ya msimu kutokana na uharibifu wa mazingira; hapo awali ilikuwa mito ya kudumu). Halmashauri ina kanda mbili za kiikolojia; ukanda wa Mashariki una mvua za wastani, udongo mweusi wa mfinyanzi, milima ina mimea aina ya miombo kama vile *Cumbretum spp* na tambarare kuna iana ya migunga (*Acacia spp)*. Ukanda wa Magharibi una mvua nyingi kuliko ukanda wa Mashariki; sehemu ya milima imestawisha kwa wingi miti aina ya Mivule(*Melicia excelsa ),* miti mingine ni kama *Maesopsis Emenii, Albizia sp* na Mtalawanda *(Markhamia sp)*. Ukerewe ni eneo la milima ambalo lilikuwa na misitu minene ya kiikweta. Kutokana na ongezeko kubwa la watu na shughuli za kuchumi, Halmashauri imebakiwa na misitu michache iliyohifadhiwa ambayo inamilikiwa na Serikali Kuu na Halmashauri. Misitu hiyo ipo katika eneo la mlimani kwenye ukanda wa Magharibi.

Shughuli kuu za kiuchumi ni pamoja na kilimo, uvuvi, biashara na uvunaji wa mbao kutoka misitu ya Rubya na mashamba ya miti ya watu binafsi. 92% ya wananchi hutegemea kilimo na mazao yanayozalishwa ni muhogo, viazi na mpunga; mazao haya ni ya chakula na biashara. Aina mbalimbali za matunda huzalishwa zikiongozwa na uzalishaji wa machungwa. Miaka ya nyuma H/W ya Ukerewe ilikuwa ikisafirisha mazao ya chakula kwenda Wilaya jirani kama Bunda, Magu, Musoma na Mwanza; hata hivyo hali ilibadilika kufikia hatua ya Halmashauri kutegemea chakula kutoka nje ya Wilaya. Hali hii ilichangiwa na ongezeko la watu na usimamizi mbovu wa mazingira uliosababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao. Kwa sasa mazao pekee yanayozalishwa na kuuzwa nje ya Halmashauri ni matunda, samaki na mbao.

Hali ya hewa inaruhusu uzalishaji wa muhogo ambalo ni zao kuu la chakula na biashara kwa H/W ya Ukerewe. Kwa wastani 14,000ha huzalisha muhogo kila mwaka na mavuno yanakadiriwa kuwa kati ya tani 2.4 hadi 2.9 kwa kila hekta. Mwaka 2005, Halmashauri ilibaini kuwepo kwa ugonjwa wa muhogo ambao kitaalamu unafahamika kama *Casava Brown Streak virus (CBSD)*. Aina ya muhogo wa asili uliathirika zaidi na ugonjwa huu. Hali hii ililazimu Halmashauri kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo – Ukiriguru na washirika wengine wa maendeleo kuanzisha aina ya muhogo ambayo ni himilifu kwa CBSD na aina nyingine ya ugonjwa ijulikanoyo kama *Cassava Mosaic Virus diseases (CMD).* Kuanzishwa kwa aina hii ya muhogo kulilenga kuongeza uzalishaji kupitia tafiti, kuzalisha na kusambaza aina bora ya mbegu ya muhogo iliothibitishwa kuhimili magonjwa. Jumla ya aina 425 za muhogo ilifanyiwa majaribio; aina 3 tu za mihogo ambazo ni Mkombozi, Nigeria, na Kashura-mpya zilithibitika

kuwa himilifu kwa magonjwa. Hata hivyo, aina mbili ambazo ni Kashura-mpya na Nigeria zilithibitika kutohimili magonjwa baada ya miaka 3 hivyo mbegu pekee iliyodhihirika kuwa bora ni Mkombozi.

## 2.0 TATIZO

Kabla ya mwaka 1970 uzalishaji wa muhogo ulikuwa mkubwa kati ya tani 2.9 kwa ekari na wakulima wengi walitumia kilimo cha kubadili mazao kila msimu. Aina hii ya kilimo ilichangia kuhifadhi rutuba ya udongo. Miaka ya 1990 wakulima walianza kubaini kupungua kwa uzalishaji. Hali ilikuwa mbaya zaidi kuanzia mwaka 2005 kutokana na kupungua kwa rutuba ya udongo na kuongezeka kwa magonjwa ya muhogo yaliyoathiri uzalishaji. Katika baadhi ya maeneo wakulima walipata hasara ya takriban 85% ya mavuno yaliyotarajiwa, hivyo kusababisha upungufu wa chakula na wakulima kushindwa kumudu gharama za chakula kwa mwaka. Licha ya uzalishaji duni, usindikaji wa muhogo ulikuwa duni kutokana na teknolojia isiyofaa .

### 3.0 MALENGO

Lengo kuu la H/W ya Ukerewe lilikuwa kusaidi kuongeza thamani kwenye zao la muhogo kwa kutatua changamoto katika uzalishaji, uchakataji na masoko ili kuboresha hali ya maisha ya wakulima kwa kuinua kipato na kuwa na uhakika wa chakula katika kaya. Malengo mahususi ni pamoja na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu bora zinazostahimili magonjwa na matumizi ya mbinu bora za kilimo, kujenga uwezo wa vikundi vilivyochaguliwa kuhusu uandaaji wa muhogo baada ya kuvunwa na kuongeza thamani kwa kuchakata na kufungasha vema. Aidha, Halmashauri ililenga kuanzisha vituo vya masoko na mfumo wa taarifa masoko ya muhogo.

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

H/W ya Ukerewe na Washirika wa Maendeleo walitekeleza jitihada mbalimbali kuboresha na kulinda uzalishaji wa muhogo. Mikakati iliyotumiwa na Halmashauri na jamii imeelezwa hapa chini.

Mkakati wa utafiti; Mwaka 2009-2010, H/W ya Ukerewe na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo kanda ya Ziwa - Ukiriguru ilifanya utafiti ndani ya Ukerewe juu ya aina mbali mbali za muhogo. Aina 425 zilibainishwa na kufanyiwa majaribio lakini ni aina 3 tu; Mkombozi, Kashura-mpya na Nigeria zilithibitika kuhimili ugonjwa wa CBSD. Hatahivyo, wakati wa uzalishaji ilibainika ni aina ya Mkombozi pekee inayostahimili magonjwa ikilinganishwa na Kashura-mpya na Nigeria.

Uundaji wa Vikundi; katika kurahisiha uzalishaji wa muhogo, Halmashauri ilihamasisha wakulima kujiunga kwenye vikundi ili kurahisisha usaidizi na usimamizi. Wakulima walijengewa uwezo kupitia mikutano. Jamii iliridhia na kuunda vikundi vilivyoanzisha mashamba ya mihogo yenye ukubwa tofauti; Jipe moyo – Gallu (hekta 5), Inuka – Bugorola (hekta 4), Songambele – Bukiko (hekta1), Umoja MUVI – Kameya (hekta5), Bure Garden – Mukunu (Hekta5) and Mpango na kazi – Hamuyebe (hekta4).

Usaji wa vikundi; Ili kuwa na vikundi ambayo vinatambulika rasmi, Halmashauri ilihamasisha vikundi kujisajili. Usajili uliviwezesha vikundi kutekeleza shughuli zao katika mazingira rasmi na kuweza kushirikiana na mamlaka nyingine. Kikundi cha Bure Garden kilisajiliwa na Halmashauri na kupewa namba ya usajili B.G. G./CBO/UK2 ya tarehe 13/10/2005 na baadae walisajiliwa na BRELA kwa namba ya usajili 270408 ya tarehe 29/08/2013.

Utoaji wa mafuzo ya awali kwa wajumbe wa vikundi; Halimashauri ikishirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kanda ya Ziwa iliandaa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mbegu bora za mihogo. Mafunzo ya nadharia na vitendo yalitolewa kwa wajumbe wa vikundi pamoja na wanakijiji waliovutiwa na uzalishaji

wa muhogo ulioboreshwa. Baadhi ya wajumbe wa vikundi walijiendeleza zaidi na mafunzo kuhusu kubaini magonjwa na namna ya kuzuia kusambaa kwa magonjwa.

Uzalishaji wa mbegu za muhogo aina ya Mkombozi; Mkombozi ndio aina pekee iliyothibitika kuhimili magonjwa. Kutokana na uhitaji wa mbegu za muhogo ambazo ni himilifu kwa magonjwa , Halmashauri ilijenga uwezo na kusambaza mbegu kwa vikundi. Aidha Halmashauri ilihamasisha aina hii ya muhogo kwa baadhi ya vijiji kwa lengo la kupata vikundi imara vinavyojishughulisha na shughuli za kilimo ili kujikita katika uzalishaji wa muhogo aina ya Mkombozi.

Kuimarisha Uchakataji wa Muhogo; Halmashauri na Washirika wa Maendeleo walitoa usaidizi kwa vikundi mbalimbali kwa kuwanunulia mashine za uchakataji, vitendea kazi na vifaa vya kuongeza thamani kwenye zao la muhogo. Vikundi vilisaidiwa mashine za uchakataji ili kuzalisha muhogo bora wa kibiashara. Vifaa vya uchakataji na usindikaji vilisimikwa. Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya mashine za uchakataji zilizonunuliwa na Halmashauri.



***Mashine ya kusaga muhogo***



***mashine ya kusigina muhogo***

**5.0 RASILIMALI**

Halmashauri kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Kanda ya Ziwa na wakulima ilitumia rasilimali mbalimbali katika kufikia matokeo ya jitihada hii kama inavyofafanuliwa hapa chini.

Rasilimali fedha; washirika wa maendeleo na wajumbe wa vikundi walichangia fedha katika kuimarisha uzalishaji wa muhogo. Jedwali Na. 1 linaonesha rasilimali fedha zilizotumiwa na wadau mbalimbali katika utekelezaji.

**Jedwali Na 1 Rasilimali Fedha**

| S/N | Shughuli iliyotekelezwa | Mwaka | Chanzo cha fedha | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ununuzi wa shamba la ekari 5 kwa ajili ya uzalishaji wa muhogo | 2010 | Kikundi cha Bure Garden | 13,000,000 |
| 2. | Ununuzi wa Power tiller | 2012 | Kikundi cha Bure Garden | 1,600,000 |
| 3. | Uchimbaji wa Kisima | 2008 | Ubalozi wa Marekani (DSM) | 4,994,000 |
| 4. | Ununuzi wa tangi la maji @2000L | 2008 | Ubalozi wa Marekani (DSM) | 800,000 |
| 5. | Ununuzi wa machine ya usindikaji muhogo (cassava grater) | 2011 | MUVI SIDO-Mwanza | 3,500,000 |
| 6. | Ununuzi wa Power Tiller | 2012 | Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe-DASIP | 6,400,000 |
| 7. | Kuandaa Shamba | | Wakulima | 48,000 |
| 8. | Ulimaji wa shamba | | Wakulima | 150,000 |
| 9. | Upandaji, upaliliaji na uvunaji, | | Wakulima | 190,000 |
| 10. | Usafirishaji na usindikaji | | Wakulima | 130,000 |
| Jumla ya gharama za uzalishaji na Usindikaji | | | | **30,812,000** |

Rasilimali watu; wanachama wa kikundi walihusika katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uzalishaji wa muhogo na uongezaji wa thamani ambazo ni uzalishaji wa muhogo, ujenzi wa ofisi na usimikaji wa mashine za kuchakata muhogo.

**6.0 MATOKEO**
Kutokana na mafunzo, ujuzi na uelewa wa wakulima kuhusu uzalishaji wa muhogo ulioboreshwa na uongezaji wa thamani umeongezeka. Uzalishaji wa muhogo kwa ekari umeongezeka kama inavyoonekana kwenye jedwali Na 2.

**Jedwali Na 2. Uzalishaji wa muhogo kikundi cha Bure Garden na faida 2011-2013**

| S/N | Mwaka | Eneo(Ha) | Uzalishaji (tani) | Gharama za uzalishaji (TZS) | Mauzo(TZS) | Faida(TZS) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 2010/2011 | 12.0 | 23.8 | 6,216,000 | 11,020,000 | 4,804,000 |
| 2. | 2011/2012 | 32.4 | 64.5 | 16,783,200 | 37,089,000 | 20,305,800 |
| 3. | 2012/2013 | 75.2 | 218 | 38,953,600 | 91,593,600 | 52,640,000 |

Ujenzi wa ofisi; Kikundi cha Bure kimeweza kujenga ofisi, choo, na jengo la kuchakata muhogo. Kikundi kilitumia fedha zilizopatikana kutokana na uuzaji wa unga wa muhogo kununua vifaa vya ujenzi. Hitaji la ofisi lilitokana na ukosefu wa sehemu ya kukutana na kufanya mkutano. Awali iliwalazimu kukutana chini ya mti wa mwembe. Aidha, kikundi hakikuwa na sehemu maalumu ya kutunza nyaraka na taarifa. Picha zifuatazo zinaonesha mti wa mwembe na ofisi mpya.



*Mti wa mwembe*




*ofisi mpya*





*Ofisi ya kikundi cha Bure garden*

Mbinu bora za uchakataji wa muhogo zimekubalika na kutumiwa na wazalishaji; kutokana na mbinu bora za uchakataji wa muhogo thamani ya muhogo imeongezaka. Awali wakulima walitumia mbinu za

kuanika muhogo juu ya mawe mazingira yaliyosababisha muhogo kuchafuka na kupata bakteria na sumukuvu. Wakulima wameboresha mbinu za kuchakata muhogo kwa kutumia vifaa safi na salama vya ukaushaji. Ubora wa unga wa muhogo umeongezeka hivyo kuvutia wateja wengi zaidi.

Kukubalika kwa tekinolojia mpya ya uzalishaji wa muhogo; wakulima wengi wamebadilika na kukubali kuachana na kilimo cha mazoea badala yake wanazalisha aina ya muhogo inayostahimili magonjwa. Vilevile, ufahamu wa wakulima kubaini magonjwa ya mihogo umeimarika hivyo huchukua tahadhari mapema kuzuia kusambaa kwa ugonjwa pale unapobainika.

Kuanzishwa kwa mashamba ya mbegu za muhogo; mashamba nane ya kuzalisha mbegu bora za muhogo yameanzishwa na yanatumika kama mashamba darasa na uzalishaji wa mbegu za mihogo iliyoboreshwa. Kupitia mashamba darasa wakulima wanaweza kujifunza uzalishaji bora wa muhogo. Picha ifuatayo inaonesha moja ya shamba darasa na uzalishaji wa mbegu.



***Shamba la mbegu za muhogo***

Kuongezeka kwa dhamani ya bidhaa za muhogo sokoni; mbali na uboreshaji wa uzalishaji wa muhogo, uvunaji na uchakataji wa muhogo, Halmashauri imewaunganisha wakulima na soko ili kuhakikisha muhogo wote unaozalishwa unapata soko. Mahitaji ya unga wa muhogo ni makubwa hivyo Halmashauri ilitoa usaidizi wa vifaa vya kuandaa unga safi wa muhogo kuvutia walaji na hatimaye kukuza soko. Picha ifuatayo inaonesha kiwanda cha uchakataji na ufungashaji wa unga wa muhogo kinachomilikiwa na kikundi cha Bure Garden.




***Kiwanda cha kuchakata muhogo (Nyumba ya mashine, stoo na chumba cha kubadilishia nguo)***

Kikundi cha Bure Garden kiliingia mkataba na wanunuzi wanne wa bidhaa za muhogo baada ya kuboresha uzalishaji; hii imewezesha kikundi kuwa na soko la uhakika. Mkataba umebainisha kiwango cha unga wa muhogo ambacho wanapaswa kupeleka kwa wateja kila mwezi. Jedwali Na.3 linaonesha wanunuzi na kiwango cha mahitaji ya unga wa muhogo.


***Jedwali Na.3 Mahitaji ya unga wa muhogo***


| S/n | Mahali | Mifuko ya kg 5 |
|---|---|---|
| 1 | Kisiwa cha Ghana | 200-300 |
| 2 | Mji mdogo wa Nansio | 100 |
| 3 | Kisiwa cha Ukara | 25-30 |
| 4 | Kituo cha biashara Muriti | 15-20 |

Kuimarika kwa ubora wa unga wamuhogo na vifungashio; vifungashio vina utambulisho wa jina la kikundi kinachozalisha hivyo in rahisi kutangaza bidhaa. Kutokana na kuboreshwa kwa uchakataji na vifungashio, wakulima wamepatiwa cheti cha kutambuliwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) kama wazalishaji wa bidhaa bora. Picha zifuatazo zinaonesha unga wa muhogo kwenye vifungashio vyenje jina la utambulisho wa kikundi pamoja na cheti cha uthibitisho cha TFDA.




***Ungo wa muhogo***







***Vyeti vya uthibitisho wa TFDA***

Bidhaa mbalimbali za muhogo huzalishwa; mbali na uzalishaji wa unga, kikundi pia kinajishughulisha na uzalishaji wa bidhaa nyingine kama tambi na keki za muhogo ambazo huuzwa na kuongeza kipato cha wanachama. Picha zifuatazo zinaonesha aina ya bidha zinaozalishwa kutokana na muhogo.




***Unga na Tambi za Muhogo***

Kuongezeka kwa kipato cha wanachama kumetokana na mauzo ya unga wa muhogo na bidhaa zingine zitokanazo na muhogo. Kutokana na kuongezeka kwa kipato wanachama wameweza kugharamia baadhi ya huduma za msingi ambazo walishindwa hapo awali. Baadhi ya wakulima wanaendelea na ujenzi wa nyumba bora na wengine wamepata mitaji ya kundesha biashara nyingine kutokana na uuzaji wa bidhaa za muhogo.

Afya za wakulima zimeimarika kutokana na kutumia bidhaa za muhogo. Kwa kawaida muhogo una virutubisho vya kutosha na ni moja ya chakula ambacho kina wanga na protini ya kutosha kuliko vyakula vingine vya mizizi kama magimbi na viazi. Majani ya mihogo hutumika kama mboga (Kisamvu) ambayo yana virutubisho na vitamin A&K kwa wingi ambayo ni muhimu katika kuimarisha seli za mwili, kusaidia kufunga kwa damu endapo mtu ameumia na kuimarisha mifupa. Vilevile muhogo una vitamini B na madini ya potasiamu ambayo ni muhimu katika kuzalisha seli za mwili na kumarisha mapigo ya moyo.

Kutokana na kupata uzoefu wa kutosha katika uzalishaji wa muhogo, uzoefu huu umetumika kuboresha uzalishaji wa mazao mengine. Kikundi cha Bure Garden wameanzisha uzalishaji na uchakataji wa alizeti kama zao jingine la kiuchumi kwa lengo la kupanua wigo wa kujiongezea kipato. Kikundi kimenunua mashine ya uchakataji wa alizeti kwa jumla ya TZS 2,600,000 na kuanzisha kiwanda cha kusindika mafuta ya alizeti. Jitihada hii imeongeza fursa za ajira katika uzalishaji na uchakataji wa muhogo na alizeti. Kikundi kimeajiri watu 3 wanafanya kazi ya kutunza kitalu cha miche ya miti, kufanya kazi za ofisi ya kikundi pamoja na ulinzi. Picha ifuatayo inaonesha kiwanda cha kusindika alizeti.



***Mashine za kukamua alizeti***

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Katika kuhakikisha uendelevu wa jitihada hii, Halmashauri na wakulima wamejiwekea mikakati mbalimabali ya uendelevu. Mikakati hii ni pamoja na kuendelea kusaidia kuzalisha mbegu bora za muhogo ambazo zinastawi na kuzaa vizuri katika eneo la Ukerewe. Halmashauri inaendelea kusimamia na kutoa huduma za ushauri wa uwekezaji wa kikundi. Ushauri huu utawezesha wanachama wa kikundi kutekeleza majukumu vyema na kwa kujiamini.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

Maafanikio ya jitihada hii yanatokana na ushirikiano uliojengeka baina ya wadau ambao walitoa utaalamu, vitendea kazi na fedha, (Halmashauri,MUVI, CAVA, Taasisi ya utafiti wa kilimo ya kanda ya ziwa, TFDA naTBS). Wadau hawa walisaidia katika kutoa utaalamu na vitendea kazi katika kuhakikisha ubora wa muhogo. Maamuzi shirikishi ni sababu nyingine ya mafanikio; masuala yote kuhusu vikundi yaliamuliwa kwa njia shirikishi kwa kuhusisha wanachama katika kutoa maoni yao na kuamua.

Ushirikiano wa karibu baina ya Halmashauri na vikundi vya uzalishaji; wakati wote kumekuwepo na mawasiliano ya pande zote mbili (vikundi na Halmashauri) ili kupata usaidizi pale unapohitajika. Kuwepo kwa visiwa vingi ambavyo vinahitaji bidhaa za muhogo kumechangia kuongezeka kwa uzalishaji. Uwezo wa viongozi wa kikundi katika kushawishi na kuunguanisha jamii kwenye vikundi na kuanza uzalishaji wa pamoja ni siri nyingine ya mafanikio.

Kupanuka kwa wigo wa matumizi ya bidhaa za unga wa muhogo katika kisiwa cha Ukerewe kumechochea ari ya wakulima kuongeza uzalishaji wa muhogo. Soko la uhakika la mazao ya muhogo limeimarika kutokana na uhitaji mkubwa wa unga wa muhogo kwa ajili ya kutengenezea bidhaa mbalimbali ambazo zina ushindani na bidhaa nyingine kwenye soko.




***Bango linaloonesha shughuli mbalimbali za kikundi***

Utayari wa wanachama wa kikundi cha Bure Garden na dhana ya umiliki iliyojengeka ndani yao huwafana wawe tayari kushiriki shughuli za kikundi mara kwa mara. Uongozi thabiti wa kikundi umechochea kuimarika kwa kikundi na ufanisi. Vilevile kikundi kimepanua wigo wa shughuli za kiuchumi kutoka uzalishaji wa muhogo hadi kuzalisha alizeti, miche ya miti na sabuni kwa lengo la ujiongezea kipato. Kutokana na shughuli hizi, kikundi kimezidi kuimarika.



***Kitalu cha miti, mashine ya kukamua alizeti na utengenezaji wa sabuni***

# HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA

**UKUZAJI WA KILIMO HIFADHI KWA UHAKIKA WA CHAKULA**




***Uzoefu H/W ya Itilima***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ni moja ya Halmashauri 6 za Mkoa wa Simiyu iliyoanzishwa mwaka 2012 ikitokana na mgawanyo wa Halmashauri za Wilaya za Bariadi na Maswa. Halmashauri inapakana na H/W za Busega upande wa magharibi, Bariadi upande wa Kaskazini, Meatu na Maswa upande wa Kusini na Ngorongoro (Mkoani Arusha) upande wa Mashariki. Kijiografia, Halmashauri inapatikana katika Latitudo $3^0$44’ Kusini na Longitudo $33^0$29’ Mashariki. Halmashauri ina eneo la 2,647.7km$^2$ ambalo 1,938.70km$^2$ ni ardhi inayofaa kwa kilimo na ufugaji, 640km$^2$ ni pori tengefu la Maswa na sehemu iliyobaki, 69km$^2$ ni mito midogo, vichaka na vilima.

Kiutawala, H/W ya Itilima imegawanyika katika Tarafa 4 yaani Kanadi, Bumera, Itilima and Kinang’weli, Kata 22, Vijiji 102, Vitongoji 581 na kaya 43,597. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ilikuwa na wakazi 313,900; 165,398 wakiwa wanawake na 148,502 wanaume. Wastani wa wakazi katika kaya ni 7.2 na ongezeko la watu la 1.8%.




***Ramani ya H/W ya Itilima na Mkoa wa Simiyu***

Shughuli kuu za kiuchumi za H/W ya Itilima ni uzalishaji wa mazao na ufugaji unaohusisha zaidi ya 80% ya wakazi. Kilimo cha kujikimu ndio mfumo mkuu ambapo mahindi ndio zao kuu la chakula na mazao mengine ni uwele, mpunga, viazi vitamu, mhogo, maharage, maharage ya kijani na njegere. Mazao ya biashara ni pamba, alizeti na dengu. Ufugaji ni shughuli kuu ya pili ya kiuchumi inayochangia kwa kiasi kikubwa kwenye uchumi wa Halmashauri.

**2.0 TATIZO**

Kijiji cha Kabale ni mojawapo ya Vijiji vya Kata ya Zaguyu. Uchumi wa Kijiji unategemea kilimo. Wakulima wengi hujihusisha na kilimo cha kujikimu ambacho hutegemea mvua. Kabla ya mwaka 2010 wananchi waliathirika na uzalishaji mdogo wa wastani wa gunia 5 hadi 8 kwa ekari ukilinganisha na uzalishaji wenye tija wa gunia 25 hadi 30 kwa ekari. Sababu kubwa iliyochangia kupungua kwa uzalishaji ni teknolojia duni ya kilimo, kupungua kwa rutuba, ukame na mmomonyoko wa udongo.

Kilimo cha mazoea kilichohusisha uchomaji moto wa mashamba na uondoaji wa masalia ya mazao shambani kilisababisha kuongezeka kwa tatizo. Matumizi ya njia hii yanaweza kuwa rahisi lakini kwa upande mwingine yanasababisha uharibifu wa mazingira kutokana na kuacha ardhi bila mimea hivyo kuchangia kuchochea mmomonyoko na kupungua kwa rutuba katika udongo. Matumizi ya moto huchangia uharibifu wa miti na misitu ambayo ingetumika kutunza mazingira na kuleta mvua. Sababu nyingine iliyochangia uzalishaji duni ni mvua zisizo za uhakika kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Kabla ya mwaka 2005 wastani wa mvua ulikuwa kati ya 700mm – 800mm kwa mwaka. Hata hivyo miaka ya karibuni wastani wa mvua umeshuka hadi chini ya 700mm kwa mwaka. Wakulima walikuwa na mazoea ya kuchunga mifugo yao kwenye mashamba; ni desturi kwa wakulima wengi Tanzania kuchunga mifugo kwenye mashamba baada ya kuvuna kama njia ya kusafisha mashamba. Desturi hii si nzuri kwani huacha ardhi wazi na kusababisha mmonyoko wa udongo ambao huondoa tabaka la juu lenye rutuba. Rutuba iliendelea kupungua kutokana matumizi mabaya ya mbolea za viwandani, zana duni za kilimo kama jembe la mkono na mbegu zisizo bora hivyo kukosekana tija katika uzalishaji. Kutokana sababu hizi, kaya zilikabiliwa na upungufu wa chakula na kipato; hivyo kushindwa kugharamia huduma na mahitaji ya msingi.

**3.0 LENGO**

Kilimo hifadhi ni matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kilimo inayoboresha uzalishaji, kulinda rasilimali za ardhi na kuhifadhi mazingira. Aina hii ya kilimo inahimiza kutifua tu sehemu ya kuotesha mmea na kuhifadhi sehemu nyingine ya ardhi. H/W ya Itilima ilitekeleza jitihada hii kwa lengo la kuleta uhakikisha wa chakula katika kaya na kuboresha maisha ya wakulima. Malengo mahsusi ni pamoja na kuwasaidia wakulima kutumia mbinu bora za kilimo ambazo zinaongeza uzalishaji, kuwawezesha wakulima kujihusisha na kilimo kinachotunza mazingira, kuwezesha wakulima kutumia teknolojia ambayo itapunguza gharama za uzalishaji hivyo kuongeza tija.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kilimo hifadhi kilianzishwa kama mbadala wa kilimo cha mazoea ambacho kilileta uharibifu wa udongo na kupunguza uzalishaji. Mbinu zinazotumika katika kilimo hifadhi ni pamoja na matumizi ya eneo dogo la ardhi kwani utifuaji hufanyika kwa mistari pale tu ambapo mimea huoteshwa na sehemu nyingine huachwa bila kutifuliwa. Kadhalika, kilimo hifadhi kinajumuisha kilimo mseto, kilimo cha mzunguko na matumizi sahihi ya pembejeo. Kilimo hiki ni rahisi na sio cha gharama kubwa; huhitaji muda mfupi wa utekelezaji na pemebejeo kidogo tofauti na aina nyingine za kilimo zenye gharama kubwa. Katika maeneo mengi duniani, Kilimo Hifadhi kimekuwa kikitumika na wakulima wengi. Kilimo hiki kimekuwa kikitumika zaidi kusini mwa bara la Amerika Kusini. Hapa nchini, Kilimo hifadhi kilianzishwa katika wilaya chache ikiwemo Itilima kwa lengo la kuongeza uzalishaji. H/W ya Itilima ilianzisha aina hii ya kilimo mwaka 2010. Katika utekelezaji wa jitihada hii, Halmashauri kwa kushirikiana na wadau ilitekeleza mikakati iliyochambuliwa hapa chini.

Kujenga uelewa kuhusu kilimo hifadhi; kushirikiana na Tanzania Gatsby Trust (TGT) Halmashauri ilitoa usaidizi kwa wakulima kuhudhuria mafunzo kwa lengo la kuwajengea uelewa kuhusu na kilimo hifadhi. Mwaka 2012 Halmashauri iliwaunganisha wakulima katika vikundi na kuteua wajumbe 60 ambao walipatiwa fursa ya kuhudhuria mafunzo yaliyofanyika mjini Moshi. Katika mafunzo haya wakulima waliwezeshwa kuelewa na kuhimizwa kutumia kilimo hifadhi ambacho kinatumia eneo dogo la ardhi na kupata mavuno ya kutosha. Baada ya kurejea washiriki waliofanya vizuri zaidi walichaguliwa na kutambuliwa kama wawezeshaji wa kueneza ujuzi, maarifa na uzoefu kwenye ngazi za kaya.

Kuendesha mikutano ya uhamasishaji; mkulima kiongozi (Bw. Emanuel Mahangila) aliendesha mikutano ya uhamasishaji na kuwafahamisha wakulima kuhusu kilimo hifadhi. Aliezea kwa wakulima wenzake faida za kilimo hifadhi na namna ambavyo mkulima anaweza kutumia eneo dogo la ardhi na kuvuna kwa wingi. Ufafanuzi ulitolewa kuhusu kutotifua eneo lote la shamba badala yake kutifua eneo lile tu ambalo mmea huoteshwa. Aina hii ya kilimo hutunza unyevu na udongo hata pale ambapo mvua itapungua au kutoweka kwa muda mmea huendelea kustawi. Uendeshaji wa mikutano ya uhamasishaji ulishirikisha wataalamu kutoka TGT pamoja na Halmashauri. Picha ifuatayo inaonesha shamba la mfano la utekelezaji wa kilimo hifadhi.



***Shamba la mfano***

Utoaji wa Mafunzo kuhusu Kilimo Hifadhi; mafunzo kwa vitendo yaliandaliwa na TGT na Halmashauri baada ya wakulima kujiunga kwenye vikundi. Wakulima walifundishwa namna ya kuandaa mashamba kwa kutumia trekta, plau na jembe la mkono. Mafunzo haya yalijumuisha kupanda kwa nafasi kulingana na aina ya zao linalopandwa. Picha zifuatazo zinainesha mafunzo kwa vitendo.





***Mafunzo juu ya namna ya kutumia zana za kilimo***

Kuanzisha mashamba darasa; katika kuhakikisha ufanisi wa mafunzo, mashamba darasa yalianzishwa. Halimashauri kwa kushirikiana na TGT ilihimiza wananchi kuanzisha mashamba darasa. Jitihada ya kuanzisha mashamba darasa ilifanyika katika vijiji vyote 102 (kila Kijiji shamba darasa moja). Vijiji vya Kabale, Zanzui, Chinamili, Lagangabilili, Ngeme na Mwalushu vilifanya vizuri zaidi katika uanzishaji wa mashamba darasa. Mashamba darasa ya vijiji yalianzishwa kwa lengo la kuwapa wakulima fursa ya kujifunza kilimo hifadhi kwa njia ya vitendo ili kutumia ujuzi huo kwenye mashamba yao. Picha ifuatayo inaonesha wakulima wakishiriki katika uanzishaji wa shamba darasa.


Wakulima wakiandaa plau


Mafunzo kwa vitendo

**5.0 RASILIMALI**

Halmashauri ikishirikiana na TGT ilitumia rasilimali mbalimbali kama fedha, watu na vitendea kazi kama inavyofafanuliwa hapa chini.

(i) Rasilimali watu; wataalamu Halmashauri na maafisa wa TGT ambao waliunda timu ya usaidizi kipindi chote cha utekelezaji wa jitihada hii. Majukumu ya timu hii yalikuwa, kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uandaaji wa mashamba, matumizi ya pembejeo na zana za kilimo.

(ii) Vitendea kazi; utekelezaji ulitumia vitendea kazi kama magari, pikipiki, pembejeo na zana za kilimo.

(iii) Rasilimali fedha; fedha zilitumika kugharamia mafuta, posho na kuendesha mafunzo na zilitolewa na TGT, Halmashauri na Jamii. TGT ilitoa TZS 22,000,000, Halmashauri TZS 2,500,000 na jamii TZS 1,500,000 ambapo jumla ya fedha zote ni TZS 26,000,000.

**6.0 MATOKEO**

Kilimo hifadhi kinalenga kuleta faida kwa mkulima na mazingira. Aina hii ya kilimo inasaidia uzalishaji wenye tija kwa kutumia ardhi, nguvukazi, maji na pembejeo kidogo. Kadhalika, kilimo hiki hulenga katika kuhifadhi na kutunza rasilimali za kibaolojia katika kilimo. Kutokana na faida za kilimo hifadhi, Nchi nyingi duniani zinatumia aina hii ya kilimo. Faida zake zimetambuliwa na wakulima, watafiti na maafisa ugani. Utekelezaji wa kilimo hifadhi kwa H/W ya Itilima umeleta matokeo chanya kama inavyo fafanuliwa hapa chini.

Kikundi cha wakulima 60 kimeanzishwa katika Kijiji cha Kabale kinachohamasisha Kilimo Hifadhi; kikundi hiki kina wanachama hai wanaowezesha jamii katika ngazi ya kaya kutambua na kutumia Kilimo Hifadhi. Kutokana na uhamasishaji na usaidizi wa kikundi, wakulima wamebadilika na kuanza kutumia kilimo hifadhi. Uzalishaji umeongezeka kutoka magunia 5-8 hadi kufikia 25-30 kwa ekari. Kaya nyingi zimeweza kuhifadhi akiba ya chakula cha kutosha katika kipindi chote hadi msimu mwingine wa mavuno. Upungufu wa chakula umekwisha na uchumi wa wananchi umeimarika. Picha ifuatayo inaonesha kuongezeka kwa mavuno.




***Kuongezeka kwa mavuno na uhakika wa chakula katika kaya***

Kazi ngumu na muda wa kutumika katika kilimo umepungua kwa kiasi kikubwa na kuwafanya wakulima kupata muda wa kuendesha shughuli nyingine. Matumizi ya nguvu kazi yanapungua kutokana na kuandaa sehemu ndogo tu ya kulima hivyo kupunguza gharama za palizi. Kilimo Hifadhi kwa kiasi kikubwa kimeleta mabadiliko kutoka kilimo cha mazoea hadi kufikia kutumia mbinu za kisasa za kilimo. Picha ifuatayo inaonesha matumizi ya teknolojia ya kisasa wakati wa kuandaa shamba.



***Kilimo cha kisasa***

Idadi ya wakulima wawezeshaji imeongezeka ndani ya jamii; hii imesaidia kurahisisha uenezaji wa maarifa na ujuzi wa kilimo hifadhi kwa wakulima wengi zaidi. Wawezeshaji jamii wanajumuisha wale walio hudhuria mafunzo Moshi na wale walionesha mafanikio makubwa baada ya kuanza kutumia Kilimo Hifadhi. Kupitia wao, 65% ya wakulima wamejifunza namna ya kutambua udongo bora kwa ajili ya kilimo, matumizi ya mbolea ya mboji, uandaaji wa mashamba, matumizi ya mbolea za viwandani na viuatilifu. Uelewa huu umewezesha wakulima kuzalisha kisasa na kuongeza uzalishaji.

Kuongezeka kwa kipato cha wakulima; kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji,kipato cha wakulima kimeongezeka. Wakulima wanazalisha ziada ambayo huuzwa na kupata fedha kwa matumizi mengine kama kujenga nyumba bora, kulipia ada za shule na kuchangia mfuko wa afya ya jamii (CHF).

Rutuba ya ardhi imeongezeka; kilimo hifadhi kinaboresha hali ya udongo na kuzuia mmomonyoko wa udongo. Kilimo hiki hakiruhusu kulima sehemu yote ya ardhi hivyo sehemu inayobaki huendelea kurutubika na kutunza tabaka la juu la udongo. Utekelezaji wa jitihada hii umehamasisha vijiji vya jirani kuiga Kilimo Hifadhi na vinapata usaidizi kutoka kwa wakulima wa mfano wa Kijiji cha Kabale.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Wanakiji wa Kijiji cha Kabale wanafahamu athari zitakazotokea iwapo tahadhari na mikakati ya uendelevu wa Kilimo Hifadhi haitachukuliwa. Katika kuhakikisha uendelevu wa matokeo ya jitihada hii, Halmashauri kwa kushirikiana na Kijiji cha Kabale na wadau wengine imeweka mikakati ifuatayo;

(i) Halmashauri itaendelea kuwashirikisha viongozi wa kisiasa, viongozi wa Kata na Vijiji kuendelea kuhamasisha matumizi ya Kilimo Hifadhi katika maeneo yao. Viongozi wa jamii wanaushawishi mkubwa kwa jamii kuliko kutumia wawezeshaji kutoka nje ya jamii husika. Kupitia wao, Halmashauri inalenga kupanua wigo wa utekelezaji wa Kilimo Hifadhi kwa vijiji vingine.

(ii) Halmashauri inaendelea kutoa mafunzo ya ziada kwa maafisa ugani kuhusu Kilimo Hifadhi.

(iii) Halimashauri ina mpango wa kuongeza mashamba darasa kwenye vijiji kwa lengo la kuwapa fursa wakulima kujifunza Kilimo Hifadhi.

(iv) Halmashauri ina mpango wa kutoa trekta moja kwa kila Kata kwa lengo la kusaidia na kuhamasisha Kilimo Hifadhi.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya utekelezaji wa jitihada hii yalitokana na;

(i) Utayari wa wakulima kubadilika kutoka kilimo cha mazoea na kukubali Kilimo Hifadhi.

(ii) Matumizi ya mashamba darasa yaliyowafanya wakulima kuona makosa waliyokuwa wanafanya kwenye kilimo cha zamani.

(iii) Utayari wa wakulima kuchangia raslimali na kutenga muda kuhudhuria mafunzo juu ya Kilimo Hifadhi.

(iv) Utashi na utayari wa TGT na Halmashauri katika kusimamia Kilimo Hifadhi.

(v) Ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi wa jamii katika ngazi zote. (Bwana Njalu Silaga) ambaye ni Mbunge wa Itilima alitoa ushawishi mkubwa kwa wakulima kukubali Kilimo Hifadhi baada ya kushuhudia mafanikio ya Kijiji cha Kabale. Katika kuhamasisha utekelezaji wa jitihada hii Bwana Silaga alitoa baiskeli 48 kwa wakulima wa mfano wa Tarafa za Kanadi, Itilima na Kinang'weli ili kurahisisha kuwafikia wakulima wengine ndani ya Halmashauri.

(vi) Uwezeshaji wa kina uliofanywa na maafisa wa TGT na Halmashauri ulieneza maarifa na ujuzi wa nadharia na vitendo kwa wakulima.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

## KUKUZA NA UZALISHAJI WA KAHAWA YA VIKONYO NA KUONGEZA KIPATO



*Uzoefu wa H/W ya Tarime*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Tarime inapatikana Kaskazini Magharibi mwa Tanzania kati ya Latitudo $1^0$ 00 - $1^0$45 Kusini na Longitudo $33^0$30 – $35^0$ 00 Mashariki. Halmashauri inapakana na Nchi ya Kenya upande wa Kaskazini, H/W ya Serengeti upande wa Mashariki, H/W ya Rorya upande wa Magharibi na H/W ya Musoma upande wa Kusini. Halmashauri ina eneo la 1,489.08$km^2$. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 4, Kata 26, na Vijiji 88.

Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo na biashara ndogo ndogo. Kilimo ndio sekta kuu ya kiuchumi inayoajiri 85% ya wakazi. Halmashauri ina jumla ya Kaya 50,600 zinazojishughulisha na kilimo mseto. Halmashauri ina kanda mbili za kiikolojia; ukanda wa juu wenye mwinuko kati ya 1500m – 1800m kutoka usawa wa bahari. Ukanda huu una mvua kati ya 1200mm – 1600mm kwa mwaka. Ukanda wa kati wenye mwinuko kati ya 1300m – 1500m kutoka usawa wa bahari. Ukanda huu una mvua kati ya 900mm – 1250mm kwa mwaka. Mvua hunyesha katika vipindi viwili kati ya mwezi Agosti na Desemba na kati ya mwezi Februari na Mei. Mazao yanayolimwa katika ukanda wa juu ni pamoja na mahindi, mtama, uwele, migomba, viazi vitamu, viazi mviringo, muhugo, maharage, vitunguu, nyanya, kahawa, chai na tumbaku. Mazao yanayolimwa katika ukanda wa kati ni mahindi, mtama, uwele na viazi vitamu.

Halmashauri ina ardhi nzuri kwa kilimo. Eneo linalofaa kwa kilimo ni 90,630ha na zinazotumika ni 69,155ha. Kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa mazao hutegemea mvua isipokuwa 210ha ambazo zina mfumo wa asili wa umwagiliaji zinazotumika kwa kilimo cha mbogamboga. Uzalishaji kwa mwaka ni tani 279,006.6 za mazao ya chakula na tani 5,505.4 za mazao ya biashara. Huduma ya ugani hutolewa kwa ushirikiano na wadau kupitia mfumo wa ubia kati ya Serikali na taasisi binafsi 12.

**2.0 TATIZO**

H/W ya Tarime iliamua kuimarisha uzalishaji wa kahawa kwa kushirikiana na TACRI na wakulima baada ya kubaini matatizo yaliyoathiri uzalishaji wa kahawa kati ya mwaka 1990 - 2008. Baadhi ya changamoto hizo ni kupungua kwa uzalishaji, kuongezeka kwa magonjwa na wadudu wa kahawa na kupungua kwa kipato cha mkulima. Kadhalika, hapakuwa na jitihada za kutosha za wadau wa kahawa katika kuendeleza zao la kahawa uliosababisha uhaba wa huduma za ugani katika ngazi za msingi. Changamoto hizi ziliwakatisha tamaa wakulima kuendelea na uzalishaji wa kahawa.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la utekelezaji wa jitihada hii lilikuwa kuboresha maisha ya wakulima na kukuza uzalishaji wa zao la kahawa kupitia mbinu ya kahawa ya vikonyo. Malengo mahsusi yalikuwa kuanzaisha aina mpya ya kahawa yenye uzalishaji mkubwa na inayohimili magonjwa, kujenga uwezo wakulima katika kutumia mbinu za kisasa, kuondoa magonjwa na wadudu wanaopunguza tija katika uzalishaji, kurudisha ari ya wakulima kuzalisha kahawa, kuongeza vipato vya wakulima, kuimarisha uhakika wa chakula na kuboresha maisha. Aidha, Halmashauri ililenga kuimarisha ubia kati ya Serikali na taasisi binafsi kukuza uzalishaji wa kahawa.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulianza mwaka 2001 wakati Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI) yenye makao yake makuu mkoani Kilimanjaro ilipoanzisha kituo kipya eneo la Sirari. TaCRI ilianzisha kahawa ya vikonyo kwa lengo la kukuza uzalishaji na ubora kwa kuzalisha na kugawa miche inayohilimi magonjwa na wadudu. Ili kufikia malengo ya jitihada hii, Halmashauri kwa kushirikiana na TaCRI ilitekeleza mikakati ifuatayo;

Kuanzishwa kwa kahawa ya vikonyo; kutokana na wakulima kukata tamaa kulikosababishwa na uzalishaji duni, kuzeeka kwa miti ya kahawa na kushuka kwa bei, TaCRI kwa kushirikiana na Halmashauri iliamua kuingilia kati na kuanzisha aina mpya ya kahawa. Aina hii ya kahawa imeboreshwa na inastahimili magonjwa ikilinganishwa na aina za zamani. Miche ya kahawa ya vikonyo ilisambazwa kwa wakulima na kuwahamasisha kung'oa miti ya kahawa ya zamani. Picha ifuatayo inaonesha wakulima waking'oa miti ya kahawa ya zamani ili kupanda kahawa ya vikonyo.



***Wakulima waking'oa miti ya kahawa na kitalu cha kahawa ya vikonyo***

Ziara ya mafuzo makao makuu ya TaCRI Kilimanjaro; ziara ya mafunzo ilishirikisha wakulima waliochaguliwa kutoka vijiji vinavyozalisha kahawa kwa lengo la kujifunza namna ya kuandaa mashamba, kuandaa miche ya kahawa, kupanda kwa nafasi, matumizi ya viuatilifu, uvunaji, uchakataji na uhifadhi wa kahawa. Bw. Petro Bururyo ambaye ni muhamasishaji wa kahawa ya vikonyo alikuwa miongoni wa wakulima wa mwanzo waliotembelea kituo cha TaCRI mkoani Kilimanjaro. Baada ya kurejea alianza kuzalisha kahawa ya vikonyo na kuhamasisha wakulima kung'oa miti ya kahawa ya zamani iliyozeeka na kupanda miche iliyoboreshwa.

Kujenga uwezo wa wakulima; Halmashauri iliandaa mafunzo katika vijiji vya Tagota, Kenyamanyori na Manguchi kuwafundisha wakulima kuhusu uzalishaji wa kahawa iliyoboreshwa. Mafunzo yalilenga kukuza ujuzi wa wakulima katika kuzalisha miche ya kahawa ya vikonyo, uboreshajii miti ya zamani ya kahawa, kuunda vikundi vya wakulima na kuanzisha vitalu vya miche. Kufikia mwaka 2015/2016 wanachama 3,024 kutoka vikundi 19 na wakulima binafsi walipatiwa mafunzo kuhusu uzalishaji wa kahawa ya vikonyo na uandaaji wa mashamba. Picha zifuatazo zianonesha wakulima wakihudhuria mafunzo kwa vitendo.




*Mafunzo ya kuandaa miche ya kahawa ya vikonyo*

Kuandaa na kusambaza miche ya kahawa; Halmashauri ikishirikiana na TaCRI ilianzisha kitalu cha kuzalisha miche ya kahawa ya vikonyo na kuisambaza kwa wakulima kama inavyoneshwa kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 1 Usambazaji wa Miche ya Kahawa ya vikonyo**

| MWAKA | KIASI CHA MICHE | ENEO Ha. |
|---|---|---|
| 2007/2008 | 3826 | 2.8 |
| 2008/2009 | 10000 | 7.40 |
| 2009/2010 | 11610 | 8.6 |
| 2011/2012 | 24480 | 18.13 |
| 2012/2013 | 26217 | 19.42 |
| 2013/2014 | 36712 | 27.19 |
| 2014/2015 | 182,468 | 135.16 |
| 2015/2016 | 32,416 | 24 |
| JUMLA | **327,729** | **242.76** |

Kuanzishwa kwa vituo vya uzalishaji wa miche; vituo vya zalishaji wa miche ya kahawa ya vikonyo vilianzishwa katika ngazi za vijiji ambapo kila kituo kilikuwa na uwezo wa kuzalisha miche 20,000 kwa mwaka. Hadi kufikia mwaka 2015/2016 jumla ya vituo 15 vilianzishwa na wakulima 3,024 walipatiwa mafunzo. Vituo vyote viligatuliwa kwenye ngazi ya kijiji kwa lengo la kuhakikisha urahisi wa kupata miche iliyoboreshwa, kusambaza teknolijia ya uzalishaji na kujenga dhana ya umiliki kwa wananchi.

Kuimarisha ushirikiano na wadau wa kahawa; ushirikiano baina ya taasisi binafsi na za Serikali umeleta tija na hatimaye umechochea kasi ya usambazaji na kukubalika kwa aina mpya ya kahawa ya vikonyo. Halmashauri iliingia mkataba wa makubaliano na kamati ya pembejeo za kilimo na wanunuzi wa kahawa kununua na kusambaza miche ya kahawa ilyozalishwa na wakulima kwa lengo la kupunguza uhaba wa miche na kuongeza uzalishaji. Jumla ya TZS 146,241,441 kutoka DADPS zilitumika kuzalisha na kugawa miche ya kahawa. Mwaka 2007/2008, Halmashauri ilitoa eneo la ekari 14.5 kuanzisha shamba la kuzalisha vikonyo vya kahawa lililoendeshwa kwa ushirikano na TaCRI kwa lengo la kuzalisha na kusambaza miche 10,000 ya kahawa iliyoboreshwa kwa wakulima kwa mwaka na kuanzisha shamba darasa. Picha ifuatayo inaonesha shamba darasa lilioanzishwa na Halmashauri kwa kushirikiana na TaCRI.




***Shamba darasa makao makuu ya Halmashauri***

Kuanzisha vikundi vya wakulima; Ili kujenga mahusiano baina ya wakulima, Halmashauri ilisaidia wakulima kuanzisha vikundi vya wazalishaji wa kahawa ili kupata usaidizi wa huduma za ugani na kufanya maamuzi kwa pamoja. Halmashauri ilfaniksha kuanzishwa kwa vikundi 4 vya wakulima mwaka 2008 na kuongezeka kufikia vikundi 25 mwaka 2016.

Ujenzi wa vinu vya kukoboa, kusafisha na kukausha kahawa; vinu vidogo vya kukoboa maganda ya nje ya matunda ya kahawa, kusafisha na kukausha matunda ya kahawa mara baada ya kuvunwa vilijengwa. Mwaka 2014, Halmashauri chini ya usaidizi wa DADPS ilijenga vinu 2 na kuvikabidhi kwa wakulima kuongeza ubora wa kahawa inayozalishwa.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulitumia raslimali mabalimbali. Rasilimali watu imejumuisha maafisa ugani katika vijiji kutoa huduma za ugani. Watalamu kutoka TaCRI walitoa ujuzi wa kuzalisha miche ya kahawa ya vikonyo. Raslimali fedha zilizotumika zinaoneshwa kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali Na 2: Raslimali Fedha**

| S/N | MWAKA | SHUGHULI | GHARAMA | CHANZO CHA FEDHA | MATOKEO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2009/2010 | Kusaidia TaCRI kuanzisha mashamba darasa kwenye vijiji vya Tagota, Kenyamanyori na Mangucha. | 4,000,000/= | DADPs | Wanachama 45 walipatiwa mafunzo na mashamba 45 yalianzishwa |
| 2. | 2011/2012 | Kusaidia TaCRI kuanzisha shamba darasa kwenye makao makuu ya Halmashauri | 25,000,000/= | DADPs. | Kinu 1 kilianzishwa , na miche 240,000 ilisambazwa kwa wakulima |
| 3 | 2012/2013 - 2013/2014 | Kusaidia TaCRI kuanzisha mashamba ya mbegu kwenye vijiji vya Bumera na Itiryo. | 53, 597,441/= | DADPs. | Miche 360,000 imesambazwa kwa wakulima kwa bei ya shs 500 kila mche |
| | | Kung'oa na kukatia miti ya kahawa ya zamani katika Kata 10. | 20,804,000/= | DADPs. | Kuongezeka kwa uzalishaji kutoka kilo 3 hadi 4 kwa mti mmoja wa kahawa |
| | | Kuzisaidia AMCOS 2 vifaa vya kuchakata kahawa katika vijiji vya Bungurere na Nyantira. | 24,240,000/= | DADPs | Mradi unaendelea |
| 4. | 2014/2015 | Kusaidia utoaji wa huduma za ugani katika shamba la mbegu la makao makuu ya Halmashauri | 15,600,000/= | DADPs. | Kulianzishwa shamba la mfano moja lenye mazao mchanganyiko ya kahawa na migomba tangi la maji na miundombinu ya umwagiliaji iliwekwa |

| JUMLA | 146,241,441/= | | |
|---|---|---|---|


### 6.0 MATOKEO

Jitihada ya kuendeleza uzalishaji wa kahawa ya vikonyo imeleta matokeo chanya kama ifuatavyo; Uzalishaji wa kahawa na kipato cha wakulima vimeongezeka. Jedwali Na 3 linaonesha ongezeko la uzalishaji na kipato cha mkulima.

**Jedwali Na 3: Uzalishaji na ongezeko la kipato**

| Mwaka | Kiwango cha uzalisahaji (Tani) | Bei kwa Kilo | Kipato cha mkulima |
|---|---|---|---|
| 2009/2010 | 2,000 | 800/= – 850/= | 1,650,000,000/= |
| 2010/2011 | 1,905 | 1,500/= – 1,600/= | 2,952,750,000/= |
| 2011/2012 | 1,753 | 1,800/= – 2,100/= | 3,497,562,900/= |
| 2012/2013 | 1,466.2 | 1200/= – 1300/= | 1,832,750,000/= |
| 2013/2014 | 1,354.4 | 700/= – 1000/= | 1,151,240,000/= |
| 2014/2015 | 1,914.23 | 1,000/= – 1,800/= | 2,679,488,000/= |
| 2015/2016 | 2,195.21 | 1541/= – 1600/= | 3,447,577,300/= |
| | | | |

Uzalishaji wa miche ya kahawa umeongezeka na kuashiria kuongezeka kwa mahitaji ya miche ya kahawa ya vikonyo kuanzia mwaka 2008 hadi 2012 kama inavyoonekana hapa chini.




Wakulima wamejengewa uwezo wa kuzalisha miche bora ya kahawa kwa kupandikiza vikonyo. Mashamba ya kuzalisha vikonyo vya kahawa yameongezeka na wakulima wanazalisha miche inayotokana kupandikizwa kwa vikonyo. Bei ya miche ya kahawa pia imeongezeka kutokana na kuongezeka kwa uhitaji hivyo kuongeza pia kipato cha wakulima. Picha zifuatazo zinaonesha bustani ya kahawa na vikonyo tayari kwa kupandikizwa.






***Vikonyo vya kahawa*** ***Shamba la kahawa lililoanzishwa***

Halmashauri imepata chanzo kipya cha mapato na kumekuwa na ongezeko la makusanyo ya mapato kutoka TZS 58,275,000 (2007/2008) hadi kufikia TZS 150,000,000 (2015/2016). Baadhi ya mapato kutokana na ushuru wa mazao yanatumika kuboresha huduma za ugani pamoja na usimamizi wa shughuli za kilimo. Kwa mfano mwaka 2012/2013 TZS million 40 zilitumika kununua gari moja kwa ajili ya shughuli za ugani. Mwaka 2015/2016 TZS million 16 za ushuru wa mazao zilitumika kutekeleza shughuli za kilimo.

Wakulima wameridhika na maisha yameimarika kutokana na uzalishaji wa kahawa. Baadhi ya watu waliofanikiwa ni Bw na Bi. Petro Mwita Bururyo (44) na mkewe Joyce (33) wa kijiji cha Nyarero. Awali waliishi maisha magumu kwa kutegemea biashara ndogo ndogo na kamari kabla ya kugundua kilimo cha kahawa ya vikonyo. Joyce katika kuthibitisha mabadiliko ya maisha yao baada ya kuanza kulima kahawa alikuwa na haya ya kusema "*Tulikuwa na wakati mgumu kabla ya kuanza kilimo cha kahawa mwaka 2009. Mume wangu alikuwa akitegemea kucheza kamari kupata kipato chake cha siku licha ya hatari za mchezo huo. Hali hii ilichangia kuzuka kwa ugomvi wa mara kwa mara ndani ya ndoa yetu. Kitu ninachoweza kusema ni kwamba kilimo cha kahawa kimekuwa mkombozi wa maisha na ndoa yetu…..,* Zaidi ya hayo, kuzunguka kijiji, familia nyingi zimebadilisha nyumba kutoka nyumba za nyasi na kujenga nyumba bora kutokana kilimo cha kahawa. Picha zifuatazo zinaonesha nyumba za nasi na mabadiliko ya ujenzi wa nyumba bora.






***Nyumba ya zamani na mpya ya bw. Petro Bururyo***

Ushiriki katika maonesho ya kitaifa; katika maonesho ya kitaifa, wakulima bora 4 wa kahawa walishinda katika mkoa na kuzawadiwa kila mmoja shs 1,00,000 kati ya mwaka 2012 na 2015. Wakulima hawa 4 pia wanatumika kama wakufunzi (afisa ugani) katika kutoa mafunzo na kuimarisha vikundi, uzalishaji na usambazaji wa miche ya kahawa ndani ya Halmashauri na nje (Ukerewe na Geita). Wakulima hawa

wamekuwa wakishiriki maonesho ya Kilimo ya Nane Nane na kushinda tuzo mbalimbali kila mwaka. Bw. Peter Buruyo alitambuliwa kama mzalishaji bora wa kahawa ndani ya Halmashauri.



***Wakulima wakishiriki maonesho ya Nane Nane***




***Tuzo ya bw. Peter Bururyo***

Halmashauri imekuwa na historia ya mafanikio katika kilimo cha kahawa; hadi mwaka 2015/2016 jumla ya miche 214,884 ya kahawa ilisambazwa kwa wakulima na kupandwa kwenye eneo la hekta 158.2. Halmashauri imeweza kuendesha miradi mingine kwa kutumia mapato yanayotokana na kahawa. Jumla ya TZS million 16 zilitumika kuboresha utoaji wa huduma za ugani, ujenzi wa ghala la mazao na uanzishaji wa vituo vya kukusanya mazao katika Kata za Pemba na Matongo. Vilevile, Halmashauri imejenga soko la kimataifa la mpakani katika kijiji cha Remagwe, kilomita 11 kutoka mpakani na Kenya.

Uhusiano thabiti kati ya taasisi za umma na binafsi kama Mogabiri farm extension, TaCRI, TSHTDA, Acacia, TAFIRI, SENAPA AMCOS, Syngeta na Via-agroforestry umeimarika na kuongeza uhamasishaji wa uzalishaji na masoko kwa wakulima.

Kutokana na kuongezeka kwa kipato, baadhi ya watu binafsi wameanzisha vituo vya kukuboa na kukausha kahawa na mazao mengine. Baadhi ya viwanda hivyo ni pamoja na kituo cha kukoboa kahawa cha Muriba, kiwanda cha kuchakata alizeti cha Isaac and sons', kituo cha kukusanya maziwa cha Komaswa na mashine ya kuchakata alizeti ya Nyabirongo.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kuhakikisha uendelevu wa mafanikio haya, Halmashauri kwa kushirikiana na TaCRI na wadau wengine wa kahawa imeweka mikakati mbalimbali ya uendelevu. Mikakati hiyo nipamoja na;

(i) Kutangaza na kuongeza idadi ya wanunuzi; Halmashauri inaendelea kutangaza, kutafuta na kuwashiriksha wanunuzi (Mara Coffee, CMS, vyama vya ushirika) kununua kahawa ya Tarime.
(ii) Halmashauri inaendelea kuanzisha vituo vya kukoboa na kukausha kahawa katika ngazi za vijiji.
(iii) Kuwaunganisha wakulima kupitia vikundi na kuwapatia utaalamu na teknolojia ya kuzalisha miche ya kahawa ya vikonyo.
(iv) Kuendelea kuimarisha vyama vya ushirika ili kujenga uwezo wa kusimamia soko la kahawa.
(v) Kuendelea kuotoa usaidizi wa karibu kwa kutumia maafisa ugani na wakulima viongozi.
(vi) Kuendelea kuwasaidia wakulima kushiriki maonesho mbalimbali ya kilimo.
(vii) Kuendelea kufanya tafiti za uzalishaji wa kahawa kwa kushirikiana na Badilika Foundation ili kuzalisha aina bora zaidi ya miche inayohimili magonjwa na kustawi vema.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya utekelezaji wa jitihada hii yamechangiwa na sababu mbalimbali. Sababu hizi ni utayari na uthubutu wa watumishi wa Halmashauri na jamii, ugatuaji wa zaoezi la uzalishaji wa miche katika ngazi za vijiji, ubia baina ya taasisi binafsi, wakulima, TaCRI na Halmashauri na kubinafisha shughuli za uzalishaji wa miche ya kahawa kwa TaCRI.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

**UMWAGILIAJI WA MPUNGA KUBORESHA KIPATO NA UHAKIKA WA CHAKULA**



*Uzoefu wa Skimu ya Umwagiliaji - Kijiji cha Irienyi*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Rorya ni moja kati ya Halamshauri 9 za Mkoa wa Mara. Halmashauri ilianzishwa mwaka 2007 baada ya kuigawa H/W ya Tarime. Halmashauri ipo kati ya Latitudo $10^0$.00 na $10^0$.45 Kusini na Longitudo $33^0$.30 na $35^0$.00 Mashariki na inapakana na Nchi ya Kenya upande wa Kaskazini, H/W ya Tarime upande wa Mashariki, H/W za Butiama na Musoma upande wa Kusini na Ziwa Viktoria upande wa Magharibi. Halmashauri ina eneo la 9,345.496$km^2$ ambapo 7,252$km^2$ zimefunikwa na Ziwa Viktoria. Halmashauri ina Tarafa 4, Kata 26 Vijiji 87 na Vitongoji 509; makadirio ya watu ni 295,197 na ongezeko ni asilima 2.8 kwa mwaka.

Halmashauri ina kanda mbili za kiikolojia ambazo ni ukanda wa kati na ukanda wa chini kwenye mwinuko wa 800m – 1200m juu ya usawa wa bahari. Hali ya hewa ni $14^0$C – $30^0$C na wastani wa mvua ni kati ya 700mm – 1200mm kwa mwaka. Shughuli za kuu za kiuchumi ni pamoja na kilimo, ufugaji na uvuvi. Sekta nyingine zinazochangia uchumi ni biashara ndogondogo, usafirishaji na mawasiliano

Kijiji cha Irienyi ni mojawapo ya vijiji vya Kata ya Irienyi, Tarafa ya Komuge. Wanachi wa kijiji hiki ni wakulima wadogo ambao maisha yao hutegemea uzalishaji wa mazao, ufugaji na uvuvi mdogo. Mpunga ni mojawapo ya zao linalozalishwa na wanakijiji kwa njia ya umwagiliaji. Eneo la ukanda wa chini la kijiji lipatalo 350ha linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo kwa sasa eneo ambalo linatumika kwa kilimo cha umwagiliaji wa mpunga ni 126ha tu. Skimu ya umwagiliaji ya kijiji cha Irienyi ilianzishwa mwaka 1996 kupitia mchakato wa O&OD ambapo wananchi waliainisha kuwa kipaumbele cha maendeleo. Skimu hii ipo umbali wa 72km kutoka makao makuu ya Halmashauri eneo la Ingri juu.

## 2.0 TATIZO

Zaidi ya 89% ya wananchi wa Halmashauri ya Rorya wanategemea kilimo kuendesha maisha yao. Halimashauri ina eneo la 291,375ha linalofaa kwa kilimo na eneo linalotumika ni 130,481ha. Eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni 17,350ha na eneo linalotumika ni 1,039ha. Mazao ya chakula yanayozalishwa ni pamoja na Mihogo, mtama,mahindi, mpunga, na maharage. Ingawa kuna eneo kubwa linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji wa mazao ya chakula hautoshelezi mahitaji na ziada ya kuuza. Wastani wa uzalisahiji wa mazao kwa kaya ni tani 1 kwa msimu. Hii inasababishwa na wakulima kutegemea kilimo cha mvua ambazo hazitabiriki na teknolojia duni za kilimo.

Kabla ya mwaka 1999, Jamii ya Irienyi ilikabiliwa na upungufu wa kipato na chakula. Kila mwaka Halmashauri ililazimika kupeleka chakula cha msaada kwa jamii hiyo. Hali hii iliongeza umasikni na wananchi kushindwa kikidhi mahitaji ya msingi kama vile kulipa karo, huduma za afya, ujenzi wa nyumba bora na samani. Jamii ilitumia eneo la bondeni kwa kilimo cha nafaka lakini uzalishaji ulikuwa mdogo sana kati ya gunia 5 hadi 8 kwa ekari. Ingawa wakulima wachache walijishughulisha na kilimo cha mpunga, mashamba hayakuwa yameboreshwa kuruhusu utumiaji wa mbinu za kisasa za uzalishaji na umwagiliaji. Wakulima walitegemea kilimo cha mvua ambazo hazitabiriki, mbegu duni, uhaba wa huduma za ugani na soko lisilo la uhakika.

Wakulima wa mpunga hawakuwa na umoja katika kupanga bei, kutafuta na kumiliki soko la mazao. Baadhi ya wakulima waliuza mazao kupitia madalali ambao hupanga bei zinazokandamiza mkulima. Vipimo vya mpunga pia havikuwa sahihi; wakulima walilaimishwa kujaza mpunga kwenye magunia ya ujazo mkubwa kuliko viwango vya kawaida hivyo kupelekea hasara kwa wakulima. Changamoto nyingine ilikuwa uduni wa miundombinu ya kusafirisha mpunga kutoka shambani hadi sokoni.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la utekelezaji wa jitihada hii ni kuboresha kipato na kuleta uhakika wa chakula kwa jamii ya kijiji cha Irienyi. Malengo mahususi ni pamoja na kuimarisha uzalishaji wa mpunga kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji, kutoa huduma za ugani za kutosheleza, kuwaunganisha wakulima kwenye vikundi ili kurahisisha uzalishaji na uuzaji katika soko na kuwasaidia wakulima kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la mpunga kwa kujenga kiwanda cha kuchakata na kupanga madaraja ya mchele.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Serikali wa kutekeleza sera ya sekta ya umwagiliaji, umwagiliaji umetambuliwa kama shughuli muhimu katika uzalishaji katika kilimo kutokana na mchango wake katika kukabiliana na madhara ya hali ya hewa isiyotabirika na mvua zisizo za uhakika. Utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji wa Irienyi unaendana na Sera ya Serikali na Mpango wa Taifa wa Uhakika wa Chakula katika Kaya, Mkakati wa Kupunguza Umasikini, Mkakati wa Maendeleo Vijijini na Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010. Skimu ya umwagiliaji ilianzishwa na wanakijiji wenyewe kupitia O&OD mwaka 1996 kama mpango wa maendeleo wa kuboresha hali ya maisha. Ili kufikia malengo ya mpango huu, mikakati ifuatayo ilitekelezwa;

Utambuzi wa eneo; Wanakijiji kwa kushirikina na wataalamu wa Halmashauri waliitisha mkutano ili kubaini eneo linalofaa kwa kilimo cha mpunga. Wamiliki wa aridhi hiyo walitambuliwa na makubaliano ya namna ya kutumia mashamba yao yalifanyika. Katika mkutano huu maeneo ya hifadhi ya maji na mashamba ya mpunga yaliainishwa. Mwaka 2000, wataalamu wa Halmashauri kwa kushirikiana na wanakijiji na ofisi ya umwagiliaji ya kanda walipima mashamba. Wakati wa utekelezaji wa zoezi hili, wananchi walishiriki katika kufyeka na wataalamu walishiriki kuweka mipaka na kuchora ramani za mashamba ili kuanzisha mashamba ya kisasa. Upimaji wa mashamba uliambatana na upimaji wa miferaji mikuu na midogo ya umwagiliaji.

Ujenzi wa Miundombinu ya umwagiliaji (bwawa la kuhifadhi maji, mifereji ya umwagiliaji) na ugawaji wa mashamba; Halmashauri ilitumia fedha za DIDT kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji ya umwagiliaji. Jamii ilishiriki kwa kujitolea nguvu kazi kwa kusafisha eneo la bwawa na kukusanya mawe na mchanga. Aidha, ugawaji wa mashamba ulifanyika ambapo eneo la 850ha lilibainishwa kama eneo la umwagiliaji na wakulima 48 waligawiwa mashamba kila mkulima ekari moja. Baada ya mgawanyo wa mashamba wakulima waliopatiwa mashamba waliungana na kutengeneza mifereji ya umwagiliaji.

Kuandaa mafunzo kwa wakulima na ziara za mafunzo; mwaka 2011/2012, Halmashauri ilisaidia baadhi ya wakulima kuhudhuria mafunzo ya uzalishaji bora wa mpunga. Mafunzo hayo yalitolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ukiriguru na Kituo cha Mafunzo cha Kilimanjaro cha Moshi. Baada ya kurejea wakulima walishirikisha wenzao stadi walizojifunza za kilimo bora cha mpunga. Wakulima walijifunza mbinu bora kundaa matuta ya mpunga, matumizi ya mbegu bora, upandaji kwa nafasi, palizi, matumizi ya mbolea na uvunaji kwa wakati. Mwaka 2015 JICA ilitoa msaada wa fedha kuendesha mafunzo kwa wakulima kuhusu uendeshaji wa skimu, kufanya matengenezo ya skimu na kutunza taarifa za kilimo.

Kuunda umoja wa wakulima; Halmashauri ilisaidia wakulima kujiunga katika vikundi. Lengo la kuanzishwa kwa umoja ni kuunganisha nguvu na kuimairisha uwezo wa kusimamia soko. Wakulima walianzisha kikundi na kuchagua uongozi baada ya kupata muongozo kutoka Halmashauri. Vilevile walianzisha kamati kushughulikia masuala mbalimbali ya kiutawala na undeshaji wa skimu. Kamati hizo ni pamoja na kilimo, mazingira, mipango na fedha, masoko na ujenzi. Aidha, Halmashauri ilisaidia

wakulima kuunda katiba na kusajili umoja kwa jina la "Umoja wa Wakulima Mpunga Irienyi Rorya" (UWAIRO).

Ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji; mwaka 2011 mifereji ya umwagiliaji iliboreshwa. Wakulima walifanikisha ujenzi wa 1200m baada ya kupatiwa fedha kutoka Halmashauri (DASIP). Mwaka 2013, kwa mara nyingine, chini ya usaidizi wa ofisi ya kanda ya umwagiliaji Halmashauri ilitumia fedha za DIDF kujenga mifereji ya umwagiliaji. Mwaka 2014 Halmashauri ilitenga bajeti kutoka fedha za ndani kusaidia ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Mbali na usaidizi wa wadau, wakulima walichangia asilimia 20 ya gharama za mradi kupitia nguvu kazi (kukusanya vifaa vya ujenzi mfano mawe na mchanga) pamoja na usimamizi wa mkandarasi wakati wa ujenzi wa mfereji wa umwagiliaji wa urefu wa 2000m. Hadi mradi kukamilika jumla ya 4,728m za mifereji ya umwagiliaji zilijengwa hivyo kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka ekari 48 hadi 160. Picha ifuatayo inaonesha ujenzi ukiendelea.



***Ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji***

Utafutaji wa rasilimali na usimamizi wa skimu; mwaka 2015, Halmashauri iliandaa andiko la mradi na kuwasilisha Wizara ya Kilimo. Wizara ilitafuta fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo; JICA ilitoa fedha kufanya upanuzi wa skimu (kuongeza mifereji) na usimamizi wa skimu. Ili kuleta ufanisi katika usimamizi imara, skimu imegawanywa katika vitalu 5 (A - E) kwa eneo la ekari 30 kila kitalu. Kamati ya maji iliweka utaratibu wa kugawa maji ambapo kila kitalu hupata maji mara mbili kwa wiki. Kamati zinatekeleza majukumu yao kama yalivyoainishwa katika mwongozo wa skimu na vikao hufanyika kwa mujibu wa mwongozo.

Ujenzi wa ghala na kusimika mashine za kuchakata mpunga; utekelezaji wa ujenzi wa ghala na ununuzi wa mashine za kuchakata mpunga ulifanyika kupitia fedha za Halmashauri chini ya mfuko wa DADIPs. Kwa upande mwingine UWARIO walishiriki kujenga jengo la kusimika mashine kwa kuchangishana fedha TZS 27,000 kila mwanachama. Ujenzi wa ghala na usimikaji wa mashine za kuchakata mpunga ulilenga kuongeza thamani kwa kupanga madaraja mchele ili kuuza kwa bei yenye tija. Picha zifuatazo zinaonesha ghala la kuhifadhi mazao na jengo iliposimikwa mashine ya kuchakata mpunga.


*Ghala la mazao*


*Jengo la mashine ya kukoboa mpunga*

## 5.0 RASILIMALI

Utekelezaji wa mradi huu ulihusisha raslimali mbalimbali; raslimali watu, vifaa na rasilimali fedha. Raslimali watu ni pamoja na watumishi wa Halmashauri, ofisi ya Umwagiliaji ya kanda, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ukiriguru, wakandarasi na wanakijiji ambao walishiriki kutoa utaalamu na nguvukazi utekelezaji. Raslimali fedha zilizotumika ni TZS 596,544,829 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1 hapa chini.

**Jedwali Na. 1. Matumizi ya Rasilimali kwenye Skimu ya umwagiliaji**

| S/N | Shughuli | Mwaka | Kiasi (TZS) | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji | 2000 | Million 92 | DIDF |
| 2. | Uchimbaji na ujenzi wa mifereji awamu ya kwanza | 2011 | Million 28 | DASIP |
| 3. | Uchimbaji na ujenzi wa mifereji awamu ya pili | 2013 | Million 41 | DIDF |
| 4. | Uchimbaji na ujenzi wa mifereji awamu ya tatu | 2013 | Million 200 | DIDF |
| 5. | Uchimbaji na ujenzi wa mifereji awamu ya nne | 2014 | Million 20 | Halmashauri |
| 6. | Uchimbaji na ujenzi wa mifereji awamu ya tano | 2014/2015 | Million 422 | JICA |
| 7. | Nguvu kazi ya wananchi (kukusanya vifaa vya ujenzi) | 2000/2015 | 20% gharama za mradi | Wakulima |

## 6.0 MATOKEO

Kujengwa kwa skimu ya umwagiliaji kumebadiliasha maisha ya wakulima wa kijiji cha Irienyi. Kipato kimeongezeka kutokana na ongezeko la uzalishaji wa mpunga kutoka gunia 5-8 kufukia 25-35 kwa ekari. Matokeo mengine yameelezwa hapa chini.

Uwepo wa umoja wa wakulima (UWAIRO) wenye wajumbe 160, kamati za uendeshaji wa skimu na katiba ya umoja; kuwepo kwa umoja wa wakulima kumesaidia kutafuta soko na kuongeza nguvu ya wakulima kuamua bei ya mchele. Umoja umefanikisha kuwa na nguvu ya pamoja ya kununua vitendea kazi katika mashamba kama trekta 1, trekta ndogo 3 na mashine ya kuvunia vinavyotumiwa na wakulima kwa kukodi. Pesa inayopatikana inatumika kuongeza uwezo wa kifedha wa umoja. Umoja una akaunti benki na kila mwanachama huchangia fedha kila mwezi zinazotumika kugharamia shughuli za usimamizi

wa skimu, matengenezo na marekebisho ya miundombinu ya skimu. Wajumbe wa kamati wamefundishwa majukumu yao na wanayatekeleza kwa ufanisi katika kuhakikisha skimu inafanya kazi muda wote. Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya wajumbe wa umoja wa wakulima (UWAIRO).



*Mwenyekiti na mweka hazina wa UWAIRO*



*Mkulima na mjumbe wa Umoja*

Uwepo wa miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji na kuongezeka kwa eneo la uwagiliaji; jitihada hii imefanikisha kujengwa kwa miundumbinu ya kisasa ya skimu ya umwagiliaji. Miundombinu inajumusha bwawa la kuhifadhi maji, mifereji mikuu ya maji na mifereji ya kugawa maji mashambani. Bwawa la maji lina uwezo wa kuhifadhi 888,300m$^3$. Mifereji mikuu ya umwagiliaji ina urefu wa 4800m, mifereji ya kugawa maji imejengwa ili kuzuia upotevu wa maji. Eneo la umwagiliaji limeongezeka kutoka 0 hadi ekari 315 na wakulima ambao awali walitegemea kilimo cha mvua kulima mpunga sasa wana uhakika wa mavuno kutokana na uwagiliaji. Picha zifuatazo zinaonesha bwawa la maji, sehemu ya kuruhusu maji na mifereji ya umwagiliaji.





*Bwawa la maji na sehemu ya kuruhusu maji*



***Mifereji ya usambazaji wa maji***

Uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka gunia 5-8 hadi 25-35 kwa ekari kutokana na uboreshaji wa mbinu za kilimo kama matumizi ya mbegu bora, upandaji kwa nafasi, upaliliaji na uvunaji kwa wakati, matumizi ya mbolea, huduma za ugani na mafunzo. Ongezeko la uzalishaji limeboresha kwa hali ya maisha ya wakulima. Wakulima wana uhakika wa chakula na ziada kwa ajili ya kuuza. Picha ifuatayo inaonesha shamba la umwagiliaji na ustawi wa mpunga.



***Shamba la umwagiliaji***

Wastani wa kipato cha wakulima kimeongezeka kutoka TZS 640,000 hadi 4,800,000 kwa mwaka. Kabla ya mradi hadi mwaka 2010 bei ya gunia moja la mpunga ilikuwa TZS 80,000. Mkulima alikuwa anavuna mara moja kwa mwaka na wastani wa juu wa mavuno ilikuwa ni gunia 8 kwa ekari hivyo ilimfanya apate TZS 640,000. Baada ya ujenzi wa skimu, wakulima huvuna mara 2 kwa mwaka na wastani wa mavuno kwa ekari ni gunia 60 kwa ekari kwa mwaka ambapo thamani yake ni TZS 4,800,000. Wakulima wapatao 40 wanamiliki maksai kurahisisha kilimo. Wakulima wameboresha maisha yao; hii inathibitishwa na uhakika wa chakula, ujenzi wa nyumba bora, uwezo wa kulipa karo za shule, ununuzi wa vyombo vya usafiri kama pikipiki, kuongezeka kwa ufanisi wa kuchangia miradi ya maendeleo kama kutengeneza (madawati, kujenga madarasa, maabara za shule za sekondari, zahanati, ofisi na nyumba za watumishi). Picha zifuatazo ni zinathibitisha.



***Nyumba ya zamani na ujenzi wa nyumba mpya ukiendelea***





***Nyumba bora na pikipiki ya mkulima***

Mradi wa skimu ya umwagiliaji wa kijiji cha Irienyi umeongeza fursa za ajira ndani ya kijiji na maeneo jirani. Wakulima huajiri vibarua msimu wa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kuvuna. Kutokana na uhakika wa ajira nguvu kazi ya vijana imeendelea kubaki kijijini badala ya kukimbilia mijini kutafuta fursa za ajira. Vilevile, skimu imeleta shughuli za biashara kutokana na kuongezeka kwa watu wanaofika kununua mchele. Ndani ya kijiji maduka mengi ya jumla na rejareja yameanzishwa, maduka ya vyakula na vifaa vya ujenzi yameongezeka. Kumeanzishwa gulio la mara moja kwa wiki ambalo wafanyabiashara huuza na kununua bidha mbalimbali ndani ya kijiji. Kuwepo kwa shughuli za biashara kunakuza uchumi wa kijiji na mazingira yanabadilika kuendana na mazingira ya miji. Aidha, Halmashauri imefaidika kutokana na na kupanuka kwa vyanzo vya mapato kutoka kwenye ushuru wa mazao na kuanza kukusanya kwenye leseni za biashara na ushuru wa huduma. Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya sehemu za biashara ndani ya kijiji.



***Sehemu za maduka***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Mafanikio ya skimu ya umwagiliaji yanapaswa kuwa endelevu hivyo umoja wa wakulima umeweka utaratibu wa kuchangisha fedha kutoka kwa wanachama kwa ajili ya kufanya matengenezo pale miundombinu inapoharibika na kuendelea kufanya upanuzi wa mradi. Utaratibu huu unamtaka kila mwanachama kuchangia gunia moja la mpunga kwa kila msimu ambapo huuzwa na fedha huwekwa kwenye akaunti ya umoja.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kukamilika kwa mradi wa umwagiliaji kumetokana na ushirikiano na uthubutu kati ya wakulima, Halmashauri, Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda, Serikali Kuu na JICA. Wakulima walipokea huduma ya ugani kuhusu uboreshaji wa uzalishaji mpunga. Utayari wa jamii ni siri nyingine ya mafanikio; wakulima walianza kujenga wenyewe miundombinu asili ya umwagiliaji kabla ya kupata usaidizi kutoka kwa wadau wa nje. Uwepo wa umoja wa wakulima katika kusimamia utekelezaji wa mradi kwa kushirikiana na Halmashauri ni siri nyingie ya mafanikio.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

**UFUGAJI WA SAMAKI KATIKA VIZIMBA NA UREJESHAJI WA MAZALIA YA SAMAKI**



***Uzoefu wa H/W ya Bunda***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Bunda inapatikana upande wa Kusini ya Mkoa wa Mara, 65km kutoka makao makuu ya Mkoa -Musoma. Halmashauri ipo pwani ya Kusini Mashariki mwa Ziwa Viktoria ambayo imetenganishwa na tambarare ikiungana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa upande wa Mashariki. Halmashauri inapakana na H/W za Serengeti kwa upande wa Mashariki, Butiama upande wa Kaskazini, Busega (Mkoa wa Simiyu) upande wa Kusini na Ukerewe (Mkoa wa Mwanza) upande wa Magharibi. Halmashauri ipo Latitudo $01^{0}30$ na $2^{0}45$ Kusini na Longitudo $33^{0}39$ na $34^{0}05$ Mashariki. Ina eneo la $3,088km^{2}$ ambapo $200km^{2}$ ni maji ya Ziwa Viktoria na $2,888km^{2}$ ni nchi kavu. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti inachukua $112km^{2}$, na Pori la Akiba la Grumet linachukua eneo la $380km^{2}$; eneo lililobaki la $2,396km^{2}$ ni ardhi nzuri kwa kilimo, ufugaji na makazi. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 335,061 ambapo ongezeko kwa mwaka ni wastani wa 2.9%. Halmashauri ina Tarafa 4 za Chamriho, Kenkombyo, Nansimo na Serengeti, Kata 33 na Vijiji 106.

Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo, ufugaji na uvuvi. Uvuvi ni shughuli kuu ya tatu ambayo imeajiri watu wapatao 15,610 unaendeshwa ndani ya Ziwa Viktoria. Aina kuu ya samaki wanaovuliwa ni sangara, sato na dagaa; aina nyingine zinazovuliwa ni gogogo na furu. Shughuli za uvuvi huchangia mapato ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kupitia leseni na ushuru.

Athari za kimazingira za ufugaji wa samaki katika vizimba ni ndogo zikilinganishwa na matokeo makubwa kiuchumi. Aina hii ya ufugaji inafanyikia ndani ya mazingira asilia ya ziwani ambayo yanaruhusu samaki kupata hewa na mazingira halisi yanayohitajika na hupunguza changamoto ya ufugaji wa samaki katika mabwawa ya kuchimbwa ardhini. Kutokana na uzalishaji mkubwa uliopo katika ufugaji wa samaki kwenye vizimba, njia hii hutumika kuongeza uzalishaji na kurejesha mazalia ya samaki kwa uwekezaji mdogo usiohitaji eneo kubwa la ardhi. Ufugaji huu unaweza kuchukuliwa kama shughuli ya kifamilia kwa kuwa unahitaji nguvukazi kidogo na inaweza kusimamiwa katika ngazi ya kaya.

## 2.0 TATIZO

Kabla ya mwaka 2000, ilibanika kuwa kiwango cha samaki waliovuliwa ndani ya Ziwa Viktoria kilipungua kutokana na uvuvi haramu ulioathiri mazalia ya samaki. Uvuvi wa samaki uwe wa matumizi ya nyumbani au wa kibiashara unapofanyika kwa njia haramu unasababisha kuharibu mazalia ya samaki na uvuaji wa samaki wachanga hivyo kupunguza kiwango cha samaki wanaovuliwa. Utafiti uliofanywa na SmartFish mwaka 2012 uliabainisha kuongezeka kwa mbinu haramu zinazotomika kuvua samaki wadogo chini ya kiwango kinachotakiwa. Vilevile, utafiti ulibaini kuongezeka kwa mitumbwi ya kawada ya uvuvi kwa 37% na mitumbwi ya kisasa kwa 50% kati ya mwaka 2000 hadi 2008.

Vikundi vya usimamizi wa fukwe (BMUs) havikuwa na mpango madhubuti wa kusimamia uvuvi ndani ya ziwa. Kulikuwa na changamoto ya uvuvi holela. Upungufu wa samaki ndani ya ziwa ulikithiri kwa kiasi kikubwa kutokana na uvuvi haramu. Taarifa za utafiti wa kitaifa wa miaka mitatu zilionesha kuongezeka kwa vitendo vya uvuvi haramu uliosababisha kupungua kwa samaki kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo.

**Jedwali Na 1: Matukio ya uvuvi haramu**

| Na. | Aina ya zana iliyotumika | Haramu/ Halali | 2012 | 2014 | 2016 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Kokoro | Haramu | 212 | 253 | 120 |
| 02 | Nyavu za matundu madogo | Haramu | 310 | 232 | 104 |
| 03 | Nyavu wima ndogo | Haramu | 405 | 336 | 258 |
| 04 | Nyavu wima kubwa | Halali | 312 | 317 | 295 |
| 05 | Kokoro la mtumbwi | Haramu | 0 | 0 | 78 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 06 | Ndoana kipimo cha 8 - 11 | Halali | 256 | 219 | 190 |
| 07 | Ndoano kipimo zaidi ya 11 | Haramu | 127 | 113 | 104 |
| 08 | Nyavu za Dagaa 8mm | Halali | 305 | 235 | 182 |
| 09 | Nyavu za Dagaa < 8mm | Haramu | 0 | 0 | 0 |
| | Jumla ya zana | | 1927 | 1705 | 1331 |
| | % ya zana haramu | | 55 | 55 | 50 |

Kupungua kwa kiwango cha samaki ziwani kulisababisha wavuvi kutafuta samaki kwa kuvamia maeneo ya mazalia, kitendo ambacho kiliharibu mazalia ya samaki na kubadilisha ikolojia ya ziwa. Licha ya kupungua kwa kiwango cha samaki ziwani, ongezeko la watu lilichangia uhitaji mkubwa wa samaki uliochochea uvuvi haramu na kuharibu mazalia ya samaki ndani ya ziwa Viktoria. Takwimu za kupungua kwa samaki kwa miaka sita ndani ya ziwa Victoria zimeoneshwa kwenye jedwali 2 hapa chini.

**Jedwali Na 2: Kupungua kwa samaki ndani ya ziwa Victoria**

| S/N | Aina ya Samaki | 2010 / 2011 | 2011 / 2012 | 2012 / 2013 | 2013/2014 | 2014/2015 | 2015/2016 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Sangara | 1,779,850 kg | 845,606 kg | 459,750 kg | 451,478kg | 537,851kg | 556,436kg |
| 2. | Sato | 1,035,098 kg | 254,301 kg | 166,627 kg | 164,011kg | 125,991kg | 131,303kg |
| 3. | Dagaa | 2,082,377 kg | 623,368 kg | 298,091 kg | 280,534kg | 312,730kg | 124,422kg |
| 4. | Aina nyingine* | 140,760 kg | 136,562 kg | 147,940 kg | 135,025kg | 226,066kg | 186,485kg |
| | Jumla | 5,038,085 kg | 1,859,837 kg | 1,072,408kg | 1,031,048kg | 1,202,638kg | 998,646kg |

*Aina nyingine Furu (Haplochromis Spp), Mumi (*Clarias*), Gogogo (*Synodontis*), Nembe (*Schilbe*), *Kamongo (Protopterus)*, Soga (*Alestes*), Ningu (*Labe), Domodomo* (*Mormyru)* na Hongwe (*Bagrus)*

Taarifa ya Umoja wa Uvuvi wa Ziwa Victoria (Lake Victoria Fisheries Organization - LVFO ) ya mwaka 2010 ilionesha kwamba sangara wamepungua kwa tani mil 1.4 kutoka mwaka 2005 hadi kufikia wastani wa tani 298,394 mwaka 2008.

**3.0 LENGO**

Kutokana na kupungua kwa samaki, suluhisho pekee lililobainishwa ni kuanzisha ufugaji wa samaki katika vizimba ndani ya ziwa. Hatua hii ililenga kukidhi hitaji la samaki kwa matumizi ya nyumbani, biashara na kurejesha mazalia ya samaki. Sera ya taifa ya uvuvi ya mwaka 2015 inasisitiza ufugaji wa samaki kwenye vizimba kama mbadala wa kuongeza samaki kwa matumizi ya jamii na biashara hivyo kupunguza shaghuli za uvuvi kwenye maziwa na sehemu nyingine za uvuvi.

Lengo la jitihada hii lilikuwa kujenga uwezo wa vikundi vya udhibiti wa fukwe za ziwa (BMUs), Kikosi cha Jeshi ( 822 KJ ) na jamii inayozunguka Ziwa Viktoria kuhusu ufugaji wa samaki kwenye vizimba ili kuongeza uzalishaji wa samaki na kurejesha mazalia ya asili. Aidha,kupunguza uvuvi haramu kutoka 95% mwaka 2015 hadi 10% mwaka 2020. Malengo mahususi ni pamoja na;

(i) Kuanzisha na kuhamasisha jamii, BMUs na Kikosi cha Jeshi kutumia teknolojia ya vizimba ya ufugaji wa samaki.
(ii) Kubuni vyazo vya kupata fedha za kuendeleza shughuli za vizimba ndani ya ziwa Viktoria.
(iii) Kushirikisha jamii, BMU na Kikosi cha Jeshi kujishughulisha na ufugaji wa samaki kwenye vizimba katika maeneo mbalimbali ndani ya Ziwa Victoria.
(iv) Kuanzisha mahusiano thabiti kati ya jamii, idara ya uvuvi na vituo vya utafiti.
(v) Kuanzisha namna bora ya uzalishaji wa chakula cha samaki na vifaranga kwa ajili ya ufugaji wa kwenye vizimba na mabwawa.
(vi) Kuanzisha namna nzuri ya kuhifadhi samaki wa kufugwa na wale wa ziwani.
(vii) Kuanzisha na kutumia kituo bora cha kutotolesha vifaranga vya samaki.

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Dhana ya ufugaji wa samaki kwenye vizimba ilianzishwa baada ya kufanyika kwa ziara ya mafunzo katika nchi za Kenya na Uganda. Ziara hii ya mafunzo iliandaliwa na ESRF (Economic and Social Research Foundation) mwezi Machi 2014 chini ya usaidizi wa Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP). Ziara ililenga kubaini fursa, kujifunza teknolojia za uvuvi katika nchi za Uganda na Kenya hivyo kuleta ujuzi huo kwa jamii za watu wa H/W za Bunda na Bukoba. Washiriki wa ziara hii walikuwa ni maafisa uvuvi wa 2 kutoka Bunda na Bukoba, wavuvi 6 kutoka na mtafiti mmoja kutoka ESRF. Timu hii ilishauri UNDP kutoa usaidizi katika kuanzisha ufugaji wa samaki kwenye vizimba kwa kuwasaidia wananchi na Taasisi zinazojishughulisha na uvuvi kama Kikosi cha Jeshi cha 822KJ RWAMKOMA. Kufikia mwezi Agosti, 2014 UNDP ilikubali andiko la mradi na kutoa usaidizi wa kuanzisha ufugaji wa samaki kwenye vizimba. Katika kutekeleza jitihada hii mikakati ifuatayo ilitekelezwa.

Kubaini wadau na kujenga uelewa; Juni 2014, Halmashauri ilibaini wadau wa uvuvi wa samaki kutoka kwenye jamii, BMUs na 822KJ. Wadau walifahamishwa kuhusu ufugaji wa samaki ndani ya vizimba na umuhimu wake. Kikosi cha 822KJ kilivutiwa na kuonyesha utayari wa kutekeleza jitihada hii kwa kushirikiana na Halmasahuri. Mwaka 2014, Halmashauri iliidhinisha matumizi ya vizimba katika ufugaji wa samaki kwa kikosi cha 822KJ, BMU, makampuni ya uvuvi, vikundi vya uvuvi na wananchi mmoja mmoja kujihusisha na ufugaji huo ndani ya Halmashauri ili kukabiliana na upungufu wa samaki ndani ya ziwa Viktoria. Halmashauri ilitambua Kikosi cha 822KJ kama watekelezaji wakuu na wasimamizi wa kazi za ufugaji wa samaki kwenye vizimba katika Ghuba ya Bowman.

Uanzishaji wa ufugaji wa samaki wa kibiashara katika vizimba na utambuzi wa maeneo bora ya ufugaji; Halmashauri ilihamasisha jamii ya Kijiji cha Karukekere na Kikosi cha 822KJ kujishughulisha na shughuli za ufugaji wa samaki katika Ghuba ya Bowman ndani ya Ziwa Viktoria. Maafisa Uvuvi 2, watafiti kutoka ESRF, mtaalam mmoja kutoka Wizara ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo walihusika katika kubaini eneo ambalo linafaa kuanzisha vizimba vya ufugaji wa samaki. Eneo la Ghuba ya Bowman linalozunguka vijiji vya Karukekere, Bujinge (Kijiji cha Muranda), Isanju, Mugara, Sikiro na Michagondo lilibainishwa kwa ajili ya ufugaji wa samaki aina ya sato.

Uanzishaji wa vikundi vya ufugaji; mwaka 2015, vikundi 2 vianzishwa ambavyo ni Kikundi cha KIUSAKA chenye wajumbe 25 kati yao 17 wanaume na 8 wanawake na kiundi cha FASAC chenye wajumbe 17 kati yao wanaume 11 na wanawake 6. Vikundi vilipewa usaidizi wa kuanzisha katiba na kusajili katika Halmashauri. Vikundi hivi vilipata usaidizi wa vizimba 5 kutoka UNDP na vikaanza kujishughulisha na kazi za ulishaji wa samaki, usafishaji wa vizimba na upangaji wa madaraja ya samaki ndani ya vizimba.

Uanzishaji wa kamati ya usimamizi wa mradi; baada ya utambuzi wa maeneo mazuri ya utekelezaji wa jitihada hii, chini ya usimamizi wa Kikosi cha Jeshi 822KJ kwa mujibu wa makubaliano na Halmashauri, kamati ya usimamizi wa mradi iliundwa na wajumbe kutoka Halmashauri,Kikosi 822KJ kama msimamizi mkuu na wajumbe kutoka kwenye jamii ya vijiji vilivyobainishwa. Kamati iliundwa na wajumbe saba ambao ni;

(i) Mkuu wa Wilaya ya Bunda (Mwenyekiti)
(ii) Mjumbe mmoja kutoka kikosi cha 822KJ (Katibu)
(iii) Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bunda (Mjumbe)
(iv) Afisa uvuvi wa Halmashauri (Mjumbe)
(v) Diwani wa Kata ya Namuhula (Mjumbe)
(vi) Mwenyekiti wa Kijiji cha Karukekere (Mjumbe)
(vii) Mkulima mmoja anayejishughulisha na shughuli za uvuvi kutoka Kijiji cha Karukekere (Mjumbe)

Kamati inatoa ushauri kuhusu utekelezaji wa mradi na kusaidia kukuza uhusiano baina ya wananchi, Halmashauri na Kikosi cha Jeshi (822KJ). Kamati ndogo ilianzishwa chini ya kamati hii ikiwa na wajumbe 14 (wajumbe 10 kutoka 822KJ, 2 kutoka kijiji cha Karukekere na 2 kutoka BMUs). Kamati ilisisitiza kujenga dhana ya umiliki na kubadilisha mtazamo wa jamii na wadau kuachana na uendeshaji wa uvuvi haramu.

Utoaji wa mafunzo kwa wajumbe wa kamati ndogo; mafunzo ya siku mbili yalitolewa kwa wajumbe wa kamati ndogo na maafisa uvuvi 2 kutoka Halmashauri. Mafunzo haya yaligusia sababu za kupungua kwa samaki ndani ya ziwa, mbinu za ufugaji wa samaki kwenye vizimba, umuhimu wa ufugaji wa samaki, usimamizi wa uvuvi na usimamizi wa fedha na mradi. Mafunzo yaliwezesha wahudumu wa vizimba na wajumbe wa kamati ndogo kujishughulisha na ufugaji wa samaki kwenye vizimba.

Ujenzi wa vizimba vya samaki; Kikosi cha Jeshi cha 822KJ kilitoa mafunzo kwa wafugaji wa samaki kutoka Kijiji cha Karukekere kuhusu utaalam wa ujenzi wa vizimba. Wajumbe wa kamati ndogo vilevile walitengeneza vizimba kwa kutumia mabomba meusi ya duara ambayo yalishikiliwa na mapipa ya plastiki yanayoelea juu ya maji na upande wanje wa vizimba ulizungushwa nyavu ya matundu ya nchi moja na nusu ili kuzuia samaki wasitoke kwenye vizimba. Jumla ya vizimba 50 vilitengenezwa ambapo Kikosi cha 822KJ kilipatiwa vizimba 45 na vikundi vya wafugaji samaki vilipatiwa vizimba 5.



***Wakulima wakibuni na kujenga kizimba katika pwani ya Kijiji cha Karukekere***

Usimamizi na uendeshaji wa vizimba; kamati ndogo inasimamia vizimba na kulisha samaki. Uwezekano wa samaki ndani ya vizimba kupata chakula cha asili na cha kutosha ni mgumu kuliko kwa samaki ambaye yupo huru ndani ya maji hivyo chakula cha ziada kinahitajika kwa samaki hawa. Aina ya chakula cha samaki hawa hutengenezwa kutokana na malighafi zitokanazo na wanyama kwa 70% na mashudu yatokanayo na usindiaji wa mafuta, pumba za mahindi na mchele 30%. Kazi nyingine muhimu ni usafishaji wa nyavu za vizimba kila baada ya mwezi mmoja. Kamati ndogo ina hakikisha ubora wa maji kwa kuangalia ya fuatayo;

(i) Kudhibiti kiwango cha taka zitokanazo na viumbe hai zinazoingia ndani ya ziwa; kazi hii hufanywa kwa kuzuia idadi ya ng'ombe wanaoingia kwenye pwani ya ziwa ili kupunguza kiwango cha mbolea kuingia kwenye maji hasa kipindi cha mvua.

(ii) Kudhibiti kiwango cha masalia ya *mimea maji* ili kuruhusu hewa safi kupenya.

(iii) kuthibiti magugu maji ili kuhakikisha kiwango sahihi cha hewa safi ndani ya maji.

Upangaji wa samaki kwenye madaraja; samaki wanaolingana nahamishwa na kuwekwa kwenye kizimba kimoja na kuwaacha samaki wadogo kwenye kisimba cha awali. Uchambunzi na pangaji wa samaki katika madaraja unafanywa kwa kunyanyua nyavu za kizimba kutoka kwenye maji na kuchambua

kutokana na ukubwa wa samaki. Nyavu ndogo au chombo cha plastiki hutumika kuwatenga zamaki kulingana na ukubwa. Hatua hii husaidia samaki kulishwa kwa uwiano sahihi.



***Zoezi la kutenga samaki kwenye madaraja***

Ziara ya mafunzo Uganda na Thailand; mwaka 2015, wajumbe 12 wa kamati ndogo walitembelea fukwe ya Musese Jinja Uganda kujifunza uendeshaji wa vizimba vya ufugaji sato. Mwezi Septemba 2015 kundi la wajumbe 8 walikwenda nchini Thailand kwa lengo hilohilo la kujifunza chini ya ufadhili wa UNDP. Ziara za mafunzo ziliwezesha waendeshaji wa mradi kupata mbinu na ujuzi wa ziada wa ufugaji wa samaki kwenye vizimba. Masomo waliyojifunza ni pamoja ukweli kuwa ufugaji wa samaki kwenye vizimba ni wa gharama nafuu kwani miazi inaweza kutumika kutengeneza vizimba badala ya mabomba yenye gharama kubwa. Aidha, uvunaji wa samaki kwenye vizimba ni rahisi kwani unahitaji kunyanyua nyavu tu na kuanza kuokota samaki ikilinganishwa na matumizi ya nyavu na mtumbwi kwenye uvuvi wa kawaida. Walijifunza pia teknolojia ya vizimba hutoa fursa ya shughuli za uvuvi kufanywa na wanawake na wanaume.

**5.0 RASILIMALI**

Halmashauri ya Bunda ilitumia aina mbalimbali za rasilimali katika kufikia malengo ya utekelezaji wa jitihada hii . Kwa upande wa raslimali fedha; UNDP ilifadhili mradi kuanzia hatua za mwanzo kwa muda wa miaka 3 (Desemba, 2015 - Desemba, 2018). Gharama za mradi huu ni TZS 150,370,500 kama inavyofafanuliwa kwenye jedwali na.3 hapa chini.

**Jedwali Na 3: Gharama za Mradi**

| No | Shughuli | Kiasi (TZS) | UNDP | BUNDA DC | 822KJ | Jamii |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Mafuzo kwa kamati ya usimamizi | 1,348,000 | 1,148,000 | | 200,000 | |
| 02 | Kusaini mkataba wa makubaliano | 1,730,000 | 1,530,000 | 200,000 | | |
| 03 | Kuteua na kuendesha mafunzo kwa watalamu wa kusimamia vizimba | 8,015,000 | 3000,000 | 3,000,000 | 2,015,000 | |
| 04 | Utengenezaji wa Vizimba | 49,800,000 | 40,400,000 | 400,000 | 8,000,000 | 1,000,000 |
| 05 | ununuzi na usambazaji wa vifaa | 20,827,000 | 16,827,000 | | 4000,000 | |
| 06 | Ziara ya Mafunzo Uganda | 22,675,000 | 22,675,000 | | | |
| 07 | Ununuzi wa vifaa vya kulishia samaki | 18,600,000 | 14,400,000 | | 4200,000 | |
| 08 | Uanzishaji kituo cha kupata na kutolea taarifa | 5,520,000 | 1200,000 | | 4,320,000 | |
| 09 | Ununuzi vifaa vya ofisi | 6,600,000 | 6600,000 | | | |
| 10 | Kuratibu na kusimamia shughuli za vizimba | 7,515,000 | | 1,515,000 | 5,000,000 | 1,000,000 |
| 11 | Uaandaji wa ripoti ya Usimamizi na | 7,740,000 | 7,740,000 | | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | tathimini | | | | | |
| | **JUMLA** | **150,370,000** | **115,520,000** | **5,115,000** | **27,735,000** | **2,000,000** |

Rasilimali watu; rasilimali watu ilihusisha maafisa uvuvi kutoka Halimashauri ya Bunda, watafiti wa ESRF na wataalamu kutoka wizarani ambao walitoa usaidizi wa kuunganisha wadau na kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na wasimamizi wa mradi kutoka Kijiji cha Karukekere. Vilevile rasilimali watu imejumuisha wasimamizi na walinzi 10 kutoka Kikosi cha 822KJ RWAMKOMA wanaofanya kazi kama kamati ndogo ya usimamizi pamoja na wajumbe 6 kutoka kwenye ngazi ya jamii.



***Wajumbe wa kamati ndogo wakitekeleza wajibu wao kwenye vizimba***

**6.0 MATOKEO**

Halmashauri imeshuhudia matokeo makubwa ambayo yanaweza kuenezwa kwa jamii yingine zilizo kwenye fukwe za maziwa na bahari. Teknolojia ya ufugaji wa samaki ndani ya ziwa imeanzishwa na tayari kuna vizimba 50 vyenye 100,000 (vizimba 45 vinamilikiwa na 822KJ na 5 vinamilikiwa na vikundi). Aidha, jitihada hii imewezesha kuwepo kwa kamati kuu na kamati ndogo za usimamizi zenye wajumbe waliopata mafunzo na vikundi vya ufugaji samaki na imejenga mahusiano yenye tija kati ya Halmashauri, UNDP, ESRF, Kikosi cha 822KJ na jami ya watu wa kijiji cha Karukekere. Uhusiano huu umesaidia kuleta teknolojia mpya ya ufugaji wa samaki, kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu, kuongezeka kwa samaki na kuimarika kwa ikolojia ya viumbe wa majini. Kikosi cha 822KJ kinaendelea kujenga uwezo wa vikundi vya wakulima kujihusisha na ufugaji wa samaki kwenye vizimb na kulinda eneo la Ghuba ya Bowman.



***Mtumishi wa 822KJ akitoa mafuzo kwa wakulima wa kijiji cha Karukekere***

Matarajio ya mapato; inakadiriwa kwamba vizimba 50 vyenye samaki 100,000 vitazalisha watani wa kilo 48,000kg zenye thamani ya TZS 288,000,000 (faida TZS 137,629,500)



***Samaki aina ya sato wakiwa kwenye nyavu katika Ghuba ya Bowman Kijiji cha Karukekere***

Kupungua kwa shughuli za uvuvi haramu kwenye maeneo ya mazalia ya samaki; kutokana na ulinzi mkali unatolewa na kikosi cha 822KJ RWAMKOMA, shughuli za uvuvi haramu zimepungua kufikia 35%. Awali zaidi ya 98% ya shughuli za uvuvi zilifanyika kwa njia haramu. Wavuvi walitumia nyavu na kemikali zisizoruhusiwa katika uvuaji wa samaki hasa aina ya sato. Uvuaji wa samaki kwa siku ulikua wastani wa kati ya samaki 5 hadi 30 kwa mtumbwi. Sasa hivi kuna ongezeko kubwa la samaki kwenye ziwa baada ya kuanzisha vizimba. Wavuvi kutoka vijiji vya Karukekere na Muranda ambao wanaojishughulisha na uvuvi kuvua kati ya samaki 80 hadi 120 kwa mtumbwi. Bw. Kasera Ochieng' ambaye ni mvuvi na mwenyekiti wa BMU katika Kijiji cha Karukekere alithibitisha kwamba ongezeko la samaki limetokana na kuanzishwa kwa jitihada za ufugaji samaki kwenye vizimba na kupungua kwa vitendo vya uvuvi haramu.

Wanawake na vijana wanajishughulisha na ufugaji wa samaki kwenye vizimba; ilibanika kwamba idadi kubwa ya wanawake na vijana wameanza ufugaji wa samaki kwenye vizimba. Zaidi ya wanawake 26 kutoka Karukekere wanajihusisha na ufugaji huu. Kwa upande wa wavuvi, ufugaji wa samaki kwenye vizimba umeonekana una tija kubwa kuliko kutumia muda na nguvu nyingi kwenye uvuvi wa mazoea na hatimaye kurudi bila samaki. Wavuvi wapatao 76 wamebadilika kutoka uvuvi wa mazoea na kujiunga na vikundi vya ufugaji wa samaki kwenye vizimba.



***Wanawake wakihudumia samaki kwenye vizimba***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

UNDP, H/W ya Bunda, Kamati ya usimamizi wa mradi na wadau wameendelea kushirikiana katika kupanga mipango ya muda mrefu ya kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi. Moja ya makubaliano ni kuanzisha mfuko wa mzunguko . Fedha zinazopatikana baada ya uuzaji wa samaki zitatengwa kiasi kwa ajili ya kusaidia shughuli za kupanua mradi. Utashi wa Halmasahuri, Mwenyekiti wa Kijiji, Diwani wa Kata , Mtendaji wa Kata na Mtendaji wa Kijiji kwa kushirikisha jamii kuliweka dira ya uendelevu wa mradi huu. Halmashauri ilianzisha usimamizi wa pamoja na wadau na kuanzisha kwa kamati ya usimamizi wa mradi na kamati ndogo zenye nguvu. Ushirikiano uliojengeka unachochea na kuchagiza kuanzishwa kwa makundi mengine ya ufugaji wa samaki kwenye vizimba. Zaidi ya wavuvi 100 wameanzisha vikundi 6 ambapo vikundi 4 viajihusisha na ufugaji kutumia vizimba. Vikundi hivi vimetumika kubadilisha mtazamo ya wavuvi kutoka uvuvi wa mazoea na kujiunga kwenye ufugaji wa samaki kwenye vizimba. Hali hii inasaidia kuhakikisha uendelevu wa jitihada hii.

Mafunzo yaliyotolewa kwa jamii na wajumbe wa Vikundi vya Usimamizi wa Fukwe (BMUs) yanaendelea kuimarisha uzimamizi wa mradi. Nidhahiri kwamba baada ya usaidizi kutoka UNDP utakapofika ukomo, jamii yenyewe itaweza kuenedeleza na kupanua wigo wa ufugaji samaki kwenye vizimba hadi kufikia lengo la vizimba 1000. Vilevile, Halmashauri ina mpango wa kutenga bajeti kila mwaka kwa lengo la kujenga uwezo wa jamii kusimamia mradi. Mwaka 2016/2017, TZS 5,000,000 sawa na 12.8% ya bajeti ya Idara ya uvuvi (TZS 39,000,000) ilitengwa kwa lengo la kutoa usaidizi wa ufugaji wa samaki kwenye vizimba.

Uanzishwaji wa kituo cha kutotolesha vifaranga vya samaki; Kikosi cha 822KJ RWAMKOMA kilipata usaidizi wa kuanzisha kituto cha kutotolesha vifaranga vya samaki ambao baadae huhamishiwa kwenye vizimba vya kufugia samaki.



***Kituo cha kutotolesha vifaranga vya samaki eneo la Bulamba JKT (822KJ-RWAMKOMA)***

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada hii yanatokana na sababu nyingi; utashi na uthubutu wa Timu ya Menejimenti ya Halmshauri, Kikosi cha 822 KJ, Diwani wa Kata, Mwenyekiti wa Kijiji na Watendaji wa Kata na Vijiji katika kutekeleza jitihada hii. Uthubutu wao ulitia hamasa kwa jamii na kuunganisha wadau na kuwaelimisha kuhusu faida za ufugaji wa samaki kwenye vizimba. Wadau walivutiwa na jitihada hii na kuamua kushiriki katika utekelezaji.

Sababu ya pili ni ufanisi wa vikundi vilivyoundwa na kusajiliwa; Baada ya kugundua upungufu wa samaki na kuongezeka kwa vitendo vya uvuvi haramu, wavuvi wa samaki na jamii waliunda vikundi ambavyo baadae vilisajiliwa na Halmashauri. Vikundi hivi vilijipanga kusimamia utunzaji wa vizimba vya samaki. Kila mjumbe wa kikundi amepangiwa majukumu anayopaswa kutekeleza kila wiki na hali hii imejenga dhana ya umiliki.

Ziara za mafunzo nchini Uganda, Kenya na Thailand zilizofadhiliwa na UNDP zilifungua upeo wa washiriki kuona na kuvutiwa na ufugaji wa samaki kwenye vizimba. Kikosi cha Jeshi (822KJ) kilijizatiti kuwa mtekelezaji mkuu na kupewa jukumu la kusimamia na kufundisha wadau wengine wanaozunguza Ghuba ya Bowman. Kutokana na usaidizi wa 822KJ hamasa ya jamii na imani kuhusu ufugaji wa samaki kwenye vizimba imeongezeka.

# Rejea

*Abiona, A. I. and Bello, W. N. (2013). Grassroots Participation in Decision-Making Process and Development Programmes as Correlate of Sustainability of Community Development Programmes in Nigeria, Journal of Sustainable Development; Vol. 6 (3):47-57. Canadian Centre of Science and Education, [www.ccsenet.org/jsd] site visited on 19 /03/ 2013.*

Apolo, Kansiime (2013). The Impact of Public Procurement Reforms on Service Delivery in Uganda; Bishop Stuart University.

Chibehe, M.M. (2004). Factors Affecting Sustainability of Farmer Groups: the case of Twikinde Malimbichi Cooperative Society. MA Dissertation, SUA, Unpublished, 90pp.

Helene Bie Lielleor and Ulrik Lund-Sorensen (2013). FARMERS' CHOICE evaluating an approach to agricultural technology and adoption in Tanzania, Rockwool Foundation research Unit, PRACTICAL ACTION Publishing, pp. 154.

Helmsing, A. H. J. (1995). *Local Government Central Finance.*An Introduction: NewYork USA

Howlett. D and J. Nagu. (1997). *Agricultural Project Planning in Tanzania, A handbook on cycles and sequences, participation, identification, planning and design, economic and financial analysis, and environmental assessment of agricultural projects.* ISBN 1898828261. pp 89.

Kusago, Takayoshi. (2008). *Sustainable Livelihood and Happy Generation in Minamata-City Japan*: A Model for Endogenous Community Development.

Makonda, K.S.C. (2003). Partnership and sustainability of water supply systems in Bukombe District, Tanzania. *MA Dissertation*, Sokoine University of Agriculture, Morogoro, Tanzania. Unpublished. pp.154

Mwanga, J.N. (2011). Empowerment of Local Society in Tanzania –the Nucleus for Development- With Experience from Indonesia and Japan, *Rare Series Policy Paper*, Local Government Training Institute, Dodoma Tanzania. 100 pp.

Ohama, Y. (2002). Basic Framework and viewpoints of Participatory Local Social Development (PLSD) and construction of its evaluation framework.

Porter, Michael E. (1998). *Competitive Advantage: Creating and Sustaining Superior Performance*, 397

pp, Amazon.

Pretty, J.N. (1995). Participatory learning for sustainable agriculture. *World Development* 23(8): 1247-1263.

Scoones, I. and John Thompson (1994). *BEYOND FARMER FIRST: Rural people's knowledge, agricultural research and extension practice*. Intermediate Technology Publications LTD, London, UK, pp.301.

Sharma, P.N. and Ohama, Y. (2007*). Participatory Local Social Development-An Emerging Discipline*, Bharat Book Centre Publishers & Distributors, Lucknow India. pp. 467.

Shikuku, O.M. (2012). Community related Variables influencing sustainability of water projects in Nyando District a case. *MA Dissertation*, University of Nairobi, Digital Repository

URT (1998). Local Government Reform Agenda

URT, (2010). Public private partnership (PPP) *Act*, no 18 of 2010, pp 21

URT (2011). Millennium Development Goals, Tanzania country report. Ministry of Finance and Economic Affairs, Dar es Salaam – Tanzania.

Zadeh, B.S. and Nobaya, A. (2010). Participation and Community Development. *Current Research Journal of Social Sciences* 2(1): 13-14, 2010. [http://maxwellsci.com/print/crjss/v2-13-14.pdf] site visited on 22/07/2014.